التوسل

أنواعه وأحكامه

AT-TAWASSUL

MKUSANYAJI

MUHAMMAD 'EID AL-'ABBASI

MTUNGAJI

SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DIN AL-ALBAANI

MFASIRI

ABU FARIDA MUHAMMAD AWADH SALIM BASAWAD

© HAKI YA UCHAPISHAJI
Uchapishaji wa kitabu hiki ni milki ya kiufundi ya **"THE QURAN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA"**. Kila kilichomo ndani, kwa ujumla, ni hifadhi ya qssea.
Hairuhusiwi kuiga kwa njia yoyote iwayo kutoka kwa wachapishaji asili; hivyobasi uchapishaji wa kitabu hiki utahitaji ridhaa kutoka kwa muandishi. Iwapo chochote kutoka kwenye kitabu hiki kitatumiwa kama sehemu ya shirika jengine la kiufundi ama isokuwa hivyo, basi ruhusa kutoka **QSSEA** itahitajika.

Ruhusa inaweza kuombwa kutoka kwa:

The Qur'an and Sunnah Society of East Africa,
P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

Ama kwa Barua Pepe (e-mail)- info@qssea.net
web-site – www.qssea.net

Chapa ya Kwanza: Nakala 1000 [2015 / 1435]

ISBN 978-9966-1824-7-0

JUMUIYA YA QUR'AN NA SUNNAH YA AFRIKA YA MASHARIKI

MEZA YA YALIYOMO

المقدمة VII

Sheikh Akram Ziyâdeh X

Sheikh Muhammad ‘Eid Al-‘Abbâsî XIV

Tawassul XVII

SAMPULI ZAKE NA HUKMU ZENYE KUHUSIANA NAYO XVII

Mlango Wa Kwanza 1

TAWASSUL KATIKA LUGHA YA KIARABU NA KATIKA QUR’ÂN 1

Maana Ya Tawassul Katika Lugha Ya Kiarabu 1

Maana Ya Wasîlah Katika Qur’an 3

‘AMALI NJEMA PEKE YAKE NDIZO WASÎLAH ZENYE KUMKURUBISHA MTU KWA ALLÂH 6

NI WAKATI GANI ‘AMALI YA MTU INAPOKUWA NI NJEMA 7

La Kwanza 7

La Pili 7

Mlango Wa Pili 9

NJIA ZA KI-MAUMBILE NA NJIA ZA KI-MALENGO KATIKA SHERIYA 9

TUTAJUAJE USAWA WA *WASÂIL (*NJIA), NA UWAJIBIKAJI WAKE KATIKA SHERIYA? 15

AT-TAWASSUL YA KI-SHERIYA NA SAMPULI ZAKE 23

TUTAWASSAL (KUTAFUTA NJIA ZA KUJIKURUBISHA) KWA ALLÂH (تعالى) KWA MAJINA MIONGONI MWA MAJINA YAKE YENYE UKAMILIFU NA YALIYO MAZURI, AU KWA SIFA ZAKE MIONGONI MWA SIFA TUKUFU 25

TUTAWASSAL KWA ALLÂH (تعالى) KWA AMALI NJEMA ALIYOWAHI KUIFANYA MUOMBAJI 30

UBATILI NA MAKOSA YA *KU-TAWASSAL* KWA NJIA NYENGINE YOYOTE ISIYOKUWA NJIA TATU ZILIZOTANGULIA 41

Mlango Wa Nne 52

SHAKA ZILIZOLETWA NA JAWABU ZAKE 52
SHAKA YA KWANZA 52
HADÎTH INAYOELEZA JINSI ‘UMAR ALIVYOKUWA AKIMTAKA AL-‘ABBĀS (رضي الله عنهما) AWAOMBEE MVUA 52
Tanbihi *61*
Pingamizi Na Ukosoaji Wake *69*
Wa Kwanza *69*
Wa Pili *69*
Wa Tatu *70*
Wa Nne *70*
KISHA MAJIBU YA HAYA VILEVILE YANATOKAMANA NA PANDE NYINGI 71
La Kwanza *71*
La Pili *72*
SHAKA YA PILI 74
HADÎTH YA MTU-KIPOFU 74
KUONDOA UFAHAMU WA KI-MAKOSA 83
NYONGEZA KATIKA HADÎTH YA MTU-KIPOFU 90
Nyongeza Ya Kwanza *90*
Nyongeza Ya Pili *92*
Tanbihi *100*
SHAKA YA TATU 103
AHĀDÎTH DHA’ÎF KATIKA TAWASSUL 103
Hadîth Ya Kwanza *103*
Hadîth Ya Pili *108*
Hadeeth Ya Tatu *110*
Hadeeth Ya Nne *110*
Hadeeth Ya Tano *112*
Hadeeth Ya Sita *114*
Tanbîh 118
VIPI HADÎTH HII INAVYOKHALIFU QUR’ÂN 123
Ya Kwanza *123*
Ya Pili *125*
Hadeeth Ya Saba *127*

ATHARI MBILI *DHA'ÎF* 130
Athari Ya Kwanza *130*
Tanbîh *133*
TAFAUTI BAINA YA *TAWASSUL* KWA DHATI YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NA KUMTAKA YEYE MWENYEWE AKUOMBEE *DU'Â'* 133
KUWAOMBA MSAADA WENGINE WASIOKUWA ALLÂH (تعالى) 136
Athari Ya Pili *139*
Tanbihi *144*
SHAKA YA NNE 145
KUWEKA VIPIMO VYA MAKISIO YA KULINGANISHA BAINA YA MUUMBA NA VIUMBE 145
SHAKA YA TANO 150
KUNA JAMBO LOLOTE LIWEZALO KUZUIYA *TAWASSUL* YA UZUSHI KUWA NI KITU TU KILICHORUHUSIWA LAKINI SI JAMBO LILILOPENDEKEZWA? 150
Suala La Pili *151*
Suala La Tatu *151*
SHAKA YA SITA 152
KUFANYA MAKISIO BAINA YA *TAWASSUL* KWA NJIA YA DHATI AU JAHA YA MTU NA *TAWASSUL* KWA 'AMALI NJEMA 152
SHAKA YA SABA 153
KUFANYA MAKISIO BAINA YA *TAWASSUL* KWA NJIA YA DHATI YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NA KUTABARUKU KWA ATHARI ZAKE 153
MAKOSA YA AL-BÛTWÎ KATIKA KUIFANYA *TABARRUK* (KUTAFUTA MANUFAA) NA *TAWASSUL* KUWA NI HICHOHICHO KITU KIMOJA 157
KUTOFAA KWA *TAWASSUL* KWA NJIA YA ATHARI ALIZOZIACHA MTUME (صلى الله عليه وسلم) BAADA YA KUFA KWAKE 160
KASHFA KUBWA 164
KOSA LAKE KATIKA KUDAI YAKWAMBA SABABU YA *TAWASSUL* KWA KUPITIA NJIA YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NI KWAMBA YEYE NDIYE MBORA WA KILA KITU KATIKA VIUMBE 166
UJINGA WAKE KATIKA MAANA YA KI-LUGHA YA 'KUMTAFUTA MTU KUMSHUFAIYA KWA NIYABA YAKE.' (AL-ISTISHFÂ') 168

KOSA LAKE KATIKA KUDAI YAKWAMBA TAWASSUL YA MTU-KIPOFU ILIKUWA NI KWA KUPITIA NJIA YA DARAJA ALIYONAYO MTUME (صلى الله عليه وسلم) MBELE YA ALLÂH 171

المقدمة

الحمد لله الذي جعل العلم رحما بين أهله، والصلاة والسلام على رسوله وعبده، نبينا محمد وعلى آله وصحبه وجنده ووفده وبعد:

فقد أسعدني الأخ الأستاذ: أبو فريدة؛ محمد باسواد (المومباسي الكيني)، كفيلُنا، ورفيقُنا، ودليلُنا، ومُضيفُنا، في رحلتنا العلمية، والدعوية إلى (كينيا)، و(تنزانيا)، في رجب سنة ١٤٣٤ هـ (1434H) بتشريفي بتقديم مختصر مني لرسالة شيخنا الإمام محمد ناصر الدين الألباني «التوسل أنواعه وأحكامه» التي حققها ونشرها الأستاذ محمد عيد العباسي، والتي قام الأستاذ أبو فريدة بترجمتها إلى اللغة (السواحلية) التي يتكلم بها مئات الملايين من المسلمين في شرق القارة الأفريقية، إضافة إلى لغات عديدة في شرق القارة السمراء.

وأخونا أبو فريدة هو المؤسس والمدير لجمعية القرآن والسنة في شرق أفريقيا، وناشط في الدعوة إلى الله في نفس الجمعية (جمعية القرآن والسنة بكندا)، وقد عرفته – حفظه الله – في المَقَرَيْنِ؛ في شرق أفريقيا، وفي كندا – على حدٍ سواء – حريصاً على وقته في أداء العبادات، أو المطالعة، أو القراءة، أو الكتابة، أو البحث، أو الترجمة، أو التصوير، أو النشر، أو غير ذلك من الأعمال التي فيها خدمة للدعوة الإسلامية عموما، والدعوة السلفية خصوصاً.

وقد شرفني الأخ المذكور – كما أسلفت – بالتقديم لترجمته للرسالة المذكورة، ولأنني لا أعرف لغته (السواحلية) التي ترجم إليها الرسالة المذكورة، والذي سبق له أن ترجم عدة كتب لأهل السنة من علماء زماننا وغيرهم إلى اللغة (السواحلية)، ولا زال ينشط في مجال الترجمة، أقول:

إن الرسالة المذكورة، والمكتوبة باللغة العربية – أصلاً – رسالة علمية شرعية عظيمة في باب عظيم من أبواب العقيدة السلفية السُنِّيَّةِ من حيث:

1- أسلوب تأليفها المبني على صريح القرآن، وصحيح السنة، وآثار الصحابة والتابعين، وأهل العلم على مر الأزمان والعصور.

2- كتابتها من قِبَلِ إمام متبحر في علوم العقل والنقل، متضلع من معارف الحقيقة والشرع، وهو شيخنا الإمام المشهود له بالإمامة والعلم والهداية من علماء وأئمة الدنيا في زماننا.

3- تحقيقها من قِبَلِ أحد أبرز تلاميذ شيخنا الإمام، ومن أقدمهم له صحبة، ومن أبرزهم في البحث والاستقصاء، والتدقيق والتحقيق وسبك العبارة العربية، ومن أكثرهم انتفاعا به في دمشق الشام قبل عقود طويلة، ألا وهو الأستاذ محمد عيد العباسي، حفظه الله تعالى.

4- نشرها في أكثر من دار نشر في أزمان مختلفة، وانتفاع ملايين المسلمين بها في مختلف البلدان، من خلال ترجمتها إلى عدة لغات أيضاً.

5- إنقاذُها كثيراً من المسلمين الذي اطلعوا عليها وقرأوها من ضلالات التوسل الممنوع، وغير المشروع، ونقلهم إلى صحيح العقيدة السليمة، وهداية السنة القويمة.

6- حثُّ كثيرٍ من أهل العلم، الناسَ على الانتفاع بالرسالة من حيث شرحهم وتعليمهم إياها في مختلف البلدان.

7- مساهمتنا في نشر تراث شيخنا الإمام إلى مختلف المسلمين بلغاتهم التي يحسنونها، ويتقنونها في مختلف بلدان العالم.

8- دعمنا لأخينا الأستاذ أبا فريدة محمد باسواد، وتشجيعه على نشر العلم الشرعي بلغته (السواحلية) من باب قول الله تعالى في سورة القصص (35) لموسى عليه السلام: ﴿سَنَشُدُّ عَضُدَكَ بِأَخِيكَ﴾، ومن باب قول النبي صلى الله عليه وآله وسلم في «صحيح مسلم» (2199) من حديث جابر بن عبد الله - رضي الله تعالى عنهما -: «مَنِ اسْتَطَاعَ مِنْكُمْ أَنْ يَنْفَعَ أَخَاهُ فَلْيَفْعَلْ».

لهذا كله – وغيره مما الله وحده – سبحانه وتعالى – أعلم به – كتبت هذه الكلمات كتقديم لترجمة رسالة شيخنا الإمام الألباني – رحمه الله تعالى – «التوسل أنواعه وأحكامه».

راجيا لله – تعالى – أن ينفع بها مؤلفها، ومحققها، وناشرها، ومترجمها، ومقدمها، وقارئها، وطابعها، وكل من كان له أدنى نصيب في شيء منها، وسائر المسلمين.

وآخر دعوانا أن الحمد لله رب العالمين.

سبحانك اللّٰهُمَّ ربنا وبحمدك، أشهد أن لا إله إلا أنت، أستغفرك وأتوب إليك.

وكتب الدكتور أبو (محمد علي)، أكرم بن محمد علي زيادة الفالوجي الأثري

باحث ومدرس متفرغ في جمعية مركز الإمام الألباني للبحوث والدراسات

عمان – المملكة الأردنية الهاشمية

الأحد، 12 رمضان، 1439هـ، 27 أيار، 2018م

Utangulizi

Sheikh Akram Ziyâdeh

Kwa Jina la Allâh, Mwingi wa Rehma,
Mwenye Kurehemu

Kila Sifa Njema Inamstahiki Allâh ambaye aliyeifanya ‘ilmu kuwa ni rehma miongoni mwa wenyeji wake, na swala na salamu zimfikie Mtume Wake na mja Wake; Mtume wetu Muhammad, na ziwafikie jamaa zake na Maswahaba zake na askari wake na ujumbe wake.

Ama baada ya hayo:

Kwa hakika amenifurahisha ndugu yangu muheshimiwa Abu Farida – Muhammad Basawad (mwenyeji wa Mombasa, Mkenya) alikuwa ni mdhamini wetu, rafiki yetu, mwenyeji wetu katika safari yetu ya ki-‘Ilmu na ulinganizi kwa ndugu zetu (wa Kenya) na (Tanzania), mnamo mwezi wa Rajab, 1434 Hijriya – kwa kuniadhimisha niandike kwa mukhtasari kwenye tafsiri ya kitabu cha Sheikh wetu Muhammad Nasiruddin Al-Albani; *“At-Tawassul – sampuli na hukmu zake”*. Kilichofanyiwa uhakiki na kuchapishwa na al-Ustâdh Muhammad Eid Al-Abbâsi. Ndugu Abû Farida akakifasiri kitabu hicho kwa lugha ya Kiswahili, inayozungumzwa pamoja na lugha nyenginezo na mamiya ya mamilioni ya Waislamu katika sehemu za Afrika ya Mashariki.

Ndugu yetu Abû Farida ndiye Muanzilishi na Rais wa “Al-Quran and Sunnah Society of East Africa” na ni msimamizi katika ulinganizi wa Dini kwenye Jumuiya hiyohiyo iliyoko Canada. Mimi nimejuana na yeye katika sehemu mbili (mahala pawili), Afrika ya Mashariki na pia Canada katika vitendo vya utekelezaji wake wa ibada kwa wakati wake, usomi wake, uandishi wake, utafiti wake, shughuli zake za

ufasiri, kurekodi video, shughuli za uchapishaji, au shughuli nyenginezo zenye kuutumikia ulinganizi wa Uislamu kwa ujumla, na ulinganizi wa Da'watus Salafiyyah khususan.

Kwa hakika amenipa heshima kubwa ndugu niliyemtaja hapo awali kwa kuniomba nimuandike utangulizi wa kitabu kilichotajwa hapo juu, yeye vilevile amewahi kufasiri kwa lugha ya Kiswahili baadhi ya vitabu vyengine vilivyoandikwa na wanavyuoni walioko katika zama zetu hizi na wengineo. Kwa vile mimi sizungumzi lugha hii ya kiswahili ambayo ndiyo aliyoifasiriya kitabu hicho kilichotajwa, basi nasema hivi:

Kitabu kilichotajwa, kilichoandikwa katika lugha asili ya kiarabu, ni kitabu kikubwa cha ta'aluma cha aina yake kutokana na yafuatayo:

1. Mfumo wake umedhihirika kuegemezwa juu ya Qur'ân, Sunnah zilizoswihi na athari za Maswahaba pamoja na wafuasi wao, na wanavyuoni kupitia kwenye zama na vizazi vilivyopita.

2. Kimeandikwa na mwanachuoni aliyebobea katika ta'luma ya akili na mila za ki-Islamu na aliye mjuzi kwenye ilmu ya uswahihishaji na sheriya ya ki-Islamu. Naye ni mwanachuoni wetu anayekubaliwa kwa uongozi, 'ilmu na uongofu na wanavyuoni maarufu walio katika zama zetu.

3. Kimepitiwa na mmojawapo wa wanafunzi wa muheshimiwa Sheikh wetu, rafiki mkongwe, aliye mashuhuri mno kwa shughuli za utafiti, upekuzi wa uhakikishaji, uswahihishaji, uchunguzi na muundo wa lahaja za kiarabu; na ambaye aliyefaidika zaidi kutoka kwake wakiwa Damascus kitambo sana. Naye si mwengine asiyekuwa Profesa Muhammad Eid Al-Abbâs, Allâh amlinde.

4. Mtunzi alikichapisha kwenye zaidi ya shirika moja la uchapishaji, na waislamu wengi wakafaidika nacho kwenye nchi nyingi kutokana na kufasiriwa kwake kwenye lugha nyingi tafauti.

5. Kimewasaidia waislamu wengi sana waliokisoma kutokana na kusambaa kwa maombi ya haramu yasiyofaa na kuyaingiza kwenye uswahihi wa itikadi ya sawa na uongofu wa Sunnah iliyosimama wima.

6. Wanavyuoni wengi wamewahimiza watu wafaidike kutokamana na kitabu hiki kwa kukisherehesha na kukifundisha kwenye nchi mbalimbali.

7. Ni miongoni mwa sehemu ya mchango wetu katika kuchapisha vitabu vya muheshimiwa Sheikh wetu kwa waislamu tafauti katika nchi mbalimbali kwa lugha zao.

8. Ni katika sehemu ya usaidizi wetu kwa ndugu yetu Abu Farida na kumuhimiza azidi kuendelea kuisambaza ‘ilmu ya ki-Islamu kwa lugha yake ya Kiswahili , kama alivyosema Allâh kumwambia Mtume Mûsa (عليه السلام):

سَنَشُدُّ عَضُدَكَ بِأَخِيكَ ٣٥

“Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako.”
[Al-Qaswas 28:35]

Na kama ilivyopokewa na Jâbir Bin ‘Abdillâh (رضي الله عنه) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

«مَنْ اسْتَطَاعَ مِنْكُمْ أَنْ يَنْفَعَ أَخَاهُ فَلْيَفْعَلْ»

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

"*Mwenye uwezo miongoni mwenu wa kumfaidisha ndugu yake na afanye hivyo.*"[1]

Kutokana na sababu hizi na nyenginezo ambazo azijuazo Allâh (سبحانه وتعالى), mimi nimeandika maneno haya kama utangulizi wa kitabu; "*At-Tawassul – sampuli na hukmu zake*" kilichoandikwa na muheshimiwa Sheikh wetu Al-Albâni (رحمه الله).

Twamuomba Allâh awanufaishe muandishi wake, muhakiki wake, mtangazaji wake, mfasiri wake, mtangulizi wake, msomaji wake, mchapishaji wake, yoyote mwenye kuchangia kitu chake kidogo chochote, na waislamu wote kwa ujumla.

Na hatima ya maombi yetu ni kila Sifa njema ni zenye kumstahiki Allâh, Mola wa viumbe vyote. Kutakasika ni Kwako, Ewe Allâh! Mola wetu; na tunakusifu Wewe. Nashuhudia yakwamba hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe. Nakuomba msamaha Wako na natubia Kwako.

Imeandikwa na:

Abu Muhammad Ali Akram ibn Muhammad Ali Ziyâdeh Al-Falûji Al-Athari,

Mtafiti na Profesa katika "Chuo Kikuu cha Al-Albâni cha Ta'luma na Utafiti, Amman, Jordan

Jumapili, Ramadhân; tarehe 12, 1439 H / May 27, 2018

[1] Swahih Muslim.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Utangulizi

Sheikh Muhammad ‘Eid al-‘Abbâsî

Kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh, Mola wa Ulimwengu mzima. Twamuomba amfikilizie swala na salamu kiongozi wa Manabii na Mitume, na juu ya jamii yake na Maswahaba zake, na kila atakaefuata uongofu wake hadi siku ya Malipo.

Amma ba’d:

Msingi wa kitabu hichi ninachokiwasilisha kwa wasomi watukufu ni khutba mbili, ambazo mwalimu wetu Muhammad Nâsirud Din al-Albânî, alizozitoa kwa kundi la vijana wa ki-Islamu katika msimu wa kiangazi wa mwaka wa 1392 H (sawiya na 1972 CE) kutoka nyumbani kwake, kwenye mahema ya Yarmûk mjini Damascus. Kwenye khutba hizo, aliangazia mas’ala yanayohusiana na *at-Tawassul* na kila lenye kuhusiana nalo, na akalifanyia utafiti kutokana na mas’ala hayo mazima, kwa aliyokuwa na ujuzi nayo kutokana na ‘ilmu maridhawa, na maono yaliyo swahîh, na uhakiki wa kina, mambo yaliyomfanya kuwa maarufu sana; kwa hakika ni nadra sana kumpata mtu mwengine mfano wake katika zama hizi. Limewashangaza wengi miongoni mwa waliohudhuria, kwa utafiti huu wa ki-uwanachuoni na dalili zake zilizokuwa wazi na zenye nguvu, na wakavutiwa na uhatimisho wake na uwasilishaji wa rai iliyofikiwa, mambo ambayo

wakati huo huo ndiwo uliokuwa msimamo wa *ma-Imâm Mujtahidina* waliotangulia (رحمه الله).

Tumeona yakwamba imekusanya faida nyingi na palikuwa na haja kubwa ya uchapishwaji wake ili ipate kufanyiwa uwezekano wa kupatikana na Waislamu, kuwasaidia wawe huru kutokana na kuviringwa na kuchanganyikiwa kukubwa kuhusu mas'ala haya. Zaidi ya hayo, shukrani juu ya fadhla zote zinamstahiki Allâh Aliyeturahisishia haya, kwani idadi kubwa ya ndugu, walizisajili darsa hizo na mmojawapo aliyekuwa na bidii katika kutafuta 'ilmu, akazinukuu kwa maandishi ya mkono yaliyokuwa mazuri na yenye kufahamika wazi, basi twamuomba Allâh (سبحانه وتعالى) amlipe kheri nyingi kutokana na juhudi hiyo. Kisha nikayapiga msasa maandishi hayo ili yapate kufaa kuchapishwa na nikaongezea nukta za faida kila palipostahiki. Vile vile nikawezesha kupatikane marejeo ya asili za Âyât na baadhi ya ahâdîth zinazopatikana ndani yake. Kisha baada ya hayo, mwalimu wetu al-Albânî akaupata tena waraka wa risala aliyoandika takriban miaka ishirini iliyopita iliyokuwa na anwani: "*Tawassul na Ahâdîth zinazohusiana nazo*". Haya yalikuwa ni miongoni mwa mfululizo kwa jina la: *"Kuifikia hukmu ya sawa kuwahusu wale wenye kudai kuwasaidia ma-Khalifa waongofu na Maswahaba*". Katika mfululizo huu, aliwajibu idadi kubwa ya *mubtadi'in* (wazushi) na *khurâfiyyîn* (wapotofu) waliokuwa wakifanya njama za kuihujumu *Da'wah Salafiyyah* kwa kuandika *rasâ'il* zilizokuwa na hatia ya udanganyifu na mashambulizi ya ki-upofu kama huo, ambazo kwa hali yoyote zisizolingana na 'ilmu na *ikhlâs* ambayo ndiyo muhimu kwake. Kwahivyo, mwalimu wetu akanionyesha *rasâ'il* hiyo, na mimi nikaichunguza, na nikakuta yakwamba imekusanya nukta za thamani ndani yake na faida ya ziyada zisizopatikana kwenye darsa zake mbili. Kwahivyo mimi nikaziongezea kila mahali mulipowezekana kufanya hivyo, na kuwacha yasiyokuwa yakihitajika. Kisha nikakiwasilisha kitabu kizima, katika mpangilio wake mpya kwa muandishi (رحمه الله), naye akaiandaa na kuiboresha ili aiongezee ubainifu wake na manufaa yake. Kwahivyo kitabu hiki, licha ya ufupi wake, kina maana pana, kwa fadhla na taufiki za Allâh, na mimi hapa ndio nakiwasilisha kwa wasomaji watukufu nikitumai yakwamba watapata mazuri mengi ndani yake na faida kwa wingi. Zaidi, mimi namuomba Mola Mtukufu na Mlinzi yakwamba amuandikie thawabu nyingi mtunzi wake, na mchapishaji wake, na kila sifa njema na

shukrani ni za Allâh, ambaye kwa baraka Zake, mambo mema hukamilika. Na yeye ni Mwenye kututosheleza na Mwenye kutuwakilishia mambo yetu.

Damascus, 27th Rabî'ul-Awwal 1395H.
Sawiya na 19th April 1975.

Muhammad 'Eid al-'Abbâsî.

TAWASSUL

SAMPULI ZAKE NA HUKMU ZENYE KUHUSIANA NAYO

Kila sifa na shukrani ni zenye kumstahiki Allâh, tunamsifu Yeye, na kumtaka msaada, na kumuomba msamaha Wake. Twamuomba Allâh atuhifadhi kutokamana na maovu ya nafsi zetu na kutokamana na matendo yetu maovu. Yoyote ambaye aliyeongozwa na Allâh, hapana awezae kumpotoa, na yoyote aliyepotolewa na Allâh, hapana wa kumuongoza. Nashuhudia yakwamba hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allâh, peke yake, pasi na mshirika, na nashuhudia yakwamba Muhammad ni Mja Wake na Mtume Wake.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ ١٠٢

“Enyi mlioamini! Mcheni Allâh kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili.”[2]

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفۡسٖ وَٰحِدَةٖ وَخَلَقَ مِنۡهَا زَوۡجَهَا وَبَثَّ مِنۡهُمَا رِجَالٗا كَثِيرٗا وَنِسَآءٗۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ ٱلَّذِي تَسَآءَلُونَ بِهِۦ وَٱلۡأَرۡحَامَۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَلَيۡكُمۡ رَقِيبٗا ١

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi (asili) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ileile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao. Na mcheni Allâh ambae kwaye

[2] Âli-‘Imrân 3:102

mnaombana. Na (mwatazame) jamaa. Hakika Allâh ni mlinzi juu yenu (anayaona kila mnayoyafanya).”[3]

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَقُولُواْ قَوۡلٗا سَدِيدٗا ٧٠ يُصۡلِحۡ لَكُمۡ أَعۡمَٰلَكُمۡ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡۗ وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ فَازَ فَوۡزًا عَظِيمًا ٧١

“Enyi mlioamini! Muogopeni Allâh na mseme maneno ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na atakusameheni madhambi yenu; Anayemtwii Allâh na Mtume wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.[4]

Kwa hakika maneno yalio bora zaidi ni kitabu cha Allâh, na uongofu bora ni uongofu wa Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Na mambo mabaya ni yenye kuzuliwa na kila lenye kuzuliwa ni bid’ah, na kila bid’ah ni upotofu, na kila upotofu (mwisho wake) ni motoni.

Watu wametatizika pakubwa kuhusiana na mas’ala ya *tawassul* na hukmu zake katika dini, na wakakhitilafiyana sana kuhusiana nayo, baadhi yao wakiitangaza kuwa inafaa na wengine wakiikataza, baadhi yao wakafikia kiwango cha kuvuka mipaka na wengine wakalegeza msimamo kupita kiyasi. Vilevile, idadi kubwa ya waisilamu kwa karne nyingi zilizopita wamekuwa na mazoea ya kusema katika maombi yao maneno kama; “Ewe mola kwa haki za Mtume wako...” au “kwa jaha yake”au kwa mkuruba wake kwako Wewe nipe afya na swiha, unisamehe madhambi yangu na, ”Ewe Mola hakika yangu mimi nakuomba kwa haki ya nyumba tukufu ... unisamehe.” Na ewe Mola nakuomba kwa Jaha (haki) ya *Mawalii* na Watu Wema, kwa mfano fulani na fulani,” na kadhalika au “Ewe Mola kwa karama za watu wa Mungu mbele Yako, na kwa jaha itokayo kwetu ya kuhudhuria, na ambao kwa msaada wao ndipo tukawepo sisi, tuepushie sisi dhiki zote, pamoja na walio na dhiki”.

[3] an-Nisâ’ 4:1
[4] Al-Ahzâb 33:70-71

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Vilevile “Ewe mola twakuomba kwa unyenyekevu kwa mikono yetu tuliyo ikunduwa tukitafuta njia ya wasila kwako kwa kupitia kwa anaye stahiki wasila na *shafa’ah* uunusuru Uislamu na Waislamu...” Wanaiita hii ‘*wasilah’* na wanadai yakwamba inaruhusiwa. Na ni jambo lililokokotezwa katika Sharia na kwamba imethubutu na kufaradhishwa katika baadhi ya âyât na ahâdith, ambazokwamba zenye kuamrisha na kuhimiza. Hata baadhi ya watu huenda mbali na kuvuka mipaka yakwamba wanaruhusu kufanya *tawassul* kwa Allâh (سبحانه وتعالى) kwa kupitia kwenye viumbe ambavyo hata havifiki kiwango kilichotajwa, kama vile makaburi ya *awliyâ*, na majengo ya vyuma yaliyojengewa makaburi yao, na mchanga, na mawe, na miti iliyo karibu nayo. Wanadai yakwamba kila kilicho karibu ya wale walio tukuzwa chenyewe kinakuwa ni kitukufu, na kwamba utukufu ambao Allâh aliompa huyo aliye kaburini hupita kwenye kaburi lenyewe, ili lipate kuwa ni njia ya wasila wa kujikurubisha kwa Allâh hapo. Kwa hakika baadhi ya watu waliokuja baadae wanaruhusu kutafuta msaada moja kwa moja kutoka kwa asiyekuwa Allâh!

Kwahivyo ni nini tawassul? Ni zipi sampuli zake? Ninini maana ya Âyât na ahâdith zenye kutaja tawassul? Na ni ipi hukmu yake ya sawa katika uislamu?

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

MLANGO WA KWANZA

TAWASSUL KATIKA LUGHA YA KIARABU NA KATIKA QUR'ÂN

MAANA YA TAWASSUL KATIKA LUGHA YA KIARABU

Kabla ya kuingia katika mada hii kwa kina, ningelipenda kuwatanabahisha fahamu zenu kwenye sababu muhimu kwa nini watu wengi wakawa na ufahamu wa kimakosa kuhusu maana ya Tawassul, na ni kwanini wakavuka mipaka kuhusiana nayo na wakaingia kwenye mambo yasiohusiana nayo. Sababu ni ukosefu wa kufahamu kwao maana yake kwenye lugha na ukosefu wa ilmu yao katika maana ya mzizi wake wa asili. Hii ni kwamba neno tawassul ni neno asili la kiarabu linalopatikana katika Qur'ân na Sunnah na katika mashairi ya kale ya kiarabu na nathari, na maana yake ni :*kujikurubisha katika kitu unachokitafuta na kukikurubia kitu ukipendacho.* Ibnul-athîr amesema katika an-Nihâyah : "*Al-Wâsil* ni mtu mwenye kupenda au kung'ang'aniya kitu, na *Al-Wasîlah* ni mkuruba na chenye kukurubisha, na kitu ambacho mtu awezacho kujikurubisha nacho katika kulifikia alitakalo. Wingi wake ni *Wasâ'il*." Amesema Mwanachuoni Al-Fayrûz Abâdî katika *al-Qâmûs*: "'Alitekeleza Wasîlah kwa Allâh (سبحانه وتعالى)', maana yake ni kwamba alifanya kitendo kwa ajili ya kujikurubisha zaidi kwa Allâh, kama njia ya kumkurubia Yeye." Na akasema Ibn Fâris katika *Mu'jamul Maqâyîs:* "*Wasîla* ni kupenda (kuwa na *raghba*), na kukitaka kitu. Husemwa, *wassala* kwa mwenye kutaka na kutamani kitu, na *Wâsil* ni mwenye *raghba* (kutamani kujikurubisha) kwa Allâh (سبحانه وتعالى) na imetokea kwenye maneno ya Labîd pindi aliposema:

أَرَى النَّاسَ لاَ يَدْرُوْنَ مَا قَدْرُ أَمْرِهِمْ بَلَى، كُلُّ ذِى دِيْنٍ إِلَى اللهِ وَاسِلُ

Nimewaona watu hawajui thamani ya hali zao...

Lakini kila mwenye msimamo wa Dini hujikurubisha kwa Allâh.”

Na akasema *ar-Râghib al-Asfahânî* katika *al-Mufradât*: *“Al-Wasîlah* (inayoandikwa kwa herufi ya س) ni kukikurubia kitu akipendacho mtu, kwa *raghba*, nayo ni makhsusi zaidi kuliko *Al-Wasîlah* (inayoandikwa kwa herufi ya ص), kwani imehusisha dhamana ya kukitaka kitu.

Amesema Allâh:

وَٱبۡتَغُوٓاْ إِلَيۡهِ ٱلۡوَسِيلَةَ ٣٥

“Na tafuteni njia ya kumfikilia (kufikilia pepo yake).”
[al-Mâidah 5:35]

Uhakika wa kutafuta *wasîlah* kwa Allâh (سبحانه وتعالى), ni: kuwa na hadhari kubwa katika kufuata njia yake kwa vitendo (vizuri) na ‘ibada, kwa kujifungamanisha na tabia njema zinazohitajika katika *Sheriya*. Ni kama mkuruba, na *Wâsil* ni mwenye kutamani kujikurubisha kwa Allâh (سبحانه وتعالى).

Mwanachuoni maarufu *ibnu-Jarîr,* amenukuu maana hii vilevile na kisha akaleta kama dalili maneno ya mashairi:

إِذَا غَفَلَ الوَاشُوْنَ عُدْنَا لِوَصْلِنَا

Watakapoghafilika wenye habari za fitina, basi sisi ndipo tunaporudi kwenye kuungana;

وَعَادَ التَّصَافِي بَيْنَنَا وَالْوَسَايِلُ

na uhusiano na njia za mkuruba (wasîlah) baina yetu zitarudi tena.

Kisha kuna maana nyengine ya *wasîlah,* nayo ni cheo na kusimama pamoja na Mfalme na kuwa na mkuruba nae. Kama ilivyo katika hadith, ni jina la daraja ya juu kabisa iliyoko Peponi, katika maneno yake (صلى الله عليه وسلم) aliposema:

« إِذَا سَمِعْتُمُ الْمُؤَذِّنَ فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ ثُمَّ صَلُّوا عَلَيَّ فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى عَلَيَّ صَلَاةً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا ثُمَّ سَلُوا اللَّهَ لِيَ الْوَسِيلَةَ فَإِنَّهَا مَنْزِلَةٌ فِي الْجَنَّةِ لَا تَنْبَغِي إِلَّا لِعَبْدٍ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ فَمَنْ سَأَلَ لِيَ الْوَسِيلَةَ حَلَّتْ لَهُ الشَّفَاعَةُ » رَوَاهُ مُسلم

"Pindi mutakaposikia mwito wa kuswali basi semeni kama anavyosema, kisha niswalieni mimi. Kwa hakika, mwenye kuniswaliya mimi mara moja, Allâh Atamswaliya yeye mara kumi. Kisha mumuombe Allâh anipe mimi al-Wasîlah, kwani hakika hapo ni sehemu katika Pepo iliyoandaliwa kwa mja mmoja tu miongoni mwa waja wa Allâh, na natumai mimi ndiye nitakayekuwa mja huyo. Kwahivyo, yoyote atakayeniombea mimi al-Wasîlah basi shafa'ah yangu itamuwajibikia".[5]

Kama ilivyo wazi, yakwamba maana hizi mbili za mwisho za *al-Wasîlah* zimeungana karibu na maana yake ya asili, lakini hatahivyo (maana hizo mbili) sizo tulizozikusudia katika utafiti wetu huu.

MAANA YA WASÎLAH KATIKA QUR'AN

Mpaka sasa tuliyoyabainisha ni maana iliyo maarufu katika lugha, na hakuna mtu yoyote anayepinga hilo. Hiyo pia ndiyo maana iliyotolewa na watu wetu wema waliotutangulia (*as-Salafus-Swâlih*) na ma-Imâmu wa tafsiri katika kuzifafanua Âyât hizo mbili ambazo ndani mwake maana ya *al-Wasîlah* inapopatikana. Nazo ni maneno yake Allâh (سبحانه وتعالى):

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱبۡتَغُوٓاْ إِلَيۡهِ ٱلۡوَسِيلَةَ وَجَٰهِدُواْ فِي سَبِيلِهِۦ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ٣٥

[5] Imepokewa na Muslim na *Ashâb as-Sunan* na wengine na imeletwa kwenye Kitabu changu Irwâ ul-Ghalîl No. 242, chapa ya *al-kutub al-Islâmiy*.

“Enyi mulioamini! Mcheni Allâh na tufuateni njia ya kumfikilia (kumfikilia pepo yake). Na pijaneni kwa ajili ya dini yake ili mpate kufaulu.”[6]

Na maneno Yake (سبحانه وتعالى):

أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ ٱلْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُۥ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُۥٓ ۚ إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ٥٧

"**Hao wanao waomba, (wenyewe) wanatafuta ukaribiano na mola wao; (hata) walio karibu sana miongoni mwao (na mungu, kama malaika, wao wanafanya yaya haya) wanatumia rehema zake na wanaogopa adhabu yake. Hakika adhabu ya mola wako ni ya kuogopwa.**[7]"

Ama kuhusu Aya ya kwanza, basi Imâm wa wanavyuoni wa Tafsiri *al-Hâfidh Ibn Jarîr (at-Twabari)*, رحمه الله, amesema katika kuifafanua:

“Enyi wenye kumswadikisha Allâh na mtume Wake katika waliyokupasheni habari zake, na kuthibitisha thawabu zozote Alizokuahidini, na adhabu zozote alizowaonya nazo**: “Mcheni Allâh.”**. Akasema: Muitikieni Allâh kwa kumtwi’i kuhusiana na chochote alichowaamrisha au kuwakataza na **“Na tafuteni njia ya kumfikilia.”** Akasema: Na mutafute njia za kujikurubisha Kwake kwa kufanya vitendo vyenye kumridhisha Yeye.”

Al –Hâfidh Ibn Kathîr amenakili kutoka kwa Ibn ‘Abbâs (رضي الله عنهما) yakwamba maana ya *Wasîlah* ni kujikurubisha zaidi. Vilevile akanakili mfano wa hayo kutoka kwa Mujâhid na Abî Wâ’il, al-Hasan, ‘Abdullâh Ibn Kathîr, as-Sudayyi, Ibn Zayd na wengineo. Vilevile amepokea kutoka kwa Qatâdah yakwamba naye alisema kuhusiana nayo: “Nayo ni: yakwamba ujikurubishe Kwake zaidi kwa kumtwi’i Yeye na kwa kupitia kitendo chenye kumridhisha.” Kisha akasema Ibn Kathîr, “Na kuhusu waliyoyasema wale ma-Imâm, hapana ikhtilafu yoyote miongoni mwa Wanavyuoni wa tafsiri kuihusu hiyo ... na *al-Wasîlah* ni

[6] Sûrah al-Mâidah 5:35
[7] Sûrah al-Isrâ’ 17:57

lile jambo lenye kukuwasilisha katika njia ambayo hulifikia jambo ulipendalo.[8]

Ama kuhusu Âya ya pili amebainisha swahaba Mtukufu, 'Abdullâh Ibn Mas'ûd (رضي الله عنه) kwa mnasaba wa kuteremshwa kwake, na akasema: "Iliteremshwa kuwahusu kundi la Waarabu waliokuwa na mazoweya ya kuwaabudu baadhi ya Majini, kisha wale Majini wakasilimu pasi na wenye kuwaabudu wao kujua."[9]

Amesema al-Hâfidh Ibn Hajar (رحمه الله): "Yaani wale watu waliokuwa wakiwaabudu Majini wakiendelea na Ibada hiyo, na Majini wenyewe hawakuridhika na mambo hayo kwa vile wao walikuwa wameukubali Uislamu, na wao ndiwo waliokuwa wakitafuta njia za kujikurubisha kwa Mola wao, haya ndiyo yakuaminika kuhusiana na tafsiri ya Âya hiyo."

Mimi nasema: "Na hayo ni ya wazi kabisa yakwamba muradi wa wasîlah ni yale mambo yenye kujikurubisha kwa Allâh (سبحانه وتعالى), kwa ajili hiyo, akasema: **"wanatafuta"** *yaani;* wanatafuta kufanya amali njema kama hizo ambazo zitakazowakurubisha kwa Allâh (سبحانه وتعالى). Vilevile inabainisha waziwazi hali ya kushangaza iliyo kinyume cha kila fikra zilizosalimika – ambazo baadhi ya watu huelekeza ibada zao na maombi yao kwa baadhi ya waja wa Allâh, kwa kuwaogopa na kuwatumainia wao, licha ya uhakika yakwamba waja hao wanaowaabudu, wenyewe wameutangaza na kuukiri waziwazi Uislamu wao na utumwa wao katika kumuabdu Allâh. Na wakaharakisha kufanya matendo mema ili wajikurubishe zaidi Kwake (سبحانه), kwa kufanya amali njema azipendazo na anazoziridhia. Wakitumaini kupata Rehma zake na kuhofia adhabu Yake. Kwahivyo Allâh (سبحانه وتعالى), ametangaza upumbavu wa matumaini matupu ya hao watu wajinga wenye kuwaabudu Majini na kuendelea kuwaabudu licha ya uhakika yakwamba wao wenyewe ni viumbe na waja wa

[8] Tafsîr Ibn Kathîr (2/52-53)

[9] Imepokewa na Muslim (8/245 – *Imâm an-Nawawi*), yamepokewa mfano wake na al-Bukhâri (8/320-321 – *Fat-hul Bâri*) na katika riwaya yake: "Kwahivyo *Ma-Jinni* walisilimu, na wale watu wakababakia katika Dini yao.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Allâh, tena walio wanyonge na madhaifu mbele Yake, kama jinsi walivyo wanaadamu wenyewe. Hawajimiliki nafsi zao kwa manufaa yoyote wala madhara, na Allâh amewalaumu watu hao kwa kutoelekeza Ibada zao kwake Yeye peke Yake (تبارك وتعالى), kwani Yeye peke yake ndiye mwenye kumiliki madhara na manufaa, na kwenye Mkono wake peke Yake ndiko kwenye Qadar ya kila kitu, na Yeye ndiye *al-Muhayminun* juu ya kila kitu.

'AMALI NJEMA PEKE YAKE NDIZO WASÎLAH ZENYE KUMKURUBISHA MTU KWA ALLÂH

Vilevile ni jambo la kushangaza kuona yakwamba baadhi ya wanaodai kuwa na 'ilmu wamekuwa na uzoefu mkubwa wa kuzitumia âyât hizi mbili kama dalili zilizowahamasisha na kujifungamanisha nazo wengi wao kuhusiana na kutafuta *tawassul* kwa kupitia kwa dhati za Mitume, au utukufu wao, au jaha zao. Hizi ni dalili za makosa, haiswihi kujitetea na kuzishikilia âyât hizo mbili, kwani haikuthubutu kulingana na *Sheriya* yakwamba *tawassul* hii imeruhusiwa na *Sheriya* na imependekezwa. Na kwa jambo hilo, haikuwahi kutajwa dalili hii na hata mmoja miongoni mwa *as-Salafus Swâlih,* wala kuipendekeza *tawassul* iliyotajwa. Lakini walivyoifahamu wao, ni kwamba Allâh (تبارك وتعالى), Alituamrisha sisi kujikurubisha Kwake kwa kila njia za mkuruba, na kumtangulizia kila sampuli ya mkuruba, na kutekeleza *tawassul* kwenye kila njia anayoiridhia.

Lakini hata hivyo, Allâh (سبحانه وتعالى) amekwisha kutufundisha katika maandiko mengine mengi ya *ki-Sharia* (*nusûs*), yakwamba ikiwa tunataka kutafuta njia za kujikurubisha Kwake, basi ni lazima tufanye hivyo kwa kutekeleza amali njema anazoziridhia. Hakutuachia sisi vitendo hivyo tufanye tutakavyo, wala hakuziachia vitendo hivyo akili zetu na ladha zetu na hisiya zetu kuamua ni vitendo gani vinavyotakiwa, kwani katika hali hiyo tutakuwa ni wenye kukhitilafiana na kuzozana, tugombane na kupigana vita. Bali, Yeye (سبحانه وتعالى) alituamrisha turegee Kwake kwenye mas'ala hayo na tufuate uongofu wake na mafundisho yake kuhusiana na hayo. Hii ni kwa sababu hakuna ajuae ni mambo gani yenye kumridhisha Allâh (سبحانه وتعالى) isipokuwa Yeye Peke yake. Kwahivyo, ili sisi tuzijuwe njia za kujikurubisha kwa Allâh, ni wajibu wetu turejee nyuma, katika kila

mas'ala, kwenye yale ambayo Allâh (سبحانه وتعالى) aliyoyafaridhisha katika Sheriya, na ambayo yaliyofundishwa na Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم). Maana ya haya ni kwamba tunarejea kwenye Kitabu cha Allâh na Sunnah za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم). Kwa hakika, haya ndiyo ambayo Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) aliyotuamrisha sisi tufanye katika maneno yake:

« تَرَكْتُ فِيكُمْ أَمْرَيْنِ لَنْ تَضِلُّوا مَا تَمَسَّكْتُمْ بِهِمَا: كِتَابَ اللَّهِ وَسُنَّةَ رَسُولِهِ »

"Nimewaachia mambo mawili, hamutopotea iwapo mutashikamana nayo: Kitâb cha Allâh na Sunnah za Mtume Wake."[10]

NI WAKATI GANI 'AMALI YA MTU INAPOKUWA NI NJEMA

Imebainishwa katika Kitâb na Sunnah yakwamba kwa amali kuwa ni amali njema na iwe ni yenye kukubalika mbele ya Allâh (سبحانه), na iwe ni yenye kumkurubisha mtu karibu na Yeye, basi haina budi kutekeleza masharuti mawili:

LA KWANZA ni kwamba ni lazima mwenye kuifanya (amali hiyo) awe amekusudia kwa ajili yake, Uso wa Allâh (عزّ وجلّ).

LA PILI ni lazima iafikiane na vile inavyo-ongoza Sheriya ya Allâh (تبارك وتعالى) katika Kitâb chake au alivyobainisha Mtume Wake katika Sunnah zake.

Na iwapo mojawapo ya sharuti hizi mbili imekosekana, basi amali hiyo haitokuwa njema wala haitokubalika. Hii imeashiriwa na maneno yake Allâh (تبارك وتعالى):

[10] Imepokewa na Mâlik kwa njia ya *mursal* na al-Hâkim kutoka katika hadith ya Ibn 'Abbâs kwa upokezi wa silsila iliyo hasan. Vilevile inaye shahidi katika hadith ya Jâbir niliyoinukuu katika *silsilatus-Swahîhah (no. 1761)*

فَمَن كَانَ يَرْجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَٰلِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدًۢا ١١٠

“Kwahivyo yoyote mwenye matumaini ya kuonana na Mola wake, basi na atende amali njema na wala asimshirikishe na yoyote katika waja wake.”[11]

Kwahivyo Yeye (سبحانه) ameamrisha yakwamba amali ni lazima ziwe ‘njema’, yaani ziwe kulingana na Sunnah. Kisha akaamrisha yakwamba zifanywe kwa kutakasiwa Yeye na wala isiwe ni kwa ajili ya motisha yoyote. Amesema al-Hâfidh Ibn Kathîr katika Tafsiri yake: “Mambo haya mawili ndizo nguzo mbili za amali yenye kukubaliwa, ni lazima itekelezwe kwa ajili ya kumtakasia Allâh, na itekelezwe kisawasawa kulingana na jinsi ilivyofundishwa katika Sheriya za Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم).” Na amepokea mfano wa haya, Qâdhi ‘Iyâdh (رحمه الله) na wengineo.

[11] Al-Kahf 18:110

MLANGO WA PILI

NJIA ZA KI-MAUMBILE NA NJIA ZA KI-MALENGO KATIKA SHERIYA[12]

Sasa tunapoelewa yakwamba *al-wasîlah* ni njia ambayo kwayo tunaweza kufikia malengo tunayoyakusudia, kisha inatupasa kujua yakwamba yamegawanyika kwenye sehemu mbili: Njia za ki-Maumbile na Njia zilizoelezwa katika Sheriya. Ama kuhusu njia za ki-Maumbile, hiyo ni kila njia ya ki-asili ambayo kwayo mtu hulifaidi lile alilokuwa akilipenda, alilolijua kwa kupitia katika hulka yake ya asili aliyoumbiwa nayo na Allâh. Hili ni jambo la kawaida kwa wote wawili, Waumini na Makafiri, pasi na tafauti yoyote baina yao. Mifano yake ni kama maji, ambayo ni njia ya kuvunja kiu ya mtu; chakula, ambayo ni njia ya kuondoa njaa; nguo, ambazo ni njia ya kumuhifadhi kutokana na joto na baridi; magari, ambayo ni njia ya kumpeleka kutoka mahali pamoja hadi kwengine, na kadhalika.

Ama kuhusu njia zilizowekwa kwa malengo ya ki-Sheriya, basi hizo ni kila njia ya kuyafikia yale uyapendayo, kwa njia ambayo Allâh (سبحانه وتعالى) aliyoibainisha na kuiamrisha kwenye Kitâb Chake na katika Sunnah za Mtume Wake. Hili linamuhusu Mu'min mwenye kufuata na aliye mtwi'ifu kwa amri za Allâh na Mtume Wake. Mfano wa haya ni;

a. Kuzitamka shahada mbili kwa utakaso wa niya na ufahamu, kwa vile hiyo ndiyo njia ya kupata kuingia Peponi na kuokolewa kutokana na kuishi milele kwenye Moto wa Jahannam.

[12] *Yaani;* Mambo yaliyoamrishwa au kuhimizwa katika Dini, yenye kufaidisha radhi za Allâh na zikampeleka mtu Peponi.

b. Vilevile kulifuatiliza jambo ovu kwa jema ni njia ya kulifutilia mbali jambo ovu.
c. Kuomba Du'â' kwa maombi ya ki-Sheriya baada ya adhana ni njia ya kujipatia shafâ'ah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم).
d. Kudumisha uhusiano kwa kuunga kizazi ni njia ya kujipatia maisha marefu na kuongezewa rizki na kadhalika.

Kwahivyo sisi tunayajua mambo haya na mfano wake kuwa ni njia za kujipatia malengo hayo, ambayo ni maarufu kutokamana na Sheriya peke yake, yasiyojulikana kwa njia ya 'ilmu zetu, ujuzi wala fahamu zetu. Kwahivyo sisi hatuwezi kujua yakwamba kudumisha uhusiano kwa kuunga kizazi ni njia ya kuongezewa maisha marefu na kuzidishiwa riziki isipokuwa kwa maneno ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم):

« مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُبْسَطَ لَهُ فِي رِزْقِهِ، وَأَنْ يُنْسَأَ لَهُ فِي أَثَرِهِ، فَلْيَصِلْ رحمه »

"Mwenye kupenda kukunduliwa riziki yake, na azidishiwe maisha marefu, basi na aunge kizazi.[13]

Na vilevile kwenye mifano mengine.

Watu wengi hufanya makosa makubwa katika kufahamu kwao kuhusiana na hizi sampuli mbili za njia. Baadhi hudhani yakamba kitu ni njia ya kimaumbile ya kupata malengo fulani, haliyakuwa mambo sio hivyo. Wengine huamini kitu kuwa ni Sheriya – njia za ki-Sheriya kufikia malengo fulani katika Sheriya, haliyakuwa uhakika ni kwamba wanayoamini si ya kweli.

Na kutokana na mifano ya njia za bâtwil zisizoleta manufaa yoyote, zote mbili kwa pamoja - za ki-maumbile na za ki-malengo katika Sheriya, ni (kwa mfano), jambo la kawaida analoweza kuliona mtu yoyote anayetembea kwenye barabara ya Nasr, mjini Damascus: Utamuona mtu ameweka meza ndogo na juu yake kuna mnyama mdogo kama panya. Kando yake ameweka mrundu wa kadi zenye maandishi wanayodai kuwa ndizo bahati-nasibu za watu – maandishi

[13] Imepokewa na Mashekhe wawili (al-Bukhâri na Muslim) na wengineo. Nayo imenukuliwa kwenye kitabu changu, *"Swahîh Abî Dâwud"* 1486.

ya kwenye kadi hizo yameandikwa na wao wenyewe au zimeandikwa na mtu mwengine kutokana na ujinga wao. Basi marafiki wawili watakuwa wanapita hapo kando na mmoja atamwambia mwenzake: 'Hebu twende tukajionee bahati zetu.' Hapo watatoa pesa kwa huyo mtu naye amuache yule mnyama mdogo achague kadi na ampe mmoja wao aisome kadi hiyo. Kisha atasoma yenye kudaiwa kuwa ndiyo bahati yake! Sasa unaona kiwango cha akili za watu hawa ambao wanaomchukuwa mnyama awaongoze ili awaonyeshe mambo haya ambayo wasiyoyajua wao, na kuwapasha habari kuhusu hatima yao iliyofichikana kwao! Ikiwa kwa hakika anaamini yakwamba mnyama huyu anayajua mambo yaliyofichikana na mambo ya ghayb basi hapana shaka yakwamba mnyama ni bora kuliko alivyo yeye! Lakini iwapo atakuwa haamini hivyo, basi itakuwa haina maana kufanya hayo yote ya upuzi wa kupoteza wakati na pesa, yasiyofaa kujiingiza mtu mwenye akili. Vilevile kitendo hicho chenyewe ni kisa cha wizi na upotofu na ni njia ya ulaji wa mali za watu bure. Hapana shaka yakwamba watu wenye kumgeukia mnyama huyu ili awajulishe mambo yaliyofichikana na ya ghayb ni, kulingana na madai yao, njia ya ki-maumbile. Lakini hata-hivyo, hayo ni madai ya bure yasiyokuwa na maana yoyote na tajriba na maarifa yanayabomoa madai hayo, kwani imedhaniwa tu waziwazi kuwa hivyo kutokana na ushirikina, ujinga na utapeli. Kisha vilevile kwa mtazamo wa ki-Sheriya ni mambo ya bâtwil yasiyoleta manufaa yoyote, kwani yanakwenda kinyume na Kitâb, Sunnah na muafaka wa wanavyuoni (*ijmâ'*). Yenye kutosheleza katika mas'ala haya ni kwamba yanakhalifu maneno ya Allâh (سبحانه) katika kujisifu Yeye mwenyewe:

عَٰلِمُ ٱلۡغَيۡبِ فَلَا يُظۡهِرُ عَلَىٰ غَيۡبِهِۦٓ أَحَدًا ٢٦ إِلَّا مَنِ ٱرۡتَضَىٰ مِن رَّسُولٖ ...

٢٧

"Yeye ndiye Mjuzi wa siri; wala hamdhihirishii yoyote siri yake. Isipokuwa Mtume wake aliyemridhia ..."[14]

Vilevile kutokana na yale mambo ambayo baadhi ya watu huyadhania kimakosa kuwa ni njia za ki-maumbile ni kwamba awapo mmoja wao anasafiri au anaowa katika siku ya 'Jumatano' basi safari yake haitokuwa na ndoa itaharibika. Vilevile itikadi zao ni kwamba

[14] Al-Jinn 72:26-27

wanapoanza jambo lolote muhimu mara wakamuona mtu-kipofu au kitu kilichodhurika, yakwamba shughuli zao hazitokamilika na zitaharibika!

Vilevile miongoni mwa mambo ambayo Waarabu wengi na Waislamu leo wanayofikiria kuwa njia kama hizo ni fikra ambazo kwa kuwa na idadi kubwa za waume peke yake wanaweza kujipatia ushindi juu ya Mayahudi na maadui wa ki-Bepari, na kwamba katika hali waliyonayo katika muda huu wanaweza kuwasukuma Mayahudi ndani ya Bahari. Lakini hata hivyo, tajriba imeonyesha kupotea na kukosa muelekeo kwenye fikra hizi, na kwamba mas'ala ni yenye kushangaza zaidi kuliko kutibiwa na fikra za kujipurukusha tu.

Vilevile kutokana na mambo ambayo wanayodhania kimakosa kuwa ni njia zilizowajibishwa katika Sheriya ni vile vitendo ambavyo baadhi ya watu hufikiriya kuwa vitawaleta wao karibu ya Allâh (سبحانه), haliyakuwa uhakika ni kwamba vitendo hivi huwapeleka wao mbali na Allâh na kupata hasira na ghadhabu Zake. Bali wanapata La'ana zake na adhabu zake. Miongoni mwa vitendo hivi ni kwamba baadhi yao huwaomba msaada *awliyâ*[15] wao waliokufa na watu wema walio makaburini mwao, wakiwaomba wawatimizie haja zao ambazo zinazoweza kutekelezwa na Allâh (سبحانه وتعالى) Peke yake. Kwa mfano, wakiwaomba wao wawaondolee dhiki na kuwaponya maradhi, kuleta riziki na kuondoa ukame, na kuwapa ushindi dhidi ya maadui zao na kadhaalika. Kwa malengo haya, wao hugaagaa kwenye vyuma vya reli vya makaburini na kwenye matofali ya makaburi, au hutumbukiza masalio ya makaratasi juu yake (makaburi) wakiwa wameandika mahitaji yao na mambo yanayoridhia nyoyo zao. Yote haya yakiwa ni madai yao yapate kuwa ndizo njia zilizowekwa katika Sheriya, lakini hatahivyo, hayo yote yakiwa hayana maana na bâtwil, na ni kinyume cha msingi mkubwa wa Uislamu, ambao ni ibada ya kumuabudu Allâh (تعالى) Peke yake, na kwamba Yeye anapaswa kupwekeshwa (سبحانه) kwa sampuli zote za ki-Ujumla na vitagaa vya ibada.

[15] *Awliyâ* ni wingi wa *walî,* maana yake ni rafiki (wa Allâh) kumkusudia mtu mwema. Walî anaweza tu, kuwa mtu aliyethibiti juu ya Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم).

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Pia miongoni mwayo ni itikadi za baadhi yao, yakwamba ni lazima awe mtu anasema ukweli ikiwa yeye au mtu mwengine aliye haadhir atachemua wakati anapozungumza.[16]

Vilevile na katika itikadi zao yakwamba pindi wanaposikia sauti za kuvuma kwenye sikio lao, wao hudhani yakwamba mmojawapo wa rafiki zao au jamaa zao huwa anasema jambo zuri kuwahusu wao.[17]

Na vilevile itikadi zao yakwamba balaa zitawashukia watakapokata kucha zao wakati wa usiku, au katika siku za Jumamosi au Jumapili ...[18]; au kutatokea mambo kama hayo iwapo watafagia nyumba zao wakati wa usiku, na kutokamana na mambo haya ni iwapo watakuwa na dhana njema na niya nzuri kulihusu jiwe, basi litakuwa ni lenye kuwafaidisha wao.[19]

---

[16] Labda huwenda ikawa asili ya itikadi hii ni hadîth: *"Mwenye kusema jambo lolote na akachemua wakati anapolisema, basi (jambo hilo) ni la kweli."* Ash-Shawkâni ameinukuu kwenye kitabu chake cha riwaya zilizo mawdhû' (*al-fawâ'id ul-Majmû'ah fiy ahâdith al-Mawdhû'ah;* Uk.224). Haya na mfano ufuatao ni dalili zinazotosha kubainisha za hatari za ahâdith dhaifu na mawdhû'ah na athari zake juu ya usambazaji wa itikadi potofu na tabia zisizokuwa na msingi. Kwahivyo haya yanawajibisha yakwamba kila Muislamu anapaswa kujitahadhari nazo na azitahadharishe kwa watu. Haya hayawezi kutekelezeka isipokuwa kwa kuwa muangalifu na kusomea kwa tahadhari ta'luma ya hadîth. Haya ndiyo yaliyonipelekea mimi kuandika kitabu [*Silsilatul-Ahâdîth adh-Dha'îfah wal-Mawdhû'ât wa-atharuhas Sayyi fiyl Ummah*]. [*Mfululizo wa ahâdîth zilizo dha'îf na mawdhû' na athari zake mbovu katika Ummah*]. Utaikuta hadîth hii ndani yake (No.136) pamoja na ufafanuzi wa kutokuwa na misingi kwake.

[17] Asili ya Itikadi hii ni hadîth ya kuzuliwa yenye maneno: *"Sikio la mmoja wenu litakaposikia mvumo, basi na aniswaliye mimi kisha aseme: "Allâh amtaje kwa kheri mwenye kunitaja mimi kwa kheri".* Ash-Shawkâni ameileta kwenye *'al-fawâidul Majmû'ah'* (Uk.224)

[18] Kuna baadhi ya watu wenye chembe-chembe za 'ilmu wameichukuwa itikadi hii potofu kisha wakaiandika kwa mfumo wa mashairi ambayo yanayofundishwa kwa wanafunzi katika baadhi ya shule za Sheriya.

[19] Asili ya itikadi hii ya upotofu ni hadith: *"Lau mmoja wenu atakuwa na dhana njema kulihusu jiwe, basi Allâh atalifanya limnufaishe."* Al-Hâfidh al-'Ajlûnî ameinukuu kwenye *Kashful Khafâ'* (2/152) na akamnukuu Ibn Taymiyyah akisema yakwamba huo ni urongo, na kutoka kwa Ibn Hajar yakwamba haina msingi wowote, na kutoka kwa muandishi wa *al-Maqâsid* yakwamba si swahih. Na akanukuu maneno ya Ibn al-Qayyim kuhusiana nayo: "Hayo yalikuwa ni maneno ya wenye kuabudu masanamu waliokuwa na

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kwahivyo hizi itikadi potofu na mfano wake, bali itikadi hizi za ki-mila na mambo ya *khurâfât*, itikadi za kidhana na udanganyifu ni mambo ambayo kwayo Allâh hakuteremsha dalili juu ya hayo, na umeona yakwamba wamezipata asili zao kwenye ahâdith maudhû' na za kuzuliwa, laana za Allâh ziwashukie wale waliozizua na awaumbue waliozitunga. Kwahivyo twajua yakwamba njia za ki-maumbile zimegawanyika baina ya mambo yaliyo halali na yaliyoruhusiwa na Allâh, na mambo ya haramu yaliyokatazwa na Allâh. Katika yaliyopita nimetowa mifano ya sampuli mbili za njia [za ki-maumbile na za ki-Sheriya] na kuhusiana na ambayo watu huteleza kwenye makosa, wakidhania yakwamba baadhi ya mambo ni halali na yenye kuwapelekea wao katika kufikia malengo waliyoyakusudia, pamoja na kwamba yanatafautiana. Nitataja katika yafuatayo baadhi ya mifano ya njia za ki-maumbile zinazoruhusiwa katika Sheriya na nyengine zisizoruhusiwa.

Kwahivyo kutokana na njia za ki-maumbile ambazo zinazoruhusiwa katika Sheriya kwa kujipatia ajira na kujipatia riziki ni uuzaji na ununuzi; biashara; ukulima na ukodishaji. Kisha, kutokana na njia za ki-maumbile lakini zilizokatazwa ni: kutoa mikopo ipate kulipwa na ziyada ya riba; riba za kujificha; ukiritimba (monopolise); udanganyifu; wizi; kamari na uuzaji wa mvinyo na masanamu. Kutokamana na dalili zake ni maneno ya Allâh (تعالى):

وَأَحَلَّ ٱللَّهُ ٱلۡبَيۡعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْۚ ٢٧٥

"Na akahalalisha biashara na akaharamisha riba."[20]

Kwahivyo zote mbili, biashara na riba, zinatokamana na njia za ki-maumbile katika kujipatia utajiri. Lakini hata hivyo, Allâh (تعالى) alihalalisha ya kwanza na kuharamisha ya pili.

---

dhana njema juu ya mawe." Na pitia kwenye kitabu changu nilichokitaja hapo awali (no. 450)

[20] Al-Baqarah (2:275)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

TUTAJUAJE USAWA WA *WASÂIL (*NJIA), NA UWAJIBIKAJI WAKE KATIKA SHERIYA?

Mfumo wa sawa wa kutambua iwapo njia za ki-maumbile (*al-wasâilul-kawniyyah)* na njia za kufikia malengo ya ki-Sheriya (*al-wasâilush-Shar'iyyah)* zimewajibishwa ni kuregea kwenye Kitâb na Sunnah, na kupekuwa kwa hadhari na kuthibitisha yaliyopokewa kuhusiana nazo, na kuzichunguza maana na ishara za maandiko husika. Hakuna njia nyengine isiyokuwa hiyo.

Kwa kuruhusiwa kutumia njia ya ki-maumbile iliyo makhsusi, kuna masharuti mawili: Kwanza ni kwamba hilo ni jambo la halali katika Sheriya, na pili ni kwamba imethibitishwa kuwa ki-hakika inalifikia lengo lake, au pana uwezekano mkubwa wa kupatikana hayo. Ama kuhusu njia zilizowajibishwa kwa malengo ya Sheriya, basi sharuti lake la pekee ni kwamba zimethubutu katika Sheriya, hilo tu peke yake.

Kwahivyo kutumia mnyama mdogo katika mfano tulioutaja hapo awali, kama njia inayodaiwa ya kujipatia 'ilmu ya mambo yaliyofichikana na ya ghayb, ndiyo ya kwenye upande wa 'njia za ki-maumbile' za bâtwil zilizobomolewa na tajriba pamoja na mazingatio. Kisha kwa upande wa njia za Sheriya, ni ukafiri na upotofu. Allâh ameubainisha waziwazi ukosefu wake wa maana na akatahadharisha dhidi ya mambo hayo. Kwa bahati mbaya watu kwa kawaida huchanganyikiwa kuhusu mas'ala haya na kudhania yakwamba kwa kuthibitisha tu jambo kuwa njia fulani inaleta manufaa, basi hilo tena linaonyesha yakwamba linaruhusiwa na kufaridhishwa katika Sheriya. Huwenda ikatokea yakwamba mmoja wao anamuomba mtu mwema aliyekufa, aliyekuwa akipendwa na Allâh (*walî*), au akawa anatafuta usaidizi kutoka kwa mtu aliyekufa. Kisha akakuta yakwamba aliyekuwa akimlingania amewasili, na akayapata aliyokuwa akiyataka. Kisha akadai yakwamba hii ni dalili ya uwezo wa waliokufa na wenyeji wema wa makaburi kuja kwa kuwasaidia watu, na kwamba inaruhusiwa kuwaomba wao na kuwataka msaada. Ushahidi wao wa pekee wa hili ni kwamba wamejipatia waliyokuwa wakiyataka. Kwa bahati mbaya, sisi tumesoma mifano mengi kama haya kwenye vitabu vilivyoandikwa kuihusu Dini. Atasema muandishi, au amnukuu mtu mwengine

akisema, kwa mfano, yakwamba yeye alikuwa kwenye dhiki kubwa sana basi akamwita *walî* fulani, au mtu mwema fulani, akamwita kwa jina lake, na kwamba mara akatokeza yeye mwenyewe kwa kiwiliwili au akaja kwenye ndoto na akamsaidia na akamletea aliyokuwa akiyataka. Mtu huyu masikini na mfano wake hawazingatii yakwamba hata kama hili limetokea ki-hakika, yakwamba ni jambo lililofanywa na Allâh (عزّ وجلّ) kama njia za kuwakubalia washirikina na wazushi wapate kuzidi kupotea katika upotofu wao, na kama mtihani kwao, na kama sehemu ya mbinu zake dhidi yao, kama malipo wanayostahili kwa kupa-mgongo kwao kutoka kwenye Kitâb na Sunnah, na kwa kufuata kwao hawaa za nafsi zao na mashetwani wao.

Kwahivyo mtu mwenye kuyasema maneno hayo anawaruhusu watu waombe dua zao na kuomba msaada kutoka kwa wengine wasiokuwa Allâh (تعالى), haliyakuwa mwito kama huo wa kutaka msaada (*istighâthah*) si jengine isipokuwa ni ushirikina mkubwa. Analiruhusu hili kwa sababu tu ya jambo lililowahi kumtokea yeye au lililomtokea mtu mwengine, na hata kwanza huwenda ikawa kisa hiki kilitungwa tu na kuzuliwa au kimepotoshwa na kuongezwa chumvi ili kiwapoteze watu. Ni jambo liwezekanalo pia yakwamba kilikuwa ni kisa cha kweli, na kwamba alikosea katika hukumu yake kumuhusu mtu aliyenusuriwa na aliyetoa msaada. Alidhania yakwamba huyo alikuwa ni mtu mwema aliyependwa na Allâh, haliyakuwa kwa hakika alikuwa ni sheitwani aliyelaaniwa aliyefanya hivyo kwa niya mbaya ambayo ilikuwa ni kuwadanganya na kuwapoteza watu, na kuwasababisha watumbukie kwenye ukafiri na upotofu kwa kukusudia au kutokusudia. Kwa hakika kuna habari nyingi kuwahusu wenye kuabudu masanamu katika zama za *Jâhiliyyah* yakwamba walikuwa wakenda kwa sanamu kisha wakimwita na huku wakidhani yakwamba mwenye kuzungumza nao na kuwajibu alikuwa ndiye huyo sanamu ambaye wanaemuabudu badala ya Allâh. Ukweli wa mambo ni kwamba hakuwa mwengine isipokuwa ni Sheitwani aliyelaaniwa aliyekusudia kuwapoteza na kuwadidimiza kwenye itikadi za upotofu.

Kwahivyo yaliyo muhimu hapa ni kwamba tumetambua yakuwa tajriba au taarifa za matukio si njia za sawa za kuthibitisha yakwamba uhakika wa vitendo vya ki-Dini ni vya sawa na vimeamrishwa kwenye Sheriya. Bali njia ya pekee inayokubalika ya kujua hilo, ni

kuithibitisha hukmu ya ki-Sheriya kuhusiana nayo, na hayo yawe yatapatikana katika Kitâb na Sunnah, lisiwe jengine lolote. Sehemu muhimu ambapo watu hutatizika hapa ni yale yenye kuhusiana na mambo ya *ghayb* na kutafuta kwao jinsi ya kupenya huko kwa njia moja au nyengine, kama vile kwenda kwa makuhani na wenye kusoma nyota, na watabiri, wata'alamu wa nyota, waganga na wachawi. Utakuta yakwamba wao wanaamini kuwa watu hawa wana 'ilmu ya ghayb na ya siri kwa vile wana uwezo wa kuwaeleza kuhusu baadhi ya mambo yaliyofichikana kwao. Kisha mara nyengine mambo hutokea kama yanavyosimuliwa na watu hawa, kwahivyo kutokana na hayo, wao hudhania yakwamba hili ni jambo linaloruhusiwa na kukubalika. Ushahidi wao ni kwamba yaliyosemwa na hawa watu kwa hakika yametokea. Haya ni makosa makubwa na upotofu wa dhahiri, kwani uhakika wa kupatikana manufaa kwa kupitia njia makhsusi ni ukweli tu, haitoshi kuthibitisha yakwamba njia hii ni halali na imeruhusiwa katika Sheriya. Kwa mfano kuuza mvinyo huwenda kukamnufaisha muuzaji na huwenda kukamtajirisha, vilevile mara nyengine uchezaji wa kamari, na kwa ajili hii Mola wetu (تبارك وتعالى) amesema kuwahusu watu hao:

يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَآ إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَـٰفِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَآ أَكْبَرُ مِن نَّفْعِهِمَا ۗ وَيَسْـَٔلُونَكَ مَاذَا يُنفِقُونَ ۖ قُلِ ٱلْعَفْوَ ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلْـَٔايَـٰتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ٢١٩

Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: "Katika hivyo mna madhara makubwa na (baadhi ya) manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake." Na wanakuuliza watoe nini? Sema: "Vilivyokuzidieni." Naam hivi Allâh anakubainishieni aya (zake) mpate kufikiri.[21]

[21] Al-Baqarah 2:219

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Na bado pamoja na hili yote hayo yameharamishwa (*harâm*), na watu kumi waliofungamanishwa pamoja na kinywaji cha ulevi wamelaaniwa, kama ilivyo kwenye hadîth.[22]
Kwenda kwa wapiga ramli vilevile imeharamishwa tangu kuharamishwa kwake katika dini kulipothibitishwa na kutahadharishwa watu wajiepushe na jambo hilo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:

« مَنْ أَتَى كَاهِنًا، فَصَدَّقَهُ بِمَا يَقُولُ، فَقَدْ بَرِئَ مِمَّا أُنْزِلَ عَلَى مُحَمَّدٍ »

"Mwenye kwenda kwa Kuhani (mpiga ramli), na akaamini anayoyasema, basi mtu huyo amejieka mbali na aliyoteremshiwa Muhammad."[23]

Akasema (صلى الله عليه وسلم):

« مَنْ أَتَى عَرَّافًا فَسَأَلَهُ عَنْ شَيْءٍ، لَمْ تُقْبَلْ لَهُ صَلَاةٌ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً »

"Mwenye kumwendea mpiga-bao na akamuuliza kuhusu jambo lolote, basi swala zake kwa muda wa siku arubaini hazitokubaliwa."[24]

Vilevile Mu'âwiyah ibn al-Hâkim as-Sulamî alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم); "Miongoni mwetu kuna wendao kwa wapiga ramli." Basi akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Musende kwa ma-Kuhani..."*[25]

---

[22] Ibn 'Umar amesimulia yakwamba, Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Allâh amelaani mvinyo, mwenye kunywa, mwenye kumtilia mtu, mwenye kuuza, mwenye kununua, mwenye kutengeneza, mwenye kuagizia itengenezwe, mwenye kupeleka, mwenye kutayarisha kupelekwa, na mwenye kutia bei,"* [Swahîh: imepokewa na Abu Dâwud (tafsiri ya ki-Ingereza 3/1042/no.3666) na al-Hâkim (2/32); Swahîh ul-Jâmi' (no.5091)]

[23] Amepokea Ahmad na Abû Dâwud na isnâd yake ni Swahîh. Tizama kwenye iliyotangulia (no.5818)

[24] Imepokewa na Muslim. Tizama katika iliyotangulia (no.5816)

[25] Imepokewa na Muslim na wengineo, na imeswahihishwa katika *"Swahîh Abî Dâwud."* (no.862)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Amekwisha kutubainishia Mtume rehma na amani zimshukie yeye ni jinsi gani ambavyo mpiga-bao na mchawi wanavyoweza kupata ujumbe kuhusu baadhi ya mas'ala yaliyofichikana. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

« إِذَا قَضَى اللَّهُ الأَمْرَ فِى السَّمَاءِ، ضَرَبَتِ المَلاَئِكَةُ بِأَجْنِحَتِهَا خُضْعَانًا لِقَوْلِهِ، كَالسِّلْسِلَةِ عَلَى صَفْوَانٍ - فَإِذَا فُزِّعَ عَنْ قُلُوبِهِمْ، ق ـالُوا: مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ، قَالُوا لِلَّذِى قَالَ: الحَقَّ، وَهُوَ العَلِىُّ الكَبِيرُ، ف ـيَسْمَعُهَا مُسْتَرِقُو السَّمْعِ، وَمُسْتَرِقُو السَّمْعِ هَكَذَا وَاحِدٌ فَوْقَ آخَرَ - وَوَصَفَ سُفْيَانُ - أحد رواة الحديث - "وهو ابن عيينة كما قال الحافظ ابن كثير فى تفسيره 537/3" بِيَدِهِ - وَفَرَّجَ بَيْنَ أَصَابِعِ يَدِهِ اليُمْنَى، نَصَبَهَا بَعْضَهَا فَوْقَ بَعْضٍ - فَرُبَّمَا أَدْرَكَ الشِّهَابُ المُسْتَمِعَ قَبْلَ أَنْ يَرْمِىَ بِهَا إِلَى صَاحِبِهِ، و ـرُبَّمَا لَمْ يُدْرِكْهُ حَتَّى يَرْمِىَ بِهَا إِلَى الَّذِى يَلِيهِ، الَّذِى هُوَ أَسْفَلَ مِنْهُ، حَتَّى يُلْقُوهَا إِلَى الأَرْضِ - وَرُبَّمَا قَالَ سُفْيَانُ: حَتَّى تَنْتَهِىَ إِلَى الأَرْضِ - فَتُلْقَى عَلَى فَمِ السَّاحِرِ، فَيَكْذِبُ مَعَهَا مِائَةَ كَذْبَةٍ، فَيُصَدَّقُ فَيَقُولُونَ: أَلَمْ يُخْبِرْنَا يَوْمَ كَذَا وَكَذَا، يَكُونُ كَذَا وَكَذَا، فَوَجَدْنَاهُ حَقًّا؟ لِلْكَلِمَةِ الَّتِى سُمِعَتْ مِنَ السَّمَاءِ

"Pindi Allâh alipotoa hukmu yake juu ya jambo kutoka juu Mbinguni, Malaika hukukuta mbawa zao kama ishara ya kusalimu amri kwa maneno Yake na kutoa sauti kama mfano wa silisili zenye kuburutwa juu ya mwamba laini. Kisha khofu inapo ondolewa kutoka kwenye nyoyo zao, husema: 'Amesemaje Mola wenu?' Hujibu kwa kusema: 'Haki, naye ni Mtukufu zaidi aliye Mkubwa zaidi.' Kisha wale wenye kusikiliza kwa siri (yaani; mashetwani) huyasikiya hayo, na hao wenye kusikiliza kwa siri wamejipanga mmoja juu ya mwengine namna hii ... [na Sufyân, mmojawapo wa wapokezi wa hadîth hiyo,

naye ni (Sufyân) Ibn 'Uyaynah kama alivyotaja al-Hâfidh Ibn Kathîr katika tafsiri yake (3/537), akaashiriya kwa mkono wake, akivichanua vidole vya mkono wake wa kulia na kuviweka kimoja juu ya chengine] ... basi hwenda kinga cha moto kikamzidi nguvu na kumchoma aliyekuwa akisikiliza kwa siri kabla ya kuweza kumsambazia mnong'ono mwezake, na hwenda yasimfikie yeye mpaka awe ameyasambaza kwa mwenzake aliye chini yake mpaka yafike kwenye ardhi (au pengine Sufyân alisema: "Mpaka habari hizo zifike kwenye ardhi.") Kisha yanatiwa ndani ya mdomo wa mchawi ambaye atakayeongezea urongo mia-moja ndani yake. Kwahivyo atakuwa mkweli kwa hilo moja, na watu nao watasema: 'Kwani hakutwambia yakwamba katika siku fulani na fulani kutatokea kitu kadha na kadha, na sisi tumeswadikisha hayo? (kuhusiana na habari zilizoshuka kutoka mbinguni.)[26]

Mfano wa haya vilevile umepokewa kutoka katika hadîth nyengine kutoka kwa Ibn 'Abbâs (رضي الله عنهما), aliyesema: "Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amekaa na kundi la Maswahaba zake mara muangaza wa nyota ukamulika, basi hapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawauliza: 'Mulikuwa mukisemaje katika zama ya *ujâhiliyyah* yalipokuwa yakitokea mambo kama hayo?' Wakasema: 'Tulikuwa tukisema yakwamba ilikuwa ikiashiriya mazazi au kifo cha mtu mtukufu.' Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *'Laa, bali hazikuvurumizwa kwa ajili ya kifo wala mazazi ya mtu yoyote. Bali pindi Mola wetu* (تبارك وتعالى) *anapolikadiria jambo, hapo aliyehimili 'Arshi Humsabihi na kumtakasa na kila sifa za upungufu. Kisha wakamsabihi walio chini yao kwenye Mbingu na kumtakasa na kila sifa za upungufu, mpaka tangazo lao la Kutakasika Kwake na ukamilifu likafikia Mbingu za chini kabisa. Kisha wakaazi wa Mbinguni walio chini ya Aliyehimili 'Arshi wakamuuliza aliyehimili 'Arshi: 'Amesemaje Mola wako?' Basi wakawapasha habari wao, na wakaazi wa kila Mbingu wakawapasha wengine waliokuwa kwenye mbingu nyengine, mpaka habari hizo zikafika kwenye mbingu za ulimwengu huu na Majini wakawa wanatafuta kusikiya minong'ono,*

[26] Imepokewa na al-Bukhâri mahali kwingi

wakawa wanashambuliwa kwa vimondo. Kwahivyo chochote wanachokifikisha kama kilivyo, basi huwa ni ukweli, lakini hatahivyo, huyachanganya na mambo duni ya ghushi na kuongezea ndani yake."[27]

Na kutokana na ahâdith hizi mbili na nyenginezo tunajua yakwamba mafungamano baina ya Wana-adamu na Majini yanapatikana, na kwamba majini huwapasha habari makuhani kuhusu baadhi ya habari zilizo za kweli, ambapo kuhani naye huongezea habari nyengine za urongo anazozitunga, kisha akawasimulia watu mambo haya. Ndipo wao nao wakaona baadhi ya mambo hayo kuwa ni ya kweli. Lakini, licha ya hayo yote, ametukataza mtunga Sheriya, Mwenye Hikma, kwenda kwa hawa makuhani na kututahadharisha dhidi ya kuwaswadiki kuhusu wayasemayo, kama ilivyotangulia.

Kwa mnasaba huu, tusiwe sisi ni wenye kusahau yakwamba hawa makuhani, wachawi na wapiga ramli wameendelea kuwa na athari kubwa sana kwa watu wengi, hata kwenye zama zetu hizi ambazo watu wanadai yakwamba ni zama za ki-'ilmu na kutaalamika, na za ustaarabu na desturi. Wao wanadhani yakwamba zama za makuhani, wachawi na waganga na athari zao zimepitiwa na wakati na ni mambo ya kale. lakini juu ya hayo, mwenye kufanya upelelezi kwa makini na akafuatilia habari za mambo hayo kutoka hapa na pale atakuja kujua kwa hakika yakwamba bado wangali ni wenye kuwashikilia watu wengi, isipokuwa tu wao wamejitambulisha nafsi zao na kujitokeza kwa sura nyengine, zisizoweza kutambulika isipokuwa na watu wachache. Kwahivyo uzushi wa mizimu yenye kusababisha mashetwani wajitokeze na kuzungumza nao, na kufanya maagano nao kwa njia tafauti si chochote isipokuwa ni mbinu mpya za uchawi na upigaji wa ramli za kuwapoteza watu na kutolewa katika dini yao na kufungamanishwa badala yake na udanganyifu wa uwongo na batili. Wao huyazingatia mambo haya kuwa ni 'ilmu na yanayotokamana na dini, haliyakuwa ukweli wa mambo ni kwamba 'ilmu na dini ziko mbali na wao na hawahusiani nao kivyovyote. Kwahivyo, katika kumalizia, hairuhusiwi kuthibitisha 'njia za ki-maumbile', wala yanayodhaniwa kuwa ni njia zinazopelekea kwenye malengo ya ki-Sheriya, wala kutumia njia kama hizo mpaka ikathibitishwa yakwamba kwa hakika ni jambo lenye kuruhusiwa katika Sheriya.

[27] Imepokewa na Ahmad, Muslim na at-Tirmidhi

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kisha, kuhusu ‘njia za ki-maumbile’, vilevile ni muhimu kuthibitisha uswahihi wake na faida zake kwa kuzichunguza na kuwa na tajriba nazo.

Na inatupasa kutanabahi yakwamba pindi inapothibitishwa yakwamba jambo fulani limeswihi kuwa ni katika ‘njia za ki-maumbile’ , basi iwapo itakuwa haikukatazwa katika Sheriya, basi hilo litakuwa linatosha kulifanya kuwa ni halali na kuweza kutumika. Kuhusiana na mas’ala haya, wanavyuoni wa Fiqhi wamesema: “Msingi wa nguzo kuhusu mambo (ya kilimwengu au yasiyokuwa ya ki-Sheriya) ni kwamba yanaruhusiwa.” Lakini, ama kuhusu njia za kujipatia malengo ya ki-Sheriya, basi ukweli tu yakwamba Mtunga Sheriya, Mwenye Hikma hakuwaharamishia moja kwa moja, haitoshi kuifanya ijuzu kuzitumia, kama wanavyodhania kimakosa watu wengi. Bali ni lazima kuwe na maandiko yaliyothubutu ya ki-Sheriya yenye kuwaruhusu na kuwapendekezea. Hii ni kwa sababu linalopendekezwa huzidi lenye kuruhusiwa tu, kwani hilo (jambo la kupendekezwa) ni jambo lenye kumkurubisha mtu kwa Allâh (تعالى), na mambo kama hayo hayawezi kuthibitishwa isipokuwa kwa uhakika tu yakwamba hapajapokewa makatazo yake. Kuhusu suala hili, amesema mmoja miongoni mwa ma-Salaf (watu wema waliotutangulia): “Sampuli yoyote ya ibada ambayo haikuwahi kufanywa na Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), basi usiifanye.” Hii imechukuliwa kutoka kwenye hadith inayokataza kuzua katika dini, na ni maarufu sana. Kwahivyo Sheikhul Islâm Ibn Taymiyyah (رحمه الله) amesema: “Asili katika ibada ni kwamba vitendo vyote ni harâm, na kuhusu mambo ya kilimwengu ni kwamba vitendo vyote vinaruhusiwa, isipokuwa iwapo itapatikana maandiko.” Kwahivyo kumbuka nukta hii kwa vile ni muhimu sana na itakusaidia kuuona ukweli kwenye mas’ala ambayo kwayo watu wanakhitilafiana.

MLANGO WA TATU

AT-TAWASSUL YA KI-SHERIYA NA SAMPULI ZAKE

Kutokana na yaliyotangulia tumeshajua yakwamba kuna mas'ala mawili yaliyo mbali mbali, la kwanza lake ni uwajibikaji wa njia (*at-tawassul)* hauna budi uwe ni wa ki-Sheriya, na hilo haliwezi kujulikana isipokuwa kwa dalili swahih kutoka katika Kitâb na Sunnah. Na la pili lake ni kwamba *at-tawassul* ni lazima iwe kwa njia ya ki-maumbile ya sawa ambayo kwayo mtu kwa hakika atalifikia lengo alilolikusudia.

Na sisi twajua yakwamba Allâh (عزّ وجلّ) ametuamrisha tumuombe Yeye (سبحانه) kwa kutaka msaada kutoka Kwake. Akasema:

وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدْعُونِيٓ أَسْتَجِبْ لَكُمْۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ٦٠

Na Mola wenu anasema: "Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila ya shaka wataingia Jahannam, wadhalilike."[28]

Na akasema (تعالى):

[28] Al-Ghâfir 40:60

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ
فَلْيَسْتَجِيبُواْ لِى وَلْيُؤْمِنُواْ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ١٨٦

"Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu, (waambie kuwa) Mimi niko karibu nao. Naitika maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka."[29]

Yeye (عزّ), Mwenye shani, ametuwekea idadi ya sampuli za njia za ki-Sheriya (*tawassul*) ambazo ni zenye faida na zinazofikia malengo tuyatakayo. Allâh amekwisha kupitisha yakwamba kwa hakika atawajibu wale wenye kumlingania Yeye kwa njia hizi, maadamu sharuti nyengine za kukubaliwa maombi zitatekelezwa. Sasa hebu tuangalieni, bila ya kushikamana ki-upofu na rai moja au kuwa na chuki, kwenye yenye kudhihirika baada ya utafiti wa makini wa yaliyopokewa kwenye Kitabu Kitakatifu na Sunnah iliyotwahirika, nayo ni kwamba kuna sampuli tatu za *Tawassul* ambazo Allâh (تعالى) alizozifaradhisha na kuzihimiza. Baadhi yake zimenukuliwa katika Qur'ân na zikatumiwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), naye akazihimiza katika kutumika kwake. Miongoni mwazo hakukupatikana sampuli yoyote ya *tawassul* kwa kutumia dhati ya mtu yoyote, wala kwa jaha yake, wala kwa haki yake na wala kwa daraja yake. Kwahivyo hii yaonyesha yakwamba hatukuwekewa njia hii na haiingii kwenye '*wasîlah'* ya ujumla ambayo iliyotajwa kwenye Âyât mbili zilizotangulia. Ama kuhusu sampuli za ki-Sheriya za *tawassul* zilizoashiriwa, basi ni:

[29] Al-Baqarah 2:186

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

TUTAWASSAL (KUTAFUTA NJIA ZA KUJIKURUBISHA) KWA ALLÂH (تعالى) KWA MAJINA MIONGONI MWA MAJINA YAKE YENYE UKAMILIFU NA YALIYO MAZURI, AU KWA SIFA ZAKE MIONGONI MWA SIFA TUKUFU.

Kama vile Muislamu kusema katika maombi yake:

« اللهم إنى أسألك بأنك أنت الرحمن الرحيم، اللطيف الخبير أن تعافينى»

"Ewe Mola, Hakika yangu mimi..."

Au kama vile:

« أسألك برحمتك التى وسعت كل شىء أن ترحمنى وتغفر لى »

"Nakuomba kwa Rehma zako..."

Ni kama maneno ya mtu asemaye:

« اللهم إنى أسألك بحبك لمحمد صلى الله عليه وسلم »

"Ewe Mola hakika yangu mimi, nakuomba kwa mapenzi Yako kwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم)*."*

Kwa vile mapenzi ni miongoni mwa Sifa zake. Na dalili ya kuruhusiwa sampuli hii ya *tawassul* ni maneno ya Allâh (عزّ وجلّ):

وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ ١٨٠

"Na Allâh ana majina mazuri mazuri; muombeni kwayo."[30]

Maana ya hii ni: Mlinganie Allâh (تعالى) kwa njia ya (kufanya *tawassul* kwa) mjina Yake mazuri, na hapana shaka yakamba sifa zake Tukufu (عزّ وجلّ) zinaingiana hapa kwa vile majina Yake ndizo sifa zenye kumuhusu Yeye (تبارك وتعالى).

[30] Al-A'râf 7:180

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kutokana na haya ni yale ambayo Allâh (تعالى) aliyoyataja kuhusu maombi ya Mtume Suleimân (عليه السلام), pindi aliposema:

وَقَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِيٓ أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ ٱلَّتِيٓ أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَٰلِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَٰلِحًا تَرْضَىٰهُ وَأَدْخِلْنِي بِرَحْمَتِكَ فِي عِبَادِكَ ٱلصَّٰلِحِينَ ١٩

Na akasema: “Ee Mola wangu! Nipe nguvu nishukuru neema yako uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri uvipendavyo, na uniingize – kwa rehma yako – katika waja wako wema.”[31]

Vilevile miongoni mwa dalili ya haya ni hadith ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika maombi yaliyothubutu ambayo aliyokuwa akiyasema kabla ya kutoa salamu katika swala yake:

«اللَّهُمَّ بِعِلْمِكَ الْغَيْبَ وَقُدْرَتِكَ عَلَى الْخَلْقِ، أَحْيِنِي مَا عَلِمْتَ الْحَيَاةَ خَيْرًا لِي، وَتَوَفَّنِي إِذَا عَلِمْتَ الْوَفَاةَ خَيْرًا لِي... »

“Ewe Mola! Kwa ‘ilmu yako iliyofichikana na kudra zako juu ya viumbe, nipe uhai kwa kiyasi ujuacho Wewe yakwamba uhai ni bora kwangu, na unifishe yatakapokuwa mauti ni bora kwangu ...”[32]

Na miongoni mwayo ni kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimsikiya mtu akiomba katika *tashah-hud* yake:

« اللهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ يَا اللهُ الْوَاحِدُ الْأَحَدُ الصَّمَدُ، الَّذِي لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ، أَنْ تَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي، إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمِ »

“Ewe Mola! Kwa hakika nakuomba, Ewe Allâh, uliye Mmoja, wa Pekee, Mwenye kustahiki kukusudiwa, ambaye hukuzaa wala hakuzaliwa, wala huna uliyefanana naye hata mmoja,

---

[31] An-Naml 27:19

[32] Imepokewa na an-Nasâ’i, al-Hâkim na akaitangaza kuwa ni swahih na adh-Dhahabi akaafikiana naye na ni kama walivyosema.

yakwamba uniswamehe madhambi yangu, hakika Wewe ni Mwenye kuswamehe, Mwenye huruma."

Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema:

«قَدْ غُفِرَ لَهُ»

"Kwa hakika ameswamehewa, ameswamehewa."[33]

Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamsikiya mtu mwengine akisema katika *tashah-hud* yake:

« اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدَ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ وَحْدَكَ لَا شَرِيكَ لَكَ، الْمَنَّانُ يابَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ، يا ذا الجلال والإكرام، يا حيُّ يا قيومُ، إِنِّي أَسْأَلُكَ الْجَنَّةَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّار »

"Ewe Mola! Hakika yangu mimi nakuomba Wewe kwa haki yakwamba kila sifa njema zinakustahiki Wewe, hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe, peke Yako, usokuwa na mshirika. Mmiliki wa Baraka zote, Ewe Muumba Mbingu na Ardhi pasi na ruwaza, Ewe Mwenye Utukufu na Heshima, Ewe Mwenye Uhai wa kimaisha, Msimamizi wa kila jambo. Hakika yangu mimi nakuomba Pepo na uniepushe na Moto."

Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawauliza Maswahaba zake: *"Mwajua nyinyi huyu ameomba kwa kitu gani?"* Maswahaba wakamjibu: "Allâh na Mtume wake ndiwo wajuao." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia:

« وَالَّذِى نَفْسِى بِيَدِهِ، لَقَدْ دَعَا اللهَ بِاسْمِهِ الْعَظِيمِ (وفى رواية: الْأَعْظَمِ) الَّذِى إِذَا دُعِىَ بِهِ أَجَابَ، وَإِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى »

"Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko katika mkono Wake, amemuomba Allâh kwa Jina lake tukufu (na katika riwaya

[33] Ameipokea Abû Dâwud, an-Nasâi na Ahmad na wengineo. Na isnâd yake ni swahih.

nyengine: kwa Jina lake Tukufu zaidi) iwapo ataitwa kwa jina hilo, Yeye hujibu na akiombwa kwa hilo Yeye hutoa."[34]

Na miongoni mwazo ni hadith yake: "Yoyote anayezongwa na dhiki na akasema:

« اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، وَابْنُ عَبْدِكَ، وابْنُ أَمَتِكَ، نَاصِيَتِي بِيَدِكَ، مَاضٍ فِيَّ حُكْمُكَ، عَدْلٌ فِيَّ قَضَاؤُكَ، أَسْأَلُكَ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ، سَمَّيْتَ بِهِ نَفْسَكَ، أَوْ عَلَّمْتَهُ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ، أَوْ أَنْزَلْتَهُ فِي كِتَابِكَ، أ ـِو اسْتَأْثَرْتَ بِهِ فِي عِلْمِ الْغَيْبِ عِنْدَكَ، أَنْ تَجْعَلَ الْقُرْآنَ رَبِيعَ قَلْبِي، وَنُورَ صَدْرِي، وَجِلَاءَ حُزْنِي، وَذَهَابَ هَمِّي »

'Ewe Mola!Hakika mimi ni mja wako, mtoto wa mja wako wa kiume na mja wako wa kike. Shungi langu liko kwenye Mkono wako. Hukmu yako ni yenye kuendelea juu yangu. Uadilifu wako kunihusu mimi ni wa sawa. Nakuomba kwa kila jina ambalo ni lako, ambalo ulilojiita Wewe mwenyewe, na ukalifunza kwa mmojawapo wa viumbe vyako, au ulililoliteremsha kwenye Kitabu Chako, au ulilojiekea Wewe Mwenyewe kwenye 'ilmu iliyofichikana (ya ghayb) Kwako, yakwamba uifanye Qur'ân kuwa ni pumbazo la moyo wangu, na muangaza wa kifua changu, na yenye kuniondolea huzuni zangu na wasiwasi wangu.'

Basi Allâh Atamuondolea wasiwasi wake na huzuni zake na ambadilishie furaha badala yake."[35]

Na miongoni mwazo ni yaliyopokewa kutoka kwenye kuomba kwake (صلى الله عليه وسلم) hifadha ya Allâh kwa kutumia maneno:

[34] Imepokewa na Abû Dâwud, an-Nasâ'i na Ahmad na wengineo kwa isnâd iliyo swahih.

[35] Imepokewa na Ahmad (no.3712) na ni lafdhi yake, na al-Hâkim (1/509) na wengineo, na isnâd yake ni swahih kama nilivyoichambua katika as-Swahihah (no.199)

« اللهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِعِزَّتِكَ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَنْ تُضِلَّنِي ... »

"Ewe Mola! Hakika yangu mimi najilinda kwako kwa Utukufu Wako, hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe, ..."[36]

Vilevile miongoni mwazo ni aliyoyapokea Anas (رضي الله عنه) amesema kumuhusu Mtume (صلى الله عليه وسلم), yakwamba anapohuzunishwa na jambo, husema:

« يا حى يا قيوم برحمتك أستغيث »

"Ewe Mwenye uhai wa milele, uliye mkwasi na mlinzi, kwa rehma zako nakuomba msaada Wako."[37]

Kwahivyo ahâdith hizi na mfano wake zinabainisha uwajibu wa *tawassul* kwa Allâh (تعالى) kwa kutumia mojawapo ya majina Yake au sifa Zake, na kwamba hili ni jambo alipendalo Allâh na linalomridhisha. Kwahivyo limewahi kufanywa na Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم), na Allâh (تبارك وتعالى) akasema:

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُواْ ۚ ٧

"Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho."[38]

Kwahivyo imefaradhishwa juu yetu kumlingania Allâh (سبحانه) kwa mfumo ambao mtume Wake aliokuwa akimlingania. Hivyo ni bora mara elfu moja kuliko kumlingania kwa maombi tunayojianzishia sisi wenyewe na kwa mbinu tunazozibuni sisi wenyewe.

---

[36] Al-Bukhâri na Muslim.
[37] Imepokewa na at-Tirmidhi (1/267; *'at-Tuhfah*) na al-Hâkim (1/509) na ni hadith hasan.
[38] Al-Hashr 59:7

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

TUTAWASSAL KWA ALLÂH (تعالى) KWA AMALI NJEMA ALIYOWAHI KUIFANYA MUOMBAJI

Kama alivyosema Muslim: "Ewe Mola! Kwa Imani yangu ya kukuamini Wewe, na mapenzi ya kukupenda Wewe, na kumfuata kwangu mtume Wako, niswamehe mimi ..." au alivyosema "Ewe Mola! Mimi nakuomba kutokana na mapenzi yangu ya kumpenda Muhammad (صلى الله عليه وسلم), na imani yangu ya kumuamini Yeye, yakwamba uniokoe mimi ..." Kutokana na hayo ni kwamba mtu huomba Du'â' na akataja kitendo chema muhimu alichowahi kukifanya, na kwa kitendo hicho anamcha Allâh (سبحانه), na kukifanya kwa kumtwi'i Yeye, akitarajia malipo kutoka Kwake na kuhofia adhabu Yake, na kutanguliza yenye kumridhisha Yeye na kumtwi'i Yeye (جلّ شئنه), kuliko kitu chochote, kisha kutumia hayo kama njia ya *tawassul* katika du'â yake, ili kupatikane uwezekano mkubwa wa kutakabaliwa na kujibiwa.

Mfumo huu wa *tawassul* ni mzuri na wa kupendeza na umewajibishwa na Allâh (تعالى) na ni wenye kumridhisha Yeye. Na dalili za kushurutishwa kwake ni maneno yake (تعالى):

ٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَآ إِنَّنَآ ءَامَنَّا فَٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ١٦

"Ambao wanasema: "Mola wetu! Hakika sisi tumeamini, basi tughufirie madhambi yetu, na tuepushe na adhabu ya moto."[39]

Maneno yake:

رَبَّنَآ ءَامَنَّا بِمَآ أَنزَلۡتَ وَٱتَّبَعۡنَا ٱلرَّسُولَ فَٱكۡتُبۡنَا مَعَ ٱلشَّٰهِدِينَ ٥٣

"Mola wetu! Tumeyaamini uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi tuandike pamoja na washuhudiao."[40]

[39] Âli Imrân 3:16
[40] Âli Imrân 3:53

Maneno Yake:

رَّبَّنَآ إِنَّنَا سَمِعۡنَا مُنَادِيٗا يُنَادِي لِلۡإِيمَٰنِ أَنۡ ءَامِنُواْ بِرَبِّكُمۡ فَـَٔامَنَّاۚ رَبَّنَا فَٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرۡ عَنَّا سَيِّـَٔاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ ٱلۡأَبۡرَارِ ١٩٣

“Mola wetu! Tumesikia mwitaji anayeita kwendea Uislamu kwamba: ‘Mwaaminini Mola wenu.’ Tukaamini. Mola wetu! Tusamehe madhambi yetu na utufutie (aibu ya) makosa yetu (hayo) na utufishe pamoja na watu wema.”[41]

Na maneno yake:

إِنَّهُۥ كَانَ فَرِيقٞ مِّنۡ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَآ ءَامَنَّا فَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَا وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلرَّٰحِمِينَ ١٠٩

Bila shaka kulikuwa na kundi katika waja wangu likisema: “Mola wetu! Tumeamini, basi tusamehe na turehemu, nawe ndiwe Mbora wa wanaorehemu!”[42]

Mfumo huu wa *tawassul* vilevile umethibitishwa na aliyoyasimulia Buraidah ibn al-Husayb (رضي الله عنه): “Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) alimsikiya mtu akisema:

« اللهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنِّي أَشْهَدُ أَنَّكَ أَنْتَ اللهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ. الْأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِي لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ»

“Ewe Mola! Nakuomba kutokana na fadhla za uhakika yakwamba mimi nashuhudia yakwamba Wewe ni Allâh, hapana asiyekuwa Wewe mwenye haki ya kuabudiwa. Mpweke, unayestahiki kukusudiwa, ambaye hukuzaa wala hukuzaliwa, wala hakuna anayefanana na Wewe hata mmoja.”

[41] Âli Imrân 3:193
[4242] Al-Mu’mimûn 23:109

Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

« قَدْ سَأَلَ اللهَ بِاسْمِهِ الْأَعْظَمِ الَّذِى إِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى، وَإِذَا دُعِىَ بِهِ أَجَابَ »

"Kwa hakika, amemuomba Allâh kwa jina lake Tukufu, ambalo iwapo akiombwa kwa jina hilo hutoa na akilinganiwa kwa jina hilo, hujibu."[43]

Vilevile kutokana na hayo ni yaliyotokea katika kisa cha *Maswahibu wa pango*, kama yalivyopokewa na 'Abdullâh ibn 'Umar (رضي الله عنهما) aliyesema: "Nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *"Watu watatu, miongoni mwa watu waliokuwepo kabla yenu walitoka na shughuli zao mpaka usiku ukawaingilia walipofika kwenye pango, wakaingia humo ndani [ya pango]. Mara jabali likabingiria kutoka mlimani likaziba sehemu ya kuingia kwenye pango hilo. Hapo wakaanza kusema: Hakuna kitakachoweza kuwaokoa kutokamana na jabali hili isipokuwa ni kumuomba Allâh kwa kuzitaja amali njema walizowahi kuzifanya (na katika riwaya ya Muslim: Basi mmoja wao akaanza kuwaambia wenzake: Hebu jaribuni kukumbuka amali njema mulizowahi kuzifanya kwa ikhlâs kwa ajili ya Allâh kwa kuzitaja, ili apate kuwaokoa). Basi mmoja wao akasema: 'Yâ Allâh, mimi nina wazazi wangu wawili wakongwe na sikuwahi kuwatangulizia wao jamii yangu na watumwa wangu katika kuwanywesha maziwa. Lakini siku moja nilichelewa nilipokuwa nikishughulikia jambo fulani (katika riwaya ya Muslim: nyasi kavu) na sikurudi na wanyama mpaka nilipowakuta [wazazi wangu] wamelala. Kwahivyo nikawakamia wao wanyama lakini nikenda kuwakuta wamelala. Hata hivyo, nilichukia kuwapa maziwa jamii yangu na watumwa wangu kabla ya kuwapa wao [wazazi wangu], basi nikasubiri waamke na bakuli mkononi mwangu. Mara kulipopambazuka wakati wa asubuhi, wakaamka na wakanywa maziwa yao. Yâ Allâh ikiwa nilifanya hivyo kwa ajili ya kuutafuta Uso wako, basi tuokoe na janga hili lililosababishwa na jabali hili.' Basi lile jabali likasongea kiyasi kidogo, lakini*

[43] Imepokewa na Ahmad (5/349/350), Abu Dâwud (1493) na wengineo na isnâd yake ni swahîh

hawakuweza kupenya mahali hapo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *Mwengine akasema: 'Yâ Allâh, mjombangu alikuwa na binti yake na alikuwa akinipendeza zaidi miongoni mwa watu na nilijaribu kumshawishi afanye uhusiano wa ki-mapenzi na mimi, lakini alinikatalia mpaka alipoathirika kutokana na ukame wa mwaka mzima. Kisha akanijia na nikampa Dinari Mia Moja na Ishirini kwa sharuti yakwamba akubaliane na matakwa yangu ya mapenzi juu yake, ikambidi akubali. Lakini nilipokurubia kutekeleza pendo langu aliniambia: Si halali kwako kuvunja (katika riwaya ya Muslim: Ewe mja wa Allâh, mche Allâh na usiifungue) pete isipokuwa kwa haki yake. Basi nikaona haya kutekeleza uhalifu dhidi yake, ndipo nilipowachana naye, na nilikuwa nikimpenda zaidi kuliko mtu yoyote, na (pia) nikamuachia ile dhahabu niliyompa. Yâ Allâh ikiwa nilifanya hivyo kwa ajili ya kuutafuta Uso Wako, basi tuokoe na janga hili lililotusibu.' Basi lile jabali likasongea tena kidogo, kiyasi cha kwamba wakawa bado hawakuweza kupenya mahali hapo.* Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *Na wa Tatu akasema: 'Yâ Allâh, mimi niliwaajiri baadhi ya wafanyi kazi na nikawalipa ujira wao isipokuwa mtu mmoja miongoni mwao ambaye hakuchukuwa ujira wake na akenda zake. Nikauchumia ujira huo wake na ukazalisha faida kubwa ya mali. Kisha baada ya muda fulani alinijia na akaniambia: 'Ewe mja wa Allâh, nilipe ujira wangu.' Basi nilimwambia: 'Ngamia wote hao, Ng'ombe, Kondoo, na hao Watumwa unao-waona hapo – huo ndiwo ujira wako.' Akasema yule mtu: 'Ewe Mja wa Allâh, usinifanyie mzaha.' Nikamwambia: 'Mimi sikufanyii mzaha.' Basi yule bwana akachukuwa mali zote hizo akenda nazo bila ya kubakisha kitu chochote. Yâ Allâh ikiwa nilifanya hivyo kwa ajili ya kuutafuta Uso Wako, basi tuokoe kutoka katika hali tuliyoko.' Basi lile jabali likasongea na wakatoka nje ya lile pango.'*[44]

Kwahivyo ni wazi kutokana na hadîth hii yakwamba pindi hawa waumini watatu walipokuwa kwenye dhiki na hali ngumu kama hizo, na walipokuwa wamekata tamaa ya mbinu zote za kukimbia, isipokuwa kwa kujitegemeza kwa Allâh (تبارك وتعالى) Peke Yake awaokoe, kisha wakamuelekea Yeye na kumuomba Yeye kwa unyenyekevu na

[44] Imepokewa na al-Bukhâri (3/260/no.472) na matamshi ni yake na Muslim (41432/no.6607) na an-Nasâ'i na wengineo.

utakaso wa hali ya juu. Vilevile waliyataja mambo mema waliyoyatenda wakiwa wanamtambua Allâh katika nyakati za raha, wakitarajia malipo kutoka kwa Mola wao awaokoe wakiwa kwenye nyakati za dhiki. Kama ambavyo ilivyokuja katika hadîth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم):

« تَعَرَّفْ إِلَى اللهِ فِي الرَّخَاءِ يَعْرِفْكَ فِي الشِّدَّةِ »

... mkumbuke Allâh katika nyakati za raha, na Yeye atakukumbuka kwenye nyakati za dhiki.[45]

Kwahivyo walitafuta njia za mkuruba (*tawassul*) Kwake (سبحانه) kwa kupitia kwenye vitendo hivyo. Wa kwanza alitumia wema wake kwa wazazi wake kama *tawassul* na huruma zake na kuwahudumikia kwa ukarimu kiyasi cha kwamba ikampelekea kwenye hicho kitendo kimoja kizuri sana, na mimi sidhani mtu yoyote mwengine, isipokuwa kwa Mitume, awezae kufikilia kiwango hicho cha ukarimu na uzuri kwa wazazi wao.

Kisha wa pili naye akatumia kama *tawassul* kujiepusha kwake na kufanya uzinifu na binti ya mjombake, na alikuwa na uchu naye, na alikuwa ashajiachia kwake na kujidhalilisha kwake bila ya kulazimishwa kutokana na njaa na mahitaji. Lakini yule binti akamkumbusha kuhusu Allâh (عزّ وجلّ) na moyo wake ukasalimu amri na kuwaidhika na viungo vyake vikatetema na akamuacha yeye pamoja na kumuachia pesa alizompa.

Na wa tatu akatumia kama *tawassul* katika kuhifadhi haki za mfanyi kazi wake, aliyewacha mshahara wake uliokuwa kiyasi cha kipimo cha mchele, kama ilivyotokea kwenye riwaya ya hadîth iliyokuwa swahîh, na akenda zake. Kwahivyo muajiri akazifanyia biashara au akazichumia mpaka zikaongezeka na kufikia thamani ya Kondoo, Ng'ombe, Ngamia na watumwa. Kisha, siku ambayo mfanyi kazi alipokuwa akihitaji mshahara wake, alimtaka muajiri wake amlipe

[45] Imepokewa na Ahmad kutoka kwa Ibn 'Abbâs na silisili yake ya upokezi ni swahîh, kutokana na usaidizi, kama nilivyoeleza katika *"Dhilâl lil-Jannah fiy takhrîj is-Sunnah."* (no.138)

mwenyewe kipato chake chembamba. Naye muajiri kwa upande wake alimkabidhi mali zote zilizomshangaza mfanyi kazi huyo mpaka akadhani yakuwa anafanyiwa mzaha. Hatahivyo, ilipobainika yakwamba mtu yule alikuwa hafanyi matani na kwamba mali hizo zote zilikuwa ndiyo mazao ya mshahara wake alichukuwa kila kitu kwa furaha na mshangao, pasi na kubakisha chochote nyuma. Kwa hakika, *Wallâhi,* kitendo cha Muajiri hapa kilifikia kiwango cha kushangaza cha fadhla za kumtendea wema mfanyi kazi na ulikuwa ni mfano wa ruwaza njema kwa msimamizi anavyopaswa kuwahudumikia kwa heshima walio chini yake. Ilifikia daraja kiyasi hicho kuona yakwamba viwango vya wanaodai kuwasaidia wafanyi kazi na mtu wa kawaida haifikii hata 1% [asili mia moja], wenye kufanya biashara ya faida kutokana na madai yao ya kuzilinda haki za masikini na wahitaji, na kuwahudumikia kwa wema na kuwapa haki zao. Kwahivyo maombi ya watatu hawa kwa Mola wao (سبحانه), wakitumia kama njia ya kujikurubisha Kwake vitendo hivi vyema kabisa na vitukufu, wakitangaza yakwamba wao walivifanya kwa kutaka radhi za Allâh (تعالى) peke yake, bila ya kutarajia kwa hayo faida zozote za kilimwengu wala za kibinafsi au utajiri wowote. Kwahivyo wakataraji yakwamba Allâh (جلّ شئنه) awafungulie na kuwaacha huru kutokana na dhiki zilizowakumba, na awafariji kutoka kwenye mitihani, kwahivyo Allâh (تعالى) akafanya kama walivyomtarajia kwa kuwaafikia miujiza ya waziwazi kwa kusababisha jabali lisongee kando na kufunguka kwa hatua tatu kila alipokuwa akiomba mmoja wao ili likaweza kufunguka lote kabisa pindi mtu wa tatu alipomaliza maombi yake, baada ya kuwa kwenye hali ambayo kifo kilikuwa karibu nao. Kisha Mtume wetu Mtukufu (صلى الله عليه وسلم) akatuhadithia kisa hiki kizuri baada yakwamba lilikuwa ni jambo tusilolijua na lililofichikana nasi, lililojulikana na Allâh (سبحانه وتعالى) peke Yake. Alitujulisha kisa hiki ili atukumbushe kuhusu vitendo vizuri na vya kuigwa vilivyotekelezwa na wafuasi wazuri na wanaostahiki kuigwa wa Mitume iliyotangulia ili tupate kufuata mifano yao, tutende kama walivyotenda wao, na kuleta mafunzo yenye thamani na mawaidha kutokamana na kisa chao. Haiwezekani kusemwa: 'Vitendo hivi vilifanywa kabla ya kuletwa kwa Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na kwahivyo havituhusu sisi,' kwa kutegemezwa juu ya misingi ya rai iliyo sawa ya ki-Fiqhi yakwamba Sheriya zilizoteremshwa za wale waliokuja kabla

yetu hazituhusu sisi. Haya hayasemwi hapa kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alinukuu kitendo hiki kwa min-ajil ya kusifu na kuheshimu, na huku ni kujuzisha kwa kunyamazia kutoka kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa hakika hii ilikuwa ni zaidi ya kujuzisha kwa kunyamazia katika kitendo chao cha ki-Dini: hayakuwa haya isipokuwa ni katika maelezo na utendaji wa ki-mifano ya kuonyesha jinsi *Āyât* zilizotangulia zilivyokuwa zikistahiki kutekelezwa. Sheriya zilizoteremshwa zinaafikiyana katika mafunzo yake na uongofu wake na haya si ya kushangaza kwa sababu yote yanatoka kwenye asili moja na kumulika kutoka kwenye muangaza mmoja, hususan kuhusiana na hali za watu na uhusiano wao na Mola wao (سبحانه), kwahivyo wametafautiana kidogo sana na kwa nadra sana kama ilivyostahili kutokana na hikma za Allâh (سبحانه).

KUTAFUTA NJIA YA KUJIKURUBISHA KWA ALLÂH (تعالى) KWA MAOMBI YA MTU MWEMA.

Iwapo Muislamu ataingia kwenye dhiki kubwa au msiba mkubwa ukampata, na akawa anajua yakwamba yeye alikuwa akipuuza amri za Allâh (تبارك وتعالى), basi akapendelea kutumia njia zenye nguvu za kujikurubisha kwa Allâh. Basi akenda kwa mtu ambaye yeye aliitakidi yakwamba alikuwa ni mtu mwema na mwenye *taqwâ* (ucha-Mungu), au mtu aliye na fadhla-bora na ujuzi wa ‘ilmu ya Kitâb na Sunnah, na akamtaka amuombee yeye kwa Mola wake, yakwamba Yeye [*yaani;* Allâh] amuondolee dhiki zake na amuondolee yaliyomsibu. Hii ni sampuli nyengine katika *tawassul* za kisheriya ambayo iliyothibitishwa na kuongozwa kwake katika Sheriya iliyotwahirika. *Mifano* yake inapatikana katika Sunnah tukufu na mifano yake inapatikana kutoka kwenye mafundisho ya Maswahaba Watukufu (رضوان الله عليهم).

Anas Ibn Mâlik (رضي الله عنه) amepokewa akisema: “Watu waliteseka kwa ukame katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), siku moja alipokuwa akitoa khutba Mtume (صلى الله عليه وسلم) [akiwa juu ya minbar], akiwa amesimama, katika siku ya Ijumaa alisimama Mbedui

mmoja [*na katika riwaya nyengine:* aliingia] [miongoni mwa watu wa kwenye Jangwa] [kupitia kwenye mlango ulioelekeana na *minbar*] [karibu na nyumba iliyouzwa kwa ajili ya kulipa deni[46], na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amesimama. Kwahivyo alisimama akiwa amemuelekea Mtume (صلى الله عليه وسلم)] akasema: "Ewe Mjumbe wa Allâh, wanyama wanakufa na watoto wana njaa [na katika riwaya nyengine: wanaangamia] [na katika riwaya nyengine: Farasi wanakufa na Kondoo wanakufa] [na katika kauli nyengine: Ng'ombe wanakufa na barabara zinabomoka], hebu tuombee kwa Allâh [atupe nasi mvua] [na katika riwaya nyengine: yakwamba atuteremshie mvua]." Basi akainua mikono yake akaanza kuomba [mpaka nikaona weupe wa makwapa yake]: [*Yâ Allâh tubariki kwa mvua, Yâ Allâh tubariki kwa mvua*] [na watu wakainua mikono yao pamoja nae katika kuomba] [na wala hakutaja yakwamba aligeuza kishali chake nje-ndani, wala yakwamba alielekea Qiblah], na [*Wallâhi*] hatukuwa tukiona [mawingu yoyote wala] ishara zozote za mawingu [wala kitu chochote, na hapakuwa na jengo lolote wala nyumba baina yetu na Sal'[47]] [na katika riwaya nyengine: Amesema Anas: na Mawingu yalikuwa mfano wa gilasi] [Akasema: Kisha nikaona wingu kubwa kama ngao na lilipofika katikati ya mbingu lilitawanyika na likaanza kunyesha]. Naapa kwa Yule ambaye Mkononi Mwake iko roho yangu, muda ule aliposhukisha mikono yake, mawingu mfano wa milima yalikuwa yamekusanyika, na hakushuka kutoka kwenye minbar mpaka nilipoanza kuona mvua ikitona kutoka kwenye ndevu zake, [na katika riwaya nyengine: mara kwa ghafula upepo ukaanza kuvuma na kukusanya mawingu yaliyokuja pamoja kisha mvua ikaanza kunyesha kutoka mbinguni] [na akashuka kutoka kwenye minbar na kuiswali swala] [basi tukatoka nje na kutembea kupitia matopeni mpaka tukafika majumbani mwetu] [na katika riwaya nyengine: ikafikia kiyasi cha kwamba ilikuwa ni vigumu kwa mtu kufika nyumbani kwake]. Basi ikaendelea kunyesha kwa siku hiyo, na siku iliyofuata, na siku iliyofuata, na siku nyengine iliyofuata hiyo, mpaka ikafika siku ya Ijumaa nyengine na haikuwacha kukoma kunyesha [kwahivyo mitaro ya maji ya al-Madinah nzima ilijaa] [na katika riwaya nyengine:

[46] *Dârul Qadhâ'*: Nyumba iliyokuwa ya 'Umar ibn al-Khattwâb na ambayo iliyouzwa kwa ajili ya kulipa deni.
[47] Mlima mdogo Mjini Madinah

Kwahivyo, *Wallâhi* hatukuliona Jua kwa wiki nzima]. Kisha Mbedui yule-yule au mtu mwengine akasimama [na katika riwaya nyengine: kisha akaingia mtu kupitia kwenye mlango uleule katika Ijumaa iliyofuata, na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amesimama akitoa khutbah, basi yule mtu akasimama akiwa amemuelekea] na akasema: Ewe Mjumbe wa Allâh, majumba yanaangamia, [na katika riwaya nyengine: Nyumba zinabomoka, mabarabara yanakatika na Ng'ombe wanakufa] [na katika riwaya nyengine: msafiri hawezi kuendelea na safari yake na barabara zimefungika] na wanyama wa mifugo wanazama. Hebu muombe Allâh [aizuiye] kwa ajili yetu [basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatabasamu] na akainua mikono yake akasema:

« اللَّهُمَّ حَوَالَيْنَا، وَلاَ عَلَيْنَا، [اللَّهُمَّ عَلَى رُءُوسِ الجِبَالِ وَالْآكَامِ
[وَالظِّرَابِ] وَبُطُونِ الْأَوْدِيَةِ وَمَنَابِتِ الشَّجَرِ»

"Yâ Allâh, kandoni mwetu na wala si juu yetu, [Yâ Allâh, juu ya vilele vya milima, viduta [na vilima vidogo] na kingo za mito na kwenye sehemu zinazomea miti].

Kwahivyo hakuashiriya mikono yake upande wowote wa Mbingu isipokuwa mbingu zilifunguka na kutandazika miviringo [na katika riwaya nyengine: basi nikaangalia na kuziona mbingu zikitawanyika katika mazingira ya al-Madinah [kuliani na kushotoni] na kutengezeka [sampuli ya taji] [na katika riwaya nyengine: kwahivyo mbingu zikatawanyika kutoka al-Madinah kama nguo zinavyovuliwa] na hapo ikaanza kutunyeshea katika sehemu tulizokuwepo, lakini haikutunyeshea juu yetu kabisa [katika riwaya nyengine: hata tone moja] [na tukatoka tukitembea chini ya miyale ya Jua]. Kwahivyo Allâh akawaonyesha miujiza ya Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) na majibu Yake kutokana na maombi aliyoyaomba. Mto wa Qanât ulifurika kwa muda wa mwezi mzima, na hakuna aliyekuja kutoka sehemu za nje isipokuwa alikuwa akisifu kuhusu mvua nyingi."[48]

[48] Imepokewa na al-Bukhâri (tafsiri: vol.2) [Uk.26, no.55] [Uk.67-72, no.126-132] [Uk.73, no.134] [Uk.77, Mlango 20] [Uk.79, no.143]; vol.4, [Uk.504, no.782]; vol.8 [Uk.74, no.115]. Nimeileta hii kwenye Mukhtasari wangu wa *Swahîhul-Bukhâri* [1/224-226, no.497] na kuzikusanya riwaya zake mbalimbali pamoja, na Mukhtasari huu unachapishwa kwa zamu... natumai

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Anas ibn Mâlik (رضي الله عنه)[49] amepokea kutoka kwa ‘Umar ibn al-Khattwâb (رضي الله عنه) yakwamba, watu walipopatwa na mateso ya ukame alikuwa akimuomba al-‘Abbâs ibn al-Muttwalib awaombee nao mvua. Alikuwa akisema: “Yâ Allâh tulikuwa tukimtaka Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) atuombee mvua kutoka Kwako (*natawassalu ilayka*) na Wewe ulikuwa ukitubariki kwa mvua. Sasa twamuomba mjombake Mtume wetu atuombee kutoka Kwako (*natawassalu ilayka*), basi tupe nasi mvua.” Maana ya maneno ya ‘Umar (*Innâ kunnâ natawassalu ilayka binabiyyinâ wainnâ natawassalu ilayka bi’ammi nabiyyinâ*) aliyokuwa akiyasema ni: “Tulikuwa tumezoeya kwenda kwa Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) tukimuomba atuombee sisi, na tukijikurubisha kwa Allâh kwa njia ya kutuombea kwake, na kwa vile sasa yeye (صلى الله عليه وسلم) ameshatuacha na kwenda kuwa pamoja na Malaika wa juu zaidi na imekuwa haiwezekani sasa kwake kutuombea sisi, ndio sasa tumekwenda kwa mjombake Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم), al-‘Abbâs, tukamuomba atuombee. Haimaanishi, kwa yakini, yakwamba walikuwa wamezoeya kusema katika maombi yao: ‘Yâ Allâh, kwa jaha ya Mtume Wako, tupe nasi mvua’, na kisha baada ya kufa kwake (صلى الله عليه وسلم) wakisema: ‘Yâ Allâh, kwa jaha ya al-‘Abbâs, tupe nasi mvua’, kwa vile du’â’ hii ni ya uzushi isiyokuwa na dalili wala msingi wowote kutoka kwenye Kitâb na Sunnah, na halikufanywa hilo na hata mmoja miongoni mwa Wema waliotutangulia, na twamuomba Allâh awe radhi nao wote, kama tutakavyoyabainisha kwa kina hivi punde, *Insha-Allâh*.

---

yakwamba Allâh (سبحانه وتعالى) Atatufanyia wepesi katika uchapishaji uliobaki, na kuharakisha hilo, kwani ina nukta nyingi sana za faida ambazo mwanafunzi wa ki-ilimu au mwenye kupenda ‘ilmu ya Fiqhi hawezi kustahamili kuzikosa

[49] Imepokewa na al-Bukhâri (tafsiri: 2/66/no.123 na 5/48/no.59) na ibn Sa’d katika *at-Tabaqât* (4/28-29) na inapatikana katika *Mukhtasarul-Bukhâri* (no.536)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Vilevile kutokana na haya ni aliyoyasema al-Hâfidh ibn Asâkir (رحمه الله) katika târikh yake (18/151/1) kwa silsila ya riwaya iliyo swahîh[50] kutoka kwa *tâbi'î* muheshimiwa Sulaym ibn 'Āmir al-Khabâirî yakwamba: "Mbingu hazikuwa na ishara ya mvua kabisa, basi Mu'âwiyah ibn Abî Sufyân na watu wa Damascus wakenda nje ya mji kwa swala ya mvua. Mara pindi Mu'âwiyah alipokaa juu ya minbar, alisema: 'Yuko wapi Yazîd ibn al-Aswad al-Jurashî ?' Watu wakamwita ajitokeze, akaja kwa kupenya-penya baina ya watu. Kisha Mu'âwiyah akamuamrisha apande juu naye akapanda juu ya minbar akakaa kwenye miguu yake. Kisha akasema Mu'âwiyah: "Yâ Allâh, leo hii sisi twamuomba aliye mbora na aliye na fadhla kubwa miongoni mwetu atuombee sisi kutoka Kwako, Yâ Allâh leo twamueka Yazîd ibn al-Aswad al-Jurashî mbele ili atuombee sisi kutoka Kwako, Ewe Yazîd muinulie Allâh mikono yako." Basi akainua mikono yake na watu nao wakainua mikono yao. Kisha, kwa haraka sana wingu la mvua kama ngao kubwa likaja kwa haraka kutoka upande wa magharibi, na upepo ukaanza kuvuma, mara kukaanza kunyesha kwa wingi mpaka watu wakashindwa kwenda majumbani mwao."

Ibn Asâkir vilevile amepokea kwa silsila ya riwaya iliyo swahîh yakwamba adh-Dhahhâk ibn Qays alikwenda pamoja na watu kwa swala ya mvua, naye pia akamwambia Yazîd ibn al-Aswad: 'Hebu simama ewe mwenye kulia sana!' na katika riwaya nyengine: "Basi akaomba kwa mara tatu peke yake kabla ya kunyesha mvua kubwa sana kiyasi cha kuwazamisha."

Tukampata tena Mu'âwiyah (رضي الله عنه) akiwacha kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa sababu iliyotangulia, bali alikuwa akitumia maombi ya huyo mtu mwema, Yazîd ibn al-Aswad (رحمه‌الله‌تعالى) kama njia ya *tawassul*. Basi akamswihi aombe kwa Allâh (تعالى) yakwamba awabariki kwa mvua. Kisha Allâh (تبارك وتعالى), akayajibu maombi yake, na likatokea tena jambo kama hilo katika utawala wa adh-Dhahhâk ibn Qays.

[50] Vilevile al-Hâfidh al-Asqalâni akainasibisha katika *al-Isâbah* (3/634) kwa Abû Zur'ah ad-Dimashqî' na Ya'qûb ibn Sufyân kwenye târikh yake kwa silsila ya riwaya iliyo swahîh kutoka kwa Sulaym ibn Āmir.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

UBATILI NA MAKOSA YA *KU-TAWASSAL* KWA NJIA NYENGINE YOYOTE ISIYOKUWA NJIA TATU ZILIZOTANGULIA

Kwahivyo kutokana na yaliyotangulia umeshafahamu yakwamba *tawassul* ya ki-sheriya, ambayo iliyothibitishwa na *nass* (maandiko) ya Kitâb na Sunnah, na ambayo iliyothibitishwa na mafundisho ya '*wema waliotutangulia*', na ambayo iliyoegemezwa juu ya muafaka (*ijmâ'*) wa waislamu ni:

1. *TAWASSUL* kwa njia ya kutumia Jina miongoni mwa Majina ya Allâh (تبارك وتعالى) na kutumia Sifa miongoni mwa sifa Zake.

2. *TAWASSUL* kwa njia ya kutumia kitendo chema ambacho alichokifanya mwenye kuomba.

3. *TAWASSUL* kwa njia ya Du'â' inayo–ombwa na mtu mwema.

Amma kuhusisha lolote jengine mbali na sampuli hizi za *tawassul*, basi kuna ikhtilafu, na tunayoitakidi sisi kwa yakini na kushikilia kuwa ndiyo dini yetu mbele ya Allâh (تعالى), ni kwamba njia nyengine zote hazikubaliwi, wala hazikufaradhishwa. Hii ni kwa sababu hakuna dalili inayokubalika kwazo, na mambo haya yameshazungumziwa na kusimamishiwa hoja na wanavyuoni wachanganuzi kwa karne za kufuatana katika historiya ya Uislamu. Hata ingawaje baadhi yake zimekubaliwa na baadhi ya wanavyuoni, kwahivyo [kwa mfano], Imâm Ahmad aliruhusu *tawassul* kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) peke yake, na wengine kama vile Imâm ash-Shawkâni aliruhusu *tawassul* kwa njia yake pamoja na Mitume wengine na watu wema. Lakini hata hivyo, sisi, kama ilivyo hali katika mas'ala yote ambapo kunapopatikana ikhtilafu, hufuata lolote linaloungwa mkono na dalili, lolote liwalo, bila ya kushikilia ki-upofu rai za watu. Sisi hatuungi mkono jambo lolote isipokuwa kwa haki. Kwahivyo kuhusiana na suala la *tawassul*, ambalo tunalolijadili hivi sasa, basi tunaona yakwamba haki iko pamoja na wenye kuonya dhidi ya *tawassul* kwa njia ya kumtumia kiumbe yoyote, na sisi tunatahadharisha dhidi ya *tawassul* kwa njia ya kumtumia kiumbe yoyote. Kwa hakika, hawawezi kupata

jambo lolote lenye kuwaunga mkono waliyoshikilia isipokuwa shaka wanazoleta na kuwepo uwezekano ambao tutakaoujibu hivi karibuni.

Kwahivyo tunapata du'â' nyingi katika Qur'ân Tukufu, na hatupati yoyote ambayo ina *tawassul* kwa njia ya jaha, utukufu, haki au daraja ya kiumbe chochote. Hizi hapa ni baadhi ya *du'â' karîmah* kama mfano tu. Mola wetu (جلّ شئنه), akitufundisha na kutuongoza jinsi ya kuomba maombi yetu:

لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفۡسًا إِلَّا وُسۡعَهَاۚ لَهَا مَا كَسَبَتۡ وَعَلَيۡهَا مَا ٱكۡتَسَبَتۡۗ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذۡنَآ إِن نَّسِينَآ أَوۡ أَخۡطَأۡنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تَحۡمِلۡ عَلَيۡنَآ إِصۡرٗا كَمَا حَمَلۡتَهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلۡنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِۦۖ وَٱعۡفُ عَنَّا وَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَآۚ أَنتَ مَوۡلَىٰنَا فَٱنصُرۡنَا عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ ٢٨٦

"Allâh haikalifishi nafsi yoyote ila yaliyo sawa na uweza wake. (Faida ya) yale aliyoyachuma (hiyo nafsi) ni yake na hasara ya yale iliyoyachuma ni juu yake. (Husema): "Mola wetu! Usitutese kama tukisahau (tukaacha yaliyo mema) au tukikosa (tukafanya mabaya). Mola wetu! Na usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu! Usitutwike tusiyoyaweza, na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tusaidie juu ya watu makafiri."[51]

Akasema:

وَمِنۡهُم مَّن يَقُولُ رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِي ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ حَسَنَةٗ وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ٢٠١

[51] Al-Baqarah (2):286

“Na miongoni mwao wako wasemao: “Mola weu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera, na utulinde na adhabu ya Moto.”[52]

Akasema:

فَقَالُواْ عَلَى ٱللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ٨٥ وَنَجِّنَا
بِرَحْمَتِكَ مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلْكَٰفِرِينَ ٨٦

“Wakasema: ‘Tunamtegemea Allâh. Ee Mola wetu! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu. Na utuokoe kwa rehma Yako na hao watu makafiri.”[53]

Akasema:

رَبِّ ٱجْعَلْنِي مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي ۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ ٤٠ رَبَّنَا ٱغْفِرْ لِي
وَلِوَٰلِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ ٱلْحِسَابُ ٤١

“Na (kumbukeni) aliposema Ibrâhim: ‘Mola wangu! Ujaaliye Mji huu (wa Makkah) uwe wa amani. Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu. Mola wangu! Nijaaliye niwe msimamishaji Swala, na kizazi changu (pia kiwe hivi) Mola wetu! Na upokee maombi yangu (mengine). Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili na wanaoamini; siku ya kusimama hisabu (Kiama).”[54]

Akasema, kwa ulimi wa Mûsa (عليه السلام):

قَالَ رَبِّ ٱشْرَحْ لِي صَدْرِي ٢٥ وَيَسِّرْ لِيٓ أَمْرِي ٢٦ وَٱحْلُلْ عُقْدَةً مِّن لِّسَانِي
٢٧

“(Mûsa) Akasema: ‘Ewe Mola wangu! Nipanulie, (nikunjulie) kifua changu (niweze kustahamili balaa zitakazonifika). Na

[52] Al-Baqarah (2):201
[53] Yûnus (10):85-86
[54] Ibrâhîm (14): 35 na 40-41

unifanyie sahali kazi yangu (hii uliyonipa). Na ufungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu (nitakayowaambia).”[55]

Akasema (سبحانه):

وَٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱصۡرِفۡ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ٦٥

“Na wale wanaosema: ‘Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannam, bila ya shaka adhabu yake ni yenye kuendelea.”[56]

Kuna du’â’ nyengine Tukufu za Qur’ân nyingi, baadhi zake ni du’â’ ambazo Allâh (تعالى) alizotufundisha tumlinganie nazo, nyenginezo ni du’â’ ambazo alizotuteremshia kupitia kwa baadhi ya Mitume Wake na Manabii, au baadhi ya waja wake na watu wema awapendao, na ni dhahiri yakwamba hapana yoyote iliyo na sampuli yoyote ya *tawassul* za uzushi ambazo walizozishikilia wafuasi vipofu na ambazo washindani huzitafutia huja na kuleta ugomvi. Kisha tukiziangalia Sunnah Takatifu katika kutafuta du’â’ ambazo alizokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiziomba na ambazo Allâh alizokuwa radhi nazo na alizomfundisha kuomba, na yeye kwa upande wake akatuongoza kwenye fadhla zake na uzuri wake, na utakuta yakwamba zinalingana kikamilifu na du’â’za Qur’ân tulizozitaja hapo juu, kwa kuwa vilevile zimeepukana na *tawassul* zozote za uzushi tulizozitaja.

Sasa zifuatazo ni baadhi ya hizo du’â’ za Mitume: Miongoni mwazo ni *Du’âul Istikhâra* (du’â’ za kumuomba Allâh msaada na uongofu kuhusu jambo) iliyo maarufu mno na ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwafundisha Maswahaba zake, pindi mmojawao anapokusudia kufanya jambo, kama ambavyo alivyokuwa akiwafundisha Qur’ân, nayo ni:

[55] Twâ Hâ (20): 25-27
[56] Al-Furqân (25):65

« اللهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِيرُكَ بِعِلْمِكَ، وَأَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ، فَإِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا أَقْدِرُ، وَتَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ، وَأَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ، اللهُمَّ إِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ (ثُمَّ يُسَمِّيهِ) خَيْرٌ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي، وَعَاجِلِه وآجِلِه، فَاقْدُرْهُ لِي وَيَسِّرْهُ لِي ، ثُمَّ بَارِكْ لِي فِيهِ، وَإِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ (ثُمَّ يُسَمِّيهِ) شَرٌّ لِي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أَمْرِي، وَعَاجِلِه وآجِلِه، فاصْرِفْهُ عَنِّي وَاصْرِفْنِي عَنْهُ ، وَاقْدُرْ لِي الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ، ثُمَّ رَضِّنِي بِهِ »

“Yâ Allâh! nakuomba uongofu Wako kwa kupitia kwenye ‘ilmu Yako, na nakuomba usaidizi wako kupitia kwenye kudra Zako, na nakuomba kutokamana na fadhla Zako kubwa. Kwa hakika Wewe ni Muweza na mimi si muweza, Wewe unajua na mimi sijui, na Wewe unajua yote yaliyofichikana.Yâ Allâh! Iwapo Wewe unajua yakwamba jambo hili ni kheri kwangu mimi (na hapa atataja mahitaji yake) katika dini yangu, na maisha yangu ya kidunia, na akhera yangu, na hali yangu ya sasa na ijayo, basi nikadiriye na unirahisishiye, kisha unibarikie nalo. Na Iwapo Wewe unajua yakwamba jambo hili ni shari kwangu mimi (na hapa atataja mahitaji yake) katika dini yangu, na maisha yangu ya kidunia, na akhera yangu, na hali yangu ya sasa na ijayo, basi niepushie na unigeuze mbali nalo, na unikadirie lolote zuri kwangu popote lilipo, kisha unibarikie nalo.”[57]

Vilevile kutokamana na hizo ni du’â’ yake:

« اللهُمَّ أَصْلِحْ لِي دِينِي الَّذِي هُوَ عِصْمَةُ أَمْرِي، و ـأَصْلِحْ لِي دُنْيَايَ الَّتِي فِيهَا مَعَاشِي، وَأَصْلِحْ لِي آخِرَتِي الَّتِي فِيهَا مَعَادِي، وَاجْعَلِ الْحَيَاةَ زِيَادَةً لِي فِي كُلِّ خَيْرٍ، وَاجْعَلِ الْمَوْتَ رَاحَةً لِي مِنْ كُلِّ شَرٍّ »

[57] Imepokewa na al-Bukhâri (tafsiri 2/146/no.263) [vilevile tizama katika *Du’â’ za Mtume zilizo swahih* cha Walîd al-Îssa (no.123)]

“Yâ Allâh! Nisahilishie mimi dini yangu ambayo ndiyo kinga ya mambo yangu, na unisahilishie dunia yangu ambayo ndipo penye maisha yangu, na unisahilishie Akhera yangu ambayo ndipo mahali pangu pa Akhera, na uyaja’aliye maisha yangu kuwa ni penye kunizidishiya katika kila la kheri, na uyaja’aliye mauti kuwa ni raha kwangu kutokana na kila la shari.[58]

« اللَّهُمَّ بِعِلْمِكَ الْغَيْبَ وَقُدْرَتِكَ عَلَى الْخَلْقِ، أَحْيِنِي مَا عَلِمْتَ الْحَيَاةَ خَيْرًا لِي، وَتَوَفَّنِي إِذَا عَلِمْتَ الْوَفَاةَ خَيْرًا لِي... »

“Yâ Allâh! Kutokana na ‘ilmu Yako iliyofichikana na uwezo wako juu ya viumbe, nipe uhai maadamu Wewe wajua yakuwa uhai wangu una kheri na mimi, na unifishe maadamu Wewe unajua yakuwa mauti ni kheri kwangu...”[59]

« اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْهُدَى وَالتُّقَى وَالْعَفَافَ وَالْغِنَى »

“Yâ Allâh! Hakika yangu mimi nakuomba uongofu, na ucha-Mungu na usafi wa moyo na kutosheka.”[60]

« اللَّهُمَّ اقْسِمْ لَنَا مِنْ خَشْيَتِكَ مَا تَحُولُ بِهِ بَيْنَنَا وَبَيْنَ مَعَاصِيكَ، وَمِنْ طَاعَتِكَ مَا تُبَلِّغُنَا بِهِ جَنَّتَكَ ... »

“Yâ Allâh! Tugawiye nasi katika ucha-Mungu utakaokuwa ni wenye kutulinda baina yetu na kuku’asi Wewe, na katika twa’a itakayotupeleka kuifikia Pepo Yako...”[61]

« اللهُمَّ رَبَّ جِبْرِيلَ، وَمِيكَائِيلَ، وَإِسْرَافِيلَ، وَمُحَمَّدٍ نَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ»

---

[58] Imepokewa na Muslim (tafsiri 4/1425/6565)

[59] Imepokewa na an-Nasâ’i kwa silsila ya riwaya iliyo swahih. [*Du’â’ zilizo swahih* no.104]

[60] Imepokewa na Muslim (tafsiri 4/1425/6566)

[61] Imepokewa na at-Tirmidhi aliyeitangaza kuwa ni hasan na ni kama alivyosema. [*Du’â’ zilizo swahih* no.253]

Yâ Allâh! Mola wa Jibrîl, na Mikâ'îl, na Isrâfîl, na Muhammad, twajilinda Kwako kutokamana na Moto."[62]

Kuna maombi mengi kama haya katika Sunnah, haliyakuwa hatupati hata mfano mmoja ulio swahîh katika *tawassul* za uzushi zinazotumiwa na wapinzani.

Kwa yakini, jambo la kushangaza mno ni kwamba utawaona watu hawa wakiziepuka sampuli za *tawassul* zilizotangulia, ambazo ni swahîh na zilizofaradhishwa. Wao huwa hawatumii chochote kutokamana nazo katika maombi yao au pindi wanapowafundisha watu, licha ya uhakika yakwamba zimethibitishwa kwenye Kitâb, Sunnah na muafaka wa Ummah. Lakini badala ya haya utawaona wakitumia maombi waliyoyazua wao na kutumia sampuli za *tawassul* walizozizua na ambazo hatukufaradhishiwa na Allâh (عزّ وجلّ), wala hazikutumiwa na Mjumbe Wake mteule (صلى الله عليه وسلم), wala hazikupokewa na wema waliotutangulia (*salaf as-swâlih*) miongoni mwa Ummah huu, watu wa karne tatu zilizosifiwa, na jambo bora linaloweza kusemwa kuhusu sampuli zao za *tawassul* ni kwamba hayo ni mambo ambayo yenye ikhtilafu. Sasa angalia jinsi watu hawa wanavyostahiki katika maneno ya Allâh (تبارك وتعالى):

أَتَسْتَبْدِلُونَ ٱلَّذِى هُوَ أَدْنَىٰ بِٱلَّذِى هُوَ خَيْرٌ ۚ ٦١

"Mnabadili vitu duni kwa vile vilivyo bora?"[63]

Kwahivyo, labda hili ni mojawapo ya ushahidi wa kwenye ukweli aliousema muheshimiwa *Tâbi'i,* Hassan ibn 'Atiyyah al-Muhâribî (رحمه الله): "Hapana watu wanaoanzisha uzushi kwenye dini yao isipokuwa Allâh atawaondolea kiwango cha Sunnah kinachofanana nao (huo uzushi), na hatowaregeshea mpaka Siku ya Kiyama."[64]

---

[62] Imepokewa na al-Hâkim na at-Twabarâni kwa silsila ya riwaya ambayo ni hasan kutokana na kuungwa mkono kama nilivyoyaeleza katika as-Swahîha (no.1544)

[63] Al-Baqarah (2):61

[64] Imepokewa kutoka kwake na ad-Dârimi (1/45) na silsila ya riwaya yake ni swahîh.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Sisi hatuko peke-yetu katika kuzikosoa hizi sampuli za uzushi za *tawassul*, bali ma-Imâm wakubwa na wanavyuoni waliotangulia walitutangulia sisi katika ukosoaji huo, na haya vilevile yamethibitishwa kwenye angalau mojawapo ya madh-hab ambayo watu huifuata, nayo ni madh-hab ya Imâm Abû Hanifah (رحمه الله).

Imepatikana katika *ad-Durrul-Mukhtâr* (2/630), nacho ni mojawapo ya vitabu mashuhuri vya ma-Hanafî: "Kutoka kwa Abû Hanifah: Haifai kabisa kwa mtu yoyote kumuomba Allâh isipokuwa kwake Yeye, na kutumia sampuli kama hizo za maombi kama zilivyoruhusiwa na kuamrishwa kwa mfano wa maneno ya Allâh (تعالى):

وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا ۖ ١٨٠

"Na Allâh ana Majina mazuri mazuri; muombeni kwayo."[65]

Mfano wake vilevile unapatikana katika *al-Fatâwal-Hindiyyah* (5/280), na *al-Qudûrî*[66] amesema katika Kitabu chake kikubwa cha *Fiqhi* kiitwacho *Sharhul-Kurkhiy* kwenye mlango wa mambo yenye kuchukiza: "Amesema Bishr ibn al-Walîd: Abû Yusuf ametusimulia, yakwamba amesema Abû Hanifah: "Si sawa kwa mtu yoyote kumuomba Allâh isipokuwa amuombe Yeye, na inanichukiza kwa mtu yoyote anaposema: 'Kwa Utukufu wa Kiti chako', au 'Kwa haki ya kiumbe chako.'" Vilevile huu ndio msemo wa Abû Yusuf. Amesema Abû Yusuf: "Mwenye kukipa utukufu Kiti ni Allâh, kwahivyo mimi sichukii hilo, bali ninalolichukia mimi ni mtu kusema: 'Kwa haki ya fulani na fulani', au 'Kwa haki ya Mitume Yako na Manabii' au 'Kwa haki ya Nyumba takatifu na sehemu takatifu (ya *Muzdalifa*)."

Amesema *al-Qudûrî*: "Kumuomba Yeye kwa (kupitia kwa) viumbe vyake hairuhusiwi kwani kiumbe hana haki mbele ya Muumba, kwahivyo haiwezi kukubalika." Imenukuliwa kutoka kwa ibn Taymiyyah katika *al-Qâ'idatul Jaliyyah*.

Amesema az-Zubaydi katika *Sharhul-Ihyâ'* (2/285): "Abû Hanifah na marafiki zake wawili wanachukia kumsikiya mtu akisema:

---

[65] Surah al-A'râf: (7):180

[66] Yeye ni Abul Hassan Ahmad ibn Muhammad ibn Ja'far ibn Hamdân, mwanachuoni wa Fiqhi, naye alikuwa ni mwalimu wa al-Khatîb al-Baghdâdî. Alizaliwa katika mwaka wa 362H, na akafa 428H.

‘Nakuomba Wewe kwa haki ya fulani na fulani’, au ‘Kwa haki ya Mitume Wako na Manabii Wako’, au ‘Kwa haki ya Nyumba Takatifu na sehemu Takatifu (ya *Muzdalifa*)’, na mfano wake kwani hakuna yoyote mwenye haki mbele ya Allâh. Vilevile Abû Hanifah na Muhammad [ibn Hassan ash-Shaybâni] anachukia kumsikiya mtu mwenye kuomba Du’â’ akisema: ‘Yâ Allâh! Nakuomba kwa Utukufu wa Kiti chako’ na imeruhusiwa na Abû Yusuf kutokana na riwaya iliyomfikia.”[67]

---

[67] Nimezinukuu idadi ya riwaya hizi kwani wafuasi wengi wa ki-Upofu wa madh-hab ya Hanafî na wengineo wanakataa uswahihi wa maneno haya kuwa ni kauli ya Abû Hanifah (رحمه الله). Kwahivyo ikiwa mfano wa riwaya hii haukuthubutu kutoka kwake, basi hakuna chochote kinachoweza kuthibitishwa kutoka kwake katika vitabu vya Fiqhi, kama ambavyo haiwezi kufichika kwa mwanachuoni yoyote anayetambua jinsi ambayo kauli za wanavyuoni wa ki-Hanafi zinavyopokewa katika vitabu vya madh-hab yao. Kisha inashangaza mno jinsi baadhi yao, pindi wanapokabiliwa na kauli hizi za Abû Hanifah, husema waziwazi yakwamba wao hawakufungwa katika kuzikubali kauli zake hizo kwani kuna ahâdîth zilizo swahih zenye kuonyesha, kama wanavyodai, yakwamba mtu anaweza kumlingania Allâh kwa njia ya asiyekuwa Allâh, kama ilivyotokea katika hadîth ya watu wa pangoni na hadîth ya Buraydah. Ahâdîth hizi mbili zimetangulia na tumezitolea ufafanuzi wa sawa. Kisha wao wanasema hivyo, licha ya uhakika yakwamba mifumo yao na njia zinazofahamika vyema ni kwamba wao wamezama kwenye *taqlîd* (kufuata ki-upofu) mpaka kwenye masikio yao, na huipa nyongo hadîth yoyote inayokhitilafiana na madh-hab yao, hata kama hadîth ina silsila ya upokezi iliyo swahîh na maana yake ikawa ya wazi. Sasa itakuwaje hapa yakwamba wanageukia kwenye mfumo wetu inapokuwa njia ya kutujibu sisi kwa kutumia madh-hab yao imefungwa? Jee, huku ni kuchanganyikiwa kwao au ni kuzembea kwao, au ni kwamba:

يَقُولُونَ بِأَلْسِنَتِهِم مَّا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ ۚ ١١

“Wanasema kwa ndimi zao (maneno) yasiyokuwamo nyoyoni mwao.” [Surah Al-Fat-h (48):11]

Kwa ajili tu ya kuikataa haki iliyosemwa na Imâm wa madh-hab yao, kwa sababu imetokea yakwamba ameafikiyana na tunayowalingania wao kuhusiana na kuwachana na kutumia njia ya *tawassul* kwa kutumia watu na kufanya *tawassul* kwa Allâh (سبحانه وتعالى) na Sifa zake. Sasa kwani wamejitayarisha kuchukuwa msimamo juu ya ahâdîth zilizo swahîh kuwa ndiwo mfumo wao katika *Fiqhi* zao zote, ili baadae na sisi tuwatake wafuate

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Hata hivyo, riwaya iliyotajwa haina msingi wowote, na wala si swahîh. Ameinukuu Ibn al-Jawzî katika *al-Mawdhû'ât* na akasema: "Hadîth hii imezuliwa na shaka." Kisha al-Hâfidh az-Zayla'î akaafikiana naye katika *Nasbur-Râyah* (4/273) kwahivyo haiwezekani kutumiwa kama dalili. Kisha ikiwa kauli ya mtu: 'Nakuomba Wewe kwa utukufu wa Kiti Chako' ni katika *tawassul* ya asili kwa kupitia katika mojawapo ya Sifa za Allâh, basi hiyo ni sampuli ya *tawassul* iliyofaradhishwa kama ilivyo bainishwa na dalili nyengine nyingi, kama ilivyotangulia. Kwahivyo hapana haja ya hadîth hii ya kuzuliwa. Amesema Ibnul-Athîr (رحمه الله): "Nakuomba Wewe kwa (asili ya) utukufu wa Kiti Chako. Yaani kwa sifa hizo zenye kukipa Kiti Utukufu wake, au katika sehemu ambazo utukufu ulipowekwa. Maana yake kwa uhakika ni: 'Kwa utukufu wa Kiti Chako', na marafiki wa Abû Hanifah wanachukia kauli kama hii katika maombi.' Kwahivyo juu ya ufafanuzi wa kwanza, yakwamba ilikuwa ikihusu tabia yenye kukipa Kiti utukufu wake, hapo itakuwa ni *tawassul* kwa njia ya Sifa za Allâh (تعالى), na itakuwa ni yenye kuruhusiwa. Lakini katika ufafanuzi wa pili, yakwamba inazihusu sehemu za Kiti ambapo utukufu ulipowekwa,

---

ma-kumi ya, au bali ma-Mia ya ahâdîth zilizo swahîh wanazozipinga kwa kuzipendelea madh-hab zao? Katika hali hiyo, rai zao na rai zetu zitaafikiyana. Au hali yao itakuwa ni kufuata hadîth tu na kukhalifu madh-hab iwapo hayo yatafuatana na mapendelewa ya nafsi zao na maslahi yao, na kwamba watashikamana na madh-hab na kupinga hadîth, ikiwa haikupatikana kwa hadîth kutosheleza mapendelewa ya nafsi zao! Ama kutafuta kwao kutaka kutumia hadîth ya Buraydah na hadîth ya watu wa pangoni kama dalili, basi hilo limekataliwa, kwani zote hizo mbili zinaonyesha waziwazi yakwamba *tawassul* kwa njia ya kutumia vitendo vyema, ambavyo ndivyo ushuhuda wa Tawhîd katika hadîth ya kwanza; na kuwatendea wema wazazi wawili, kuzuiya kutokamana na yaliyokatazwa na kuamiliyana na mfanyi kazi kwa uadilifu katika hadîth ya pili, na huu ndiwo msimamo wetu, na wala sisi hatugandami ki-upofu kwenye kauli zilizotangulia za Abû Hanifah ambazo kudhihirika kwake zinazuiya sampuli hii ya *tawassul*. Wala si wajibu juu yetu kushikilia hilo iwapo itakwenda kinyume na hadîth, kwani msimamo wetu ni kwamba hadîth tunaipa kipa-umbele kuliko kauli yake. Kwahivyo ikhtilafu baina yetu na wafuasi vipofu ni kutokana na haya, ambao wanaoubainisha ulinganizi wao kuwa ni *tawassul* 'du'â' ya kumlingania Allâh kwa kupitia kwa asiyekuwa Yeye', basi hiki ni mojawapo ya vitendo vya batili vya ufichaji wa haki, na makosa yao ya dhahiri kama ambavyo hautofichika kwa watu wenye ufahamu.

hapo itakuwa ni *tawassul* kwa njia ya kitu kilichoumbwa na hiyo hairuhusiwi. Kwa hali yoyote iwayo, hadîth hii haistahiki kujadiliwa zaidi na kufafanuliwa kwa vile haikuswihi (si swahîh), kwahivyo tunatosheka na yaliyotangulia.

MLANGO WA NNE

SHAKA ZILIZOLETWA NA JAWABU ZAKE

Wenye kukhalifu maudhui haya wameleta idadi ya vipingamizi na shaka (*shubuhât*) nyingi katika mas'ala haya kwa ajili ya kutafuta njia za kuyatilia nguvu maoni yao ya kimakosa, na kuwasababisha watu wa kawaida wayaamini kuwa ni ya kweli, na kuficha ukweli wa mambo kutoka kwao. Mimi nitazinukuu shaka hizo, katika yafuatayo, moja baada ya jengine, nikiwajibu kwa jawabu ambazo zitakazolingana na misingi ya ki-ilimu na ushawishi apendapo Allâh. Jambo hili litatilia nguvu yaliyothibitishwa kwenye mlango uliotangulia. Litamtosheleza yoyote mwenye uaminifu na uadilifu, na kuwakosoa wote wenye kuzua madai ya urongo dhidi yetu, na taufiki inatokamana na Allâh (تعالى) peke Yake, Naye ndiye Mwenye kuombwa msaada.

❖ SHAKA YA KWANZA

HADÎTH INAYOELEZA JINSI 'UMAR ALIVYOKUWA AKIMTAKA AL-'ABBĀS (رضي الله عنهما) AWAOMBEE MVUA

Wanatumia, kama ushahidi wa kuruhusiwa kwa *tawassul* kwa njia ya jaha ya mtu, utukufu na haki, hadîth ya Anas iliyotangulia:

أَنَّ عُمَرَ بْنَ الخَطَّابِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، كَانَ إِذَا قَحَطُوا اسْتَسْقَى بِالعَبَّاسِ بْنِ عَبْدِ المُطَّلِبِ ، فَقَالَ: « اللَّهُمَّ إِنَّا كُنَّا نَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ بِنَبِيِّنَا فَتَسْقِينَا، وَإِنَّا نَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ بِعَمِّ نَبِيِّنَا فَاسْقِنَا » قَالَ: فَيُسْقَوْنَ.

Yakwamba ‘Umar ibn al-Khattwâb (رضي الله عنه), katika nyakati za ukame alikuwa akimtaka al-‘Abbâs ibn ‘Abdul-Muttwalib aombe mvua kwa niyaba yao. Alikuwa yeye mwenyewe akisema: “Yâ Allâh tulikuwa tukimtaka Mtume Wako atuombee mvua kwa niyaba yetu kutoka Kwako na Wewe ulikuwa ukitubariki kwa mvua. Sasa twamtaka mjombake Mtume wetu atuombee kutoka Kwako kwa niyaba yetu, basi tupe nasi mvua.” Akasema: “Basi walikuwa wakibarikiwa na mvua.”[68]

Kwahivyo walifahamu kutokana na hadîth hii yakwamba, ‘Umar ibn al-Khattwâb (رضي الله عنه), alikuwa akitumia jaha ya al-‘Abbâs (رضي الله عنه), kama njia ya *tawassul*, na daraja yake mbele ya Allâh. Utadhani kana kwamba *tawassul* yake ilikuwa ni kulitaja jina la al-‘Abbâs tu katika maombi yake na kumuomba Allâh awape mvua kwa sababu ya hilo. Vilevile yakwamba na Maswahaba nao wakalikubalia hilo, kwahivyo jambo hili, kulingana na madai yao, linathibitisha msimamo wao. Ama kuhusu sababu ya kwanini ‘Umar (رضي الله عنه) aliwacha kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na badala yake akatumia *tawassul* kupitia kwa al-‘Abbâs (رضي الله عنه), basi wanadai yakwamba hilo lilikuwa ni kwa sababu tu ya kuonyesha uhalali wa kufanya *tawassul* kwa njia ya kupitia kwa mtu mwenye fadhla, hata kama ingawaje palikuwa na wengine waliokuwa na fadhla zaidi kuliko yeye.

Fikra yao hii ni ya makosa, na ufafanuzi wao unakataliwa kutokana na sababu nyingi, muhimu zaidi miongoni mwazo zikiwa:

[68] Imepokewa na al-Bukhâri na wengine.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

1. Msingi muhimu sana katika Sharia ya ki-Islamu ni kwamba maandiko ya ki-Sharia ni yenye kutafsiriana, na hapana baina yake zinazoweza kufahamika kuhusu suala fulani kando na maandiko mengine yenye uhusiano yaliyopokewa pamoja. Sasa juu ya msingi huu, hadîth iliyotangulia kuhusu *tawassul* ya 'Umar inatakiwa ifahamike kwa muangaza wa riwaya nyengine zilizothubutu na *ahâdîth* zilizopokewa kuhusiana na *tawassul*, baada ya kukusanywa pamoja na kuchambuliwa. Kisha sisi pamoja na wahasimu wetu tumekubaliana yakwamba kuna *kitendawili*[69] katika maneno ya 'Umar: "Tulikuwa na mazoweya ya kukufanyia *tawassul* Wewe kwa njia ya kumtumia Mtume wetu... na sasa twakufanyia Wewe *tawassul* kwa njia ya Mjombake Mtume wetu," na vilevile *kitendawili* hiki hakina budi kiwe na maana yake: "Tulikuwa na mazoweya ya kukufanyia Wewe *tawassul* kwa njia ya (jaha ya) Mtume wetu... lakini sasa twakufanyia Wewe *tawassul* kwa njia ya (jaha ya) Mjombake Mtume wetu', kulingana na rai yao, au "Tulikuwa na mazoweya ya kukufanyia *tawassul* Wewe kwa njia ya (maombi ya) Mtume wetu... lakini sasa twakufanyia Wewe *tawassul* kwa njia ya (maombi ya) Mjombake Mtume wetu', kulingana na rai yetu. Sasa mojawapo ya maana hizi mbili yenye uwezekano ni lazima ichukuliwe katika kutaka kufahamu waziwazi linalosemwa.

Kisha, ili tujue ni ipi iliyo sawa baina ya maana hizi mbili yenye uwezekano ni lazima turejee kwenye Sunnah kwa ajili ya kujionea ni njia ipi ya *tawassul* kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) iliwahi kutumiwa na Maswahaba watukufu. Tunahitaji kuangalia ili tuone iwapo, pindi walipopata maafa ya ukame, kila mmoja wao alijikalia nyumbani kwake, au mahali pengine popote, au waliitana pamoja, bila ya kuwepo Mtume (صلى الله عليه وسلم) kisha wakaomba kwa Mola wao, wakisema: 'Yâ Allâh! Kwa (ajili ya) Mtume Wako Muhammad, na kwa jaha yake Kwako Wewe, na kwa daraja yake mbele Yako, tubariki nasi kwa mvua,' kwa mfano, au iwapo walikuwa wakija kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwepo hai na wakimtaka awaombee wao kwa Allâh (تعالى), na kisha yakwamba alikuwa akikubaliana na matakwa yao na akiomba kwa Mola Wake kwa unyenyekevu uliokamilika mpaka walipobarikiwa na mvua.

---

[69] **Maneno ya Mfasiri**: *Yaani*; Maneno ambayo hayakutamkwa yenye maana yanayofahamika katika kubainisha maana kamili ya kifungu cha maneno.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Amma kuhusu la kwanza katika mas'ala haya basi hilo halipatikani popote katika hadîth Takatifu za ki-Utume, wala katika mafundisho ya Maswahaba watukufu (رضوان الله عليهم), na hakuna njia yoyote yakwamba yoyote miongoni mwa wapinzani wa njia ya Wema Waliotutangulia wala wafuasi wa U-sufi atakaeweza kuleta dalili ya kuthibitisha yakwamba *tawassul* yao ilikuwa ni kulitaja jina la Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika maombi yao na kuweka matakwa kwa Allâh kwa haki yake na daraja yake mbele ya Allâh. Bali mifano mengi tunayoikuta, na ambayo vitabu vya Sunnah vilivyojaa, ni suala la pili. Kwahivyo tutakuta yakwamba njia ambayo Maswahaba watukufu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walivyotekeleza *tawassul* ni kwamba pindi walipokuwa na haja, au walitaraji kuondolewa dhiki zilizowakumba, walikuwa wakimuendea (صلى الله عليه وسلم) na wakimuuliza ana kwa ana awaombee kwa Mola wake kwa niyaba yao, *yaani;* walitumia du'â' ya Mtume mtukufu (صلى الله عليه وسلم) kama njia ya kujikurubisha (*tawassul*) kwa Allâh (تعالى), wala hakuna jengine lisilokuwa hilo. Vilevile tumeelekezwa kwenye jambo hili kwa kauli ya Allâh (تبارك وتعالى):

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوٓاْ أَنفُسَهُمْ جَآءُوكَ فَٱسْتَغْفَرُواْ ٱللَّهَ وَٱسْتَغْفَرَ لَهُمُ ٱلرَّسُولُ لَوَجَدُواْ ٱللَّهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ٦٤

"Na lau wangalikuja walipojidhulumu nafsi zao (kwa kwenda kuhukumiwa kwa njia isiyokuwa ya Sharia) wakaomba msamaha kwa Allâh, na (yeye) Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Allâh ni Mwenye kupokea toba (na) Mwenye kurehemu."[70]

Mfano wake mwengine ni hadîth ya Anas iliyotangulia inayomtaja Mbedui aliyekuja msikitini katika siku ya ljumaa wakati ambapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akitoa *khutbah*. Kwahivyo aliitaja hali yao ngumu na ukame na vifo vya Ng'ombe wao, na akamwambia amuombe Allâh (سبحانه), awaokoe kutokamana na mashaka yaliyowakumba. Kwahivyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akajibu

[70] Surah an-Nisâ' (4):64

matakwa haya, naye ni kama alivyosifiwa na Mola Wake katika kauli yake:

لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ١٢٨

“Amekufikieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (Na) kwa walioamini ni mpole na mwenye huruma.”[71]

Kwahivyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaombea kwa Mola wake, na Yeye (سبحانه), akajibu maombi ya Mtume wake na akaonyesha Huruma kwa waja wake, na akawamiminia Rehma Zake juu yao, na akahuisha ardhi yao kavu.

Vilevile kutokamana na haya ni kuja tena kwa Mbedui yuleyule au mtu mwengine katika Ijumaa iliyofuata kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akitoa *Khutbah*. Kisha akamlalamikia kuhusu kuharibika kwa barabara, na kubomoka kwa Majumba, kuzama kwa Ng’ombe, na akamtaka aombe kwa Mola wake awazuilie mvua. Kwahivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akafanya hivyo na Mola wake (جلّ شئنه), akamjibu tena maombi yake.

Mfano mwengine wa haya, ni yale ambayo mwanamke mtukufu ‘Āishah (رضي الله عنها), aliyoyasimulia aliposema, “Watu walimlalamikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu ukosefu wa mvua, basi akaagizia kutengezewa minbar iwekwe kwenye uwanja wa kuswalia, na akapanga siku ya watu wajitokeze.” Akasema: “Basi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatoka wakati mviringo wa Jua ulipojitokeza na akaketi juu ya minbar na akatangaza Utukufu wa Allâh, akamsifu Yeye, kisha akasema: *Mumelalamika kuhusu ukame kwenye makaazi yenu, na kuchelewa kwa mvua mwanzoni mwa msimu wake, na Allâh ameamrisha yakwamba mumuombe Yeye, na akaahidi yakwamba Yeye atawajibu maombi yenu...* (hadîth)[72].

---

[71] Surah at-Tawbah (9):128

[72] Imepokewa na Abû Dâwud (tafsiri 1/302/1169), na akasema: “Hadîth hii ni ngeni (*gharîb*) na silsila ya riwaya ni swahîh,” nayo ni kama alivyosema, na

Kwenye hadîth imetajwa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimlingania Allâh (سبحانه) na akawaongoza watu kwenye swala, na kwamba Yeye (تعالى) akawateremshia mvua, mpaka mito ikatiririka mikondo ya maji, na watu wakakimbilia majumbani mwao, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akacheka kiyasi cha kwamba magego yake yakawa yanaonekana na akasema: "Mimi nashuhudia yakwamba Allâh ana Uwezo kamili juu ya kila kitu na kwamba mimi ni mja wa Allâh na Mtume Wake".

Kwahivyo ahâdîth hizi na mfano wake zilizotokea katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na zama za Maswahaba watukufu (رضي الله عنهم), na kubainisha mas'ala bila ya kuwacha nafasi yoyote ya majadiliano au mdahalo, yakwamba *tawassul* inayofanywa kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au watu wema iliyofanywa na Wema Waliotutangulia ilikuwa ni kwamba mwenye kutaka kufanya *tawassul* alikuwa akija kwa mtu ambaye aliyependa kumtumia afanye *tawassul* na alikuwa akitaka amuombee kwa Allâh (سبحانه), ili alipate alilolikusudia. Kwahivyo alikuwa akikubali na kuridhika kwa hilo kisha Allâh (سبحانه وتعالى) alikuwa akijibu maombi yake.

2. Ufafanuzi wa maana ya *tawassul* tulioutoa vilevile ndio ulio maarufu kutokamana na maisha ya watu ya kila siku, kwani awapo mmoja wao anahitaji kitu kutoka kwa *meneja* wa idara, Rais, au yoyote mwenye cheo, kwa mfano, basi atamtafuta mtu yoyote anayemjua ambaye atakayeweza kwenda kwake, azungumze naye na ataje maombi ya yule muhitaji, ili aitekeleze hiyo haja. Kwahivyo huyu mjumbe atasambaza ujumbe wa matakwa yake kwa mwenye mamlaka, ambaye kwa kawaida ndiye atakayelifanya linalohitajika. Hii ndiyo *tawassul* ijulikanayo na Waarabu kuanzia zamani na mapaka sasa hali ni kama hiyo. Kwahivyo iwapo mmoja wao atasema: '*tawassul* ilâ fulân (*nimemfanyia tawassul fulani na fulani*), kisha alichomaanisha ni kwamba alikwenda kwa mtu wa pili akamtajia mahitaji yake, ili naye kisha ende akamtajie mtu mwenye mamlaka, awasilishe matakwa yake na atekelezewe. Hakuna hata mmoja

---

kundi la wanavyuoni wameitangaza kuwa ni swahîh kama nilivyoashiriya katika swahîh Abî Dâwud (no.1064)

atakayefahamu kutokamana na haya yakwamba aliyofanya ni kumuendea mwenye mamlakaa na kumwambia: ‘Kwa haki (ya mjumbe) kwako wewe, na daraja yake kwako wewe, nitekelezee mahitaji yangu.’

Vilevile, *tawassul* kwa Allâh si kwa njia ya dhati ya mtu mwema au jaha yake, lakini ni kwa njia ya maombi yake na unyenyekevu katika kumswihi Allâh (سبحانه وتعالى), na kumtaka msaada Wake kwa dhati. Hii vilevile ndiyo maana ya kauli ya ‘Umar (رضي الله عنه): “Yâ Allâh! Tulikuwa na mazoweya ya kufanya *tawassul* kwako Wewe kwa njia ya Mtume wetu na Wewe ulikuwa ukitubariki kwa mvua...,” kwa maana yakwamba: Pindi ulipotokea ukame, kwa mfano, tulikuwa na mazoweya ya kumuendea Mtume (صلى الله عليه وسلم) ili atuombee kwa Allâh (جلّ شئنه).

3. Hili limezidi kutiliwa mkazo na kubainishwa kwa ukamilifu wa kauli ya ‘Umar (رضي الله عنه): “... na sasa twamuomba mjombake Mtume wetu atuombee kutoka Kwako, basi tupe nasi mvua.” Kwa maana yakwamba baada ya kifo cha Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم), sasa tumekuja na al-‘Abbâs, mjombake Mtume (صلى الله عليه وسلم) na twamtaka atuombee kwa Mola wetu (سبحانه), yakwamba atubariki na mvua.

Amma kuhusu suala la, ni kwa nini ‘Umar (رضي الله عنه) alibadilisha kutoka kwenye njia ya *tawassul* ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) mpaka kwenye *tawassul* ya kupitia kwa njia ya al-‘Abbâs (رضي الله عنه), licha ya uhakika yakwamba hata kama al-‘Abbâs alikuwa na daraja kubwa ya jaha na fadhla, na isitoshe, itakavyokuwa daraja yake haiwezi kupewa kipa-umbele kuliko jaha na fadhla za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Jawabu la suala hilo ni, kwa rai yetu, yakwamba *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni jambo lisilowezekana baada ya kufa kwake, kwani watawezaje kwenda kwake (صلى الله عليه وسلم), waeleze hali yao, na kumtaka awaombee, na kwa wao kuitikia ‘Āmîn, akiwa ameshapita na kwenda kwa rafiki wa Malaika walioko juu zaidi, na kuingia kwenye uhai ulio tafauti kabisa na maisha ya hapa

ulimwenguni na hali ambayo isojulikana na yoyote asiyekuwa Allâh (سبحانه وتعالى) ? Sasa watawezaje kupata fungu la *du'â'* yake na *shifâ'* yake kwao inapokuwa baina yake na wao kunapatikana, kama alivyosema Allâh:

وَمِن وَرَآئِهِم بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ١٠٠

"... na mbele yao kuna maisha ya baada ya kufa (ya tabu kwa wabaya na ya raha kwa wazuri) mpaka siku watakapofufuliwa."[73]

Kwahivyo 'Umar (رضي الله عنه) ambaye asili yake ni Muarabu swafi na ambaye ni Swahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na aliyekuwa akifuatana naye kwa muda mwingi, na aliyemjua sana, na aliyeifahamu sana dini yake, na ambaye kwenye matukio mengi *Āyât* za Qur'ân zilipokuwa zikiteremshwa zilikuwa zikiafikiyana na rai yake; alitumia njia ya *tawassul* ambayo iliyokuwa ni jambo lenye uwezekano, akamchagua al-'Abbâs (رضي الله عنه), kutokana na mkuruba wake wa ujamaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na pia kwa ajili ya wema wake, msimamo wake katika dini na ucha-Mungu wake, na akamtaka awaombee mvua. Zaidi ya hayo ni kwamba haimkiniki kwa 'Umar, wala kwa mtu yoyote mwengine asiyekuwa 'Umar kuwachana na *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na badala yake ageukie *tawassul* kwa kupitia kwa al-'Abbâs lau kama ingeliwezekana kufanya *tawassul* kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Wala haiwezekani hata kudhaniwa yakwamba Maswahaba wote (رضي الله عنهم) wangelilikubali hilo lau kama 'Umar angelilifanya, kwani kuwacha *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kuipendelea *tawassul* kwa kupitia kwa watu wengine itakuwa ni kama kuacha kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika swala kwa kupendelea kumfuata mtu mwengine; ni sawa tu. Bali Maswahaba (رضي الله عنهم) wanaelewa kikamilifu jaha, daraja na fadhla za Mtume wao (صلى الله عليه وسلم) na kwamba hakuna mtu yoyote mwengine awezae kwa njia yoyote kuikurubia daraja hiyo. Twayaona haya waziwazi jinsi

[73] Surah Al-Mu'minûn (23):100

yalivyobainishwa kwenye hadîth ya Sahl ibn Sa'd as-Sâ'îdî (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikwenda kwa Banû 'Amr ibn 'Awf kwa ajili ya kuwapatanisha miongoni mwao. Basi wakati wa swala ukafika na *mu'adh-dhin* akaja kwa Abû Bakr akamwambia: 'Wewe utatuongoza katika swala, ili nitangaze *Iqâmah*?' Basi Abû Bakr akawaongoza watu katika swala. Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuja watu walikuwa wakiendelea na swala, basi akaja kwa kupitia katika mistari mpaka akasimama kwenye mstari (wa kwanza) na watu wakaanza kupiga makofi. Hatahivyo, Abû Bakr hakutizama kando. Lakini watu walipokuwa wakiendelea kupiga makofi, aliangalia kando na kumuona Mtume (صلى الله عليه وسلم). Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuashiriya abakie hapohapo mahali pake, lakini Abû Bakr akainua mikono yake na kumsifu Allâh (عزّ وجلّ) kwa amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kisha Abû Bakr akarudi nyuma kwenye mstari wa kwanza na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akenda mbele na kuongoza swala. Alipomaliza kuswalisha akasema: *'Ewe Abû Bakr ni jambo gani lililokuzuiya wewe kubakia mahali pako nilipokuamrisha?* Akasema Abû Bakr: 'Si mahali pake mwanae Abû Quhâfah kuongoza swala mbele ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم).'"[74]

Kwahivyo wawaona jinsi Maswahaba (رضي الله عنهم) ambavyo hawakuliona kuwa ni jambo la sawa yakwamba waendelee kuongozwa kwenye swala na Abû Bakr (رضي الله عنه) wakati ambapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa pamoja nao, kama ambavyo Abû Bakr (رضي الله عنه) hakuweza kubakia kwenye nafasi yake pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomuarisha afanye hivyo. Kwanini? Yote haya yametokana na ta'dhima kubwa waliyokuwa nayo kwa Mtume wao (صلى الله عليه وسلم) na adabu zao mbele yake na jinsi walivyokuwa wakizitambua haki zake na daraja yake. Kwahivyo ikiwa Maswahaba hawakuridhika isipokuwa waongozwe kwenye swala na Mtume (صلى الله عليه وسلم) linapoweza kufanyika hilo, hata kama walikuwa wameshaanza kuswali wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa hayuko, basi tena itawezekanaje

[74] Imepokewa na al-Bukhâri (tafsiri 1/368/no.652) na Muslim (tafsiri 1/233/no.845)

wakatae kufanya *tawassul* kwa kupitia kwake baada ya kufa kwake lau kama ingelikuwa ni jambo linalowezekana, na badala yake wafadhilishe *tawassul* kwa kupitia kwa mtu mwengine? Zaidi ya hayo, kama ambavyo Abû Bakr alivyoshindwa kukubali yakwamba awaongoze watu katika swala, basi imedhihirika kwa nafsi yake yakwamba vilevile al-'Abbâs hangelikubali watu wafanye *tawassul* kwa kupitia kwake, na kukataa kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), lau kama hayo yangeliwezekana.

Tanbihi: Kwa upande mwengine hili vilevile laonyesha fikira za kipumbavu za wale wenye kudai yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) yuko hai kwenye kaburi lake, tena maisha yanayofanana na maisha yetu ya kilimwengu. Ikiwa hali ni hiyo basi hapangelikuwepo na sababu inayokubalika kabisa kwao wao kukataa kuongozwa na yeye kwenye swala, na badala yake wakawa wanaongozwa kwenye swala na watu wengine, ambao wasoifikia, kwa njia yoyote iwayo, daraja yake na fadhla zake. Basi hili halipasi kupingwa kwa uhakika yakwamba imepokewa kuwa amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mimi niko hai na katika hali nzuri (ya mwili) kwenye kaburi langu; yoyote atakaenitumia maamkuzi ya 'salâm' basi na mimi nitamtumia naye maamkuzi ya 'salâm'*. Wala si kwa uhakika yakwamba wanasema kuwa maana yake ni kwamba yuko hai katika maisha yanayofanana na maisha yetu, ili iwapo tutamtumia yeye kama njia ya *tawassul*, basi atakuwa ni mwenye kutusikiya na kutujibu, ili tuweze kupata malengo yetu na tuyapendayo. Wanazidi kudai yakwamba hapana tafauti katika mambo yote haya baina ya hali yake (صلى الله عليه وسلم) kwenye uhai wake na kwenye hali yake, baada ya kufa kwake. Sasa, kwa haya yote nasema: Hapana awezae kutumia hili kama pingamizi kwa vile limekataliwa kutoka katika pande mbili: la kwanza, kulingana na ta'luma ya hadîth. Hii ni kwa sababu 'hadîth' hii haina msingi kabisa kwa kauli hii. Vilevile hili tamko la *(twariy)* 'hali nzuri ya mwili' halipatikani kwenye idadi ya *ahâdîth* zilizo swahîh, miongoni mwazo ni maneno yake (صلى الله عليه وسلم):

« إِنَّ مِنْ أَفْضَلِ أَيَّامِكُمْ يَوْمَ الْجُمُعَةِ، فِيهِ خُلِقَ آدَمُ، وَفِيهِ قُبِضَ، وَفِيهِ النَّفْخَةُ، وَفِيهِ الصَّعْقَةُ، فَأَكْثِرُوا عَلَيَّ الصَّلَاةِ فِيهِ، فَإِنَّ صَلَاتَكُمْ

مَعْرُوضَةٌ عَلَيَّ» قَالَ: قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ، وَكَيْفَ تُعْرَضُ صَلَاتُنَا عَلَيْكَ وَقَدْ أَرِمْتَ، (قال: يَقُولُونَ: بَلِيتَ) ، قَالَ: «إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَ عَلَى الْأَرْضِ أَجْسَادَ الْأَنْبِيَاءِ »

"Hakika miongoni mwa siku iliyo bora katika masiku yenu ni siku ya Ijumaa, katika siku hiyo aliumbwa Ādam, na katika siku hiyo roho yake ilichukuliwa, na katika siku hiyo parapanda litapulizwa, na katika siku hiyo kilio kikubwa kitatokea, basi kithirisheni swala zenu juu yangu katika siku hiyo, kwa hakika swala zenu zitawasilishwa kwangu." Akasema; "wakasema: 'Ewe Mjumbe wa Allâh, Swala zetu zitawasilishwa vipi kwako haliyakuwa mwili wako utakuwa umeshaoza?" Akasema: *"Allâh ameiharamishia ardhi kutokana na kula miili ya Mitume."*[75]

Vilevile miongoni mwazo ni maneno yake (صلى الله عليه وسلم):

« الأَنْبِيَاءُ أَحْيَاءٌ فِي قُبُورِهِمْ يُصَلُّونَ »

"Mitume wako hai makaburini mwao wanaswali."[76]

« مَرَرْتُ لَيْلَةَ أُسْرِيَ بِي عَلَى مُوسَى قَائِمًا يُصَلِّي فِي قَبْرِهِ »

"Katika usiku niliochukuliwa juu Mbinguni nilimpitia Mûsa naye alikuwa amesimama akiwa anaswali kaburini mwake."[77]

« إِنَّ لِلَّهِ مَلَائِكَةً سَيَّاحِينَ يُبَلِّغُونَ عَنْ أُمَّتِي السَّلَامَ »

"Kwa hakika, Allâh ana Malaika wenye kusafiri kila sehemu kwa ajili ya kunisambazia salamu za maamkuzi kutoka kwa Ummah wangu."[78]

---

[75] Imepokewa na Abû Dâwud (tafsiri 1/269/no.1042), an-Nasâ'î na wengineo kutoka katika hadîth ya Aws ibn Aws na silsila yake ya upokezi ni swahîh.
[76] Imepokewa na Abû Ya'lâ na al-Bazzâr na wengineo kutoka kwa Anas ibn Mâlik na silsila ya riwaya yake ni swahîh na inapatikana katika kitabu changu *Silsilatul-Ahâdith as-Swahîhah* (no.62)
[77] Imepokewa na Ahmad, Muslim (tafsiri 4/1266/no.5858), vilevile kutoka kwa Anas ibn Mâlik

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Jawabu la pili ni kutoka kwenye upande wa *Fiqhi*: Katika kiini chake ni kwamba maisha yake (صلى الله عليه وسلم) ya baada ya kufa kwake ni tafauti na maisha yake ya kabla ya kufa kwake. Hiyo ni kwa sababu maisha ya baada ya kufa baina ya mauti na kufufuliwa (*al-bayânatul-barzakhiyyah*) ni katika sehemu ya ulimwengu wa maficho na *ghayb*. Hapana ajuaye ulivyo isipokuwa Allâh Mwenyewe (سبحانه وتعالى). Lakini hata-hivyo, lijulikanalo na lililothubutu ni kwamba ni tafauti na maisha ya kilimwengu, na wala hayana mafungamano na sheria zake na vigezo. Kwahivyo katika maisha ya kilimwengu mtu hula na kunywa, huvuta pumzi na kuowa, anatembea na anatumia choo, anakuwa mgonjwa na anazungumza. Lakini hakuna awezae kuthibitisha yakwamba mambo haya vilevile ndiyo yatakayokuwa kawaida za watu baada ya mauti, hata kwa Mitume pia (عليهم السلام) akiweko kiongozi wao Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Hili limetiliwa mkazo kwa uhakika yakwamba Maswahaba walikhitilafiana juu ya mas'ala mengi baada ya kufa kwake (صلى الله عليه وسلم), na hapana yoyote miongoni mwao aliyewaza kwenda kwake (صلى الله عليه وسلم) kwenye kaburi lake na kumuuliza kuhusu naswaha kutoka kwake na kuuliza kuhusu jambo la sawa. Kwanini hawakufanya hivyo? Mas'ala yako wazi kabisa, wote hao walijua yakwamba yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameyaacha nyuma haya maisha ya kilimwengu na hali zake na majukumu yake. Kwahivyo baada ya kufa kwake, kwa hakika Mtume (صلى الله عليه وسلم) yuko hai, akiwa anaishi maisha yaliyo kamilika kabisa anayoishi mtu mwengine yoyote baina ya mauti na kufufuliwa. Lakini ni maisha yasiyofanana na maisha haya ya kilimwengu na labda hilo linaweza kuonekana kutokamana na maneno yake:

« ما مِنْ أحَدٍ يُسلِّمُ على إلا ردَّ اللهُ علىَّ رُوحى حتى أردَّ عليه السَّلامَ »

---

[78] Imepokewa na an-Nasâ'î, ad-Dârimi, Ibn Hibbân na al-Hâkim (2/21) kutoka kwa Ibn Mas'ûd, na (al-Hâkim) akaitangaza kuwa ni swahîh na adh-Dhahabi na Ibn Hibbân wakaiafiki, nayo ni kama walivyosema. Inaweza kupatikana katika *al-Mishkât* (no.924) na *Fadhlus-Swalât 'alan-Nabî* (no.21)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

"Hakuna yoyote anayenitumia mimi maamkuzi ya salâm isipokuwa yakwamba Allâh atanirudishia roho yangu ili nipate kumjibu kwa maamkuzi ya salâm."[79]

Kwa hali yoyote iwayo uhakika wake unajulikanwa na Allâh (سبحانه وتعالى) pekee. Kwahivyo hairuhusiwi kuleta Qiyâs baina ya maisha ya baada ya kufa (*al-Hayâtul-barzakhiyyah*) au maisha ya ki-Akhera (*al-hayâtul ukhrawiyyah*) na maisha ya ki-Duniya (*al-hayâtu ad-Duniyawiyyah*), kama ambavyo haijuzu kumpa mmoja wao hukmu za mwengine. Bali kila mmoja wao ana sifa fulani makhsusi na hukmu zake. Hakuna kufanana isipokuwa kwa jina, na ama kwa uhakika wa maisha hayo, basi anayeyajua ni Allâh peke Yake (تبارك وتعالى).

Baada ya *tanbihi* hii, twarudi kwenye kuwajibu wapinzani wetu kuhusiana na *tawassul* ya 'Umar kwa kupitia kwa al-'Abbâs, na tunasema: Ufafanuzi wao wa sababu ya kwanini 'Umar aliwachana na *tawassul* kwa njia ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa *tawassul* ya kupitia kwa al-'Abbâs (رضي الله عنه), iwe yakwamba ilikuwa ni kwa ajili ya kuonyesha kuruhusiwa kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa mtu mwenye fadhla hata lau kama kuna mtu mwengine hapo mwenye fadhla zaidi. Basi tunasema yakwamba huu ni ufafanuzi ya kushangaza na kuchekesha. Hii ni kwa sababu itawezekanaje kwa kitu kama hicho kuingia kwenye akili ya 'Umar (رضي الله عنه), au mtu yoyote katika Maswahaba watukufu (رضوان الله عليهم)? Itawezekanaje fikira hizi za kupiga nywele mapande za waliokuja baadae kuingia akilini mwake, wakati alipowaona watu katika hali hiyo ngumu yenye dhiki, hali ya maafa na huzuni, walipokuwa kwenye hali ya vifo kutokana na njaa na kiu kutokana na ukosefu wa maji, vifo vya Ng'ombe, na ukosefu wa mimea na nyasi za kijani juu ya ardhi, kiyasi cha kwamba mwaka huo unaozungumziwa uliitwa 'mwaka wa ukame/maangamivu'. Nukta hii ya ki-Falsafa ingelipita vipi kwenye akili yake katika mazingira haya magumu, ili aiwache njia kubwa ya *tawassul* katika maombi yake, *yaani; tawassul* kupitia kwa njia ya Mtume mkubwa zaidi (صلى الله عليه

[79] Imepokewa na Abû Dâwud (tafsiri 2/542/no.2036) kutoka kwa Abû Hurairah kwa silsila (*hasan*) nzuri ya riwaya, na inapatikana katika kitabu changu *as-Swahîhah* (no.2266)

وسلم), hata kama lau ingelikuwa inaruhusiwa, na badala yake akatafuta kutumia njia ya chini ya *tawassul* isiyoweza kulinganishwa na ya kwanza, akafanya *tawassul* kupitia kwa al-'Abbâs? Kwanini? Isipokuwa kuwafafanulia watu yakwamba ilikuwa inaruhusiwa kwao kufanya *tawassul* kwa njia ya mtu mwenye fadhla hata kama atakuwepo mtu mwengine aliyekuwa na fadhla kubwa zaidi?!

Kama ilivyo maarufu na kushuhudiwa wakati mtu akiwa na dhiki hujaribu kutumia njia yenye nguvu zaidi atakayoweza kuondoa dhiki hiyo na kuwachana na njia nyengine zozote katika wakati wa starehe. Huu pia ndio uliokuwa uhakika ambao wenye kuabudu masanamu walioufahamu katika masiku ya *Ujâhiliyyah*. Kwenye nyakati za raha walikuwa wakiwalingania masanamu yao, na pia kwenye nyakati za dhiki walikuwa wakiwatupilia mbali na kumlingania Allâh peke Yake. Kama alivyosema (تبارك وتعالى):

فَإِذَا رَكِبُواْ فِى ٱلْفُلْكِ دَعَوُاْ ٱللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ فَلَمَّا نَجَّىٰهُمْ إِلَى ٱلْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ ٦٥

"Na wanapopanda katika vyombo (wakafikwa na misukosuko), humuomba Allâh, na haliyakuwa wanamtakasishia utwiifu. Lakini Anapowafikisha salama barani, mara wanamshirikisha."[80]

Kwahivyo kutokana na haya tunajua yakwamba mwana-adamu kwa asili ya kuzaliwa nayo atakuwa kwenye nyakati za dhiki na mahitaji akitafuta usaidizi wa nguvu kubwa uwezekanayo na njia kubwa zaidi. Kisha akiwa katika nyakati za amani na raha huwenda mara nyengine akazigeukia njia zisizokuwa za nguvu na katika nyakati hizo huwenda ikampitikia akili ya mtu akabainisha hukmu za ki-Fiqhi walizozipendekeza, *yaani;* yakwamba inaruhusiwa kufanya *tawassul* kwa njia ya mtu mwema licha ya kuwepo mtu mwengine aliye mbora zaidi kuliko huyo. Mas'ala mengine tuliyoyataja katika kuzijibu shaka za watu hao ni kwamba hata lau kama sisi tutakubali yakwamba ilipita kwenye akili ya 'Umar (رضي الله عنه), katika kuifafanua hukmu hii ya ki-Fiqhi kwenye madai yao, sasa wewe unadhani yakwamba

[80] Surah al-'Ankabût (29):65

vilevile ilipita kwenye akili ya Mu'âwiyah na adh-Dhahhâk ibn Qays walipofanya *tawassul* kwa kupitia kwa muheshimiwa *Tâbi'î*, Yazîd ibn al-Aswad al-Jurashî? Hapana shaka yakwamba hiki ni kitendo tu katika kutafuta kutumia ujanja wa kuunga mkono fikra zao za kubuni, na wala sio kitu cha kuhusudiwa nacho.

4. Vilevile tunaona kwenye hadîth inayotaja maombi ya 'Umar akimtaka al-'Abbâs (رضي الله عنه), nukta ambayo ni muhimu sana kuitaja, nayo ni maneno yake: "Katika nyakati za ukame, 'Umar alikuwa na mazoweya ya kumtaka al-'Abbâs ibn 'Abdul-Muttwalib awaombee nao mvua." Kwahivyo hii yaashiriya yakwamba matakwa ya 'Umar kwa al-'Abbâs (رضي الله عنهما), awaombee mvua yamerudiwa mara nyingi, na jambo hili lina dalili ya wazi kabisa dhidi ya wale wenye kufasiri kimakosa kitendo cha 'Umar, katika kuwachilia mbali *tawassul* ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na badala yake kupendelea *tawassul* ya kupitia kwa mjombake, wakisema yakwamba alifanya hivyo ili kuonyesha kuruhusiwa kufanya *tawassul* kwa njia ya mtu mwenye fadhla hata kama kutakuwa na mwengine mwenye fadhla kubwa zaidi. Kisha sisi tunasema yakwamba hata kama hali ingelikuwa namna hiyo, basi angelifanya hivyo mara moja tu sio awe anaendelea nalo kila wanaposwali kwa ajili ya kuomba mvua. Hili liko wazi kabisa na wala halifichiki (إنشاءالله تعالى) kwa wanavyuoni na wenye uadilifu.

5. Baadhi ya riwaya zilizo swahîh zinafafanua maneno hayo ya 'Umar yaliyotangulia na makusudio yake. Riwaya hizo zimenukuu *du'â'* hiyo ya al-'Abbâs (رضي الله عنه), aliyo-omba katika kujibu matakwa ya 'Umar (رضي الله عنه). Miongoni mwazo ni yale aliyoyasimulia *al-Hâfidh al-'Asqalânî* (رحمه الله) katika *al-Fat-h* (3/150), aliposema: "Az-Zubair ibn al-Bakkâr amenukuu katika al-Ansâb sampuli ya maombi ya al-'Abbâs katika tukio hili na wakati huo, basi akasimulia kwa silsila hii ya riwaya yakwamba pindi al-'Abbâs alipotakwa na 'Umar awaombee mvua, alisema:

« اللهُمَّ إِنَّهُ لَمْ يَنْزِلْ بَلَاءٌ إِلَّا بِذَنْبٍ، وَلَم يُكْشَفُ إِلَّا بِتَوْبَةٍ، وَقَدْ تَوَجَّهَ الْقَوْمُ بِى إِلَيْكَ لِمَكَانِى مِنْ نَبِيِّكَ ، وَهَذِهِ أَيْدِينَا إِلَيْكَ بِالذُّنُوبِ وَنَوَاصِينَا إِلَيْكَ بِالتَّوْبَةِ، فاسقِنا الْغَيث »

“Yâ Allâh, hakika Wewe huteremshi balaa isipokuwa huwa imetokana na madhambi, na wala haiondoi isipokuwa kwa kutubia, na watu wamekugeukia Wewe kwa kupitia kwangu kutokana na uhusiano wangu na Mtume Wako. Hii hapa mikono yetu imekuelekea Wewe tukiwa na madhambi yetu, na vipaji vyetu vimekuelekea Wewe kwa kutubia. Basi twakuomba ututeremshie mvua.”

Akasema: “Basi mara Mbingu zikateremsha mvua kama milima, ardhi ikarutubika na watu wakaishi.” Hadîth hii yaonyesha:

i. Yakwamba *tawassul* hii ilikuwa ni kwa kupitia kwenye maombi ya al-‘Abbâs (رضي الله عنه), sio kwa dhati yake, kama ilivyofafanuliwa na az-Zubayr ibn Bakkâr na wengineo. Kwahivyo hii ina jawabu ya wazi kwa wale wenye kudai yakwamba *tawassul* ya ‘Umar ilikuwa ni kwa njia ya dhati ya al-‘Abbâs na sio *du’â’* yake, kwani iwapo hilo lingekuwa ni kweli basi hapangelikuwa na haja ya al-‘Abbâs kusimama na kuomba upya baada ya maombi ya ‘Umar.

ii. Yakwamba ‘Umar alieleza waziwazi yakwamba walikuwa wamezoweya kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika uhai wake, na kwamba katika tukio hili sasa alikuwa akifanya *tawassul* kwa kupitia kwa mjombake, al-‘Abbâs. Kwahivyo jambo hili haliwachi kipengee chochote cha shaka kuhusu ukweli yakwamba haya ni matukio ya sampuli moja ya *tawassul*, zote mbili, *tawassul* ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na *tawassul* ya kupitia kwa al-‘Abbâs. Kwahivyo ikiwa imefahamika kwa msomaji, kama itakavyofuata, yakwamba *tawassul* yao kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ilikuwa ni *tawassul* kwa njia ya maombi yake, kisha hii ina maana yakwamba *tawassul* yao kwa njia ya kupitia kwa al-‘Abbâs vilevile ilikuwa ni kwa njia ya maombi yake, kwa vile sampuli zote mbili hizi za mifano ya *tawassul* zilikuwa ni aina moja. Ama kuhusu

dalili yakwamba *tawassul* zao kwa njia ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ilikuwa ni *tawassul* kwa kutumia *du'â'* yake kwao, basi ushahidi wa hili unaonekana wazi katika riwaya ya Ismâ'îl katika kitabu chake cha *Mustakhraj 'alas-Swahîh* ya hadîth hii kwa kauli: "Katika nyakati za ukame kwenye zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa wakitafutia mvua kupitia kwake, basi alikuwa akiwaswalisha swala ya mvua, kisha katika zama za 'Umar..." na akaendelea kuitaja sehemu iliyobaki ya hadîth. Mimi nimenukuu haya kutoka katika *al-Fat-h* (2/399). Kwahivyo, kauli yake: "Basi alikuwa akiwaswalisha swala ya mvua" inaonyesha wazi yakwamba yeye, (صلى الله عليه وسلم) alimuomba Allâh (تعالى) Awateremshie mvua. Kama ilivyo katika *an-Nihâyah* cha Ibnul Athîr: "Maana ya *al-istisqâ'* ni kuomba mvua, *yaani;* yakwamba mvua inyeshe kwenye ardhi na iwanyeshee waja wenye kufanya ibada... na maana ya *istasqaita fulânan:* yakwamba umemtaka fulani na fulani alete mvua kwako." Hili linapokuwa wazi, basi kauli yake katika riwaya hii: "Wameomba mvua kupitia kwake" maana yake ni kwa kutumia njia ya *du'â'* yake na haiwezekani kufahamu kitu chochote isipokuwa maana hii kutokamana na ukusanyaji wa riwaya za hadîth. Kisha itazidi kuungwa mkono na :

iii. Lau kama hali ingelikuwa yakwamba *tawassul* ya 'Umar ilitokamana na dhati ya al-'Abbâs, au daraja yake mbele ya Allâh (تعالى), basi hangeliwachana na *tawassul* inayofanana na hiyo ya kupitia kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kwani hii ingeliwezekana lau kama ingelifaradhishwa katika shariya. Kwahivyo uhakika yakwamba 'Umar aliwacha kufanya *tawassul* kwa njia ya kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kufadhilisha *tawassul* kwa njia ya kupitia kwa *du'â'* ya al-'Abbâs (رضي الله عنه), ndiyo dalili kubwa zaidi yakwamba 'Umar na Maswahaba waliokuwa pamoja nae hawakutumia mashiko yakwamba palikuwa na kitu kama hicho cha *tawassul* kwa njia ya dhati yake Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kisha Wema Waliotutangulia wakaendelea na mafundisho hayo baada yao, kama mulivyowaona katika *tawassul* ya Mu'âwiyah ibn al-Aswad al-Jurashî. Matukio haya mawili yanaonyesha waziwazi yakwamba alivyofanya ilikuwa ni kuomba *(du'â').*

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Sasa itawezekana yakwamba wote wakusanyike pamoja katika kususia kufanya *tawassul* kupitia kwa njia ya dhati yake, Mtume (صلى الله عليه وسلم), lau kama lilikuwa ni jambo linaloruhusiwa? Hususan kwa vile mahasimu wetu wanadai yakwamba ni jambo lililo bora kuliko *tawassul* kupitia kwa njia ya *du'â'* ya 'Abbâs, au mtu mwengine yoyote?! *Wallâhi!* Hilo haliruhusiwi, wala kukubalika na wenye fahamu zao timamu. Bali *ijmâ'* yao hii (muafaka huu) ni mojawapo ya dalili kubwa yakwamba *tawassul* iliyotangulia [*yaani;* kwa kupitia kwa njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)] ilikuwa ni jambo ambalo halikuamrishwa katika shariya kulingana na maoni yao, kwani wao walikuwa na fadhla kubwa kuliko yakwamba wabadilishe lililo zuri kwa ambalo lisilokuwa na uzuri kama huo!

PINGAMIZI NA UKOSOAJI WAKE

Ama kuhusiana na majibu ya muandishi wa *Misbâhuz-Zujâjah fî Fawâ'id Qadhâ'il-Hâjah* kwenye suala la kwanini 'Umar angeliwachana na *tawassul* kupitia kwa njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kisha akasema: "'Umar hakusikiya kuhusu hadîth ya *tawassul* ya mtu aliyekuwa kipofu (Tizama katika Ukurasa wa 63 kwa *nass* ya hadîth hiyo), na lau kama ingelimfikia basi angelifanya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم)." Basi haya ni madai ya bâtwil kwa pande nyingi:

Ya Kwanza: Yakwamba hadîth ya mtu-kipofu inaonyesha kitu hichohicho kama hadîth hii kuhusu *tawassul* ya 'Umar, *yaani;* yakwamba ilikuwa ni *tawassul* kwa kupitia kwa njia ya maombi yake, sio kwa dhati yake, kama ilivyotangulia.

Ya Pili: Hakuna kilichofanywa kwa siri katika *tawassul* ya 'Umar, bali ilifanywa dhahiri mbele ya watu, wakiweko kati yao baadhi ya Maswahaba wakubwa kutoka katika *Muhâjirûn, Answâr* na wengineo. Kwahivyo hata kama ilikuwa yawezekana kuwa hadîth hiyo haikuwa ikijulikana na 'Umar, basi ingewezekanaje ati vilevile haikujulikana na Maswahaba wote waliokuwepo hapo pamoja na 'Umar?!

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Ya Tatu: Yakwamba ‘Umar, kama ilivyotangulia, alikuwa akiirudia-rudia na kuifanya tena *tawassul* kama hii kila kunapotokea hali ya hatari kwa watu wa al-Madînah, au kila walipokuwa na haja ya kuswali kwa ajili ya mvua, kama inavyo-onyeshwa kwa kauli isemayo ‘Alikuwa na mazoweya ya...’ katika hadîth iliyotangulia ya Anas: “Yakwamba kulipotokea ukame ‘Umar alikuwa na mazoweya ya kumtaka al-‘Abbâs aswalishe swala ya kuwaombea mvua.” Yamepokewa kama hayo kutoka kwa Ibn ‘Abbâs; kutoka kwa ‘Umar kama alivyoeleza Ibn ‘Abdul-Barr kwenye *al-Istî’âb* (3/98), kwahivyo, hata kama hilo lilikuwa halijui katika mara ya kwanza, basi ingewezekana yakwamba atabakia katika hali ya kutolijua hilo kila mara anapomuuliza al-‘Abbâs aswalishe swala ya mvua kwa kuwaombea wao mvua, tena akiwa pamoja na *Muhâjirûn* na *Answâr*, kisha wanyamaze wasidhihirishe ‘ilmu waliyokuwa nayo ya hadîth ya mtu-kipofu?! *Wallâhi!* Jawabu kama hilo litakuwa ni tuhuma ya ujinga wa hadîth ya mtu-kipofu dhidi ya Maswahaba wote, au kwa uchache ukosefu wao wa kujua kuhusu uhakika yakwamba ni dalili ya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake. Ni wazi yakwamba la kwanza ni makosa kabisa, na la pili ni ukweli, kwani lau kama wangelijua yakwamba hadîth ya mtu-kipofu imethibitisha sampuli ya *tawassul* wanayoidai, basi katika hali hiyo hawangeliiwacha *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kuipendelea *tawassul* kwa kupitia njia ya *du’â’* ya al-‘Abbâs, kama ilivyotangulia.

Ya Nne: ‘Umar hakuwa peke yake katika kuifadhilisha *tawassul* kwa kupitia njia ya du’â’ ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuliko *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake, bali yalifanywa kama hayo na Mu’âwiyah ibn Abî Sufyân ambaye pia alifanya *tawassul* kwa kupitia njia ya du’â’ ya Yazîd ibn al-Aswad na wala sio kupitia kwa njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), na idadi ya Maswahaba na *ma-tâbi’în* walikuwa pamoja naye. Kwahivyo inatakiwa isemekane vilevile yakwamba Mu’âwiyah na wale wote waliokuwa naye hawakujua kuhusu hadîth ya mtu-kipofu? Na kisha itatulazimu sisi vilevile kusema kama hivyo kuhusu *tawassul* ya adh-Dhahhâk ibn Qays kwa Yazîd pia?

Muandishi wa *al-Misbâh* anatoa jawabu nyengine, naye amefuatwa katika hilo na mmojawapo wa wafuasi vipofu wanaotukhalifu sisi na walionyimwa usawa, akisema: “Aliyokusudia ‘Umar kwa *tawassul*

yake kwa kupitia njia ya al-‘Abbâs ilikuwa ni kufuata mifano ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika kumkirimu na kumtukuza al-‘Abbâs. Mfano wa haya umebainishwa waziwazi na ‘Umar. Az-Zubeir ibn Bakkâr amesimulia katika *al-Ansâb*, kwa kupitia kwa Dâwud ibn ‘Atwâ’, kutoka kwa Zayd ibn Aslam, kutoka kwa ibn ‘Umar aliyesema: “Katika mwaka wa Ukame/Maangamivu ‘Umar ibn al-Khattwâb aliomba mvua kwa kupitia njia ya ‘al-‘Abbâs, basi ‘Umar akatoa Khutbah na akasema: ‘Kwa hakika Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akimchukulia al-‘Abbâs kama ambavyo kijana wa kiume anavyomchukulia babake, kwahivyo, Enyi watu! fuateni mfano wa Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) na mumfanye yeye kuwa ni njia ya kujikurubisha kwa Allâh...,’ Vilevile imesimuliwa na al-Balâdhurî kwa njia ya Hishâm ibn Sa’d kutoka kwa Zayd ibn Aslam kutoka kwa babake.”

KISHA MAJIBU YA HAYA VILEVILE YANATOKAMANA NA PANDE NYINGI

La Kwanza: Sisi hatukubali uswahîh wa riwaya hii, kwani imepokewa kwa njia ya Dâwud ibn ‘Atwâ’ ambaye ni al-Madanî, naye ni mtu dha’îf kama ilivyo katika *at-Taqrîb*, na imepokewa kutoka kwake na az-Zubeir ibn Bakkâr kama alivyoisimulia al-Hâkim (3/334), na akainyamazia. Hatahivyo, adh-Dhahabî aliipinga hii kwa maneno yake: “Dâwud ametupiliwa mbali (*matrûk*).” Mimi nasema: Mpokezi kutoka kwake ni Sâ’idah ibn ‘Ubaydullâh al-Muzanî na mimi sioni wasifu wake wowote. Kisha vilevile kuna mgongano (*idhtirâb*) baina ya silsila ya riwaya yake, kwani imepokewa, kama mulivyojionea, na Hishâm ibn Sa’d, kutoka kwa Zayd ibn Aslam, yakwamba alisema: “kutoka kwa babake” badala ya “kutoka kwa ibn ‘Umar.” Lakini hata hivyo Hishâm ni mtegemewa zaidi kuliko Dâwud, lakini hatuoni kauli yake ili tulinganishe iwapo imekhalifiana na kauli ya Dâwud au laa. Basi usifanywe mpumbavu kwa maneno yao katika *al-Misbâh* baada ya silsila hii ya riwaya: [به] “kwa hiyo,” inayoleta hisiya yakwamba zote mbili zina kauli zilizo sawa, kwa vile msingi wake kwa anayoyanukuu kutoka kwenye *al-Balâdhurî* ni *Fat-hul-Bâri* tu ambayo mtunzi wake hakusema [به] “kwa hiyo,” [Tizama katika *Fat-hul-Bâri* 2/399]

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

La Pili: Hata kama riwaya hii ingelikuwa ni swahîh, basi yote ingelionyesha ni sababu iliyomfanya ‘Umar atekeleze *tawassul* kwa kupitia njia ya al-‘Abbâs, badala ya kwa kupitia njia ya Maswahaba wengine waliokuwepo wakati huo. Lakini kutokana na kuonyesha kwake kuruhusiwa kuwachana na *tawassul* ya kupitia kwa njia ya dhati ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم), lau kama ingelikuwa inaruhusiwa kwao, kwa *tawassul* ya kupitia kwa njia ya al-‘Abbâs, (*yaani;* kwa kupitia njia ya dhati yake), basi haionyeshi kitu kama hicho kabisa, kwani sisi twajua kwa dharura na kama inavyodhihirika yakwamba iwapo kundi la watu wamekumbwa na mkasa mkubwa wa Ukame na wakataka kumuweka mmoja wao mbele kwa niyaba yao wafanye *tawassul*, basi haitowezekana kwao wamuache kando ambaye *du’â’* yake iliyo na uwezekano mkubwa wa kutakabaliwa, na ambaye aliye karibu na rehma za Mola wake (سبحانه وتعالى). Vilevile akiwa mtu amepatwa na msiba mkubwa na akawa naye mbele yake Mtume na mtu mwengine ambaye si Mtume, kisha akamtaka mmoja wao amuombee, hatomtaka isipokuwa Mtume. Kisha iwapo atamtaka yule asiyekuwa Mtume badala yake, na kumuachilia mbali Mtume atahesabiwa kuwa ni mtu mjinga na mwenye madhambi. Sasa itadhaniwa vipi kwa ‘Umar pamoja nae Maswahaba yakwamba watawachana na *tawassul* ya kupitia kwa njia ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) kwa kufadhilisha *tawassul* ya kupitia kwa mtu mwengine, lau kama *tawassul* ya kupitia kwa njia ya dhati ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) ingelikuwa inaruhusiwa? Sasa itakuwaje hali hiyo ikiwa kwa wapinzani wetu ni bora kuliko *tawassul* kwa kupitia njia ya *du’â’* ya al-‘Abbâs au mtu yoyote mwengine aliye mwema?! Hususan ikiwa hilo limefanywa kwa mara nyingi kama ilivyotangulia, na hawakutafuta kumtumia kama njia ya *tawassul* hata mara moja, na vilevile hilo lilikuwa ni jambo lililorudiwa tena baadae. Licha ya haya hakuna miongoni mwao aliyefanya jambo lolote tafauti na alivyofanya ‘Umar. Kwa hakika yaliyopokewa kutoka kwa Mu’âwiyah na wale waliokuwa naye wamekubaliana kikamilifu na vitendo vyake kwani walitafuta kutumia kama njia ya *tawassul*, maombi ya muheshimiwa *Tâbi’i* Yazîd ibn al-Aswad. Sasa itakuwaje sawa kusema yakwamba kutafuta *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake ndilo lililofanywa kwa ajili ya kufuata mafundisho ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم)?! Bali ukweli ni kwamba kitendo cha Maswahaba cha kuendelea

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

kuwacha kufanya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) pindi wanapokumbwa na mikasa, baada yao kutokuwa na mazoweya ya *tawassul* kwa kupitia njia ya mtu mwengine yoyote wakati wa maisha ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم), ndiyo kwa hakika mojawapo katika dalili ya wazi na yenye nguvu zaidi yakwamba *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) haikufaradhishwa. Kwa upande mwengine, kwa hakika ingelipokewa kutoka kwao kwa silsila za riwaya kuhusiana na idadi ya matukio. Kwani huwaoni jinsi wapinzani wetu wanavyozigeukia *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa motisha kidogo kwani wanaidhania kuwa ni jambo lililofaradhishwa kwetu?!

Lau kama hali ni kama hivyo, basi mfano wake ungelipokewa kutoka kwa Maswahaba, hususan kwani wao walikuwa na heshima kubwa zaidi na mapenzi juu yake (صلى الله عليه وسلم) kuliko watu waliokuja baadae. Basi itakuwaje hili likose kupokewa kabisa kutoka kwao, hata kusipatikane angalau mfano mmoja? Bali yaliyopokewa kutoka kwao ni kujiepusha nayo kwa kufadhilisha *tawassul* ya kupitia kwa njia ya maombi ya watu wema!

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

❖ **SHAKA YA PILI**

HADÎTH YA MTU-KIPOFU

Baada ya kukamilisha uhakiki wa yaliyo ya sawa kuhusiana na hadîth ya *tawassul* ya ‘Umar kwa kupitia kwa njia ya al-‘Abbâs (رضي الله عنهما), na kubainisha yakwamba hakuna dalili hapo ya wapinzani, bali hilo ni dalili dhidi yao, sasa tutachunguza yaliyo ya sawa kuhusu hadîth ya mtu kipofu. Tutaizingatia maana yake na tuone iwapo ni dalili kwao au ni dalili nyengine dhidi yao:

أَخْرَجَ أَحْمَدُ وَغَيْرِهِ بِسَنَدٍ صَحِيْح عَنْ عُثْمَانَ بْنِ حُنَيْفٍ، أَنَّ رَجُلًا ضَرِيرَ الْبَصَرِ أَتَى النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، فَقَالَ:ادْعُ اللَّهَ أَنْ يُعَافِيَنِي، قَالَ: «إِنْ شِئْتَ دَعَوْتُ لَكَ، وَإِنْ شِئْتَ أَخَّرْتُ ذَاكَ، فَهُوَ خَيْرٌ (وَفِي رِوَايَةٍ: وَإِنْ شِئْتَ صَبَرْتَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكَ)». فَقَالَ: ادْعُهُ. " فَأَمَرَهُ أَنْ يَتَوَضَّأَ، فَيُحْسِنَ وُضُوءَهُ، فَيُصَلِّيَ رَكْعَتَيْنِ، وَيَدْعُوَ بِهَذَا الدُّعَاءِ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ، وَأَتَوَجَّهُ إِلَيْكَ بِنَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ نَبِيِّ الرَّحْمَةِ، يَا مُحَمَّدُ إِنِّي أَتَوَجَّهُ بِكَ إِلَى رَبِّي فِي حَاجَتِي هَذِهِ، فَتَقْضِي لِي، اللهُمَّ شَفِّعْهُ فِيَّ (وَشَفِّعْنِي فِيهِ). قَالَ: فَفَعَلَ الرَّجُلُ، فَبَرَأَ.

Imepokewa kutoka kwa Ahmad na wengineo kwa isnad iliyo swahîh ya riwaya kutoka kwa ‘Uthmân ibn Hanîf: “Yakwamba mtu mmoja kipofu alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akamwambia, ‘Niombee nami kwa Allâh anipoze maradhi yangu.’ Basi akamjibu, ‘*Ukipenda nitakuombea na ukipenda nitaichelewesha du’â’ hiyo, kwani hivyo ni bora (*na katika riwaya nyengine: *‘Na ukipenda, fanya subira, na hilo ni bora kwako)’*. Basi akasema, ‘Hebu Muombe.’ Basi akamuamrisha atawadhe, na aukamilishe wudhû’ wake kisawasawa, kisha aswali *raka’ât* mbili, na aombe kwa *du’â’* hii: ‘*Yâ Allâh! Nakuomba Wewe na kukuelekea Wewe kwa kupitia kwa Mtume*

Wako Muhammad,[81] *Mtume wa Rehma, Ewe Muhammad mimi nime-elekea kwa kupitia kwako (yaani; du'â' yako) kwa Mola wangu katika haja yangu hii, ili nipate kutakabaliwa nayo, Yâ Allâh! Mkubali yeye kama muombezi kwa niyaba yangu, na umtakabaliye du'â' yangu kutoka kwake (itakabaliwe kwa ajili yangu).'* Akasema, 'Basi yule mtu akafanya hivyo na akatibika.'"[82]

Wapinzani wetu wameshikilia yakwamba hadîth hii ni dalili yakwamba inaruhusiwa kufanya *tawassul* katika *du'â'* kwa jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au jaha ya watu wengine wema, kwa vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimfundisha mtu-kipofu amtumie yeye kama

---

[81] *Yaani:* kwa njia ya Du'â' yake, kama itakavyodhihirika.

[82] Imepokewa katika al-Musnad (4/138) na at-Tirmidhi (4/281-282...), Ibn Mâjah (1/418), at-Twabarâni katika *al-Kabîr* (3/2/2) na al-Hâkim (1/313...) wote hao kwa kupitia kwa 'Uthmân ibn 'Umar (Sheikh wa Ahmad ndani yake) kutoka kwa Shu'bah kutoka kwa Abû Ja'far al-Madani, aliyesema, "Nimemsikiya 'Ammârah ibn Khuzaymah akisimulia kutoka kwa 'Uthmân akiwemo. Amesema at-Tirmidhi, *hasan swahîh gharîb*, na katika Ibn Mâjah inapatikana baada yake: "Amesema Abû Ishâq, *Hadîth Swahîh*. Kisha akaipokea Ahmad, "Shu'bah akatusimulia sisi, na inayo ndani yake riwaya nyengine, na amefuatwa kwa hilo na Muhammad Ibn Ja'far: Shu'bah akatusimulia sisi. Al-Hâkim akaipokea (1/519) na akasema, isnâd yake ni swahîh, na adh-Dhahabi akaiafiki. Baadhi yao wakatangaza yakwamba inayo udhaifu fulani, kama vile mtunzi wa *Siyâhatul insân* na mtunzi wa *Tathîrul Janân* (Uk.37) na wengineo, kwa kuwa isnâd yake ina Abû Ja'far, at-Tirmidhi akasema, "Sisi hatuijui isipokuwa kwa silsila hii, kutoka kwenye hadîth ya Abû Ja'far, naye siye al-Khatamî." Kwahivyo wanasema, "Kwahivyo yeye ni ar-Râzî ambaye ni mkweli lakini hana kumbukumbu nzuri." Mimi nasema hayo yamekataliwa kwa uhakika kuwa yaliyo ya sawa ni kwamba kwa hakika yeye ndiye al-Khatamî, na hili ndilo jina analomwita nalo Ahmad kwenye riwaya (4/138) na kwenye nyengine akamwita Abû Ja'far al-Madani, na vilevile kama alivyofanya al-Hâkim, na ndiye 'al-Khatamî' ambaye pia ni 'al-Madani', wala sio 'ar-Râzî'. Hivi ndivyo kama ilivyopokewa katika *mu'jamus-Swaghîr* cha at-Twabarânî na kwenye Chapa ya Bûlaq ya at-Tirmidhi pia. Na hilo limethibitishwa pasi na shaka yoyote kwa uhakika yakwamba aliyepokea kutoka kwa 'Ammârah ibn Khuzaymah ni 'al-Khatamî', na ndiye ambaye kutoka kwake alipokea, Shu'bah, kama ilivyo katika isnâd hii, naye ni *Swadûq* (anayekubaliwa kwa ujumla). Kwahivyo isnâd hii ni nzuri, isiyokuwa na upofu wowote.

njia ya kujikurubisha katika *du'â'* yake, na kipofu huyo akafanya hivyo na akarudishiwa kuona kwake.

Ama kutuhusu sisi, basi twashikilia msimamo yakwamba hadîth hiyo haina dalili ya kuwaunga wao kuhusiana na sampuli hii ya *tawassul* ambayo kwayo kuna kukhitilafiana, ambako ni kutafuta mkuruba kwa njia ya dhati yake. Bali ni dalili nyengine ya sampuli ya tatu ya *tawassul* inayoruhusiwa na kufaradhishwa ambayo tuliyoizungumzia hapo awali, kwa vile *tawassul* ya huyo kipofu ilikuwa ni kwa kupitia njia ya *du'â'* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), na ushahidi wa tuyasemayo ni mwingi hata kwenye hadîth yenyewe, ulio muhimu zaidi:

1. Sababu ya mtu-kipofu kuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ilikuwa ni kwake yeye amuombee (*du'â')*, kama alivyosema, "Niombee nami kwa Allâh anipoze maradhi yangu." Kwahivyo alitafuta kutumia *du'â'*ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama njia ya kujikurubisha kwa Allâh (تعالى), kwa vile alijua yakwamba *du'â'* yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) ina uwezekano mkubwa kutakabaliwa na Allâh kuliko *du'â'* ya watu wengine, na iwapo niya ya kipofu ilikuwa ni kutafuta mkuruba na Allâh kwa njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au jaha yake au haki yake, basi hangelikuwa na haja ya kwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), au amtake amuombee *du'â'*, bali angelijikalia nyumbani kwake, na kumuomba Mola wake kwa kusema, kwa mfano, "Yâ Allâh! Nakuomba Wewe kwa jaha ya Mtume Wako na daraja yake Kwako, yakwamba unipoze mimi na uniwezeshe kuona."

Lakini hivyo sivyo alivyofanya. Kwanini? Kwa vile alikuwa ni Muarabu na anajua vilivyo maana ya *tawassul* katika lugha ya Kiarabu, na alikuwa anajua yakwamba halikuwa ni neno la kusemwa na mtu mwenye haja, kwa kulitaja jina la mtu akawa ni kama mjumbe, bali ilibidi ihusishe kumjia mtu ambaye anayeamini kuwa ni mtu mwema na mwenye 'ilmu ya Kitâb na Sunnah na amtake amuombee *du'â'*.

2. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliahidi yakwamba atamuombea du'â', baada ya kumnaswihi juu ya yatakayo kuwa bora kwake, na hii ndiyo iliyokuwa kauli yake, "*Ukipenda nitakuombea na ukipenda nitaichelewesha du'â' hiyo, kwani hivyo ni bora (*na katika riwaya

nyengine*: 'Na ukipenda, fanya subira, na hilo ni bora kwako)'"*. Na hili suala la pili ndilo jambo ambalo yeye, Mtume (صلى الله عليه وسلم), alililoliashiriya katika hadîth aliyoisimulia kutoka kwa Mola wake (تبارك وتعالى) yakwamba Yeye alisema:

« إِذَا ابْتَلَيْتُ عَبْدِى بِحَبِيبَتَيْهِ - أى عَيْنَيْهِ - فَصَبَرَ،عَوَّضْتُهُ مِنْهُمَا الجَنَّةَ

«

"Nitakapomuonja mja wangu kwa vipenzi vyake viwili – yaani macho yake – akasubiri, nitamlipa badala yake Pepo."[83]

3. Kusisitiza kwa kipofu yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) **amuombee du'â'**, kama alivyosema, "Hebu Muombe", yenye maana yakwamba hapana shaka Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuombea, kwa vile yeye (صلى الله عليه وسلم) ndiye aliyekuwa mbora katika kutimiza ahadi na alikuwa tayari ashamuahidi kumuombea *du'â'* iwapo alipendelea hivyo kama ilivyotangulia, na alikuwa anataka *du'â'* kutoka kwake, na kwahivyo nukta hiyo ikawa imethibitishwa. Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم), kutokana na rehma zake na mapendelewa yake, yakwamba Allâh (تعالى) aikubali *du'â'* yake kwa niyaba ya yule kipofu, vilevile akamuongoza kipofu katika kutumia sampuli ya pili ya *tawassul* inayofaa na ya kisharia, ambayo ni *tawassul* ya kupitia njia ya vitendo vyema, kwa ajili ya kuchanganya pamoja sampuli tafauti za mambo mazuri.

Kwahivyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuombea akamuamrisha akatawadhe na aswali *raka'ât* mbili, kisha ajiombee *du'â'* yeye mwenyewe, na vitendo hivi vya utwi'ifu kwa Allâh (سبحانه وتعالى) alivyovitekeleza pamoja na *du'â'* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa niyaba yake, na haya yanaingia kwenye maneno Yake, Allâh (تعالى):

وَٱبْتَغُوٓاْ إِلَيْهِ ٱلْوَسِيلَةَ ٣٥

[83] Imepokewa na al-Bukhâri (tafsiri 7/377/no.557) kutoka kwa Anas, imenukuliwa katika *as-Swahîhah* (2010)

“Na tafuteni njia ya (*wasîlah*) Kumfikilia.”
[al-Mâidah 5:35]

kama ilivyotangulia.

Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakutosheka na kumuombea *du’â’* kipofu, kama alivyoahidi, vilevile alimpa na kitendo atekeleze kilichohusisha utwi’ifu kwa Allâh (سبحانه وتعالى), na kujikurubisha karibu Naye zaidi, ili matakwa yenyewe yakamilike kwa pande zote, na kuwa karibu zaidi na kukubaliwa na kupata radhi kutoka kwa Allâh (سبحانه وتعالى), kwahivyo matukio yote hayo yanazunguka kwenye mduara wa *du’â’* kama ilivyo dhahiri na ikiwa haina lolote katika wanayoyataja wao.

Sheikh al-Ghummârî ameghafilika na hili au anajifanya tu kughafilika, kwani amesema katika *al-Misbâh* (24), maana ya “... *ukipenda nitakuombea*, ‘ukipenda nitakufundisha du’â’ utakayoiomba na nitakukaririya,’ maelezo haya ni wâjib ili mwanzoni mwa hadîth iafikiane na mwisho wake.”

Mimi nasema: Maelezo haya ni *baatil* kutokana na sababu nyingi, miongoni mwake ni kwamba yule mtu-kipofu alimuomba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amuombee yeye kwa Allâh, na wala sio amfundishe du’â’, na kwa vile maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwake yeye, ‘*Na ukipenda nitakuombea du’â’*, ilikuwa ni jawabu ya matakwa yake, kwahivyo hapana shaka yakwamba ilikuwa ni kutaka kuombewa du’â’, na hili halina budi liwe, na hii ndiyo maana inayokubaliana na mwishoni mwa hadîth, ndiyo sababu tunaona yakwamba al-Ghummârî hakuwa akijaribu kufafanua kauli yake mwishoni, *Yâ Allâh! Mkubali yeye kama muombezi kwa niyaba yangu, na umtakabaliye du’â’ yangu kutoka kwake (itakabaliwe kwa ajili yangu)*, kwani hii yaonyesha waziwazi yakwamba *tawassul* yake ilikuwa ni ya kupitia kwenye du’â’ ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama tulivyo-onyesha katika yaliyotangulia.

Kisha akasema, “Hata kama tutakubali yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimuombea du’â’ mtu-kipofu, basi hilo halipingi ahâdîth hizo kutokamana na kujumuishwa kwake ili zihusishe nyenginezo.”

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Mimi nasema: Haya ni makosa ya wazi, kwani hakuna anayepinga hadîth hiyo kutokamana na kutumika kwa mtu mwengine asiyekuwa mtu-kipofu, kutokamana na wale ambao walio-ombewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Lakini hatahivyo, kwa vile *du'â'* kutoka kwake (صلى الله عليه وسلم) baada ya kuondoka na kujiunga na rafiki wa juu zaidi ni jambo ambalo wale wenye kutafuta *tawassul* kwa mahitaji yao yote na mapendelewa hawalijui, na pia wao wenyewe hawatafuti *tawassul* kwa *du'â'* zake Mtume (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake, kwahivyo hukmu ni tafauti, na huku kujisalimisha kwa al-Ghummârî ni huja dhidi yake.

Katika du'â' ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyomfundisha kuisoma, inapatikana ndani yake, *"Yâ Allâh! Mkubali yeye kama muombezi kwa niyaba yangu",* na ni jambo lisilowezekana kulichukulia hili kumaanisha na kuwa ni *tawassul* kwa kupitia kwa dhati yake (صلى الله عليه وسلم), au jaha yake au haki yake, kwani maana yake ni, *""Yâ Allâh! Mkubali du'â' yake (*Mtume (صلى الله عليه وسلم)*) kwako Wewe unirudishie kuona kwangu."*

Maana ya *Shafâ'ah* katika lugha ni *du'â'*, na hili ndilo lililokusudiwa kwa *Shafâ'ah* iliyothibitishwa kwa ajili yake (صلى الله عليه وسلم) na kwa ajili ya Mitume wengine na Watu Wema katika siku ya kufufuliwa. Hili linaonyesha yakwamba *Shafâ'ah* ni makhsusi zaidi kuliko *du'â'* kwani njia yake ya pekee ni iwapo kutakuwa na watu wawili wanao-omba jambo fulani, ili mmojawapo awe ni muombezi wa mwengine, kama ilivyo kinyume cha mtu mmoja mwenye kuomba kitu na asilete mtu mwengine kuwa ni muombezi wake, kama ilivyo katika *Lisânul-'Arab:*

SHAFĀ'AH (KUOMBEA): ni mazungumzo ya mwombezi kwa Mfalme kuhusu haja fulani ambayo anayoiomba kwa ajili ya mtu mwengine, na mwombezi ndiye mwenye kutaka kitu kwa ajili ya mtu mwengine, ambaye kwa kupitia kwake anaomba kulipata linalotakwa..."

Kwahivyo imethibitishwa kwa njia hii vilevile, yakwamba *tawassul* ya mtu-kipofu ilikuwa ni kwa kupitia kwenye *du'â'* yake (صلى الله عليه وسلم) na wala sio kwa dhati yake.

4. Kutokamana na ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyomfundisha mtu-kipofu ayasema yalikuwa ni, *"na umtakabaliye du'â' yangu kutoka kwake (itakabaliwe kwa ajili yangu)*[84]*"*, *yaani;* nitakabalie *Shafâ'ah* yangu kwa ajili yake, *yaani;* nitakabalie *du'â'* yangu yakwamba uitakabali *Shafâ'ah* yake, *yaani*; itakabali du'â' yake yakwamba Wewe unirudishie kuona kwangu, na haiwezekani kabisa kufahamu chochote kilicho kinyume chake kutokana na kauli hii. Hii ndiyo sababu utawakuta wapinzani wetu wakisingizia ujinga kuhusiana na hilo na wakijiepusha na kulitaja hilo kwa vile inabomoa jengo lao kutoka kwenye misingi na kuporomosha kuta zake, na pindi wanapolisikia hilo utawaona kana kwamba mtu aliyezimia.

Hii ni kwa sababu wao wanadhania yakwamba wameifahamu *shafâ'ah* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa mtu-kipofu, lakini itamaanisha nini *shafâ'ah* ya mtu-kipofu *kumshufaiya* Mtume (صلى الله عليه وسلم) ? Hawana jawabu la hilo kabisa. Uhakika yakwamba wao wanatambua kuwa ibara hii inabatilisha makosa katika tafsiri yao imedhihirika kutokana na ukweli yakwamba hutompata hata mmoja wao akiitumia hiyo katika mafundisho yao, *yaani;* akiomba hivi, *"Yâ Allâh! Itakabali shafâ'ah ya Mtume Wako kwangu mimi na shafâ'ah yangu mimi kwake."*

5. Wanavyuoni wanaitaja hadîth hii miongoni mwa miujiza ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na miongoni mwa *du'â'* zake zilizotakabaliwa, na kwamba Allâh alisababisha miujiza na wagonjwa kutibika kwa kupitia kwenye Baraka za *du'â'* za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم), kwa sababu kwa kupitia kwenye *du'â'* za Mtume kwa huyu mtu-kipofu Allâh alimrudishia kuona kwake.

---

[84] Ibara hii ni katika sehemu ya hadîth iliyo swahîh. Imepokewa na Ahmad na al-Hâkim, aliyeithibitisha, na akaiafiki adh-Dhahabi, nayo peke yake ni huja ya kukatikiwa yakwamba kuichukulia hadîth na kuihusisha na *tawassul* kwa dhati yake ni *baatwil*, huo ukiwa ndio msimamo wa baadhi ya waandishi wa hivi karibuni. Inaonekana kana kwamba wameizingatia nukta hii na kwahivyo hawaitaji ibara hii kabisa, jambo linalo-wafedhehesha ni kiwango gani wanachoweza kuaminika katika kuzisimulia nukuu. Iliyo karibu na hii ni katika kunukuu kwao kauli zilizotangulia, *"Yâ Allâh! Itakabali Shafâ'ah yake kwa ajili yangu",* kuwa ndiyo dalili ya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake, lakini katika kufafanua jinsi inavyo-onyesha hilo, basi hawaelezi hilo kwa wasomaji, kwani asiyekuwa na kitu hatokuwa na cha kuwapa wengine.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kwahivyo, waandishi wameinukuu miongoni mwa alama za Utume wake, kama vile al-Baihaqî na wengineo. Kwahivyo hii yaonyesha yakwamba sababu zilizomfanya mtu-kipofu aje apate matibabu ilikuwa ni *du'â'* za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na hii imezidi kuonyeshwa na watu wote wale vipofu wenye kumlingania Allâh (تعالى) Peke Yake, na kumuelekea Yeye kwa *ikhlâs* atibike kwa kupitia hilo. Lau kama ufahamu wa watu wengine ungelikuwa ni wa kweli,[85] basi kwa uchache angalau mmoja wao angelitibika, na hili ni jambo ambalo lisilotokea, na pengine halitokei.

Vilevile ikiwa sababu ya kutibika mtu-kipofu ilikuwa ni kwamba alifanya *tawassul* kupitia njia ya jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na daraja na haki, kama wengi miongoni mwa waliokuja baadae wanavyofahamu, basi ingelitarajiwa yakwamba tiba hii itapatikana kwa watu wengine vipofu wanaotafuta kufanya *tawassul* kwa jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), na mara nyengine wanaongezea juu ya hayo jaha za Mitume wote na Manabii na Ma-Awliyâ' wote, na Mashahidi, na Watu Wema, na daraja za wote wale ambao wenye daraja zozote walizonazo mbele ya Allâh, wale wanaotokamana na Malaika, Bina-Adamu na Majini! Sisi hatujui, na wala hatudhani yakwamba mtu yoyote anayajua hayo kuwahi kufanyika kwa yoyote katika karne zote hizi ndefu baada ya kifo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) mpaka siku hii ya leo.

Kwahivyo itakapobainika kwa msomaji mtukufu kutokana na dalili mbali mbali tulizozidhihirisha yakwamba hadîth ya mtu-kipofu inazunguka katika mduara wa *tawassul* kupitia kwa njia ya *du'â'* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kwamba haina mafungamano yoyote na *tawassul* kupitia kwa dhati yake, kisha ndio inabainika wazi yakwamba muradi wa kauli ya mtu-kipofu katika *du'â'* yake, '*Yâ Allâh! Nakuomba Wewe na kukuelekea Wewe kwa kupitia kwa Mtume Wako Muhammad* (صلى الله عليه وسلم)', ni 'Natafuta njia ya kujikurubisha Kwako kwa njia ya *du'â'* ya Mtume Wako (صلى الله عليه وسلم),' kwa

[85] *Yaani;* Ikiwa hali ilikuwa namna hiyo yakwamba mtu-kipofu alitibika kwa sababu alitumia *du'â'* na akafanya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama wanavyodai hawa watu!

kuliwacha neno lenye kutawala [*yaani; du'â'*], na hili ni jambo maarufu sana katika lugha, kama maneno ya Allâh (تعالى) yasemayo:

وَسْـَٔلِ ٱلْقَرْيَةَ ٱلَّتِى كُنَّا فِيهَا وَٱلْعِيرَ ٱلَّتِىٓ أَقْبَلْنَا فِيهَا ۖ وَإِنَّا لَصَٰدِقُونَ ٨٢

"Na waulize watu wa mji tuliokuwa, na (waulize watu wa) msafara tuliokuja nao; na hakika sisi tunasema kweli."[86]

Kwa maana yakwamba "watu" wa mji na "washirika"[87] wa msfara, na sisi pamoja na wapinzani wetu tunakubaliana juu ya hilo, *yaani;* yakwamba inatubidi tuje na neno lililotawala ambalo lililowachwa. Kwa maoni yetu hali ni ileile kama katika *du'â'* ya 'Umar (رضي الله عنه), na *tawassul* yake kwa kupitia kwa njia ya al-'Abbâs (رضي الله عنه), emma ichukuliwe kuwa, "Nakuelekea Wewe kwa kupitia njia ya (jaha) ya Mtume Wako," na "Ewe Muhammad Mimi naelekea kwa (dhati) yako, au kwa (daraja) yako kwa Mola wangu," kama wanavyodai wao, au, "Nakuelekea Wewe kwa njia ya (*du'â'*) ya Mtume Wako," na "Ewe Muhammad Mimi naelekea kwa (*du'â'*) yako kwa Mola wangu," ambao ndiwo msimamo wetu.

Mojawapo ya njia hizi mbili za uwezekano haina budi ikubaliwe na kupendekezwa kutokana na ushahidi wenye kuthibitisha usawa wake. Kwahivyo ama kuhusu msemo wao yakwamba neno lenye kutawala lililoachwa ni 'Jaha/daraja', basi hawana dalili ya hilo, si kwa hadîth hii wala hadîth yoyote nyengine, kwani hakuna kilichotajwa pamoja nacho chenye kuleta ushauri au kutoa taarifa ya kutaja "jaha" au kuliashiriya kabisa. Kama ambavyo hawana lolote kutoka katika Qur'ân wala Sunnah, au kutokamana na mafundisho ya Maswahaba ambapo kulipofanyika *tawassul* kwa jaha ya mtu yoyote. Kwahivyo rai hii yao waliyoipendekeza haina chochote cha kuiunga mkono, na kwahivyo imekuwa haina msingi na haikupewa mazingatio yoyote ya ziyada. Ama kuhusiana na msemo wetu, basi umeungwa mkono na dalili nyingi zilizotangulia.

Kuna jambo jengine linalostahili kutajwa. Ikiwa hadîth ya mtu-kipofu imechukuliwa ili ipatikane maana yake ya dhahiri, ambayo ni

[86] Surah Yûsuf (12):82

[87] Hata kama maneno haya yamewachwa

tawassul kwa kupitia njia ya dhati yake basi itapambana na kubatilisha kauli yake ifuatayo, *"Yâ Allâh! Itakabali shafâ'ah yake kwa niyaba yangu na uitakabali shafâ'ah yangu kwake,"* na hili haliruhusiwi kama ilivyo uwazi wake. Kwahivyo ni sharuti tulete upatanishi baina ya sentensi ya kwanza na ya mwisho na hakuna njia ya kufanya hilo isipokuwa kwa njia ambayo tuliyo-onyesha, *yaani;* yakwamba *tawassul* ilikuwa ni kwa kupitia njia ya *du'â'*. Kwahivyo hili lilithibitishwa, na matumizi yake kama dalili ya *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake limebatilishwa, na kila Sifa njema zinamstahiki Allâh.

Hata kama ingelikuwa ni sawa yakwamba mtu-kipofu alitafuta kufanyiwa *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم), basi itakuwa ni jambo ambalo ni makhsusi kwake yeye, Mtume (صلى الله عليه وسلم), na wala sio jambo la kushirikishwa na Mitume waliobaki na Watu Wema, na kuwaunganisha katika hilo pamoja naye si jambo la kukubalika, kwani yeye, Mtume (صلى الله عليه وسلم), alikuwa ni kiongozi na mtukufu kuwashinda wote. Kwahivyo ingeliwezekana kuwa ni jambo ambalo Allâh alilomuhusisha nalo, kama mambo mengine mengi yaliyopokewa kwenye riwaya zilizo swahîh, na mas'ala ya sifa za kuhusishwa [*khususwiyyât*] hayako ndani ya maeneo ya vipimo vya Qiyâs. Kwahivyo anadhani yakwamba *tawassul* ya mtu-kipofu kwa Allâh ilikuwa ni kwa kupitia njia ya dhati yake Mtume (صلى الله عليه وسلم), basi na akome hapo na wala asiongeze wengine kwenye hilo, kama ilivyopokewa kutoka kwa Imâm Ahmad na ash-Sheikh al-'Izz ibn 'Abdus-Salâm (رحمه الله).

Hili ndilo ambalo linalodaiwa na utafiti wa kitaalamu na haki, na ni Allâh Mwenye kuongoza, na kutuafikia katika yaliyo ya sawa.

KUONDOA UFAHAMU WA KI-MAKOSA

Kufuatia haya imetulazimu yakwamba tufafanue nukta muhimu sana inayohusiana na mas'ala haya nayo ni kwamba tunapokataa *tawassul* kwa kupitia njia ya Jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم*)* na jaha za wengineo miongoni mwa Mitume na Watu Wema, kisha hiyo si kwa sababu ati tunakataa kuwa wao wana daraja ya juu, heshima na

kutambulika mbele ya Allâh, wala sio kutokana na chuki juu yao au kwa sababu nyoyo zetu hazina mapenzi makubwa kwao, ambayo sisi tumetuhumiwa kwa urongo na Dr. Al-Bûtwî kwenye Kitabu chake: *Fiqhus-Sîrah* (Uk.354), ambapo aliposema: "Baadhi ya watu wamepotoka, wale ambao nyoyo zao hazina mapenzi ya Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم), kwahivyo wao wanakataa *tawassul* kupitia kwa njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake..." Kwa hakika Laa! Sio hivyo kabisa. Bali sisi ni, na kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh, miongoni mwa wale wenye kutoa heshima kubwa kwa Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) na wenye mahaba makubwa zaidi kwake, na kuzitambua fadhla zake. Bali ikiwa maneno ya mtu huyu yanaashiriya kitu chochote, basi inaonyesha uovu wa upofu mtupu unaojaza nyoyo za maadui wa *da'wah as- salafîyyah* na chuki walizonazo kwa *da'wah* hii na watu wake, mpaka kufikia kiwango kinachowapelekea kwenye msimamo huu wa hatari mno ulio mgumu. Inawapelekea wao kutekeleza uhalifu huu wa chuki na ukinzani, na kula nyama za ndugu zao Waislamu na kuwatangaza wao kuwa makafiri pasi na dalili yoyote, isipokuwa kwa dhana ambayo ni katika maneno ya urongo zaidi, kama ilivyosemwa na Mtume aliye Mkarimu zaidi (صلى الله عليه وسلم).[88]

Sasa mimi hata sijui jinsi mtu huyu mwenye kujidhulumu nafsi yake anavyojiruhusu kutoa hukmu hii isiyowezekana kutolewa isipokuwa na Allâh (عزّ وجلّ), ambaye Yeye peke Yake ndiye ajuaye siri zote za nyoyo na kilichofichika ndani ya vifua. Wewe wadhania yakwamba yeye hajui hukmu inayomungoja mwenye kufanya hivyo, au ni kwamba anaijua, lakini hata hivyo, chuki zake na uovu wake uliojificha kwa walinganizi wa Sunnah zimempofua kwenye hayo? Ni yoyote mojawapo baina ya hizo mbili, sisi twamkumbusha kuhusiana na hadîth hizi mbili tukufu yakwamba pengine huwenda akatubia kutoka katika makosa yake, aamke kutoka kwenye kutojali kwake kusikokuwa na busara, na atubie kutokamana na vitendo vyake.

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

[88] Imepokewa na al-Bukhârî (tafsiri 8/53/no.90) na Muslim (tafsiri 1361/4/no.6214) na wengineo kutoka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما)

« أيُّما رَجلٍ أكفَرَ رَجُلاً مسلماً، فإن كان كافراً، وإلا كان هو الكافرَ »

"Mtu yoyote mwenye kumtangaza Muislamu kuwa ni kafiri, basi ema kweli ni kafiri, au yeye mwenyewe (yaani; mwenye kuyasema hayo) ndiye kafiri."[89]

Na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

« إِنَّ مِنْ أَرْبَى الرِّبَا الِاسْتِطَالَةَ فِي عِرْضِ الْمُسْلِمِ بِغَيْرِ حَقٍّ »

"Hakika miongoni mwa sampuli mbovu za riba ni kuituhumu heshima ya Muislamu pasi na haki."[90]

Kisha hatimae twamwambia: Wewe huzingatii yakwamba kwa kuyasema maneno haya, wewe unawakanusha Watu Wema wa Ummah huu na kuwatangaza kuwa ni makafiri ma-Imâm wake ambao ni *mujtahidîn*, wasiojuzisha kufanya *tawassul* kupitia kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au yoyote mwengine baada ya kufa kwake. Wakiwemo miongoni mwao kama Abû Hanîfah (رحمه الله) na wenzake, na akasema Abû Hanîfah: "Inanichukiza mimi kwa mtu yoyote kufanya *tawassul* kwa Allâh isipokuwa kupitia njia ya Allâh" kama ilivyotangulia hapo awali.

فَـإِن كُنْــتَ لاَتَــدْرِى فَتِلْــكَ مُصِيْبَــةٌ

'Ikiwa ulikuwa hujui basi huo ni msiba;

وَإِنْ كُنْـتَ تَــدْرِىْ فَـالمُصِيْبَــةُ أَعْظَــمُ

lakini kama ulikuwa wajua, basi msiba ndio mkubwa zaidi.'

Twarudia tena na kusema yakwamba kila mtu mwenye *inswâf* na *ikhlâs* atajua kwa yakini yakwamba sisi, na kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh, ni miongoni mwa wenye mapenzi makubwa kabisa kwa Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) na kutokamana na wenye

[89] Imepokewa na al-Bukhârî (tafsiri 8/80/no.125) na Muslim (tafsiri 1/41/no.116) kutoka kwa Abû Hurairah (*radhiallâhu 'anhu*) na wengineo.
[90] Imepokewa na Ahmad na Abû Dâwud (3/1359/no.4858) kutoka kwa Sa'îd ibn Zayd na isnâd yake ni swahîh.

kuheshimu zaidi daraja yake (صلى الله عليه وسلم), haki zake, na ubora wake, na kwamba yeye ndiye mbora zaidi katika Mitume , na ni Mtukufu wa Manabii, wa mwisho wao na Mbora wao, na rafikiye bendera ya sifa, na *Hawdh*, na *Shafâ'ah* kubwa, na *wasîlah* yenye fadhla kubwa, miujiza ya wazi, na kwamba Allâh (تعالى) amefuta kila dini iliyotangulia kwa dini yake, na akaziteremsha *Āyât* saba zenye kurudiwa mara kwa mara kutoka katika Qur'ân Tukufu, na akalija'aliya Taifa lake kuwa ndilo bora lililowahi kuletewa watu, mpaka mwishoni mwa sifa zake zote na fadhla zake zenye kudhihirisha wazi daraja yake na utukufu wake, twamuomba Allâh Amteremshie Sifa Zake na Baraka Zake za Amani zilizo kamilifu juu yake na jamii yake na wafuasi wake wa kweli.

Kila sifa na shukrani zinamstahiki Allâh, sisi ni miongoni mwa wa kwanza katika watu, juu ya kuthibitisha hayo yote, na labda cheo chake (صلى الله عليه وسلم) kimesalimika katika kulindwa kwa mbali, na sisi kuliko walivyo wengine wenye kudai kumpenda na kujionyesha kuwa wanatambua daraja yake.

Hatahivyo, lenye kuhesabika hapa ni kule kumfuata yeye (صلى الله عليه وسلم) kwa kweli, kumfuata katika maarisho yake, na kujiepusha na aliyotukataza. Kama alivyosema Allâh (سبحانه وتعالى):

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۚ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ٣١

Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda Allâh, basi nifuateni; (hapo) Allâh atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. Na Allâh ni Mwenye maghufira (na) Mwenye rehema."[91]

Kutokana na fadhla za Allâh, sisi ni miongoni mwa walio mahodari zaidi katika upande wa kumtwi'i Allâh (عزّ وجلّ) na katika kumfuata Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم), na hizi ndizo dalili mbili za kihakika za mapenzi ya dhati na mahaba, kinyume cha kutia chumvi katika

[91] Sûrat Āli-'Imrân (3):31

kumtukuza na kuvuka mipaka katika kumsifu mtu, mambo yote hayo mawili ambayo yaliyokatazwa na Allâh (سبحانه):

يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ لَا تَغۡلُواْ فِي دِينِكُمۡ وَلَا تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡحَقَّۚ ١٧١

“Enyi watu wa Kitabu (Mayahudi na Manaswara)! Msipindukie mipaka katika dini yenu, wala msiseme juu ya Allâh ila yaliyo kweli.”[92]

Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwakataza, kwa kuwaambia:

« لَا تُطْرُونِي كَمَا أَطْرَتِ النَّصَارَى ابْنَ مَرْيَمَ ، فَإِنَّمَا أَنَا عَبْد، فَقُولُوا:عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ »

“Musitie chumvi katika kunisifu mimi kama walivyotia chumvi Manaswara katika kumsifu ibn Maryam (‘Isa). Kwani kwa hakika mimi ni mja, basi semeni ‘Mja wa Allâh na Mtume Wake’.[93]

Na katika yanayostahiki kuelezwa ni kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyatangaza hayo kutokamana na kuvuka mipaka katika dini kumuhusu mwenye kufanya Hajj yakwamba amekhiyarishwa pindi anapotaka kurusha vijiwe kwenye nguzo akiwa Minâ atumie changarawe kubwa, na akaamrisha changarawe zenyewe ziwe za kiyasi kinachoweza kurushika (kwa vidole). Kutoka kwa ibn ‘Abbâs (رضي الله عنهما), aliyesema: “Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) aliniambia katika wakati wa asubuhi wa *al-‘Aqabah*: *Hebu nipe vijiwe vidogo vya kurusha*”. Akasema: “Basi nikamtafutia vijiwe vikubwa kiyasi, kisha nilipomkabidhi mikononi mwake akaniambia: *mfano wa haya* (mara tatu) *na jitahadharini na kuvuka mipaka katika dini, kwani wale waliokuja kabla yenu waliangamizwa kutokana na kuvuka mipaka katika dini.*[94]

---

[92] Sûrah an-Nisâ’ (4):171

[93] Imepokewa na al-Bukhârî (tafsiri 4/435/no.654) na wengineo.

[94] Imepokewa na Ahmad (1/215 na 347), an-Nasâ’î, Ibn Mâjah na wengineo. Inapatikana katika kitabu change *as-Swahîhah* (no.1283) na *Takhrîj as-Sunnah Li-ibn Abî ‘Āsim* (no.98)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Hii ni kwa sababu alihisabu kule kurusha vijiwe kuwa ni miongoni mwa vitendo vya kisheriya ambako lengo lake lilikuwa ni kumkanusha na kumpiga vita Sheitwani, na wala kihakika sio kumuuwa hapohapo. Kwahivyo Muislamu hapa anatakiwa atekeleze amri na amkanushe na kumkataa Sheitwani, adui wa ki-maadili wa wana-adamu, aonyeshe uadui kwake, hilo tu. Kisha licha ya tahadhari hii kali dhidi ya kuvuka mipaka katika dini, Waislamu kwa bahati mbaya wametumbukia ndani yake na wakafuata njia za watu walioteremshiwa Kitabu, mpaka akasema mmoja wao:

> "Weka kando wanayodai Manaswara kumuhusu Mtume wao – Lakini wewe fikiliza sifa yoyote nyengine upendayo juu yake [Muhammad (صلى الله عليه وسلم)] na ufanye hivyo kama utakavyojiamulia wewe mwenyewe."

Shairi hili limetukuzwa mno na Waislamu wengi, wenye kuiimba mara kwa mara Qaswida hii iliyo maarufu kwa jina la *al-Burdah*, na wanatafuta kuitumia kama baraka; huisoma katika siku wanapoadhimisha kusherehekea mazazi, na katika baadhi ya mikusanyiko ya vikao vya mawaidha au vikao vya 'ilmu; kwa sababu wanadhania yakwamba hili ni jambo lenye kuwakurubisha kwa Allâh (تبارك وتعالى), na kwamba ndiyo dalili ya mapenzi yao kwa Mtume wao (صلى الله عليه وسلم). Mshairi huyu anadhani yakwamba makatazo yaliyopokewa kutoka kwenye hadîth iliyotangulia ni ya kujilinda na madai yakwamba Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni mtoto wa Allâh, kwahivyo amekataza matamshi haya makhsusi, lakini akawa analingania kwenye matamshi yoyote mengine sura yawayo. Hili ni kosa la hatari kubwa na upotofu ulio wazi kwani sifa za kupita mipaka zilizokatazwa kwenye hadîth zina maana mbili. Ya kwanza yao ni sifa zisizo na mipaka, na ya pili yao ni sifa zinazovuka mipaka. Sasa juu ya haya huwenda ikawa yakwamba hadîth yenye kukataza maana yake ni makatazo ya kumsifu yeye (صلى الله عليه وسلم), kwa ajili ya kuzuiya kuvuka mipaka, na kutosheka na uhakika yakwamba Allâh (تعالى), alimchagua yeye kuwa ni Mtume na Nabii, na kama kipenzi chake mteule, na kwa hayo Alimsifu kwa maneno:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ؛

“Na bila shaka una tabia njema kabisa.”[95]

Ni kwa lipi inamkinika mwana-adamu yoyote kusema la kumuhusu yeye baada ya maneno haya ya Allâh (تبارك وتعالى)? Ni thamani gani ya neno lolote watakalosema itakayobeba zaidi ya ushahidi huu wa Allâh (تبارك وتعالى)? Kwa hakika sifa kubwa zaidi tuwezayo kumpa yeye (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba twayasema ya kumuhusu yeye yale ambayo Mola wetu (عزّ وجلّ) aliyoyasema: yakwamba yeye ni Mja Wake na Mtume Wake. Hii ni shahada kubwa zaidi ipatikanayo katika fadhla zake (صلى الله عليه وسلم) na haina vishawishi vya kupinduka mipaka, wala vya kulegeza kuhusiana na haki zake anazostahiki na heshima yake. Kwahivyo Mola wetu (سبحانه), alimsifu yeye pindi alipokuwa kwenye daraja ya juu kabisa ya heshima aliyopewa na Allâh (تعالى), na hiyo ilikuwa wakati alipomchukuwa kwenye safari ya usiku na kumfanya apande mpaka katika wingu wa juu zaidi, na akamuonyesha alama kubwa kubwa za Mola wake, kufikia hapo alimsifu kwa sifa ya kuwa kwake ni mtumwa/mja, kwa kusema:

سُبۡحَٰنَ ٱلَّذِيٓ أَسۡرَىٰ بِعَبۡدِهِۦ لَيۡلٗا مِّنَ ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡحَرَامِ إِلَى ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡأَقۡصَا ١

“Utukufu ni wake Yeye [mbali na yote wanayomshirikisha Nae] ambaye alimpeleka mja wake usiku (mmoja tu) kutoka Msikiti Mtukufu (wa Makkah) mpaka Msikiti wa mbali (wa Baytul Muqaddas-Falastini).”[96]

Vilevile pana uwezekano yakwamba maana (ya hadîth) ni: Musivuke mipaka katika kunisifu mimi, mpaka mukawa munanisifu kwa mambo yasiyokuwa ya sawa kwangu, na kwamba mukanisifu kwa baadhi ya mambo yaliyo makhsusi kwa Allâh (تبارك وتعالى).

Labda huwenda ikawa maana iliyo ya sawa zaidi ni ya kwanza kutokana na mas’ala mawili:

[95] Sûrah al-Qalam (68):4
[96] Sûratul Isrâ’ (17):1

i. Ukamilifu wa hadîth ambayo ni maneno yake (صلى الله عليه وسلم):

« فَقُولُوا: عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ »

Basi semeni: Mja wa Allâh na Mtume Wake.

Kumaanisha: Toshekeni na sifa ambayo Allâh (عزّوجلّ) aliyonipa mimi, yakwamba Yeye amenichagua mimi kama Mja Wake na Mtume Wake.

ii. Kichwa cha Mlango ambacho baadhi ya wanavyuoni walichokipa jina kwa hadîth hii. Kwahivyo kwa mfano, Imâm at-Tirmidhî ameiweka chini ya kichwa: "*Ukarimu wa Mtume (* صلى الله عليه وسلم*)."* Kwahivyo ameichukulia hadîth kuwa ni makatazo ya kusifu, kwani kwa vile hilo ndilo lililothubutu kwa maana ya ukarimu na kuingiliana nalo.

NYONGEZA KATIKA HADÎTH YA MTU-KIPOFU

Inatakiwa ijulikane yakwamba katika riwaya nyengine za hadîth iliyotangulia ya mtu-kipofu palitokea nyongeza mbili ambazo hapana budi kuzibainisha udhaifu wake na kwenda kinyume kwake na yaliyoswihi, ili msomaji apate uangavu kuhusiana nazo na hatoweza kudanganyika kwa kauli za wale wenye kuzitumia kama dalili ili wapate kupinga yaliyo ya kweli na haki.

Nyongeza ya Kwanza

Nyongeza ya Hammâd ibn Salamah aliyesema yakwamba Abû Ja'far al-Khatwamî alitusimulia sisi: ..., na akainukuu silsila yake ya riwaya kama katika riwaya ya Shu'bah, na vilevile *matn* yote (maandiko) isipokuwa yakwamba aliifanyia mukhtasari kiyasi na akaongezea mwishoni mwake baada ya kauli yake: "Na Mtume wangu akaniombea kwa niyaba yangu nirudishiwe kuona kwangu." Aliongezea: "Na uwapo una mahitaji basi fanya kama hivyo." Imepokewa na Abû Bakr ibn Abî Khaithamah katika *tarîkh* yake, na akasema: "Ametusimulia Muslim ibn Ibrâhîm, akatusimulia Hammâd ibn Salamah ..."

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Nyongeza hii imetangwa kuwa ni *dha'îf* na Sheikh ul-Islâm ibn Taymiyyah katika *al-Qâ'idatul-Jaliyyah* (Uk.102) kutokana na kupokewa kwake na Hammâd ibn Salamah peke yake, na uhakika yakwamba amekhalifu riwaya ya Shu'bah ambaye ndiye mpokezi anayeaminika zaidi aliyeipokea hadîth hii. Tangazo hili la udhaifu kwa ajili hii kwa hakika linaafikiyana na misingi wa ta'luma ya Hadîth na wala haikhalifiani kivyovyote. Ama kuhusu kauli ya al-Ghummârî katika *al-Misbah* (Uk.30) yakwamba Hammâd ni mtu *thiqah* (mtegemewa), na ni mpokezi anayetegemewa na waandishi wa swahîh, na kwamba nyongeza za mpokezi anayetegemewa zinakubaliwa, basi hii ni ema kupitikiwa kutokana na kughafilika au ni kujifanyiza kusahau katika 'ilmu ya hadîth. Hii ni kwa sababu kukubali kwa sampuli hiyo ni mpaka ipatikane sharuti juu ya uhakika yakwamba mpokezi asimukhalifu mpokezi mwengine anayetegemewa zaidi kuliko yeye, amesema *al-Hâfidh* katika *Nukhbatul-Fikr*: "Na nyongeza inakubalika maadamu haikhalifiani na mpokezi anayetegemewa zaidi. Lau itakwenda kinyume na ambayo inayotegemewa zaidi, basi ile inayotegemewa zaidi ndiyo ambayo itakayotangazwa kuwa ni ya sawa na kuhifadhiwa (*mahfûdh*) na hiyo nyengine kutangazwa kuwa ni *dha'îf* kutokana na kukhalifiana na ambayo inayotegemewa zaidi (*shâdh*).

Sharuti hili halipatikani hapa kwani Hammâd ibn Salamah, hata ingawa yeye akiwa ni mmojawapo wa wapokezi waliotumiwa na Muslim, bado atabaki bila ya shaka yoyote yeye yuko chini ya daraja ya Shu'bah katika kuhifadhi. Uhakika utakubainikia iwapo utarejelea kwenye wasifu wao, wote wawili katika vitabu vya chimbuko. Wa kwanza wao ametajwa na *adh-Dhahabî* katika kitabu chake *al-Mîzân*, na ndani yake alitaja wale ambao ukosoaji wao uliosawazishwa tu, na akamsifu yeye kama "mtegemewa lakini hufanya makosa," haliyakuwa hamtaji Shu'bah kabisa katika kitabu hicho. Vilevile tafauti iliyoko baina yao itaonekana kwa kuzingatia kwa makini wasifu wa kila mmoja wao ambao aliouleta *al-Hâfidh* [Ibn Hajr]. Amesema katika *at-taqrîb*: "Hammâd ibn Salamah: Mtegemewa, mwenye kufanya 'Ibada, mpokezi anayetegemewa zaidi kutoka kwa Thâbit, na fahamu zake zilidhoofika katika maisha yake ya baadae," na akasema: "Shu'bah ibn al-Hajjâj: Mtegemewa, mwenye kuhifadhi kwa haraka, muangalifu mwenye hadhari; ath-Thawrî alikuwa akipenda kusema: 'Huyu ni (*Amîrul-Mu'minîn*) kiongozi wa waumini kuhusiana na hadîth,' naye ndiye aliyekuwa wa kwanza miongoni mwa

watu wa ‘Irâq kuanza kuchunguza ukweli wa wapokezi; aliitetea Sunnah na alikuwa ni mwenye kufanya ‘Ibada.” Haya yanapokudhihirikia wewe, hapo ndipo utakapojua yakwamba Hammâd ibn Salamah anapomukhalifu Shu’bah katika riwaya yake ya hadîth ina maana yakwamba nyongeza hii haikubaliki, kwani ni kinyume cha riwaya ya mpokezi ambaye ni mtegemewa zaidi, na kwahivyo ni *shâdh* (riwaya iliyo *dhaifu* inayokwenda kinyume na riwaya inayotegemewa zaidi), kama inavyo-onekana kutoka katika kauli ya *al-Hâfidh* iliyonukuliwa hapo awali kutoka katika *Nukhbatul-Fikr*. Vilevile huwenda ikawa yakwamba Hammâd aliipokea hadîth hii baada ya fahamu zake kudhoofika na akatumbukia kwenye makosa. Ni kama kwamba Imâm Ahmad alikuwa akiashiriya udhaifu wa nyongeza hii kwani aliipokea hadîth kwa njia ya Mu’ammal (ambaye ni Ibn Ismâ’îl), kutoka kwa Hammâd, baada ya riwaya iliyotangulia ya Shu’bah, lakini hakuyanukuu matamshi ya hadîth (pamoja na nyongeza), bali, aliihusisha nyuma kwenye matamshi ya hadîth ya Shu’bah na akasema: “Na akaitaja hadîth.” Vilevile inawezekana yakwamba nyongeza haipatikani katika riwaya ya Mu’ammal kutoka kwa Hammâd, jambo ambalo pia litakalofafanua ni kwa nini Imâm Ahmad hakuitaja, kwani mafundisho ya wanavyuoni na [*mahuffâdh*] wenye kuhifadhi pindi wanapoihusisha riwaya kama hiyo nyuma kwenye kauli yake iliyotangulia ni kwamba vilevile hutaja matamshi yoyote ya nyongeza yasiyopatikana katika riwaya ya kwanza. Kwahivyo katika kuhitimisha, matamshi ya nyongeza hayakuswihi kutokana na yenyewe kuwa ni *shâdh* (kwenda kinyume na riwaya inayotegemewa zaidi).

Lau hata kama ingelikuwa ni swahîh haingelikuwa ni dalili ya kuruhusiwa kwa *tawassul* kwa kupitia njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم) binafsi, kwani kauli yake: “Kisha ufanye tena kama hivyo” yanaweza kufahamika: uje tena kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiwa bado yuko hai na umtake akuombee na ulifanye hilo kuwa njia ya *tawassul*, na utawadhe, na uswali, na kisha aisome ile *du’â’* ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyomfundisha aombwe kwayo, na Allâh ni Mjuzi zaidi.

Nyongeza ya Pili

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kisa cha mtu aliyekuja kwa ‘Uthmân ibn ‘Affân na akamtumia Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama njia ya *tawassul* ili mahitaji yake yapate kutekelezwa. Imepokewa na at-Twabarânî katika *al-Mu’jamus-Swaghîr* (Uk.103-104) na katika *al-Kabîr* (3/2/1-2) kwa njia ya ‘Abdullâh ibn Wahb, kutoka kwa Shabîb ibn Sa’îd al-Makkî, kutoka kwa Rawh ibn al-Qâsim, kutoka kwa Abû Ja’far al-Khatamî al-Madanî, kutoka kwa Abû Umâmah ibn Sahl ibn Hanîf, kutoka kwa Mjombake [kwa upande wa baba] ‘Uthmân ibn Hanîf: “Yakwamba mtu mmoja alikuwa na mazoweya ya kwenda kwa ‘Uthmân ibn ‘Affân (رضي الله عنه), kwa mahitaji aliyokuwa nayo, na ‘Uthmân hakuwa akimtafiti na kumtimizia haja zake, basi akamkuta ‘Uthmân ibn Hanîf na akamlalamikia kuhusu suala hilo, basi ‘Uthmân akamwambia: “Nenda mahali pa kutawadha, utawadhe, kisha uje Msikitini uswali ndani yake rak’ât mbili, kisha useme: ‘Yâ Allâh! Nakuomba Wewe na nakuelekea Wewe kwa kupitia kwa Mtume Wako Muhammad (صلى الله عليه وسلم), Mtume wa Rehma, Ewe Muhammad naelekea kwa kukutumia wewe kwa Mola wako (عزّوجلّ), ili Yeye apate kunitekelezea mimi haja zangu,’ na hapo uyataje mahitaji yako, kisha urudi kwangu ili nipate kuondoka pamoja na wewe. Basi yule mtu akenda na akafanya kama alivyoelezwa, kisha wote wakenda kwenye mlango wa ‘Uthmân ibn ‘Affân (رضي الله عنه). Basi mlinzi wa mlangoni akaja akamshika mkono wake akamuingiza ndani na akamkalisha kwenye mkeka pamoja naye [‘Uthmân ibn ‘Affân]. Akamwambia: “Mahitaji yako ni nini.” Basi akamueleza naye akamkidhia haja yake, kisha akamwambia: “Mpaka sasa sijakumbuka mahtaji yako,” na akasema: “Kila utakapokuwa wahitaji kitu basi wewe njoo kwetu.” Kisha yule mtu akamuacha hapo na akakutana na ‘Uthmân ibn Hanîf na akamueleza: “Namuomba Allâh akujazi kheri, hakuwa akinishughulikia katika mahitaji yangu wala hakunitambua kamwe mpaka pale wewe ulipomzungumzia suala lenyewe.” Basi ‘Uthmân ibn Hanîf akasema: “Wallâhi mimi hata sijawahi kuzungumza naye, lakini niliwahi kushuhudia tukio fulani pindi mtu mmoja aliyekuwa kipofu alipomjia Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akamlalamikia kuhusu kupoteza uwezo wa kuona. Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia yakwamba afanye subira, basi akasema: “Ewe Mjumbe wa Allâh, mimi sina mtu yoyote wa kunishika mkono akaniongoza njia.” Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *Nenda*

kwenye sehemu ya kutawadha, na utawadhe, kisha uswali rak'ât mbili, kisha uombe kwa du'â' hii." 'Uthmân ibn Hanîf akasema: Wallâhi hatukuwachana, na tukazungumza kwa muda mrefu, mpaka yule mtu-kipofu akatuingilia tena na ilikuwa utadhani kana kwamba hakuwahi kuwa na matatizo yoyote na macho yake."

Amesema *at-Twabarânî*: "Hakuna yoyote aliyeipokea kutoka kwa Rawh ibn al-Qâsim isipokuwa Shabîb ibn Sa'îd, Abû Sa'îd al-Makkî na yeye ni mtegemewa. Yeye pia ndiye ambaye Ahamd ibn Shabîb anapokea kutoka kwake, akipokea kutoka kwa babake, kutoka kwa Yûnus ibn Yazîd al-Aylî. Hadîth vilevile imepokewa kutoka kwa Shu'bah kutoka kwa Abû Ja'far al-Khatamî, ambaye jina lake ni 'Umayr ibn Yazîd, naye ni mtegemewa. Imepokewa kutoka kwa Shu'bah peke yake na 'Uthmân ibn 'Umar ibn Fâris, *na hadîth ni swahîh."*

Hapana shaka kuhusu uswahîh wa hadîth hiyo, bali kinachohitaji kuchunguzwa hapa ni kisa hiki kilichosimuliwa na Shabîb ibn Sa'îd peke yake kama ilivyoashiriwa na *at-Twabarânî.* Kwa hakika mpokezi huyu Shabîb amekosolewa, hususan kuhusiana na yale ambayo Ibn Wahb aliyoyapokea kutoka kwake. Kisha tunakuta hapa yakwamba vilevile kuna wengine wenye kupokea kutoka kwake: Ismâ'îl na Ahmad, vijana wawili wa Shabîb ibn Sa'îd aliyetangulia kutajwa. Ama kumuhusu Ismâ'îl, basi mimi simjui na wala simuoni yoyote mwenye kumtaja yeye. Kwa hakika walimuachilia mbali kiyasi cha kwamba wakawa hata hawamtaji miongoni mwa waliokuwa wakipokea kutoka kwa babake, kinyume cha alivyokuwa ndugu yake, Ahmad, kwani huyu ni *Sadûq* (anyekubalika kwa ujumla). Ama kuhusu babake, Shabîb, basi wanachosema kumuhusu yeye ni, katika kuhitimisha, yakwamba alikuwa ni mtu wa kutegemewa, ingawa alikuwa na udhaifu katika fahamu zake, isipokuwa kwa zile riwaya zilizopokewa na mwanae, Ahmad, kutoka kwake, ambazo yeye mwenyewe alizozipokea, *hususan,* kutoka kwa Yûnus aliyekuwa ni dalili katika hali yoyote iwayo. Amesema adh-Dhahabî katika *al-Mîzân*: "*Sadûq* (anyekubalika kwa ujumla) anayekosea, Ibn 'Adiyy amemtaja katika kitabu chake *Kâmil* na akasema: "Ana nakala za stakabadhi za maandishi za hadîth kutoka kwa Yûnus ibn Yazîd, ni jambo la sawa. Ibn Wahb amepokea baadhi ya mambo dhaifu yanayostahiki kukemewa kutoka kwake. Amesema Ibnul-Madînî: "Alikuwa na mazoweya ya kwenda Egypt kwa biashara na riwaya zake za kunukuu

ni za kutegemeka na ameandikiwa kutoka kwake na mwanaye, Ahmad." Amesema Ibn Adiyy: "Mara nyengine Shabîb huteleza akafanya makosa pindi akinukuu kutoka kwenye fahamu zake, natumai hakuwa akifanya hivyo kwa makusudi. Kisha pindi mwanaye Ahamd anapopokea kutoka kwake kwa hadîth ya Yûnus, basi utadhani yakwamba ni Yûnus mwengine tafauti, kwa maana yakwamba: huzifanya kuonekana nzuri." Kwahivyo kauli hii inamaanisha yakwamba *ahâdîth* zote za mpokezi huyu, Shabîb, ziko sawa kwa masharuti mawili:

i. Yakwamba zimepokewa kutoka kwake na mwanaye Ahmad.

ii. Shabîb huyu anapokea kutoka kwa Yûnus. Sababu ikiwa ni kwamba alikuwa na stakabadhi za maandishi ya Yûnus ibn Yazîd, kama alivyosema Ibn Abî Hâtim, katika *al-Jarh wat-Ta'dîl,* kutoka kwa babake (2/1/359), kwahivyo pindi anaponukuu kutoka kwenye vitabu vyake, basi hunukuu kisawasawa, lakini anaponukuu kutoka katika fahamu zake hufanya makosa kama anavyosema Ibn 'Adiyy.

Kwahivyo maneno ya al-Hâfidh kwenye wasifu wake katika *at-Taqrîb*: "*Ahâdîth* zake zote ziko sawa zinapopokewa kutoka kwake na mwanaye Ahamd, lakini sio zinapopokewa kutoka kwake na Ibn Wahb," huwa na upungufu, kwani huleta hisiya yakwamba riwaya zote za mwanaye Ahamd za kutoka kwake ni zenye kukubalika. Hali si kama hivyo. Bali hili ni sharuti juu ya uhakika yakwamba hizo ni ahâdîth ambazo yeye mwenyewe binafsi amezipokea kutoka kwa Yûnus, kama zilivyotangulia. Hili limezidi kuthibitishwa kwa uhakika yakwamba *al-Hâfidh* mwenyewe ameashiriya sharuti hili mahali kwengine. Kwa hakika, alimtaja Shabîb akiwa miongoni mwa wale wapokezi waliotumiwa na al-Bukhârî ambao waliokosolewa, ipatikanayo kwenye utangulizi wa *Fat-hul Bârî* (Uk.133), kisha akakataa ukosoaji huu, baada ya kuwanukuu wale ambao waliomtangaza yeye kuwa ni mtegemewa na kutaja kauli ya Ibn 'Adiyy kumuhusu yeye, akisema: "Mimi nasema: al-Bukhârî anazileta ahâdîth zake zilizopokewa kutoka kwake na mwanaye, ambazo yeye mwenyewe amezipokea kutoka kwa Yûnus, lakini haleti kitu chochote alichokipokea yeye kutoka kwa yoyote asiyekuwa Yûnus, na wala hanukuu kitu chochote ambacho Ibn Wahb alichopokea kutoka kwake.." Sasa kwahivyo, huyu hapa (رحمه الله), anatoa ishara yakwamba ukosoaji uko sawa kumuhusu Shabîb pindi anapopokea kutoka kwa

asiyekuwa Yûnus, hata kama ni mambo ambayo mwanaye Ahmad amepokea kutoka kwake. Hili ndilo la sawa kama tulivyoeleza sasa hivi, na kwa muangaza wake inatupasa kufahamu anayoyasema katika *at-Taqrîb* kwa ajili ya kufanya upatanishi baina ya kauli yake na kujiepusha kuleta mfarakano.

Kwahivyo hili linapobainika, basi udhaifu wa kisa hiki utakuwa wazi, na ukosefu wa uzuri wake kama dalili. Kisha udhaifu wa zaidi ndani yake umejitokeza kwangu, nao ni kuwepo kwa riwaya zinazokhalifiana kutoka kwa Ahmad ibn Shabîb. Hadîth hiyo vilevile imepokewa na Ibn Sunnî' katika *'Amalul-Yawm wal-Laylah* (Uk.202) na cha al-Hâkim (1/526) kwa njia ya silsila tatu kutoka kwa Ahmad Ibn Shabîb pasi na utajo wowote unaohusiana na kisa hicho kilichoshikamanishwa. Inaelekea kana kwamba imepokewa na 'Awn ibn 'Umârah al-Basrî: Rawh ibn al-Qâsim ametusimulia sisi kwa hiyo. Hii imepokewa na al-Hâkim. Kisha hata kama mpokezi huyu, 'Awn, alikuwa ni dha'îf, lakini angalau riwaya yake inastahiki kutangulizwa kuliko riwaya ya Shabîb kwa sababu yeye amekubaliwa ndani yake na Shu'bah na Hammâd ibn Salamah, kutoka kwa Abû Ja'far al-Khatamî.[97]

Kwahivyo katika uhitimisho ni kwamba kisa hiki ni dha'îf na kinaeleza ilivyo kinyume cha yaliyoswihi kupokewa kutokana na sababu tatu:

i. Kudhoofika kwa fahamu za aliye pekeyake katika kuipokea;

ii. Na riwaya zinazokhitilafiana zitokazo kwake;

iii. Kuwakhalifu kwake hao wapokezi wenye kutegemewa ambao hawakuitaja katika hadîth.

Moja tu katika sababu hizi itatosha kukikataa kisa hiki, jee itakuwaje zitakapokuwa zote tatu zipatikane kwa pamoja?

Mojawapo miongoni mwa mifano ya *ta'assub* [ushupavu wa ki-Upofu] za kushangaza na kufuata matamaniwa ya nyoyo ni kwamba Sheikh al-Ghumârî amenukuu riwaya mbalimbali za kisa hiki katika *al-Misbah* (Uk.12 na 17) kwa njia ya al-Bayhaqî katika *ad-Dalâ'il*, na at-Twabarânî, na kisha hasemi kitu chochote kuhusiana na udhaifu au uswahîh wake. Sababu yake iko wazi. Ama kuhusu uthibitishaji wa

[97] Nukta ya Mfasiri: Hakuna miongoni mwao anayesimulia kisa cha nyongeza chenye kumuhusu 'Uthmân ibn 'Affân.

kuswihi kwake, basi haimkiniki kulingana na 'ilmu ya hadîth, na kuhusu uthibitishaji wa udhaifu wake, basi hiyo ndiyo haki, lakini...

na mfano wake ametekeleza yule aliyenyimwa kuwa na usawa katika *al-Isâbah* (Uk.21-22) aliyeinukuu hadîth pamoja na kisa hiki na kisha wakasema: "Na hadîth hii imetangazwa kuwa ni swahîh na at-Twabarânî katika *as-Swaghîr* na *al-Kabîr*"?! Lakini kauli hii, licha ya ujasiri wake imejaa nukta za kijinga:

I. At-Twabarânî hakuitangaza hadîth hii kuwa ni swahîh katika *al-Kabîr* lakini badala yake aliitangaza katika *as-Swaghîr* peke yake. Nawanukulia wasomaji hadîth, moja kwa moja kutoka katika kitabu chake, wala siichukui kutoka kwenye asili yoyote ya *wâsita* kama wafanyavyo hawa watu wenye kiwango kichache sana cha fungu la hii 'ilmu tukufu. "Na yoyote atekae maji kutoka kwenye bahari ataijaza mifereji ya umwagiliaji wa kilimo."

II. At-Twabarânî aliitangaza hadîth peke yake kuwa ni swahîh, na wala si kisa kama inavyo-onyesha katika kauli yake, kama ilivyotangulia: "Na hadîth imepokewa na Shu'bah... na hadîth ni swahîh." Kwahivyo hii ni kauli iliyo wazi yakwamba aliyokuwa akiyazungumza yalihusu hadîth hiyohiyo kama ile iliyopokewa na Shu'bah, na Shu'bah hakusimulia kisa hicho, kwahivyo At-Twabarânî hakuitangaza hadîth hiyo kuwa ni swahîh, kwahivyo hawana dalili katika kauli yake.

III. Hata kama kisa hicho kingelikuwa ni swahîh kutoka kwa 'Uthmân ibn Hanîf, basi kwenye kisa chenyewe hakuifundisha *du'â'* kamili kwa mtu-kipofu. Bali alikinyamazia kifungu kisemacho: "Yâ Allâh! Ikubali *Shafa'ah* yake kwangu mimi, (*yaani;* mtakabalie yeye awe ni muombezi wangu), na uikubali *Shafa'ah* yangu kwake yeye, (*yaani;* nitakabalie *du'â'* yangu ya kumkubalia maombi yake)." Kwani angelikuwa ni mwenye kufahamu, kwa ufasaha wake wa lugha ya Ki-Arabu, yakwamba kauli hii ingelishurutisha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) angelipaswa kumuombea mtu huyu, kama ambavyo alivyomuombea yule mtu-kipofu. Kisha kwa vile hilo halikuwezekana kuhusiana na mtu yule hakuyataja maneno hayo. Amesema Sheikhul-Islâm ibn Taymiyyah (Uk.104): "Na kama ijulikanavyo iwapo mtu atasema baada ya kufa kwake, Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Yâ Allâh! Mtakabalie kama muombezi wangu, na uitakabali *du'â'* yangu ya

kumtakabalia *du'â'* yake,' licha ya uhakika yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumuombea *du'â'*, kisha kauli hii ya mtu itakuwa ni ya *bâtwil*. 'Uthmân ibn Hanîf hakumuamrisha amuombe Mtume (صلى الله عليه وسلم) kitu chochote, wala hakumwambia aseme "Mkubalie kama muombezi wangu," wala hakumuamrisha aombe *du'â'* yote kamili, bali alimuamrisha kwa sehemu yake. Hapakuwa na haja ya kuwepo na *du'â'* kwa niyaba yake kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala jambo lolote liwezekanalo kudhaniwa kama hivyo, kwahivyo iwapo mtu angelisema baada ya kifo chake: "Basi mtakabalie yeye kama muombezi wangu" hapo itakuwa ni kauli isiyokuwa na maana yoyote. Kwahivyo 'Uthmân hakuamrisha, wala hakuamrisha *du'â'* kama ilivyoamrishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). La zaidi ni kwamba, aliloamrisha lilikuwa ni jambo ambalo halikupokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na jambo kama hili haliwezi kutumiwa katika kuthibitisha chochote katika Sheriya, kama ambavyo kitu chochote ambacho ni rai ya Swahaba mmoja peke yake, emma kihusiane na fadhla za baadhi ya vitendo vya 'ibada, vitendo vya kuruhusiwa, vitendo vya kuwajibika, au vya haramu, pindi kauli zao zisipopata kuungwa mkono na Maswahaba wengine, na yale yaliyopokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni ema kinyume chake, au kwa uchache hayayathibitishi hayo. Kisha katika hali kama hiyo kitendo chake hakitokuwa ni katika sehemu ya Sunnah ambayo ni lazima ifuatwe na Waislamu. Bali la zaidi liwezalo kusemwa kuhusiana nalo ni kwamba ni jambo ambalo hatima ya kukatikiwa ya wanavyuoni (*ijtihâd*) inaweza kutumika, na suala ambalo Ummah walilokhitilafiana kwalo, kwahivyo ni lazima liregeshwe nyuma kwa Allâh na Mtume Wake."

Kisha akataja mifano mengi ya mambo ambayo yaliyokuwa ni rai za Maswahaba fulani na ambayo hayakupata kufuatwa, kwa mfano kupenyeza maji kwa Ibn 'Umar chini ya kigubiko cha jicho wakati wa kutawadha na kadhaalika, kwahivyo rejea kwenye hilo. Kisha akasema: "Basi ikiwa hali itakuwa hivyo, basi kama ijulikanavyo, kama ingelikuwa imethibitishwa kutoka kwa 'Uthmân ibn Hanîf au mtu mwengine yakwamba alitangaza yakuwa imefaradhishwa au kukokotezwa yakwamba mtu na afanye *tawassul* kwa kupitia njia ya jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake, pasi na Mtume

(صلى الله عليه وسلم) kumuombea yeye *du'â'*, wala kumshufaiya kwa hilo, basi tutajuwa yakwamba 'Umar na Maswahaba wakubwa hawakulizingatia hilo kufaradhishwa baada ya kufa kwake kama lilivyofaradhishwa katika uhai wake. Bali katika zama za uhai wake walikuwa wakifanya *tawassul* kwa kumtumia Mtume (صلى الله عليه وسلم) walipokuwa wakiomba mvua alipokuwa hai, lakini baada ya kufa kwake hawakufanya *tawassul* kwa kupitia kwake. Bali 'Umar alisema katika *du'â'* iliyoswihi kupokewa na ambayo ni mashuhuri kutoka kwake, iliyoafikiwa na wanavyuoni, na ilifanywa kwenye mwaka uliokuwa maarufu wa ukame na maangamivu katika hadhara ya Muhâjirûn na Answâr, pindi maafa ya ukame yalipozidi mpaka 'Umar akaapa yakwamba samli swafi isitumiwe mpaka mazao yarudi. Kisha akawaswalisha watu swala ya mvua na akasema: "Yâ Allâh! tulipokuwa tukikumbwa na ukame tulikuwa na mazoweya ya kumtumia Mtume wetu kama njia ya kujikurubisha Kwako Wewe na Wewe ulikuwa ukitupa mvua, sasa twatafuta kujikurubisha Kwako kwa kumtumia mjombake Mtume wetu, basi twakuomba utupe mvua," na walikuwa wakibarikiwa na mvua. Kisha maombi haya yaliafikiwa na Maswahaba wote waliokuwepo hapo, na wala hakuna miongoni mwao aliyelikosoa jambo hilo nalo lilikuwa ni jambo maarufu sana. Kwahivyo hii ndiyo iliyokuwa mojawapo ya hali ya kudhihirika ya muafaka wa mjumuiko (*ijmâ'*). Kisha maombi kama hayo yalifanywa na Mu'âwiyah ibn Abî Sufyân katika zama za Ukhalifa wake, na iwapo kutafuta *tawassul* kwa njia ya kupitia kwa Mtume baada ya kufa kwake ni kama kutafuta *tawassul* kwa njia ya kupitia kwake katika uhai wake, basi wangelisema: "Tutatafutaje *tawassul* kwa kupitia kwa 'Abbâs na Yazîd ibn al-Aswad na wengine mfano wao, na kuwacha kufanya *tawassul* kwa kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambaye ndiye mbora wa viumbe wote na njia bora iliyo kubwa zaidi ya *ku-tawassal* kwa Allâh?" Kwa vile hapakuwa na hata mmoja wao aliyesema hivyo, na sisi twajua yakwamba katika uhai wake walikuwa wakitafuta *tawassul* kwa kutumia *du'â'* zake kwa niyaba ya watu, na kwamba baada ya kufa kwake wakatafuta *tawassul* kwa kupitia njia ya *du'â'* za watu wengine, kwahivyo twajua yakwamba walichofaradhishiwa ilikuwa ni kutafuta *tawassul* kwa kutumia *du'â'* ya mtu, na wala sio kwa kutumia dhati yake."

Zaidi ya hayo kuna ibara fulani kwenye kisa ambayo lau mtu muerevu mwenye busara anayejua kuhusu fadhla za Maswahaba angezingatia

ataikuta kuwa ni dalili ya ziyada katika udhaifu na makosa ya kisa chenyewe. Ni kauli ambayo Khalifa muongofu 'Uthmân (رضي الله عنه) hakuwa na mazoweya ya kuyatafakari mahitaji ya yule mtu na akiyapuuza! Sasa haya yataafikiana vipi na yaliyoswihi kupokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba Malaika walikuwa wakimuonea 'Uthmân haya, na pamoja na yote yaliyo maarufu kumuhusu yeye (رضي الله عنه), kisha akiwahudumikia watu kwa ukarimu, wema na upole? Yote haya yanatusababisha sisi kuzidi kuwa na shaka iwapo kisa hiki kilitokea kweli, kwani kinaonyesha dhulma ambayo iliyo kinyume kabisa na tabia zake (رضي الله عنه).

Tanbihi: Baada ya kumaliza kuandika yaliyo na umuhimu hapa, kwa bahati tulikuta kitabu kiitwacho: *at-Tawassul Ilâ Haqîqatit-Tawassul* cha Sheikh Muhammad Nasîbur-Rifâ'î, aliyeongezea *cheo* kwenye jina lake: "Muasisi na Mtumishi wa ad-Da'wah as-Salafiyyah..." Kwahivyo hayo yanahitaji amana za ki-'ilmu na ikhlâs, na uwajibikaji wa kutoa naswiha za dhati na umuhimu wa kusema ukweli unahitaji yakwamba tuibainishe hukmu ya Allâh waziwazi kama tunavyoifahamu, na kufafanua tunayoshikilia kama dini mbele ya Allâh (تعالى) kuhusiana na cheo hicho. Inatupasa kubainisha yakwamba *Salafi Da'wah* ndio ulinganizi wa kweli wa Uislamu, kama jinsi ambavyo Allâh (تعالى) alivyoiteremsha juu ya wa mwisho katika Mitume Wake na Manabii, Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Kwahivyo Allâh peke Yake (سبحانه) ndiye Muasisi na Muanzilishi, na hapana mwana-adamu yoyote bila ya kujali yoyote atakaekuwa awezae kudai kuwa ati yeye ni muasisi au muanzilishi wake. Hata Mtume aliye Mtukufu wao (صلى الله عليه وسلم), jukumu lake lilikuwa ni kukubali kwa uaminifu na kurejesha, na kufikiliza kikamilifu kwa uswahîh, na haikuruhusiwa kwake kufanya mabadiliko yoyote kwenye jambo lolote ambalo Allâh (تعالى) alilolifaradhisha na kuliteremsha. Kwahivyo, kwa mtu yoyote bila ya kujali utukufu wake, kudai kuvumbua *da'wah* hii iliyobarikiwa itokayo kwa Mungu kwa hakika atakuwa amefanya makosa makubwa sana na jambo la hatari, yaani iwapo sio suala linalohusiana na *Shirk Kubwa*, na twaomba hifadha kutoka kwa Allâh (تعالى). Kwahivyo hatujui sisi jambo hili jinsi lilivyotumbukizwa na mtu aliyeishi kwa muda mrefu

pamoja na ndugu zake katika Mji wa Aleppo na kwengineko nchini Syria kwenye *Salafi Da'wah*, iliyo na kama mojawapo ya sifa zake zilizo bainifu iliyo makhsusi zaidi na inayotoa umuhimu mkubwa katika kupiga vita *Shirk* na 'ibada za Masanamu kwa kauli, licha ya *Shirk* katika mas'ala ya 'aqîdah. Kisha ndugu huyu akajitenga kando na upotofu huu wa hatari ulikuwa ni mmojawapo wa matokeo ya kujitenga na mwili mmoja ulioshikamana wa Waumini juu ya haki. Twamuomba Allâh (تعالى) atuongoze sisi na yeye, na atuepushe na makosa, mitihani na mapendelewa ya nyoyo yenye kuwapoteza watu. Pengine mtu huwenda akatafuta udhuru kwa huyo mtunzi kwa kusema yakwamba aliyomaanisha kwa kujipa cheo hicho ni kwamba yeye alikuwa ni mwenye kuihuisha *Salafi Da'wah*, na wala sio kwamba yeye ndiye aliyekuwa ni muanzilishi na muasisi wa mafunzo yake, na kwamba kwa hakika paliwahi kuwepo na wahuishaji wa dini kwenye zama zilizotangulia na hizi zama zetu, na pengine mtunzi alidhania yakwamba naye alikuwa ni miongoni mwao. Naam, ndio kwa hakika palikuwepo na wahuishaji kwenye ulinganizi wa Uislamu wa kweli kwa zama za kufuatana, lakini ni tafauti iliyoje baina ya mtunzi huyu na hao wahuishaji, na ingelikuwa inamtosha yeye kuwa ni mfuasi wa mmoja wao. Hata kama tungelikuwa ni wenye kukubali kwa kujiweka kwake miongoni mwao, basi vilevile ingelikuwa ni muhimu kwake kunukuu viwango vya daraja ya kujidai kwake kama mwenye kuhuisha, kama vile kujipimia hilo kwenye nchi fulani au sehemu. Lakini hata hivyo matumizi yake ya cheo hicho bila ya mipaka yoyote katika kueleweka kwa upana wake mzima huleta hisiya kwa wasomaji yakwamba yeye ni muhuishaji wa Uislamu kwenye ulimwengu mzima tunaoishi wa ki-Islamu, na atawezaji kudai hivyo?

Kutokamana na adabu za kimsingi ambazo anatakiwa kuwa nazo mlinganizi wa Uislamu ni kuwa na tabia njema, na kujiepusha na kupenda majisifu, kujivuna na kujidai nafsi yako. Mambo haya ni maradhi mabaya yanayomtoa mtu mwenye kuyang'ang'aniya na kuyapapiya katika umahiri wa kusambaza *da'wah*. Yanampokonya silaha zake zenye athari kubwa dhidi ya maadui zake na kusababisha vitendo vyake kubatilika na kukosa malipo, twamuomba Allâh atulinde na atuongoze.

Kwa haraka haraka tukakichunguza kitabu kilichotajwa hapo juu na tukaona makosa ndani yake, ambayo baadhi yake tutayaashiriya

panapofaa. Miongoni mwayo ni kwamba amesema katika Uk.237 alipokuwa akizungumzia kuhusu silsila ya riwaya ya kisa kilichotangulia: “Katika silsila ya riwaya ya kisa hiki kuna mtu ambaye jina lake ni Rawh ibn Swalâh na ambaye aliyetangazwa kuwa ni *dha’îf* na kundi kubwa na Ibn ‘Adiyy, na akasema Ibn Yûnus: Anapokea *ahâdîth dha’îf* zinazokwenda kinyume na yaliyo swahîh.” Haya ni makosa kwa ukamilifu na hatujui aliingiaje kwenye makosa hayo, kwani mtu huyu, Rawh ibn Swalâh, ndiye aliyesababisha kupatikana kwa udhaifu wa hadîth ya tatu ambayo itakayofuata.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

❖ **SHAKA YA TATU**

AHĀDÎTH DHA'ÎF KATIKA TAWASSUL

Wanaotafuta kuruhusu njia za uzushi za *tawassul* hutumia ahâdîth nyingi kuwa ni kama dalili, lakini pindi tunapowazingatia tunakuta yakwamba wanaangukia kwenye orodha mbili:

i. Zile ambazo zilizoswihi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) lakini zikawa hazionyeshi yale wanayoyadai watu hawa, wala kuunga mkono rai zao. Kwa mfano hadîth ya mtu-kipofu, na tayari tushazungumzia kuhusu orodha hii.

ii. Zile ambazo hazikuswihi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), baadhi yake zikionyesha dalili za malengo yake na nyenginezo zisizokuwa na dalili. Āhâdîth hizi zisizokuwa swahîh ni nyingi na sisi tutatosheka kwa kuzitaja zile zilizo maarufu. Nazo ni:

Hadîth Ya Kwanza: Kutoka kwa Abû Sa'îd al-Khudhrî', ikinukuliwa kama maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Yoyote atakaetoka nyumbani kwake kwenda kuswali na akasema: 'Yâ Allâh! Nakuomba kwa haki za wenye kukuomba Wewe, na nakuomba kwa haki ya mwendo wangu huu, kwani mimi sitoki kwa shari wala kwa majivuno...', basi Allâh humgeuzia yeye Uso Wake." Imepokewa na Ahmad (3/21) na matamshi ni yake, na Ibn Mâjah, na inaweza kupatikana kwa marejeo kamili katika *Silsilatul-Ahâdîth adh-Dha'îfah* (no.24) na silisili ya riwaya yake ni dhaifu kwani imepokewa kwa kumpitia 'Atiyyah al-'Awfî kutoka kwa Abû Sa'îd al-Khudhrî'. 'Atiyyah ni mtu dhaifu kama alivyotangazwa na an-Nawawi katika *al-Adhkâr*, Ibn Taymiyyah katika *al-Qâ'idatul Jaliyyah* na adh-Dhahabî katika *al-Mîzân;* kwa hakika katika *adh-Dhu'afâ'* (88/1) alisema: "Wamekubaliana juu ya udhaifu wake." Vilevile na Al-Hâfidh al-Haithamî kwenye mahali chungu nzima katika *Majma'uz-Zawâ'id* kutoka kwao (5/236). Vilevile ametajwa na Abû Bakr ibn al-Muhibb al-Ba'labakî katika *adh-Dhu'afâ' wal-Matrûkîn*, na vilevile na al-Busayrî kama itakavyofuata. Vilevile al-Hâfidh Ibn Hajr amesema kumuhusu yeye: "Ni mkweli lakini anafanya makosa mingi sana; alikuwa ni *Shi'i mudallis.*" Kwahivyo amebainisha udhaifu wa mpokezi wake na hayo yametokana na mambo mawili: (i) Udhaifu wa fahamu zake kama

ulivyojitokeza kwenye kauli yake: “Anafanya makosa mingi sana.” Hii ni kama kauli yake kumuhusu yeye katika *Tabaqâtul-Mudallisîn:* “Ni dhaifu katika hadîth.” Hata iliyo wazi zaidi ni kauli yake kumuhusu yeye katika *Talkhîsul-Habîr* (Uk.241, Chapa ya India) alipokuwa akiijadili hadîth nyengine: “Inae ndani yake ‘Atiyyah ibn Sa’îd al-‘Awfî naye ni dhaif.” (ii)*Tadlîs* yake. Lakini hata hivyo, al-Hâfidh angeliifafanua sampuli ya *tadlîs* ambayo aliyoifanya, kwani *tadlîs* kwa mtazamo wa wanavyuoni wa hadîth una sampuli nyingi, zilizomashuhuri mno miongoni mwazo ni:

a) Yakwamba mpokezi anasimulia riwaya kutoka kwa mtu aliyeonana naye haliyakuwa kwa hakika hakuisikiya yeye mwenyewe riwaya hiyo kutoka kwake, au kwamba anasimulia kitu kutoka kwa mtu wa zama zake ambaye kwa hakika hakuonana naye, akileta hisiya yakwamba alisikiya kutoka kwake. Kwa mfano, kwa kusema ‘Kutoka kwa fulani na fulani’ au ‘fulani na fulani alisema.’

b) Yakwamba msimulizi anamwita Sheikh wake kwa jina lisilokuwa maarufu na cheo, lililo tafauti na jina ambalo kwa kawaida anajulikana nalo kwa ajili ya kuficha kutambulika ukweli wake. Wanavyuoni wamesema waziwazi yakwamba hili ni jambo lililokatazwa ikiwa Sheikh wake alikuwa si mpokezi wa kutegemewa, na anafanya hivi kwa ajili ya kuficha kutambulika kwake, au kuleta hisiya yakwamba yeye alikuwa ni mpokezi tafauti mwenye kutegemeka mwenye jina hilohilo au cheo[98]. Hii inajulikana kama *Tadlîs ash-Shuyûkh*.

Tadlîs ya ‘Atiyyah ilikuwa ni katika hizi sampuli zilizokatazwa kama nilivyoyaeleza katika kitabu changu: *Silsilatul-Ahâdîthudh-Dha’îfah* (no.24).

Kwahivyo katika kumalizia tunasema yakwamba ‘Atiyyah alikuwa akipokea kutoka kwa Abû Sa’îd al-Khudhrî’ (رضي الله عنه), kisha alipokufa alikuwa akikaa na mmojawapo wa watu warongo wakubwa ambaye akijulikana sana kwa kudanganya katika hadîth, ambaye ni *al-Kalbî.* Kisha ‘Atiyyah alikuwa akipokea kutoka kwake, lakini pindi anapofanya hivyo alikuwa akimwita kama ‘Abû Sa’îd’ ili aonyeshe

[98] *Ikhtisâr ‘Ulûmil Hadîth* cha Ibn Kathîr (Uk.59) na ufafanuzi wa Ahmad Shâkir.

hisiya kwa wenye kusikiliza yakwamba amezisikiya riwaya hizi kutoka kwa Abû Sa'îd al-Khudhrî'! Hili peke yake kwangu mimi litatosha kuharibu uaminifu wa 'Atiyyah, sasa jee iwapo tunapokuwa katika nyongeza ndani yake fahamu zake dhaifu! Kwahivyo mimi ningeliridhika kwa *al-Hâfidh* kubainisha uhakika yakwamba hatia iliyomkabili 'Atiyyah ilikuwa ni sampuli hii mbaya ya *tadlîs*, hata kama angalau ni kwa kuashiriya kama afanyavyo katika *Tabaqâtul-Mudallisîn* kwa kauli yake: "Ni mashuhuri sana kwa *tadlîs* mbaya," kama ilivyotangulia. Ni kana kwamba al-Hâfidh alisahau au alikosea, au jambo jengine, kama ilivyo kwa wana-adamu hukabiliwa na kufanya makosa wakati mwengine, kwani alisema kuhusu hadîth hii yakwamba katika riwaya moja 'Atiyyah amesema: "Abû Sa'îd amenisimulia mimi," na yeye mwenyewe akasema kuhusu haya: "Kwahivyo kwa kuyapitia haya twajua yakwamba tumesalimika kutokamana na '*tadlîs* ya 'Atiyyah," kama Ibn 'Alân alivyopokea kutoka kwake, na baadhi ya watunzi wa siku hizi walikuwa wakimfuata yeye ki-Upofu katika jambo hilo. Mimi nasema: Tangazo hili peke yake ambalo alilosikiya kutoka kwake litatumika tu, iwapo *tadlîs* yake ingelikuwa ni ya sampuli ya kwanza, lakini *tadlîs* ya 'Atiyyah ni ya sampuli ya pili na ambayo ndiyo mbaya zaidi na haitoweza kutibika kwa kauli hii kwani yeye bado anaendelea kusema "Abû Sa'îd amenisimulia mimi" ambayo ndiyo sampuli mbaya haswa ya *tadlîs* ambayo anayojulikaniwa kwayo.[99]

[99] Kutokamana na haya itabainika kwa wasomaji watukufu yakwamba wale ambao bado humfuata al-Hâfidh ki-Upofu juu ya kauli hii baada ya ufafanuzi wetu wa sampuli za *tadlîs* ambazo 'Atiyyah anatuhumiwa nazo, basi mtu huyu ni mwenye kupendelea na kufuata matamaniwa. Hii ndiyo hali kwa mwenye kunukuu hizi kauli ya al-Hâfidh, akiyatumia kama majibu kwa tangazo langu la udhaifu wa hadîth. Mimi nasema yakwamba yeye anapendelea kwani najua yakwamba yeye anaelewa kuhusu sampuli ya *tadlîs* iliyotumika hapa na ambayo ninayoizungumzia mimi; hii ni kwa sababu yeye anayajibia maneno yangu haya kuhusu hadîth hii. Lakini hata hivyo, anajibandikizia ujinga wa uhakika huo na hasemi hata neno moja katika jawabu lake. Bali anajidai yakwamba *tadlîs* hiyo ilikuwa ni ya sampuli ya kwanza ambayo inayoweza kuondolewa kwa riwaya ambapo inapobainishwa waziwazi yakwamba mpokezi ameisikiya moja kwa moja kutoka kwa Sheikh wake. Jee wasomaji wanaweza kunipa udhuru iwapo nitasema: Jee, watu aina hiyo hawastahiki wao wenyewe kuorodheshwa miongoni mwa wale walio na hatia ya *tadlîs* kama 'Atiyyah?!

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kwahivyo kutokamana na yaliyotangulia itabainika yakwamba'Atiyyah ni mtu dhaifu kutokana na hifdhi yake mbaya na *tadlîs* yake chafu, kwahivyo hadîth hii yake ni dhaifu. Ama kuhusiana na tangazo la al-Hâfidh yakwamba ni *hasan*, jambo ambalo lililowadanganya baadhi ya watu wasiokuwa na 'ilmu, basi imejengewa juu ya kughafilika. Kwahivyo tahadhari na usiwe ni miongoni mwa wale wasiojali. Katika hadîth kuna udhaifu mwengine ambao niliouzungumzia kwenye kitabu nilichotangulia kukitaja hapo awali, kwahivyo haina haja ya kuyarudia tena kwani yoyote apendaye anaweza kuyarejelea hayo.

Ama kuhusu ufahamu wa baadhi ya watu leo yakwamba kauli ya al-Hâfidh ibn Hajr katika *at-Taqrîb* inatilia nguvu kunako tangazo la kutegemewa kwa 'Atiyyah, basi hili ni jambo lisilokuwa la sawa kabisa. Mimi vilevile nimemuuliza Sheikh Ahmad ibn as-Siddîq nilipo onana naye katika Maktaba ya adh-Dhâhiriyyah Mjini Damascus kuhusu ufahamu huu na hata yeye pia akaona ni jambo la kushangaza mno. Kwani pindi makosa ya mpokezi yanapokuwa ni mengi basi kutegemewa kwake hubomoka, kinyume cha yule ambaye makosa yake ni machache. Wa kwanza katika wawili hawa ni *dha'îf* haliyakuwa wa pili ni *hasan* katika hadîth. Hii ndiyo sababu al-Hâfidh katika *Sharhun-Nukhbah* akasema, yakwamba yule ambaye makosa yake ni mengi ni mwenzake yule ambaye hifdhi yake ni dhaifu, na yeye akazitangaza ahâdîth za wote wawili kukataliwa, kwahivyo rejea nyuma huko pamoja na kiambatisho cha chini cha Sheikh 'Alî al-Qârî. (Uk.121 na 130).

Watu hawa wamedanganyika kwa waliyoyapokea kutoka kwa al-Hâfidh yakwamba alisema katika*Takhrîjul-Adhkâr:* "Udhaifu wa 'Atiyyah umetokamana na yeye kuwa ni Mshi'ah, na kutokamana na uhakika yakuwa imesemekana yakwamba alifanya *tadlîs;* mbali na hayo ni kwamba yeye anakubalika ." Kwahivyo watu hawa, kutokamana na uchache wa 'ilmu au ukosefu wao wa 'ilmu, hawana ujasiri wa kueleza na kufafanua rai zao yakwamba kwa hakika wanavyuoni hukosea. Bali wao hunukuu maneno yao kana kwamba wao wamehifadhiwa kutokamana na makosa au kuteleza kivyovyote, hususan iwapo maneno yao yataafikiyana na mapendelewa ya nafsi zao, mfano kama huo ndiyo hali na nukuu hii. Kwani imebainika hapa yakwamba maneno haya yanakwenda kinyume na kauli ya al-Hâfidh katika at-*Taqrîb* ambapo anaonyesha yakwamba 'Atiyyah ni mtu dhaifu kutokamana na hali mbili:

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

i. Kuwa kwake *Mshi'ah*, jambo ambalo kwa kawaida si sababu ya udhaifu kulingana na mtizamo wa sawa.

ii. *Tadlîs* ambayo ni udhaifu uwezao kuondolewa kama itakavyofuata. Lakini hatahivyo alionyesha kuikosesha nguvu sababu hii kwa kusema: "Imesemekana..." Haliyakuwa katika at-*Taqrîb* alidhihirisha waziwazi yakwamba yeye ni *mudallis*, kama ambavyo alivyomtangaza yeye kuwa ni *Mshi'ah*. Kwahivyo, al-Hâfidh, yeye mwenyewe vilevile amemzungumza katika *Tabaqâtul-Mudallisîn* (Uk.18): "*Tâbi'î* aliye maarufu, dhaifu katika fahamu zake, na ni mashuhuri sana kwa *Tadlîs* mbaya zaidi," na akamtaja katika daraja ya nne na akamsema kumuhusu: "Wale wenye kumuhusu, ambao miongoni mwao waliokubaliana basi hakuna katika hadîth zao inayokubaliwa mpaka waeleze waziwazi yakwamba waliisikiya moja kwa moja kutoka kwake. Hii imetokamana na mzunguko wao katika kupokea kwa njia ya *tadlîs* kutoka kwa wapokezi madhaifu na wasiojulikana, kama vile Baqiyyah ibn al-Walîd." Ameyataja haya katika utangulizi wake. Kwahivyo zote mbili hizi ni kauli za wazi kutoka kwa al-Hâfidh mwenyewe zinazodhihirisha yakwamba alikosea kwenye matamshi ya suala linalozungumziwa alipotia shaka kuhusu juu ya hali ya 'Atiyyah kama *mudallis*. Hii ni njia moja ambayo iliyo na mgongano baina ya kauli hii na yaliyopatikana katika *at-Taqrîb*. Kisha njia nyengine ya zaidi iliyo na mgongano ni ile ya kwenye matamshi ya suala linalozungumziwa aliposhindwa kumbainisha kwa lililo sababu nyengine ya udhaifu wake, kama ilivyowahi kutangulia kutoka kwake katika nukuu ya kutoka kwenye *Sharhun-Nukhbah*, na hiyo ndiyo kauli yake katika *at-Taqrîb*: "Anafanya makosa mengi." Haya yote yanatuonyesha sisi yakwamba al-Hâfidh (رحمه الله تعالى) hakusaidika na kuhifadhi kwake kwenye tukio la kutoa maoni yake juu ya hadîth hii. Kwahivyo akatumbukia ndani ya kasoro iliyoshuhudiliwa kwa kauli zake katika vitabu vyake vilivyo na haki zaidi ya kutegemewa. Hii ni kwa sababu kwenye vitabu hivyo alinukuu waliyoyasema moja kwa moja kutoka kwenye asili na mukhtasari, kinyume cha alivyofanya katika *Takhrîjul-Adhkâr*.

iii. Kutokana na udhaifu wa al-'Awfî, idadi ya wanavyuoni waliitangaza hadîth hii kuwa ni dha'îf. Wakiwemo miongoni mwao al-

Hâfidh al-Mundhirî katika *at-Targhîb*[100], an-Nawawi na Sheikhul-Islâm Ibn Taymiyyah katika *al-Qâ'idatul-Jâliyyah* na kama hivyo al-Bûsayrî alivyosema katika *al-Misbâhuz-Zujâjah* (2/52): "Silsila hii ya riwaya imekusanya mfululizo wa wapokezi walio madhaifu: 'Atiyyah na Fudhayl ibn marzûq na al-Fadhl ibn al-Muwaffaq, wote hao ni madhaifu." Vilevile Siddîq Hasan Khân amesema katika *Nuzulul-Abrâr* (Uk.71), baada ya kuinukuu hadîth hii na hadîth ya Bilâl ifuatayo: "Silsila za riwaya ni dha'îf, kama zilivyobainishwa waziwazi na an-Nawawi katika *al-Adhkâr*."

Hadîth Ya Pili*:* Hadîth ya Bilâl iliyoashiriwa na Siddîq Hasan Khân ndiyo iliyonasibishwa kutoka kwake yakwamba alisema: "Pindi alipotoka Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) kuelekea kwenye swala alikuwa na mazoweya ya kusema: 'Kwa jina la Allâh, Namuamini Allâh, Najitegemeza kwa Allâh, hapana kitendo chochote wala nguvu zozote isipokuwa kwa (kupenda kwa) Allâh. Yâ Allâh! Kwa haki za wale wenye kukuomba Wewe, na kwa haki ya huku kutoka kwangu, kwani mimi sitoki kwa maovu, wala kwa majivuno...' hiyo *hadîth*. Imepokewa na Ibn as-Sunnî katika *al-'Uqaylî,* kutoka kwa Abû Salamah ibn 'Abdur-Rahmân, kutoka kwa Jâbir ibn 'Abdillâh, kutoka kwake. Silsila hii ya riwaya ni dhaifu sana na matatizo yake ni huyu al-Wâzi' [maana ya jina lake ni 'kujizuiya'] ambaye hakuwa na kujizuiya kokote kwenye kumzuiya asidanganye kama nilivyoyafafanua katika *Silsilatudh-Dha'îfah*. Kwahivyo amesema an-Nawawi katika *al-Adhkâr*: "Hadîth hiyo ni dha'îf. Mmojawapo wa wapokezi wake, al-Wâzi' ibn Nâfi' al-'Uqaylî ni mtu dha'îf kwa kuafikianwa, na ni dha'îf mno (*munkar*)." Kisha akaongezea al-Hâfidh alipoisherehesha hadîth yenyewe. "Hadîth hii ni dha'îf mno, ameinukuu ad-Dâraqutnî katika hali hii katika *al-Afrâd* na akasema: "al-Wâzi'ni peke yake katika kuisimulia hii na kwamba wamekubaliana juu ya udhaifu huu na kwamba alikuwa ni dha'îf mno." Kisha kwa hakika kauli yenyewe ni kali mno kuliko hayo; kwani

[100] Amesema (2/265): "Ameipokea Ibn Mâjah kwa silsila ya riwaya iliyokosolewa," na akaitangaza kuwa ni dhaifu mahali kwengine (1/130-131), kwa kuitanguliza kwa kauli: "(*Ruwiya*) – 'imewahi kupokewa' ..." ambayo aliyoashiriya kwayo yakwamba ni jambo lisiloweza kuinuliwa kwenye daraja ya *hasan*, kama alivyofafanua katika utangulizi wake.

Ibn Ma'în na an-Nasa'î wamesema: "Ametupiliwa mbali katika hadîth," na al-Hâkim akasema: "Anapokea hadîth za urongo."[101]

Hairuhusiwi kuitumia kama dalili, kama ilivyofanywa na Sheikh al-Kawtharî, Sheikh al-Ghumârî katika *Misbâhuz-Zujâjah* (Uk.56) na wazushi wengineo. Kisha juu ya uhakika yakwamba ahâdîth hizi mbili, zote ni dha'îf, na vilevile hazina kwa njia yoyote dalili hata chembe kwa kufanya *tawassul* kwa kutumia njia ya viumbe. Bali zote hizo mbili zinarejea kwenye mojawapo ya sampuli iliyoidhinishwa na sheriya iliyotangulia, nayo ni *tawassul* kwa Allâh (تعالى), kwa njia ya Sifa Zake. Hii ni kwa sababu zote mbili zinataja *tawassul* kwa kutumia njia ya wale wenye kuleta maombi kwa Allâh, na kwa haki za wale wenye kutembea kuelekea kwenye swala. Ni zipi haki za wale wenye kuleta maombi kwa Allâh? Hapana shaka yakwamba ni kuwa atawajibu maombi yao, na kujibu Kwake maombi ya waja wake wenye kumuabudu Yeye ni mojawapo ya sifa Zake (عزّ وجلّ). Vilevile haki ya Muislamu mwenye kutembea hadi Msikitini ni kwamba Allâh amsamehe na amuingize Peponi, na msamaha wa Allâh (تعالى), na rehma Zake, na kuwaingiza Kwake wale ambao wenye kumtwi'i Yeye kwenye Pepo Yake, hizi zote ni katika sifa Zake Yeye (تبارك وتعالى). Kwahivyo kutokamana na haya inajulikana yakwamba hadîth ambayo wazushi wanayoitumia kama dalili kwa uhakika ni dhidi yao, na ufahamu wake wa kisawasawa ulioelekea kwenye usawa

---

[101] Nimesema katika adh-Dha'îfah baada ya kuizungumzia hadîth hii ya Bilâl na hadîth iliyotangulia: "Kwahivyo kwa mukhtasari hadîth hiyo ni dha'îf kwa riwaya zote mbili na mojawapo ni dha'îf mno kuliko nyengine." Kwahivyo baadhi ya watunzi walijitia hamnazo kuhusiana na kauli hii na kisha wakanibandikizia lawama za urongo dhidi yangu na wakasema: "Kwahivyo ni wazi yakwamba hizo ni ahâdîth mbili tafauti katika silsila za riwaya zao, kuanzia mwanzo hadi mwisho sasa itakuwaje ni sawa kwake yeye kuzifanya hizi mbili kuwa ni hadîth moja na kupitisha hukmu moja juu yake, hii ni dalili ya daraja ya kuchanganyikiwa kwake." Mimi nasema: Muache msomaji azingatie, jee wao ni wakweli katika madai yao, na kisha wao hawanipi nami udhuru nikiwa nitaitaja hadîth yake (صلى الله عليه وسلم):

« مِنْ كَلاَمِ النُّبُوَّةِ الأَوْلى : إِذَا لَمْ تَسْتَحْيِ فأَصْنَعْ مَاشِئْتَ! »

"Miongoni mwa maneno ya ki-Utume: ukiwa huna haya basi fanya utakalo."

unausababisha kuwa ni dalili kwetu dhidi yao, na kila shukrani na sifa zinamstahiki Allâh kwa kutuongoza na kutupa kila lililo la sawa.

Hadeeth ya Tatu: Kutoka kwa Abû Umâmah aliyesema: “Mtume wa Allâh (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiomba du’â’ hii kila usiku na asubuhi: “Yâ Allâh! Wewe una haki zaidi kuliko kila anayetajwa, na una haki zaidi kuliko kila anayeabudiwa ... nakuomba Wewe kwa muangaza wa Uso Wako unaosababisha Mbingu na Ardhi kung’ara kwa muangaza mkubwa, na kwa kila haki iliyo Yako, na kwa haki za wenye kuomba kutoka Kwako ...” Amesema al-Haithumî katika *al-Majma’ uz-Zawâid* (10/117): “Ameipokea at-Twabarânî na ndani yake yumo Fadhâl ibn Jubayr, ambaye ni *dha’îf*, na udhaifu wake umeafikianwa.” Mimi nasema: “Bali ni dhaifu mno: Ibn Hibbân amemshutumu kwa kusema: “Ni Sheikh anayedai yakwamba amesikiya kutoka kwa Abû Umâmah. Anasimulia kutoka kwake mambo yasiyotoka kwenye ahâdîth zake.” Vilevile amesema: “Hairuhusiwi kumtumia kuwa ni dalili katika hali yoyote, yeye husimulia ahâdîth zisizokuwa na msingi wowote.” Ibn ‘Adiyy amesema katika *al-Kâmil* (2/13): “Ahâdîth zake zote ni mambo ambayo hayakuhifadhiwa.” Mimi nasema: Kwahivyo hadîth hiyo ni *dha’îf* mno na haiwezi kutumiwa kabisa kuwa ni dalili, kama ilivyofanywa na mtunzi wa *al-Misbâh* (Uk.56).

Hadeeth ya Nne: Kutoka kwa Anas Ibn Mâlik aliyesema: “Pindi Fâtimah bint Asad ibn Hâshim, mamake ‘Ali (رضي الله عنهما) alipokufa, alimwita Usâmah ibn Zayd, Abû Ayyûb al-Answârî, ‘Umar ibn al-Khattwâb na kijana mmoja mweusi aliyechimba kaburi... kisha walipomaliza, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaingia ndani na kumlaza chini kisha akasema: “Ni Allâh mwenye kutupa uhai na mauti, Naye ni wa milele asiyekufa, msamehe mamangu Fâtimah bint Asad, na umpe yeye hoja yake, na umpe makaazi yenye nafasi kwa haki ya mtume Wako, na mitume waliokuja kabla yangu, kwani kwa hakika Wewe ni Mwenye huruma kati ya wale wenye kuonyesha huruma...” Amesema al-Haithumî katika *al-Majma’ uz-Zawâid* (9/257): “Ameipokea at-Twabarânî katika *al-Kabîr* na *al-Awsat* na ndani yake yumo Rawh ibn as-Swalâh aliyetangazwa kuwa ni mtegemewa na ibn Hibbân na al-Hâkim, lakini ni *dha’îf* kwa kiyasi fulani. Kisha wapokezi wake waiobaki ni wale wa kwenye swahîh.” Mimi nasema: “Kwa njia ya at-Twabarânî imepokewa na Abû Nu’aym katika *Hilyatul-Awliyâ’* (3/121) na silsila ya riwaya yao ni *dha’îf*, kwani huyu Rawh ibn as-Swalâh

ambaye ni mmojawapo wa wapokezi wake alikuwa peke yake katika kuipokea, kama alivyosema Abû Nu'aym, yeye mwenyewe. Basi Rawh ametangazwa kuwa ni *dha'îf* na Ibn 'Adiyy, na akasema Ibn Yûnus: "Udhaifu na mambo ya kukemewa yamepokewa kutoka kwake." Amesema ad-Dâraqutnî: "Huyu ni mtu *dha'îf* katika hadîth." Amesema Ibn Mâkûla: "Wanamtangaza kuwa ni *dha'îf*." Amesema Ibn 'Adiyy baada ya kuzinukuu hadîth zake mbili: "Huyu anapokea ahâdîth nyingi na baadhi yake zinastahiki kukemewa." Kwahivyo wamekubali juu ya udhaifu wake, kwahivyo hadîth yake ni *dha'îf* (*munkar*) kwani alikuwa yu-peke yake katika kuipokea. Kuna baadhi ya watu wanaojaribu kuipa nguvu hadîth hii kwa kujitegemeza juu ya matangazo ya Ibn Hibbân na al-Hâkim yakwamba Rawh ni mtu wa kutegemewa. Lakini hata hivyo, hili halitowafaidisha kutokana na yajulikanayo kuhusiana na ulaini wao katika kumtangaza mtegemewa. Kwahivyo kauli hii yao pindi inapopingwa na kauli ya wanavyuoni wengine haibebi uzito wowote hata kama utangazaji wa udhaifu kutoka kwa wanavyuoni wengine haukufafanuliwa, sasa huwaje hali iwapo sababu ya udhaifu imebainishwa kama jinsi hali ilivyo hapa? Vilevile nimechambua kikamilifu kuhusu udhaifu wa hadîth hii katika *adh-Dha'ifah* (no.23) na kwahivyo sitoirudia tena hapa. Mahasimu (wapinzani) wetu tuliowaashiriya wameyanukuu mambo ambayo yasiyoweza kusababisha chochote isipokuwa kicheko tu, kwa kusema: "Sheikh Nâsir ameihukumu kuwa ni *dha'îf*, kwahivyo sisi twauliza yakwamba atwambie ni nani katika wanavyuoni wa hadîth aliyeitangaza hadîth hii kuwa ni *dha'îf*." Sisi tumewanukuu wale ambao waliomtangaza mpokezi wake, Rawh ibn as-Swalâh, kuwa ni mtu *dha'îf*, naye alikuwa yu-peke katika kuipokea. Hii inamaanisha moja kwa moja udhaifu wa hadîth isipokuwa apatikane mtu mwenye kuipokea pamoja naye, na Abû Nu'aym amekataa hilo yakwamba kuna yoyote mwenye kuiunga mkono riwaya yake, isipokuwa riwaya yake nyengine ipatikane, na hali si hivyo! Ndio tunasema: "Hata kama tunakubali yakuwa ni *dha'îf*, basi ni *dha'îf* kwa uchache ambako hakutozuiya kitendo juu yake, kwani kwa vile ni hali ya kuitendea kazi hadîth ambayo udhaifu wake sio mbaya sana katika mambo yanayohusiana na faraja na maonyo, mambo ambayo yanayoruhusiwa na wanavyuoni wa hadîth na fiqhi." Mimi nasema: Hakuna faraja katika hadîth hii, wala haielezi kuhusu fadhla kwa kitendo ambacho tayari kilichothibitishwa kuamrishwa katika sheriya. Bali inazungumzia kuhusu jambo linalowezekana kuruhusiwa au

kutoruhusiwa, kwahivyo imetumiwa kuthibitisha hukmu ya ki-sheriya, lau kama ingelikuwa ni swahîh. Zaidi ya hayo ni kwamba watu hawa wanainukuu kama dalili ya sampuli hii ya *tawassul* ambayo kwayo kuna ikhtilafu. Kwahivyo utakapoikubali udhaifu wake, basi haitoruhusiwa kuitumia kuwa ni dalili. Mimi sidhani mtu yoyote muerevu atakubali yakwamba linafungamana na faraja na maonyo tu. Bali hii ndiyo njia ya wale wenye kukimbia mbali na kujisalimisha na haki, wao husema mambo yasiyosemwa na mtu muerevu.

Hadeeth ya Tano: Kutoka kwa Umayyah ibn 'Abdillâh ibn Khâlid ibn Usayd, aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiomba ushindi kwa njia ya *Muhâjir* wanyonge."

Kwahivyo Mahasimu wetu hudhani yakwamba hadîth hii inaonyesha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akimuomba Allâh (تعالى), ampe ushindi kutokana na wanyonge na mafukara wanaotokamana na *Muhâjir*, na jambo hili, kama wanavyodai, lilikuwa ni kama sampuli hii ya *tawassul* ambayo kwayo kuna ikhtilafu. Kwahivyo jawabu ya suala hili linatokamana na pande mbili:

i. Hadîth hiyo ni *dha'îf*. Imepokewa na at-Twabarâni katika *al-Kabîr* (1/81/2): Muhammad ibn Is-hâq ibn Râhoyah ametusimulia sisi: Babangu amenisimulia: 'Isâ ibn Yûnus ametusimulia: Babangu amenisimulia: kutoka kwa babake[102]: kutoka kwa Umayyah kwa hiyo." Vilevile: "'Abdullâh ibn Muhammad ibn 'Abdil-Azîz al-Baghawî ametusimulia: 'Ubaydullâh ibn 'Umar al-Qawârîrî ametusimulia: Yahya ibn Sa'îd ametusimulia: kutoka kwa Sufyân: kutoka kwa Abû Is-hâq: kutoka kwa Umayyah ibn Khâlid kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa matamshi: "... alikuwa akipigana na kutafuta nusra kwa njia ya Waislamu wanyonge." Mimi nasema: Riwaya yake imetulia tu juu ya Umayyah, na haikuthubutu yakwamba yeye alikuwa ni Swahaba, kwahivyo hadîth hiyo ni *mursal*[103] *na dha'îf*. Ibn 'Abdul-Barr amesema katika *al-Isti'âb* (1/38): "Si sawa kwangu yakwamba alikuwa ni Swahaba, na hadîth ni *mursal*." Vilevile amesema al-Hâfidh katika *al-Isâbah* (1/133): "Hakuwa ni Swahaba na hakusikiya kitu chochote

[102] Aliyekuwa ni Abû Is-hâq as-Sabî'î

[103] *Yaani;* Kuna kiungo kilichokosekana baina ya mpokezi wa mwisho na Mtume (صلى الله عليه وسلم)

kutoka kwake (صلى الله عليه وسلم) ili apokee." Mimi nasema: Vilevile inayo ila nyengine ambayo ni kwamba Abû Is-hâq alichanganyikiwa katika maisha yake ya baadae na pia sifa yake ya kuwa *mudallis* na kupokea kwa njia ya *'an'anah*[104]. Lakini hatahivyo Sufyân alisikiya riwaya kutoka kwake kabla hajachanganyikiwa, kwahivyo hilo linawacha udhaifu mwengine tu ambao ni kupokea kwake kwa njia ya *'an'anah'*. Kwahivyo imethibitishwa yakwamba hadîth ni *dha'îf* na haiwezi kutumiwa katika kuthibitisha dalili. Hilo ni jawabu la kwanza.

ii. Hata kama lau hadîth hiyo ingelikuwa ni swahîh, basi haingeliashiriya chochote isipokuwa yaliyoashiriwa na hadîth ya 'Umar na hadîth ya mtu-kipofu, ambayo ni *tawassul* kwa njia ya *du'â'* ya watu wema. Amesema al-Manâwî katika *Faydhul-Qadîr*: "Alikuwa akitaka njia za usaidizi: *yaani;* alikuwa akitaka msaada kwenye vita, kama ilivyo katika kauli ya Allâh (تعالى);

إِن تَسْتَفْتِحُواْ فَقَدْ جَآءَكُمُ ٱلْفَتْحُ ١٩

"Kama (nyinyi Maqureshi) mnataka hukumu (ya kupambanua baina ya haki na batili) basi hukumu imekwisha kufikieni."[105]

Ameyataja az-Zamakhsharî, 'alitafuta ushindi kwa njia ya Waislamu wanyonge,' *maana yake*: kwa njia ya *du'â'* za wanyonge walio mafukara."

Ufafanuzi huu vilevile umetokea kwenye hadîth yake (صلى الله عليه وسلم), iliyopokewa na an-Nasâ'î (2/15) kwa matamshi:

«إِنَّمَا يَنْصُرُ اللَّهُ هَذِهِ الْأُمَّةَ بِضَعِيفِهَا، بِدَعْوَتِهِمْ وَصَلَاتِهِمْ وَإِخْلَاصِهِمْ»

"Kwa hakika Allâh huleta nusra Yake kwa Ummah huu kutokana na wanyonge wao, kwa kupitia kwenye du'â' zao, swala zao na ikhlâs zao."

[104] Kusema: 'kutoka kwa fulani na fulani' na kutobainisha wazi iwapo aliyasikiya moja kwa moja kutoka kwake au laa.
[105] Sûrat al-Anfâl (8):19

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Silsila ya riwaya yake ni swahîh, na msingi wake unapatikana katika *swahîhul-Bukhâri* [tafsiri 4/94/no.145]. Kwahivyo hadîth inaonyesha yakwamba kutafuta nusra kulifanywa kwa njia ya *du'â'* za watu wema, sio kwa njia ya dhati zao au jaha zao.

Hili limezidi kuthibitishwa kwa uhakika yakwamba hiyo hadîth kwa matamshi yaliyotangulia iliyopokewa na Qays ibn Rabî' ilikuwa: "Alikuwa akitafuta msaada kwenye vita na nusra..." Kwahivyo twajua yakwamba kutafuta kwake ushindi kwa njia ya watu wema ilikuwa ni kwa njia ya *du'â'* zao, Swala na Ikhlâs na vilevile kuhusiana na kutafuta kwake msaada kwenye vita. Kwahivyo hadîth hii, lau kama ingelikuwa ni swahîh, ni dalili nyengine ya sampuli ya kisheriya ya *tawassul*, na dalili dhidi ya sampuli ya tawassul ya uzushi, na kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh.

Hadeeth ya Sita: Kutoka kwa 'Umar ibn al-Khattwâb kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Pindi Âdam alipotumbukia kwenye madhambi alisema: 'Ewe Mola wangu! Nakuomba Wewe kwa haki ya Muhammad unisamehe.' Akasema: 'Ewe Âdam, na ulijuaje kumuhusu Muhammad haliyakuwa bado sijamuumba?' Akasema: "Ewe Mola wangu! pale uliponiumba mimi kwa Mkono Wako, na ukanipulizia mimi uhai, niliinua kichwa changu na nikaona imeandikwa juu ya nguzo za Kiti: 'Hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allâh, Muhammad ni mjumbe wa Allâh.' Kwahivyo mimi nilijua yakwamba hutoweza kuongezea baada ya Jina Lako jina la mwengine yoyote isipokuwa kipenzi zaidi cha viumbe Kwako." Basi akasema: 'Nimekusamehe wewe, na lau kama si kwa ajili ya Muhammad, basi Mimi nisingelikuumba wewe.'" Imepokewa na al-Hâkim katika *al-Mustadrak* (2/615) kwa njia ya Abul Hârith 'Abdullâh ibn Muslim al-Fihriyy: Ismâ'îl Ibn Maslamah ametusimulia sisi: 'Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam ametusimulia: kutoka kwa babake: kutoka kwa babu yake: kutoka kwa 'Umar, na akasema: isnâd swahîh na ni hadîth ya kwanza ya 'Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam ambayo niliyoitaja kwenye kitabu hiki." Adh-Dhahabî amemshutumu, akisema: "Mimi nasema: bali ni ya urongo (*mawdhû'*) na 'Abdur-Rahmân ni mtu dhaifu mno (*wâhin*), na ama kumuhusu huyu 'Abdullâh ibn Aslam al-Fihriyy, basi mimi sijui ni nani huyu." Mimi nasema: Kutokamana na kujitatiza mwenyewe kwa al-Hâkim katika *al-Mustadrak* ni kwamba anapokea hadîth nyengine ya huyu huyu 'Abdur-Rahmân (3/332) na

haitangazi kuwa ni swahîh, lakini badala yake alisema: “Masheikh wawili hawamkubali ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd kuwa ni uthibitisho!”

Ama kuhusu al-Fihriyy, adh-Dhahabî amemtaja katika *al-Mîzân* na akainukuu hadîth hii yake na kisha akasema: “Riwaya *bâtwil* isiyokuwa na msingi wowote.” Yamesemwa mfano wake na al-Hâfidh ibn Hajr katika *al-Lisân* (3/360) na akaongezea kwenye maneno yake kumuhusu al-Fihriyy: “Na siidhanii hali hiyo kuwa si ya kawaida yakwamba yeye ndiye huyo na ni mtu huyo-huyo aliyetajwa hivi punde, kwani yeye yuko kwenye daraja moja na zama hizo-hizo.” Mimi nasema: Muandishi aliyemzungumza kabla yake alikuwa ni ‘Abdullâh ibn Muslim ibn Rushayd, ambaye al-Hâfidh aliyemzungumza yakuwa: “Ibn Hibbân amemtaja, ametuhumiwa kwa kuzua *ahâdîth*. Alikuwa akizua riwaya ambazo alizokuwa akizinasibisha kwa Layth, Mâlik na Ibn Lahî’ah. Hairuhusiwi kuziandika ahâdîth zake. Yeye ndiye aliyepokea stakabadhi ya hadîth kutoka kwa Ibn Lahî’ah, na inaonekana kuwa ni jambo lililozuliwa kwa makusudi.”

Hadîth hiyo vilevile imepokewa na at-Twabarânî katika *Majmû’ as-Swaghîr* (Uk.207): “Muhammad Ibn Dâwûd ibn Aslam as-Sadafî’ al-Misrî alitusimulia: Ahmad ibn Sa’îd al-Madanî al-Fihriyy alitusimulia: ‘Abdullâh ibn Ismâ’îl al-Madanî alitusimulia: kutoka kwa ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam kwa hiyo.” Silsila hii ya riwaya ina giza kwani wapokezi wote kabla ya ‘Abdur-Rahmân hawajulikani na hili pia ni jambo lililoashiriwa na al-Hâfidh al-Haithamî katika *Majma’ az-Zawâ’id* (8/253) ambapo aliposema: “Imepokewa na at-Twabarânî katika *al-Awsat* na *as-Swaghîr* na ndani yake wakiwemo wapokezi nisiowajua.” Mimi nasema: Hili ni tangazo la udhaifu lenye kasoro kwani linaleta hisiya kwa wale wasiokuwa na ‘ilmu yakwamba haina wapokezi wowote wanaojulikana kwa udhaifu wao. Hali sio kama hivyo kwani riwaya zake zinamtegemea huyo ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam, na al-Baihaqî akasema: “Yeye peke yake ndiye aliyeipokea,” na ametuhumiwa kwa kuzua, ambamo alipotuhumiwa na al-Hâkim mwenyewe. Kwahivyo wanavyuoni walimkanusha kwa kutangaza kwake kuhusu uswahîh wa hadîth hii na wakatangaza hilo kuwa lilikuwa ni kosa na utata. Kwahivyo, mrathi wa ‘ilmu ya Maswahaba, *tâbi’în* na *ma-Imâm* wanaofuatwa, Sheikhul Islâm Ibn

Taymiyyah (رحمه الله)[106] amesema katika *al-Qâ'idatul Jaliyyah* (Uk.89):

"Kupokea kwa al-Hâkim hadîth hii ni jambo lililomfanya alaumiwe kwani yeye mwenyewe alisema katika kitabu chake: *al-Madkhal ilâ Ma'rifatis-Swahîh minas-Saqîm:* "'Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam alipokea ahâdîth za uzushi kutoka kwa babake, na haitofichika kwa wajuzi kwenye ta'luma hii wenye kuzifanyia utafiti yakwamba yeye ndiye wa kulaumiwa kwa hizo.[107] Mimi nasema: "'Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam ni mtu dhaifu kwa muafaka wa wanavyuoni, na alifanya makosa mengi sana.[108] Alitangazwa kuwa ni *dha'îf* na Ahmad ibn Hanbal, Abû Zur'ah, an-Nasâ'î, ad-Dâraqutnî' na wengineo. Ibn Hibbân amesema: 'Alikuwa na mazoweya ya kuzichanganya riwaya bila ya kutambua, kiyasi cha kwamba alikuwa akifanya kwa mfululizo. Alikuwa akishikamanisha mambo yaliyokuwa ni *mursal* na maneno ya kunukuu kuwa ni ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo yaliyokuwa ni *mawqûf* (yaliyokoma kwenye daraja ya Swahaba), kwahivyo anastahili kutupiliwa mbali. Ama kuhusu uswahihishaji ambao al-Hâkim alioufanya kwenye hadîth hii na mfano wake, basi hili ni jambo ambalo kwalo wanavyuoni wa hadîth walimkosoa nalo, na wakatangaza yakwamba al-Hâkim hata huswahihisha riwaya ambazo ni za urongo na kuzua, yanajulikana haya kwa wale wenye ujuzi wa hadîth. Kwahivyo wanavyuoni wa hadîth hawategemei uswahihishaji wa al-Hâkim kivyake ."

Al-Hâkim yeye mwenyewe amemtaja 'Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam katika kitabu chake cha wapokezi madhaifu *adh-Dhu'afâ'*, kama kilivyopewa jina na mwanachuoni Ibn 'Abdul-Hâdî na mwishoni mwake akasema: "Wale wapokezi ambao niliowataja, ni wale ambao waliotangazwa kuwa ni *dha'îf* kwa sababu za kweli zilizodhihirika,

---

[106] Kama alivyosifiwa na mwanachuoni, Sheikh Muhibbuddîn al-Khatwîb kwenye utangulizi wake wa kitabu: *al-Qâ'idatul-Jaliyyah*.

[107] Maneno haya vilevile yamepokewa kutoka kwa al-Hâkim na Ibn Hibbân na al-Hâfidh Ibn 'Abdul-Hâdî katika *Sârimul-Munkî* (Uk.29), na al-Hâfidh Ibn Hajr katika *at-Tahdhîb*.

[108] Hii ni kauli ya wazi kutoka kwa Sheikhul-Islâm yakwamba, kifungu cha maneno: 'hufanya makosa mengi sana' ni matamshi ya lawama, si kila aina ya tangazo la mategemezi na kama inavyodhihirika hapana tafauti baina yake na matamshi: 'hufanya makosa mengi' ambayo ndiyo ibara iliyotumiwa na al-Hâfidh katika kumueleza 'Atiyyah al-'Awfî, kama ilivyotangulia hapo awali.

kwani utangazaji wa udhaifu huthibitishwa tu kutokana na dalili za wazi, na kwahivyo hawa ni watu ambao udhaifu wao mimi naweza kuueleza kwa uwazi kabisa kwa mtu yoyote atakaeniulizia habari hizo, kwa vile mimi siruhusu utangazaji wa udhaifu kwa kutegemea kufuata ki-upofu kauli ya mwengine. Kwahivyo ninayopendelea mimi kwa mwanafunzi wa ‘ilmu hii ni kwamba asiandike hata hadîth moja kutoka kwa wale watu ambao niliowaandika majina yao. Mwenye kusimulia hadîth zao hutumbukia chini ya maneno yake (صلى الله عليه وسلم):

« مَنْ حَدَّثَ بِحَدِيثٍ وَهُوَ يَرَى أَنَّهُ كَذِبٌ فَهُوَ أَحَدُ الْكَاذِبِينَ »

“Yoyote mwenye kusimulia hadîth akijua yakwamba ni ya urongo, basi yeye atakuwa ni mmojawapo wa warongo.”[109]

Yoyote mwenye kuzingatia kwa tahadhari maneno haya ya al-Hâkim na yale yaliyokuja kabla yake atajionea waziwazi yakwamba hadîth hii ya ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd ni ya uzushi hata kwa mtazamo wa al-Hâkim mwenyewe, na kwamba yoyote mwenye kuisimulia baada ya kujua hali yake atakuwa yeye mwenyewe ni mmojawapo wa warongo.

Misemo ya wenye kuzihifadhi hadîth:

Ibn Taymiyyah, adh-Dhahabî na Ibn Hajr al-‘Asqalânî wameafikiyana yakwamba hadîth hii haina msingi wowote. Wamekubalika kwenye hitimisho hilo kutoka kwa wanavyuoni wengine wenye kuhakikisha (*muhaqqiqîn*) kama vile al-Hâfidh Ibn ‘Abdul-Hâdî kama itakavyofuata. Kwahivyo hairuhusiwi kwa mwenye kumuamini Allâh na Siku ya Mwisho kuitangaza hadîth hiyo kuwa ni swahîh baada ya muafaka wa wanavyuoni hawa yakwamba ni *dha’îf*; na hairuhusiwi kuitangaza kuwa ni swahîh kutokana tu na kukubali ki-upofu kwa mojawapo ya kauli mbili za al-Hâkim, hususan pale katika kauli nyengine alipopendelea yakwamba mwanafunzi wa ki-‘ilmu hafai kuiandika hadîth hii ya ‘Abdur-Rahmân na kwamba kwa kufanya hivyo yeye atakuwa ni mmojawapo wa warongo, kama ilivyotangulia.

[109] Imepokewa na Muslim katika utangulizi wa Swahîh yake na Ibn Hibbân katika swahîh yake (1/27) kutoka katika hadîth ya Samurah Ibn Jundub, na Muslim kutoka katika hadîth ya al-Mughîrah Ibn Shu’bah, na akasema: “Ni hadîth mashuhuri.”

Tanbîh: Utakapoyajua haya, basi utaona yakwamba kauli za baadhi ya Mashekhe: “Hukumu ya Sheikh Nâsir juu ya hadîth hii yakwamba ni urongo na ya kuzuliwa ni kwamba yenyewe ni *bâtwil* kwa sababu imeegemezwa juu ya kauli ya uzushi ya adh-Dhahabî, hii kauli yenyewe ni *bâtwil* kwani adh-Dhahabî alikubaliwa kwenye hilo na *Mahuffâdh* mashuhuri wa hadîth ambao tuliowataja.” Kisha wakasema: “Msingi wa kauli ya adh-Dhahabî ulikuwa tu ni kwamba kuna mtu ambaye yasemekana – amekosolewa kwenye *Isnâd* ya al-Hâkim” Mimi nasema: “Hii vilevile ni *bâtwil* kwani huyo anayezungumzwa alikuwa ni ‘Abdullâh ibn Muslim al-Fihriyy ambaye adh-Dhahabî aliyesema kuwa hamjui, na hakumtuhumu, kama ilivyotangulia. Sidhani kuwa ukweli huu umefichika kutoka kwao, lakini wamejifanya hawaijui kwa hatima zao wenyewe, na hiyo ni kwa sababu kisha watakuwa ni wenye kuweza kufuatilia hilo kwa kusema: “Lakini hata hivyo, hadîth hiyo inayo silsila nyengine ya riwaya iliyopokewa na at-Twabarânî ambayo isiyokuwa na mtu huyu aliyetuhumiwa, na la zaidi liwezalo kusemwa dhidi yake ni kwamba ndani yake yumo mpokezi/wapokezi ambaye/ambao asiye julikana vizuri.” Mimi nasema: Bali wamo ndani yake wapokezi watatu wasiojulikana, na iwapo hawajui hayo, basi mbona wanageuka kutokamana na kuyafuata ki-upofu aliyoyasema al-Haithumî katika kauli yake: “Ndani yake muna wale ambao mimi siwajui,” kama ilivyotangulia, kwani wao ni kundi la kufuata ki-upofu mpaka kwenye maangamivu, lakini hapa wanapendelea kusema: “Ndani yake wamo wapokezi/wapokezi ambaye/ambao asiye julikana vizuri”?! Sababu ya haya ni kwamba kauli ya al-Haithumî ni kauli iliyo wazi kabisa tena ambayo idadi kubwa ya watu wasiojulikana, haliyakuwa kauli zao hazionyeshi hilo. Bali kauli zao zinaweza kumficha mpokezi mmoja asiyejulikana au wengi, kwahivyo kihakika ni jaribio la kuuficha ukweli kwa msomaji, na twamuomba Allâh atuhifadhi na asitufedheheshe. Kisha la zaidi ni kwamba wanasema baada ya yaliyotangulia: “Na vilevile ndani yake yumo ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd na yeye yumo kwenye kauli iliyopendelewa na al-Hâfidh Ibn Hajr – ni kwamba yeye alikuwa ni mmojawapo waliosemekana kuwa dha’îf, na hiyo ni mbaya iliyo na afadhali katika daraja za udhaifu.”

Mimi nasema: Hatahivyo, kauli ya sawa mbali na ile ya al-Hâfidh ni kwamba yeye ni dhaifu mno kuliko hivyo. Abû Nu’aym alisema kumuhusu yeye: “Yeye hupokea ahâdîth za kuzua kutoka kwa babake.” Al-Hâkim mwenyewe pia alisema jambo hilohilo kama

ilivyotangulia, na wote wawili, yeye na Abû Nu'aym ni miongoni mwa walio maarufu kwa kuwatangaza wapokezi kuwa ni wategemewa. Kwahivyo pindi wanapomtangaza mpokezi huyu kuwa ni *dha'îf*, basi huwa ni kwa sababu imebainika kwao yakwamba kihakika 'Abdur-Rahmân ni *dha'îf*. Kwahivyo wanavyuoni wameafikiyana juu ya kuwa *dha'îf* kwake, kama ilivyoelezwa na Sheikhul-Islâm Ibn Taymiyyah (رحمه الله). Kwa hakika amethibitishwa kuwa ni dhaifu sana na 'Alî Ibn al-Madînî, Ibn Sa'd na wengineo, na at-Twahâwî akasema: "Hadîth zake, kwa mtazamo wa wanavyuoni wa hadîth, ziko kwenye kingo za udhaifu." Kwahivyo kutokea kwenye zama za kale hadi za sasa alijulikana kwa udhaifu mbaya sana, sasa ni lipi lililowasababisha mahasimu wetu kuzipa mgongo kauli hizi zilizoungana katika kuthibitisha yakwamba 'Abdur-Rahmân ni *dha'îf* sana, awapo si mrongo, na badala yake washikamane na kauli ya al-Hâfidh kumuhusu yeye yakwamba ni "*dha'îf"*?! Mimi nayasema haya pamoja na uwezekano yakwamba pengine inawezekana ilitokamana na kuteleza kwa kalamu ya al-Hâfidh au mmojawapo wa wapokezi, alilikosa neno 'sana' lililokuwa pamoja na '*dha'îf'*.

Lakini kwa hali yoyote iwayo kufuata kwao ki-upofu juu ya neno hili hakutokuwa na faida yoyote kwao baada yake yeye mwenyewe kuihukumu hadîth kuwa "riwaya *bâtwil,* isiyokuwa na msingi wowote" kama ilivyonukuliwa kutoka katika *al-Lisân!* Kwahivyo hii ni mojawapo ya dalili nyingi yakwamba watu hawa ni wafuasi wa matamaniwa ya nafsi na wala sio wenye kutafuta haki. Kama wangelikuwa basi wangeliikubali hii kauli makhsusi ya al-Hâfidh inayokubaliana na ile ya adh-Dhahabî na wengineo kutoka kwa wanavyuoni wenye kuhakikisha. Hawangeliigeukia kauli yake nyengine yakwamba 'Abdur-Rahmân alikuwa ni *dha'îf* tu, kwa ajili ya kuitumia hii katika kuipinga kauli ya adh-Dhahabî, na kutoa hisiya ya urongo ya hadîth hii kwa watu, kuifanya ionekane kana kwamba ni hadîth ambayo wanavyuoni wamekhitilafiana kwayo. Jambo hili kisha litawarahisishia kuzua maoni mapya kuhusu hadîth inayo-onekana kukubaliana na kauli ya mmojawapo wa wanavyuoni kuhusu mmoja wa wapokezi wake! Tizama jinsi hatimae wanavyosema baada ya yaliyotangulia kutoka kwao: "Sasa iwapo hali ni kama hiyo kwa mtu katika mtizamo wa wanavyuoni wa hadîth, basi haitokuwa ni ya urongo, wala si jambo ambalo ni *dha'îf* sana. Bali iko katika daraja ya zile riwaya zinazoweza kutekelezwa kuhusiana na vitendo mbalimbali"!

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Hili halifai kutokana na pande mbili:

La Kwanza: Ni kuwa imeegemezwa juu ya uhakika yakwamba ‘Abdur-Rahmân ni ‘*dha’îf’* tu, na ilhali sivyo hivyo. Bali yeye ni ‘*dha’îf* sana’ (*dha’îf Jiddan*) kama ilivyotangulia, na kauli ya wazi kuhusu hilo kutoka kwa mmojawapo wa mchanganuzi mkali wa hadîth utakaofuata hivi karibuni.

La Pili: Inatatanisha hukmu ya al-Hâfidh mwenyewe juu yake, kwa hakika hukmu ya wanavyuoni wengine vilevile, yakwamba hadîth hiyo haina msingi wowote, kama ilivyotangulia. Sasa itaruhusiwa vipi kwao kuzikhalifu, hususan ikiwa mmoja wao alisema katika *at-Ta’qîbul-Hadîth* (Uk.21), yakwamba yeye “hamiliki uwezo kutangaza jambo kuwa ni swahîh au ni *dha’îf*!” Kwahivyo labda amelisema hilo kutokana na kuona haya kwake! Kwa vile hapa unaona jinsi alivyojipa nafasi inayomruhusu ajilete kwenye hatima yake mwenyewe ya kujitegemea hata iwapo itamaanisha kuwakhalifu hawa wanavyuoni wachanganuzi wakali wa hadîth! Tunayoyasema kumuhusu yeye kunaungwa mkono na uhakika yakwamba yeye ameongezea juu ya yaliyotangulia: Kwahivyo kuhusiana na hadîth hii sisi twashirikiana kwenye maoni ya wale wasiokuwa na msimamo huo [*yaani;* yakwamba imezuliwa], kama vile al-Hâkim, al-Hâfidh na as-Subkî. Kwahivyo sisi hatutaraji kumkanusha al-Hâfidh adh-Dhahabi, lakini hatahivyo rai yetu ni kwamba msimamo wa wanavyuoni hawa wawili uko karibu na haki.”

Uhakika yakwamba kauli hii ina urongo ndani yake na kuficha ukweli wenye kubainika unaweza kuonekana waziwazi kwani al-Hâkim ameitangaza hadîth hiyo kuwa ni swahîh katika *al-Mustadrak*, kama ilivyotangulia, na kisha as-Subkî akajikubaliya tu jambo hilo ki-upofu kutoka kwake kama ilivyoelezwa na al-Hâfidh Ibn ‘Abdul-Hâdî, aliyesema katika jawabu lake kwa as-Subkî kwa jina la *as-Swârimul-Munkî* (Uk.32): “Mimi nimeshangazwa na jinsi anavyofuata al-Hâkim ki-upofu katika kuitangaza hadîth hiyo kuwa ni swahîh kwani ni hadîth ambayo isiyokuwa swahîh wala haikuthibitishwa. Kwa hakika ni hadîth ambayo silsila yake ya riwaya ni dhaifu sana, na baadhi ya wanavyuoni wameihukumu kuwa imezuliwa. Hata silsila yake ya riwaya kutoka kwa al-Hâkim mpaka kwa ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd si swahîh, bali ilibandikizwa kwa ‘Abdur-Rahmân kwa njia ya urongo kama tutakavyokuja kuieleza. Hata kama ingelikuwa ni swahîh mpaka kwa ‘Abdur-Rahmân, bado ingeliendelea kuwa ni *dha’îf* na isiwe ni

dalili kwani ‘Abdur-Rahmân yumo ndani ya silsila yake, na al-Hâkim amefanya utata mkubwa sana, kama ajulikanavyo kuwahi kufanya mahali kwengine kwingi. Hii ni kwa sababu amesema katika kitabu chake *adh-Dhu’afâ’*, baada ya kumtaja ‘Abdur-Rahmân miongoni mwa wapokezi madhaifu...” na kisha akasema hayo yaliyotangulia (tizama ukurasa wa 116) kisha akasema: “Kwahiyo angalia kosa kubwa na utata mzito ambao al-Hâkim aliotumbukia ndani yake hapa. Kisha huyu mshindani mdhalilifu akajitweka makosa haya na utata wa al-Hâkim, akamfuata ki-upofu na kujitegemeza juu yake, huku akisema: “Na katika kuitangaza na kuithibitisha kuwa ni swahîh tumemtegemea al-Hâkim.’ Haliyakuwa muda mchache kabla ya kudai yakwamba lilikuwa ni jambo ambalo uswahîh wake umebainika kwake. Sasa hebu tizama, *Allâh akurehemu*, udhalilifu huu wa wazi na kosa la hatari! Jinsi mtu huyu alivyokuja kwenye hadîth ambayo si swahîh, na ambayo haikuthibitishwa, bali ni hadîth ya kuzuliwa, na akaitangaza kuwa ni swahîh na akajitegemeza juu yake, kwa kumfuata al-Hâkim ki-upofu kwenye hilo hata baada ya kosa lake na utatanishi wake kubainishwa. Hata pia baada ya mshindani huyu kujua kuhusu udhaifu wa mpokezi wake na yaliyo dhidi yake na akawa anafahamu vyema kuhusu yaliyosemwa kumuhusu yeye.” Mimi nasema: “Hivi ndivyo ilivyokuwa hali ya as-Subkî (رحمه الله), kuhusiana na hadîth hii, na akamfuata al-Hâkim ki-upofu katika kuitangaza kuwa ni swahîh. Kwanza ikifuatana na uhakika yakwamba kosa hili lenyewe ni kosa, vilevile linakwenda kinyume na maoni ambayo waliyoshikilia wao wenyewe, *yaani;* yakwamba ni *dha’îf*, si swahîh na si ya kuzua, kwahivyo watu hawa na wale wenye kuwafuata ki-upofu na kuwaunga mkono wamewakhalifu al-Hâkim na as-Subkî, kama ambavyo walivyowakhalifu wanavyuoni wengine wakubwa ambao sisi tuliowataja ambao walioitangaza hadîth hiyo kuwa imezuliwa au haina msingi wowote. Kwahivyo wao sio kwamba wanampinga adh-Dhahabi tu, bali wote wale ambao waliomkubali au hata kumukhalifu yeye! Sasa hebu muache mtu aliye muerevu atizame jinsi kufuata matamaniwa ya nafsi kunavyomfanya hali yake awe! Wanataka kujikomboa nafsi zao kutoka katika hatia ya kumpinga adh-Dhahabi, na njia ya pekee iwezekanayo ni kusema jambo lililo ovu zaidi, nalo ni kuwapinga wanavyuoni wote tuliowataja!

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kosa lao jengine la zaidi lililodhahiri kutoka kwa wanavyuoni ni jambo jengine wanalosema wakati wa matamshi yao yaliyotangulia ambayo ni kuitaja silsila ya riwaya ya at-Twabarânî ambayo tumeshawahi kuizungumzia na wakasema: “Kwahivyo adh-Dhahabi hakuwahi kuiona silsila hii ya riwaya kwani lau kama angeliiona hangeliyasema hayo.” Haya ni maneno ya *bâtwil* kwani adh-Dhahabi ameihukumu hadîth hiyo kuwa haina msingi wowote na ni *bâtwil* kwa njia ya al-Hâkim, na riwaya yake yumo ndani yake ‘Abdur-Rahmân Ibn Zayd na mtu mwengine ambaye yeye hakumjua, kama ilivyotangulia ubainifu wake katika mwanzoni mwa *tanbihi* hii. Riwaya ya at-Twabarânî, imewakusanya pamoja na ‘Abdur-Rahmân, wapokezi wengine watatu wasiojulikana, sasa itakuwaje kisha ni sawa kusema yakwamba iwapo adh-Dhahabi angeliiona hangelisema?! *Wallâhi* hii ni hali ya kosa la wazi na jeuri, au ujinga wa uhakika wa hali yao ya ujinga! Kwahivyo tunaomba rehma za Allâh na uongofu Wake! Kutokamana na yaliyotangulia itadhihirika wazi kwa wasomaji watukufu yakwamba hadîth hiyo ina udhaifu wa sampuli mbili:

i. ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd ibn Aslam ambaye ni dhaifu sana.

ii. Wapokezi wasiojulikana katika silsila ya riwaya mpaka kwa ‘Abdur-Rahmân.

Kwa maoni yangu hadîth hiyo ina udhaifu mwengine ambao ni kujipinga yenyewe (*idhtirâb*) kwa ‘Abdur-Rahmân au mtu aliye upande wake mwengine katika silsila. Hi ni kwa sababu mara nyengine anaisimulia kama kauli ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama ilivyotangulia, na mara nyengine alikuwa akiisimulia kama kauli ya ‘Umar peke yake, sio kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama ilivyopokewa na Abû Bakr al-Âjurrî katika kitabu chake *ash-Sheriya* (Uk.427), kwa njia ya ‘Abdullâh Ibn Ismâ’îl ibn Abî Maryam, kutoka kwa: ‘Abdur-Rahmân ibn Zayd pamoja nayo. Ama kumuhusu mpokezi huyu, ‘Abdullâh, basi mimi simjui. Kwahivyo hii haikuswihi kutoka kwa ‘Umar, si kauli ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala si kauli ya ‘Umar. Al-Âjurrî ameipokea kwa silsila nyengine kutoka kwa ‘Abdur-Rahmân ibn Abiz-Zinâd, kutoka kwa babake, yakwamba alisema: “Kutokamana na matamshi ambayo kwa ajili yake Allâh alimsamehe Âdam yalikuwa ni matamshi: ‘Yâ Allâh! Nakuomba kwa haki ya Muhammad juu

Yako...'" kwa sampuli ya mukhtasari lakini iliyofanana nayo. Haya pamoja na uhakika yakwamba kiungo cha/viungo vya mwisho kwenye silsila yake imekosekana/zimekosekana, na kwamba haikunukuliwa kama ni matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kisha juu ya haya silsila yake ya riwaya mpaka kwa ibn Abiz-Zinâd vilevile ni dha'îf, akiwemo ndani yake 'Uthmân ibn Khâlid babake Marwân al-'Uthmânî, amesema an-Nasâ'î kumuhusu yeye: "Si mtegemewa kabisa huyu." Kwahivyo haimkiniki yakwamba hadîth hii inatokamana na yale mambo ambayo yaliyochukuliwa kutoka kwa watu wa kitabu yaliyofundishwa kati ya Waislamu na watu wa Kitabu waliosilimu, au kutokamana na wale ambao hawakusilimu, au yaliyochukuliwa kutoka vitabuni mwao ambavyo visivyotegemeka kutokana na mabadiliko na mageuzi yaliyodhurika nayo, kama ilivyochambuliwa na Sheikhul-Islâm kwenye vitabu vyake. Mojawapo ya riwaya hizo dhaifu huwenda ikanasibisha jambo hilo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), ema kwa njia ya ki-makosa au kwa makusudi.

VIPI HADÎTH HII INAVYOKHALIFU QUR'ÂN

Msimamo wa wanavyuoni yakwamba hadîth hii ni uzushi usiokuwa na msingi wowote umezidi kuungwa mkono na uhakika yakwamba inakhalifu Qur'ân Tukufu katika sehemu mbili.

Ya Kwanza:Yakwamba imedhamini yakuwa Allâh (تعالى) alimsamehe Âdam kwa ajili ya *tawassul* kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), haliyakuwa Allâh (عزّ وجلّ) amesema:

فَتَلَقَّىٰٓ ءَادَمُ مِن رَّبِّهِۦ كَلِمَٰتٍ فَتَابَ عَلَيۡهِۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ٣٧

"Kisha Âdam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake akapokea toba yake; hakika Yeye ndiye mwingi wa kupokea toba (kwa wenye kutubia) na mwingi wa kurehemu (kwa wanaostahiki kurehemewa. Ama Iblisi hakutubia kwahivyo hakustahiki kurehemwa)."[110]

[110] Sûrah al-Baqarah (2):37

Imekuja tafsiri ya maneno haya kutoka kwa mfasiri mkubwa wa Qur'ân, Ibn 'Abbâs (رضي الله عنه), na tafsiri hii inakhalifiana na hadîth hii. Kwahivyo al-Hâkim amepokea (3/545) kutoka kwake, kuhusu maana ya Âyah: "Alisema: 'Ewe Mola wangu kwani Wewe hukuniumba kwa Mkono Wako?' Akasema: "Kwa hakika nimefanya hivyo." Akasema: "Kwani Wewe hukunipulizia uhai ndani yangu?" Akasema: "Kwa hakika nimefanya hivyo." Akasema: "Ewe Mola wangu kwani Wewe hukunifanya mimi kuwa ni mkaazi wa Pepo Yako?" Akasema: "Kwa hakika nimefanya hivyo." Akasema: "Kwani rehma Yako haichukuwi nafasi ya mbele kuliko ghadhabu Zako?" Akasema: "Kwa hakika ninafanya hivyo." Akasema:"Basi nikitubia na kurekebisha utanirudisha tena Peponi?" Akasema: "Kwa hakika nitafanya hivyo." Akasema [Ibn 'Abbâs]: "Basi hayo ndiyo matamshi yake:

فَتَلَقَّىٰٓ ءَادَمُ مِن رَّبِّهِۦ كَلِمَٰتٍ ٣٧

"Kisha Âdam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake."[111]

Amesema al-Hâkim: "Silsila ya riwaya yake ni swahîh', na adh-Dhahabî amekubaliana naye, na ni kama walivyosema.

Maneno haya ya Ibn 'Abbâs yamebeba hukmu ya kuwa ni maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutokana na sababu mbili:

i. Inazungumzia kuhusu suala linalotokamana na *ghayb* [lililofichikana], ambalo lisiloweza kuzungumziwa kwa rai tu, na..

ii. Yakwamba imepokewa katika ufafanuzi wa Âyah na lolote kama hilo, kama ambavyo hiyo imekuwa na hukmu yake kama ilivyothibitishwa mahali pake, hususan pindi inapokuwa ni kutoka kwenye kauli ya Imâm wa wanavyuoni wa tafsiri, 'Abdullâh ibn 'Abbâs (رضي الله عنهما), ambaye aliyeombewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) :

« اللَّهُمَّ فَقِّهْهُ فِي الدِّينِ وَعَلِّمْهُ التَّأْوِيلَ »

""Ewe Mola! Mpe ufahamu katika dini, na umfundishe ufafanuzi wa sawa."[112]

---

[111] Sûrah al-Baqarah (2):37

[112] Musnad Ahmad (1/266)

Vilevile imesemwa katika ufafanuzi wa maneno haya yakwamba ni yale yaliyotokea katika Âyah nyengine:

قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَآ أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ

٢٣

Wakasema: "Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (kubwa kabisa)."[113]

Haya ndiyo ambayo as-Sayyid Rashîd Rîdha aliyoyasema kuwa ya sawa katika tafsiri yake (1/279), lakini hatahivyo Ibn Kathîr akaashiriya udhaifu wa hayo (1/81). Kulingana na maoni yangu, hapo hapana utata baina ya kauli hizo mbili, bali moja ni ukamilifu wa nyengine. Kwahivyo hadîth ya Ibn 'Abbâs haitaji maneno ya kutubia ambayo Âdam (عليه السلام) aliyojifunza kutoka kwa Mola wake, haliyakuwa hii kauli ya pili imeitaja kauli yenyewe. Kwahivyo hakuna ikhtilafu, *walillâhil-Hamd*, haliyakuwa ikhtilafu ya hadîth inayojadiliwa imethubutu, na kwahiyo haina msingi wowote.

Ya Pili: Mahali mwa pili ni yale yaliyotokea mwishoni mwake: "Lau kama si kwa ajili ya Muhammad Mimi singelikuumba wewe." Hili ni suala la hatari kubwa linalohusiana na itikadi (*'Aqîdah*), ambayo inayostahiki kuthibitishwa kwa maandishi yaliyo *mutawâtir* ambayo watakayokubaliana nayo wote, au kwa maandishi yoyote yaliyo swahîh, kama ilivyo misimamo ya wengine[114]. Lau kama hili lingelikuwa ni jambo lililoswihi basi lingelipokewa kwenye kitabu au Sunnah swahîh. Kwahivyo kushikilia hili kuwa ni jambo lililoswihi ikiwa hakuna maandiko yanayotosheleza kuthibitisha dalili itakwenda kinyume na maneno ya Allâh (تبارك وتعالى):

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا ٱلذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ٩

"Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Qur'ân); na hakika sisi ndio tutakayoyalinda."[115]

---

[113] Sûrah al-A'râf (7):23

[114] Nukta ya Mfasiri: Rejea kwenye kitabu *Hadîth ni Uthibitisho wa Kivyake katika Imani na Sheriya* cha Sheikh al-Albânî (Dâr of Islamic Heritage, USA)

[115] Sûrah al-Hijr (15):9

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Hapa neno *"dhikr"* linajumuisha Sheriya yote, zote mbili, inayopatikana katika Qur'ân na katika Sunnah, kama ilivyothibitishwa na Ibn Hazm katika *al-Ihkâm*. Allâh (عزّ وجلّ) anasema:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ٥٦

"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu."[116]

Kwahivyo yoyote anayetaka kupingana na hikma hii iliyoelezwa, au kuongezea kitu, basi hilo halitokubaliwa kutoka kwake mpaka atoe andiko lake lililo swahîh kutoka kwa Mjumbe (صلى الله عليه وسلم) aliyehifadhiwa na makosa. Hili linatumika kwenye utata wa hadîth hii isiyokuwa na msingi wowote na yale ambayo mara kwa mara husikiwa yakitamkwa juu ya ndimi za watu: "Lau kama usigelikuwa ni wewe, lau kama usigelikuwa ni wewe, hata nisingeliziumba nyota." Kwahivyo hii vilevile ni riwaya iliyozuliwa (*mawdhû'*) kama ilivyotajwa na as-San'ânî na kuafikiwa na ash-Shawkânî katika *al-Fawâidul-Majmû'ah fil-Ahâdîthil-Maudhû'ah* (Uk.116). Vilevile inashangaza jinsi mdai uongo wa Utume Mirza Gulam Ahmad al-Qâdiyânî alivyoiba hadîth hii ya uzushi, na kisha kudai yakwamba lilikuwa ni jambo ambalo Allâh alilomzungumzia yeye, kwa kusema: "Lau kama si kwa ajili yako, Mimi nisingeliziumba nyota"!! Hili ni jambo lililokubaliwa na wafuasi wake Ma-Qâdiyânî hapa Damascus na kwengineko, kwani imesajiliwa kwenye kitabu cha mdai uongo wao wa Utume: *Haqîqatul-Wahy* (Uk.99).

Hata kama pangelikuwa na uwezekano wa kuyakubali madai yakwamba hadîth inayojadiliwa ni *dha'îf* tu, kama inavyodaiwa na baadhi yao katika kuwakhalifu wanavyuoni na wenye kuzihifadhi hadîth ambao tuliowataja, basi hata hivyo pia haitoruhusiwa kuitumia kama dalili kwa usawa wa sampuli ya *tawassul* ambayo ndani yake kunapatikana ikhtilafu. Hii ni kwa sababu ni kulingana na wasemavyo wao wenyewe kuwa ni sampuli ya kisheriya ya Ibada, na daraja ya chini ya sampuli yoyote ya Ibada ni kwamba ni jambo lililopendekezwa (*mustahabb*), na lililopendekezwa ni mojawapo ya daraja tano za hukmu za Sheriya ambayo isiyoweza kuthibitishwa isipokuwa kwa kupitia maandiko yaliyo swahîh yenye kujitosheleza kuthibitisha dalili. Kwahivyo ikiwa mtu ameshikilia yakwamba hadîth

[116] Sûrah adh-Dhâriyât (51):56

hiyo ni *dha'îf* basi hawezi kupata dalili juu yake kabisa. Hili liko wazi kabisa, apendapo Allâh.

Hadeeth ya Saba: "Fanyeni *tawassul* kwa *Jaha* yangu, kwani *Jaha* yangu mbele ya Allâh ni kubwa mno."

Baadhi yao wameipokea kwa lafdhi: "Munapomuomba Allâh, basi muombeni kwa Jaha yangu, kwani Jaha yangu mbele ya Allâh ni kubwa sana."

Hii ni *bâtwil* kabisa; haikupokewa kamwe katika kitabu chochote cha hadîth. Bali imenukuliwa na baadhi ya watu walio wajinga na Sunnah, kama ilivyotanabahishwa na Sheikhul-Islâm Ibn Taymiyyah (رحمه الله), katika *al-Qâ'idatul Jaliyyah* (Uk.132-150) ambapo aliposema: "Hata kama *Jaha* yake mbele ya Allâh ni kubwa kuliko *Jaha* ya Mitume wote na Manabii, lakini hatahivyo *Jaha* ya kiumbe mbele ya Muumba si kama *Jaha* ya kiumbe mbele ya viumbe wenzake. Kwa hakika hakuna awezae kuruhusiwa mbele Yake, kumuombea mwengine isipokuwa baada ya ruhusa Yake, haliyakuwa viumbe wanaweza kuwaombea viumbe wengine hata pasi na ruhusa. Kwahivyo kiumbe ni mshirika wa mwenzake muhusika kuhusiana na alitakalo, haliyakuwa Allâh (تعالى), hana washirika, kama alivyosema Yeye mwenyewe (سبحانه):

قُلِ ٱدۡعُواْ ٱلَّذِينَ زَعَمۡتُم مِّن دُونِ ٱللَّهِ لَا يَمۡلِكُونَ مِثۡقَالَ ذَرَّةٖ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَلَا فِي ٱلۡأَرۡضِ وَمَا لَهُمۡ فِيهِمَا مِن شِرۡكٖ وَمَا لَهُۥ مِنۡهُم مِّن ظَهِيرٖ ٢٢ وَلَا تَنفَعُ ٱلشَّفَٰعَةُ عِندَهُۥٓ إِلَّا لِمَنۡ أَذِنَ لَهُۥۚ حَتَّىٰٓ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمۡ قَالُواْ مَاذَا قَالَ رَبُّكُمۡۖ قَالُواْ ٱلۡحَقَّۖ وَهُوَ ٱلۡعَلِيُّ ٱلۡكَبِيرُ ٢٣

Sema: "Waiteni mnaowadaia uungu kinyume cha Allâh; (wakusaidieni; hawawezi kukusaidieni kitu); hawamiliki (hata) uzito wa mdudu chungu mbinguni wala ardhini, wala hawana ushirika (na Allâh) katika hizo (mbingu wala ardhi); wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao. Wala hautafaa uombezi mbele Yake (Allâh) ila kwa yule aliyempa idhini. Hata inapo-ondolewa hofu nyoyoni mwao, husema: 'Mola

wenu amesema nini?' (Na wao) huwaambia: '(Amesema maneno ya) Haki, naye ndiye Aliye juu, Mkubwa."[117]

Kwahivyo, uhakika yakwamba *Jaha* yake (صلى الله عليه وسلم) ni kubwa sana mbele ya Mola wake haimaanishi yakwamba tuifanyieni *tawassul* kwa Allâh, kwani hakuna amri ya kuifanya kutoka kwake (صلى الله عليه وسلم). Hili limebainishwa kwa uhakika yakwamba *rukû'* na *sujûd* ni alama za heshima zinazojulikana kwa watu, nao walikuwa na mazoweya ya – na mpaka sasa wengine wanaendelea – kuwasimamia, kuwainamia na kuwapomokea wafalme wao, ma-Rais na wale wanaowaheshimu. Kisha, kama ilivyoafikiwa na Waislamu, Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni mbora wa watu wote na aliye kwenye daraja ya juu zaidi. Lakini jee, inaruhusiwa kumsimamia, kumuinamia au kumpomokea katika uhai wake au baada ya kufa kwake? Jawabu ni kwamba iwapo mtu yoyote akipendelea kulitangaza jambo hilo kuwa ni halali basi ni lazima alithibitishe hilo yakwamba limethubutu kwenye Sheriya. Lakini kwenye utafiti tumegundua yakwamba *sujûd* na *rukû'* haziruhusiwi isipokuwa kwa Allâh (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلى الله عليه وسلم) amekataza mtu yoyote asimsujudie wala kumfanyia rukû' mtu yoyote. Vilevile tunaona kwenye Sunnah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amechukia kuona yakwamba watu wanawasimamia wengine, inayo-onyesha yakwamba jambo hilo halikushurutishwa. Unadhani kuwa mtu yoyote anaweza kudai yakwamba sisi tunapomkataza mtu yoyote asimsujudie Mtume (صلى الله عليه وسلم) sisi tutakuwa tunaikanusha daraja yake (صلى الله عليه وسلم) na heshima yake? Laa, sivyo kabisa. Kwahivyo, vilevile kuna yoyote awezae kukiri yakwamba tumsujudieni na kumfanyia *rukû'* Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa sababu ya uhakika yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) ana daraja kubwa? Jawabu ni vilevile tena, laa, kwa hakika laa.

Jambo hili waziwazi linatuwezesha sisi kuona, *Insha-Allâh*, yakuwa uhakika wa kuthibitishwa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) ana daraja kubwa haimaanishi yakwamba tunatakiwa kumtukuza kwa kumfanyia *tawassul* kwa njia ya *Jaha* yake, maadamu hilo halikuthibitishwa kwenye Sheriya.

[117] Sûrah Saba (34): 22-23

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kutokamana na daraja yake (صلى الله عليه وسلم) kubwa ni kwamba imewajibishwa juu yetu kumfuata na kumtwi'i kama ambavyo inavyotupasa kumtwi'i Mola wake. Kwahivyo imethibitishwa kutoka kwake (صلى الله عليه وسلم) yakwamba alisema:

« مَا تَرَكْتُ شَيْئًا يُقَرِّبُكُمْ إِلَى اللَّهِ إِلَّا أَمَرْتُكُمْ بِهِ »

"Sikuwaachia kitu chochote chenye kuwakurubisha kwa Allâh isipokuwa niliwaamrisha mushikamane nacho."[118]

Kwa vile hakutuamrisha kwa sampuli hii ya *tawassul*, hata pia angalau si kwa amri ya kupendekeza, kwahivyo hiyo si Ibada. Kwahivyo ni lazima tumfuate yeye kwa hilo na tuwache hamasa zetu upande moja, na tusipumbae sana mpaka tukaanza kuingiza mambo kwenye dini ambayo yasiyotokamana nayo kutokana na madai yakwamba sisi tunadhihirisha mapenzi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Bali mapenzi ya kikweli na ya dhati hudhihirishwa kwa kumfuata yeye (صلى الله عليه وسلم) kihakika, sio kwa kuzua mambo mapya kama alivyosema Allâh (عزّ وجلّ):

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ ٣١

Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda Allâh, basi nifuateni; (hapo) Allâh atakupendeni."[119]

Vilevile kama shairi lilivyosema:

تعْصى الإِلَه وأنتَ تُظْهِرُ حُبَّهُ ... هَذَا لَعَمْرك فى القِياسِ بَديعُ

لَوْ كَانَ حُبُّكَ صَادِقًا لأطعْتَهُ ... إِنَّ المُحِبَّ لِمَنْ يُحِبُّ مُطيعُ

Unamu'asi Mola, na huku wewe unadai yakwamba unampenda;

Kwa hakika hii ni hali katika vipimo vya kushangaza;

Kwani lau kama penzi lako lingelikuwa ni la yakini basi ungelimtwi'i;

---

[118] Imepokewa na ash-Shâfi'i, at-Twabarânî na wengineo.
[119] Sûrah Âli-'Imrân (3):31

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kwa hakika mwenye kupenda kwa ampendae ni mwenye kumtwi'i.

ATHARI MBILI *DHA'ÎF*

Athari Ya Kwanza*:* Athari inayohusu kuomba kwao kwa mvua kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake.

Baada ya kuzinukuu ahâdîth zilizo *dha'îf* na ambazo si swahîh na kuzifafanua, sasa tutainukuu athari ambayo inayonukuliwa mara kwa mara na wale wenye kuruhusu sampuli hii ya kuzuliwa ya *tawassul* kwa ajili ya kuifafanua iwapo ni swahîh au ni *dha'îf*, na ema inayo mafungamano yoyote na tunayojadiliana nayo au laa?

Al-Hâfidh amesema katika *al-Fat-h* (2/397):

"Ibn Abî Shaybah amepokea kwa silsila ya riwaya iliyo swahîh, kutoka katika riwaya ya Abî Swâlih as-Samân kutoka kwa Mâlik ad-Dâr, ambaye aliyekuwa muweka hazina wa 'Umar, alisema: "Watu walipatwa na msiba wa ukame katika zama za 'Umar, basi akaja mtu kwenye kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akasema: "Ewe Mjumbe wa Allâh! Waombee Ummah wako mvua, kwa sababu wanaangamizwa." Basi mtu mwengine akamjia yule mtu kwenye usingizi na akamwambia: 'Nenda kwa 'Umar...' *hadîth."* Kisha Sayf akasimulia katika *al-futûh* yakwamba yule mtu aliyeota alikuwa ni Bilâl ibn al-Hârith al-Muzanî, mmojawapo wa Maswahaba."

Jawabu kwa suala hili linatokamana na pande nyingi:

1. Sisi hatukubali yakwamba kisa hiki ni swahîh kwani Mâlik ad-Dâr si maarufu katika uadilifu na kudhibiti, na hii ni misingi miwili ya sharuti zenye kulazimisha kuswihi kwa riwaya yoyote, kama ilivyothibitishwa katika ta'luma ya hadîth. Ibn Abî Hâtim alimtaja katika *al-Jarh wat-Ta'dîl* (4/1/213) na hakumtaja mpokezi yoyote aliyepokea kutoka kwake isipokuwa Abî Swâlih huyu. Kwahivyo hii inaashiriya yakwamba hajulikani, na hii imezidi kutiliwa mkazo kwa uhakika yakwamba Ibn Abî Hâtim, yeye mwenyewe ambaye anayejulikana kwa kuhifadhi kwake na 'ilmu yake kunjufu, hakumnukuu yoyote ambaye aliyemthibitisha huyu kuwa ni mtu wa kutegemewa, kwahivyo amebakia kuwa ni mtu asojulikana. Kisha hili halipingani na kauli ya al-Hâfidh: "... kwa silsila ya riwaya iliyo swahîh, kutoka kwenye riwaya ya Abî Swâlih as-Samân..." kwani sisi

tunasema: Si tangazo yakwamba silsila yote ya riwaya ni swahîh, bali ni kwamba ni hivyo tu mpaka kwa Abî Swâlih, ikiwa hali si kama hivyo basi asingelianzia kuitaja silsila ya riwaya kutoka kwa Abî Swâlih. Bali angelianzia: "Kutoka kwa Mâlik ad-Dâr... na silsila yake ya riwaya ni swahîh." Lakini aliisema kwa njia ambayo hakutanabahi yakwamba palikuwa na kitu kilichohitaji uchunguzi ndani yake. Wanavyuoni waliyasema haya kwa sababu mbalimbali; miongoni mwa sababu hizo ni kwamba hawangelikuwa na uwezo wa kupata wasifu wa baadhi ya mpokezi/wapokezi na kwahivyo hawangelijiruhusu nafsi zao kupitisha hukumu juu ya silsila yote ya riwaya. Lau kama wangelifanya hivyo ingelimaanisha yakwamba watakuwa wakipitisha hukmu ya uswahîh pasi na yakini na kuwasababisha wengine waidhaniye kuwa ni swahîh na kuitumia kama dalili. Kwahivyo kitu ambacho afadhali wangelifanya katika hali kama hiyo ni kuinukuu sehemu inayohitaji uchunguzi wa zaidi, ambalo ndilo jambo alilolifanya hapa al-Hâfidh (رحمه الله). Vilevile ni kana kwamba aliashiriya uhakika yakwamba Abî Swâlih as-Samân alikuwa yu-pekee katika kuipokea kutoka kwa Mâlik ad-Dâr, au kwamba alikuwa hajulikani. Na Allâh Ndiye Mjuzi zaidi. Kwahivyo hii ni nukta nzuri sana ya ki-'ilmu ambayo itakayozingatiwa tu na wale wenye tajriba kwenye uwanja huu. Ambayo tuliyoyasema pia yamepata usaidizi kwa uhakika yakwamba al-Hâfidh al-Mundhirî amepokea kisa chengine kutoka katika riwaya ya Mâlik ad-Dâr, kutoka kwa 'Umar katika *at-Targhîb* (2/41-42) na akasema baada yake: "*at-Twabarâni* ameisimulia katika *al-Kabîr*. Wapokezi wake mpaka kwa Mâlik ad-Dâr ni maarufu na ni wenye kutegemewa, lakini kumuhusu Mâlik ad-Dâr basi mimi simjui." Maneno kama hayo yamesemwa na al-Haithumî katika *al-Majma' uz-Zawâid* (3/125). Lakini hatahivyo, nukta hii imemkwepa muandishi wa kitabu *at-Tawassul* (Uk.241), kwahivyo amedanganyika na yaliyojitokeza kutokamana na matamshi ya al-Hâfidh na kwahivyo akaitangaza hadîth hiyo kuwa ni swahîh na hatimae akasema: "Kwahivyo imetaja peke yake: Mtu fulani alikuja..." na akasema yakwamba riwaya iliyomtaja mtu huyo kuwa ni Bilâl Ibn al-Hârith imepokewa na Sayf, ambaye hali yake (*dha'îf*) inajulikana.

Lakini kwa hakika hakuna faida itakayopatikana kutokamana na haya, bali *athar* yote hiyo ni *dha'îf* kutokana na uhakika yakwamba Mâlik ad-Dâr ni mtu asojulikana, kama tulivyo-onyesha.

2. Kisa hiki kinakwenda kinyume na yaliyothubutu kwenye sheriya kuhusiana na kupendekezwa kwa Swala ya mvua (*Swalâtul-Istisqâ'*) kuomba kuteremshiwa mvua. Hii imepokewa kwenye ahâdîth nyingi, na imetendewa kazi na idadi kubwa mno ya wanavyuoni. Kwa hakika kisa hiki kinakhalifiana hata na yaliyo-onyeshwa kwenye Âyah ya Qur'ân, yakwamba katika mazingira kama hayo mtu na aombe *du'â'* na aombe msamaha, kama ilivyotokea katika Kauli ya Allâh (تعالى):

فَقُلْتُ ٱسْتَغْفِرُواْ رَبَّكُمْ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّارًا ١٠ يُرْسِلِ ٱلسَّمَآءَ عَلَيْكُم مِّدْرَارًا

١١

"Nikawaambia: Ombeni msamaha kwa Mola wenu. Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha. Atakuleteeni mawingu yanyeshayo mvua nyingi."[120]

Haya ndiyo aliyoyafanya 'Umar alipokuwa akiomba mvua kwa kutumia *du'â'* ya al-'Abbâs kama njia ya *tawassul*, kama ilivyotangulia. Hivi ndivyo walivyokuwa wakifanya Watu Wema Waliotutangulia, kila walipokuwa wakikumbwa na ukame walikuwa wakiswali na kuomba, na haikupokewa kabisa kutoka kwa hata mmoja wao yakwamba ati alikwenda kwenye kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kumtaka awaombee wao mvua. Kwahivyo lau kama hili ni jambo lililopasishwa katika sheriya basi wangelilifanya angalau hata kwa mara moja, kwahivyo ikiwa hiyo ndiyo hali yakwamba hawakufanya hivyo, basi hii yaonyesha yakwamba yaliyopokewa katika kisa hiki si jambo lililopendekezwa katika sheriya.

3. Hata kama kisa hiki kingelikuwa ni swahîh, bado pia hapangelikuwa na dalili ndani yake ya kuwaunga wao kwani huyo mtu kwenye kisa hicho, yeye mwenyewe hakuwa na jina, na kwahivyo ni mtu asiyejulikana. Uhakika yakwamba aliitwa Bilâl ibn al-Hârith katika riwaya ya Sayf haina thamani yoyote kwani huyo Sayf ni Sayf ibn 'Umar at-Tamîmî, na wanavyuoni wa hadîth wameafikiyana yakwamba yeye ni mtu *dha'îf*. Kwa hakika Ibn Hibbân amesema kumuhusu yeye: "Anapokea mambo ya kuzua kutoka kwa wapokezi wenye kutegemewa, na wanasema yakwamba alikuwa na mazoweya

[120] Sûrah Nûh (71):10-11

ya kuzua hadîth.” Kwahivyo riwaya za mtu sampuli hiyo hazikubaliwi kwa hali yoyote iwayo hususan ikiwa zinakhalifiana na riwaya nyengine.

Tanbîh: Mtu huyu, Sayf ibn ‘Umar at-Tamîmî, mara nyingi hutajwa kwenye vitabu vya historiya (*târîkh*) na at-Twabarî na Ibn Kathîr na wengineo, kwahivyo wale wenye kufanya kwenye viwanja vya historiya hawapaswi kupuuza taarifa kuhusu hali yake, ili wasije wakazipa riwaya zake ithbati zaidi kuliko zinavyostahiki. Mwengine anayefanana na yeye ni Lût Yahyâ, Abû Mikhnaf. Adh-Dhahabî amesema kumuhusu yeye katika *al-Mîzân*: “Mpokezi wa riwaya za ki-historiya, hana thamani yoyote na hawezi kutegemewa.” Abû Hâtim na wengineo wamemthibitisha kuwa atupiliwe mbali. Ad-Dâraqutniyy alimtangaza kuwa ni *dha’îf*. Akasema yahyâ Ibn Ma’în: “Huyu si mtegemewa kabisa.” Amesema Ibn ‘Adiyy: “Mlokole wa ki-Shi’ah na ni mpokezi wa riwaya zao za ki-historiya.” Vilevile anayefanana naye ni Muhammad ibn ‘Umar, maarufu kwa jina la al-Wâqidiyy, ni Sheikh wake Ibn Sa’d, muandishi wa *at-Tabaqât*, mwenye kupokea kiyasi kikubwa kutoka kwake. Dr. Al-Bûtwiyy alidanganyika kwenye kumkubali na kupokea mengi kutoka kwake katika *Fiqhus-Sîrah* hata ingawaje aliandika kwenye utangulizi wake yakwamba yeye atapokea tu yale yaliyokuwa swahîh na kuyapokea kwenye vitabu vinavyotegemeka! Lakini al-Wâqidiyy ni mtu aliyetupiliwa mbali (*matrûk*) katika hadîth kama ilivyowahi kusemwa na wanavyuoni wa hadîth, basi jitahadhari.

TAFAUTI BAINA YA *TAWASSUL* KWA DHATI YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NA KUMTAKA YEYE MWENYEWE AKUOMBEE *DU’Â’*

4. Hakuna lolote lililotajwa kwenye *athar* hii kuhusu *tawassul* kwa njia ya dhati ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), bali yote yaliyomo ndani yake ni kutakwa yeye awaombee kwa Allâh (تعالى) awateremshie Ummah mvua, na haya ni mas’ala ya kando ambayo hayakuguswa na hadîth iliyotangulia. Wala hakuna yoyote miongoni mwa Watu Wema Waliotutangulia (رضوان الله عليهم) aliyewahi, hata kuitangaza pia kuwa inaruhusiwa; *yaani*, yakwamba mtu anaweza kutaka kitu chochote kutoka kwake, (صلى الله عليه وسلم), baada ya kufa kwake. Sheikhul-Islâm Ibn Taymiyyah amesema katika *al-Qâ’idatul-Jaliyyah* (Uk.19-20): “Si

kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala kwa yoyote miongoni mwa Mitume waliokuja kabla yake kuweka Sheriya yakwamba watu waelekeze maombi yao kwa Malaika, Mitume au watu wema, wala yakwamba wawaombee wao, si baada ya kufa kwao, wala wanapokuwa hawapo pamoja nao. Kwahivyo hakuna asemaye: “Ewe Malaika wa Allâh nifikiliziye (*nishufaiye*) kwa Allâh maombi yangu, muombe Allâh atupe ushindi, au turuzuku au tuongoze.’ Vilevile hapana aruhusiwae kuwaambia hao Mitume au watu wema waliokufa: ‘Ewe Mtume wa Allâh, Ewe kipenzi cha Allâh, niombee nami *du’â’* kwa Allâh, muombe Allâh kwa niyaba yangu, nitakie kutoka kwa Allâh anisamehe...’ wala kuruhusiwa mtu kuwaambia wao: ‘Mimi nakulalamikia wewe kuhusu madhambi yangu, kupungua kwangu kwa riziki, au yakwamba maadui zetu wametuzidi nguvu,’ au: ‘Mimi nakulalamikia kuhusu mtu aliyenidhulumu mimi,’ wala ‘Nimeshuka kuja kuwa pamoja nawe, mimi ni mgeni wako, mimi ni jirani yako, au unatoa ulinzi kwa wale wenye kuomba kutoka Kwako.’ Wala mtu aandike maombi yake kwenye kipande cha karatasi na kukiweka juu ya makaburi, wala mtu asiandike taarifa yakwamba amechukuwa ulinzi wa fulani na fulani, na kisha kuitumia hiyo kwa watu, kama inavyofanywa na wazushi miongoni mwa watu wa Kitâb na Waislamu, kama wafanyavyo Wakristo kwenye Makanisa yao, na kama wafanyavyo wazushi miongoni mwa Waislamu katika Makaburi ya Mitume na Watu Wema, au wakiwa hawapo. Haya ni mambo ambayo kwayo hujulikana kwa umuhimu unaotokamana wa dini ya Uislamu, kwa riwaya *mutawâtir*, na kwa ijmâ’ ya Waislamu, yakwamba hakuna miongoni mwa Mitume kabla yake aliyeshurutisha lolote katika haya. Wala hakupatikana yoyote miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala yoyote katika wale waliowafuata wao juu ya uongofu aliyewahi kufanya chochote katika mambo haya, wala yoyote katika wanavyuoni wa ki-Islamu, wala ma-Imâm wanne walio maarufu wala yoyote mwengine, aliyetangaza mafundisho yoyote katika haya yapendekezwe. Wala hakuna yoyote katika wanavyuoni aliyeandika hayo kwenye sheriya za Hajj, wala katika wakati wowote mwengine, yakwamba hayo yamependekezwa kwa yoyote apeleke maombi yake kwenye kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala yakwamba mtu yoyote amtake yeye awashufaiye, wala yakwamba wamtake aombe *du’â’* kwa Ummah wake, wala yoyote amlalamikie kwa msiba wowote unaowasibu Waislamu kwenye maisha yao ya kilimwengu au dini yao.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kwa hakika Maswahaba walipatwa na mitihani ya kila aina ya balaa na maafa baada ya kifo chake. Wakati mwengine kwa ukame, wakati mwengine ukosefu wa rizki, nyakati nyengine kutokamana na kuwa na khofu na nguvu za maadui, wakati mwengine kwa madhambi na ma'asiya, wala hakuna yoyote katika wao aliyejaribu hata kwenda kwenye kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala kaburi la Ibrâhîm al-Khalîl, wala kwenye kaburi la Mtume yoyote na akasema: 'Sisi twakulalamikia wewe kuhusu ukame, au nguvu za maadui, au madhambi tufanyayo.' Wala hakuna yoyote aliyesema: 'Omba kutoka kwa Allâh, kwa niyaba yetu, au kwa Ummah wako, yakwamba na awafungulie nao rizki, au awape ushindi, au awasamehe.' Bali yote haya na mfano wake yanatokamana na mambo ya *bid'ah* mpya za uzushi, ambazo hazikupendekezwa kabisa na yoyote miongoni mwa wanavyuoni wa ki-Islamu. Kwahivyo haya ni mambo ambayo yasiyokuwa wâjib, wala kupendekezwa, kwa muafaka wa wanavyuoni wa Waislamu, na kila uzushi usiokuwa wâjib wala kupendekezwa basi ni uzushi muovu na upotofu kwa muafaka wa Waislamu.[121] Kwahivyo mtu yoyote mwenye kusema kuhusu aina yoyote ya uzushi yakwamba ni 'uzushi mzuri', basi hilo linaweza kusemwa tu iwapo ipo dalili kwenye sheriya kuonyesha yakwamba (uzushi huo) umependekezwa. Ama kuhusu zile ambazo hazikuwajibishwa wala kupendekezwa, basi hakuna yoyote katika Waislamu asemaye yakwamba mambo kama hayo ni mazuri ambayo yatakayomkurubisha mtu kwa Allâh. Mtu

---

[121] Kauli ya Sheikhul-Islâm haina budi kuchukuliwa kumaanisha ema

(i) Yakwamba alikuwa akiwazungumzia wenye kutukhalifu (mahasimu wetu) kwa misimamo yao, *yaani;* yakwamba uzushi umegawanyika kulingana na hukmu za ki-sheriya, zinazotokamana na yenye kuwajibika na mapendekezo, au

(ii) Yakwamba alikuwa akirejea kwenye yale mambo yaliyojulikana kwa ibara ya uzushi kwa lafdhi ya lugha peke yake, ambayo ni yale mambo yaliyozuka baada ya kufa Mtume (صلى الله عليه وسلم), lakini yakawa yana dalili kwenye sheriya ya kuwaunga wao mkono. Twayasema haya kwa vile ni mambo yanayojulikana kutoka kwake (رحمه الله), yakwamba msimamo wake yeye mwenyewe ni kwamba kila kitu kilichokuwa ni uzushi katika sheriya kuwa ni cha upotofu, na hili vilevile limeashiriwa kwa ukamilifu wa kauli yake hapa.

yoyote atafutae njia za kujikurubisha kwa Allâh kwa mambo yasiyokuwa katika amali njema, *yaani;* mambo ambayo yaliyoamrishwa kwa uwajibikaji au pendekezo, basi mtu huyo huwa amepotoka na ni mwenye kumfuata Sheitwani. Njia zake ni mojawapo ya njia za Sheitwani. Kama alivyosema 'Abdullâh ibn Mas'ûd (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alituchorea mstari ulionyo-oka, na akachora mistari mengine kwenye upande wake wa kuliani na kushotoni mwake, kisha akasema:

وَأَنَّ هَٰذَا صِرَٰطِى مُسْتَقِيمًا فَٱتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا تَتَّبِعُوا۟ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِۦ ۚ ذَٰلِكُمْ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ١٥٣

(Na sema uwaambie): "Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyoka. Basi ifuateni wala msifuate njia nyengine, zikakutengeni mbali na njia Yake (Allâh). Amekuusieni haya ili mpate kujilinda (na kila mabaya ya duniani na Akhera)."[122]

Baadhi ya waliokuja baadae wametumbukia ndani mwa kosa hili la wazi kabisa kwa sababu wanafanya makisio ya kulinganisha baina ya maisha ya Mitume katika *Barzakh* (hali ilivyo baina ya mauti na kufufuliwa) na maisha yao hapa ulimwenguni. Lakini haya ni makisio ya kulinganisha ya *bâtwil* yaliyo kinyume na Kitâb, Sunnah, na ukweli ulivyo. Mfano wenye kutosheleza kwa muda huu tulionao ni kwamba hakuna yoyote katika Waislamu anayeruhusu kuswali nyuma yao haliyakuwa wamo kwenye makaburi yao, wala hakuna yoyote awezae kujadiliana nao, wala kuzungumza nao, na tafauti zote zilizobaki ambazo hazitofichika kwa mtu mwenye busara.

KUWAOMBA MSAADA WENGINE WASIOKUWA ALLÂH (تعالى)

Makisiyo haya ya ki-ufisadi na yaliyo *bâtwil* yamewapelekea wao kwenye upotofu mkubwa, na msiba mkubwa wa maafa ambao Waislamu wengi wa kawaida, na baadhi ya wasomi wao, wametumbukia ndani mwake, nayo ni mafundisho ya kuwaomba Mitume na watu wema badala ya Allâh (تعالى), katika wakati wa shida na misiba. Kwa hakika hata huenda ukasikiya makundi mengi ya watu

[122] Sûrah al-An'âm (6):153

wakisimama kwenye makaburi wakiwalingania waliomo ndani mwake wawasaidie kwenye mahitaji yao mbalimbali. Utadhani yakwamba hawa waliokufa wanawasikiya maneno yao, na wanawauliza kila aina ya mahitaji, kwa lugha tafauti. Kwahivyo kulingana na maoni ya wale wenye kuwaomba, wao wanazijua lugha zote za ulimwenguni na wanaweza kuzipambanua kila moja kutoka kwenye nyenginezo, hata kama lau watu wanazungumza lugha tafauti katika wakati mmoja! Kwa hakika hii ni *Shirk* kuhusiana na Sifa za Allâh (تعالى), na watu wengi hawayajui hayo, na kwahivyo hutumbukia ndani ya upotofu mkubwa. Mafundisho haya yamekosolewa na kubatilishwa na Âyât nyingi; miongoni mwazo ni maneno ya Allâh (تعالى):

قُلِ ٱدۡعُواْ ٱلَّذِينَ زَعَمۡتُم مِّن دُونِهِۦ فَلَا يَمۡلِكُونَ كَشۡفَ ٱلضُّرِّ عَنكُمۡ وَلَا تَحۡوِيلًا ٥٦

Sema (Ewe Muhammad (صلى الله عليه وسلم)): "Waiteni wale mnaodai (kuwa ni waungu) mkamwacha Yeye (ili wakuondosheeni baa zinazokufikieni). Hawataweza kukuondosheeni shari wala kubadilisha (kuwa kheri)."[123]

Kwa hakika kuna Âyât nyingi kuhusu suala hili, na idadi kubwa ya vitabu na tasnifu zimeandikwa katika kuyachambua hayo.[124] Kwahivyo mtu yoyote mwenye shaka yoyote kuhusu mas'ala haya, basi na arejee kwenye vitabu hivi na ukweli utambainikia *Insha-Allâh*. Nimezipitia baadhi ya nukuu za baadhi ya wanavyuoni wa ki-Hanafî ambazo nadhania yakwamba zitakuwa na faida iwapo zitanukuliwa hapa, ili mtu yoyote asije akadhania yakwamba tuliyoyasema si mambo yaliyoshikiliwa na wafuasi wa *madh-hab* zilizo maarufu.

Ash-Sheikh Abut-Twayyib Shamsul-Haqq al-'Adhwîm Âbâdî katika *At-Ta'lîq al-Mughnî 'alâ Sunanid-Dâraqutniyy* (Uk.520-521), amesema:

[123] Surah al-Isrâ (17):56

[124] Miongoni mwazo ni *Qâ'idah Jaliyyah fit-Tawassul wal-wasîlah* na *ar-Radd 'alal Bakrî* cha Sheikhul-Islâm Ibn Taymiyyah, na kimojawapo cha kina ni *Majmû'atut-Tawhîd an-Najdiyyah* ambacho unachohitajika kukisoma.

"Miongoni mwa vitendo vya kinyonge zaidi na uzushi mkubwa zaidi na kuzua kuliko kukubwa ni mafundisho ya watu wa uzushi yakwamba wanamtaja Sheikh 'Abdul-Qâdir al-Jaîlânî (رحمه الله), kwa kusema: 'Ewe Sheikh 'Abdul-Qâdir al-Jaîlânî unayetokamana na Allâh; na swala zao wakazielekeza Baghdâd, na mambo mengine mengi. Watu hawa ni wenye kuabudu asiyekuwa Allâh na hufanya makisio ya kulinganisha yenye dhulma na upungufu mbele ya Allâh. Watu hawa wajinga hawajui yakwamba Sheikh (رحمه الله), hana uwezo wa kuwaletea uzito wa chembe wa jambo zuri, wala kuwaondolea uzito wa chembe wa maovu kutoka kwao. Kwanini wanamlingania yeye awasaidie na kwanini wanatafuta mahitaji yao kutoka kwake?![125] Kwani Allâh si mwenye kuwatosheleza waja wake?! Yâ Allâh! Twajilinda katika hifadha Yako kutokamana na kukushirikisha Wewe na kitu chochote, au kumtukuza kiumbe chako chochote kwa Utukufu unaokustahiki Wewe."

Vilevile wanasema katika *al-Bazzâziyyah* na vitabu vyengine vya hukmu za ki-dini: "Yoyote mwenye kudai yakwamba roho za ma-Sheikh zinahudhuria, na kwamba wanajua yanayotokea, atakuwa amekufuru."[126]

Na pia Sheikh Fakhrud-Dîn Abû Sa'd 'Uthmân al-Jiyânî ibn Suleimân al-Hanafî amesema katika risala yake: "Yoyote mwenye kudhania yakwamba mtu yoyote aliyekufa ana uwezo wowote wa kuendesha pasi na Allâh, na akaamini hivyo, basi huyo ni kafiri." Haya ndiyo yaliyoelezwa katika *al-Bahrur-Râ'iq*. Amesema al-Qâdhi Hamîdud-Dîn Nâkorî al-Hindî katika *at-Taushîsh*: "Miongoni mwao ni wale wenye kuwaomba Mitume na watu wema pindi wanapokuwa na mahitaji au wanapofikwa na mikasa, wakidhania yakwamba roho zao ziko haadhir na zinasikiya maombi yao na kujua kuhusu mahitaji yao. Hii ni *Shirk* mbaya sana na ujinga wa wazi kabisa; amesema Allâh (تعالى):

[125] Nutka ya Mfasiri: Tizama Sûrah az-Zumar (39):36
[126] *Al-Bahr* (5/134).

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُواْ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُۥٓ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَـٰمَةِ وَهُمْ عَن دُعَآئِهِمْ غَـٰفِلُونَ ۝

"Na wapotofu (wapotevu) wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Allâh ambao hawatawajibu mpaka siku ya Kiama, na hawatambui dua zao."[127]

Katika *al-Bahr* (3/94) munapatikana ndani yake: "Iwapo mtu atafunga ndoa, akishuhudilia imani yake kwa Allâh na Mtume Wake, basi ndoa hiyo haitokuwa ni ya sawa. Bali yeye ni kafiri kutokamana na imani yake yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) anayajua yaliyofichikana na mambo ya *ghayb*."[128]

Mfano wake umetokea kwenye *Fatâwâ* za *Qâdhi Khân; al-'Aynî; ad-Durrul-Mukhtâr,* na *al-'Âlimakîriyyah* na vitabu vyengine vya wanavyuoni wa ki-Hanafî, kisha kuhusu *Âyât* takatifu na maneno katika Sunnah iliyotwahirika katika kuyakosoa misingi ya *Shirk*, na katika ukemeaji halisi wa wale wenye hatia ya hayo, basi wao ni wengi kwa kuhisabika. Sheikh wetu, mwanachuoni, as-Sayyid Muhammad Nadhîr Husain ad-Dehlawî ana risala ya wazi yenye faida katika kuyajibu haya mambo ya uzushi maovu."

Athari Ya Pili*: Athari* inayohusu kutengeneza upenyo ulio wazi kwenye mbingu juu ya kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Amepokea ad-Dârimî katika Sunan yake (1/43): Aban-Nu'mân ametusimulia: Sa'îd ibn Zayd ametusimulia: 'Amr ibn Mâlik an-Nukrî ametusimulia: Abul-Jawâz Aws ibn 'Abdullâh ametusimulia, akisema: "Watu wa al-Madînah waliteseka kwa ukame mkali, basi

---

[127] Surat al-Ahqâf (46):5

[128] Yanayofanana na haya ni mazoweya ya kawaida ya watu wengi yakwamba wanajibu masuali kwa kusema: "Allâh na Mtume Wake ndiwo wajuao zaidi"! Kwani yaliyopokewa kuhusiana na hayo kama kauli za baadhi ya Maswahaba, basi hayo yalikuwa ni katika zama za uhai wake. Lakini baada ya kifo chake hilo haliruhusiwi kabisa. (*yaani;* mtu anatakiwa kusema tu 'Allâh ndiye Mjuzi zaidi')

wakamlalamikia ‘Âishah, naye akawaambia: ‘Tizameni kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم), tengenezeni upenyo kwenye paa juu yake, ili pasiwe na kitu baina yake na mbingu.” Akasema: Basi wakafanya hivyo, mara tukabarikiwa na mvua kiyasi cha kwamba mimea ikaanza kuchipuka na Ngamia wakanenepa na kuvimba, basi mwaka huo ukaitwa kwa jina la mwaka wa kuzidi.”

Silsila hii ya riwaya ni *dha’îf* na haiwezi kutumiwa kama dalili kutokana na sababu tatu:

i. Sa’îd ibn Zayd ambaye ni nduguye Hammâd ibn Zayd ni *dha’îf* kiyasi fulani. Al-Hâfidh amezungumza kumuhusu yeye katika *at-Taqrîb*: “Anakubalika kwa ujumla, lakini hufanya makosa.” Adh-Dhahabi amezungumza kumuhusu yeye katika *al-Mîzân*: “Yahyâ ibn Sa’îd amesema: ‘*dha’îf’*, na as-Sa’dî akasema: ‘Huyu si dalili’, wamezitangaza ahâdîth zake kuwa ni *dha’îf*.’ An-Nasâ’i na wengineo wamesema: ‘Hana nguvu’, na Ahmad akasema: ‘Yuko sawa.’ Yahyâ ibn Sa’îd hawezi kumkubali.”

ii. Hiyo ni *mawqûf* juu ya ‘Âishah, ikija kutoka kwa ‘Âishah peke yake na wala sio *marfû’* kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na hata kama silsila ya riwaya yake mpaka kwa ‘Âishah ingelikuwa ni swahîh basi haiwezi kuwa ni dalili kwani ni jambo lililo wazi katika hukmu ya kibinafsi ambapo hata Maswahaba nao pia hupatia mara nyengine na hukosea, na sisi haitupasi kutenda hilo.

iii. Yakwamba huyo Aban-Nu’mân kwenye *isnâd* yake ni Muhammad ibn al-fadhl, ambaye anaitwa “Ârim”. Ambaye asili yake alikuwa ni mpokezi wa kutegemewa isipokuwa tu alidhoofika mwishoni mwa maisha yake. Al-Hâfidh Burhânud-Dîn al-Halabi alimuorodhesha miongoni mwa watu waliodhoofika mwishoni mwa maisha yao kwenye kitabu chake: *al-Muqaddimah* (Uk.391) na akasema: “Hukmu kuwahusu watu hawa ni kwamba riwaya za watu hawa zinakubaliwa iwapo zitakuwa ni zenye kupokewa kutoka kwao na watu waliopokea kutoka kwao kabla ya kudhoofika kwao. Lakini riwaya zilizopokewa kutoka kwao na wale waliosikiya kutoka kwao baada ya kudhoofika kwao, au riwaya zilizopokewa kutoka kwao na watu ambao tusiowajua, ema walisikiya kutoka kwao kabla ya kudhoofika au baada, basi riwaya hizi zinafaa kukataliwa.”

Mimi nasema: Sisi hatujui iwapo *athar* hii ilisikiwa na ad-Dârimî kutoka kwake kabla au baada ya fahamu zake kudhoofika, kwahivyo haikubaliki, na haiwezekani kutumika kama dalili.[129]

Kisha, sheikh ul-Islâm ibn Taymiyyah alisema katika *ar-Radd ‘alal-Bakrî* (Uk.68-74): “Yaliyopokewa kutoka kwa ‘Âishah (رضي الله عنها), yakwamba upenyo ulitengenezwa juu ya kaburi lake kuelekea mbinguni, kwa lengo la mvua inyeshe, basi hilo si swahîh. Silsila ya riwaya yake si ya kutegemewa, na dalili ya wazi ya kuwepo kwake ni urongo na ni uhakika yakwamba hapakuwepo na upenyo kama huo kabisa juu ya nyumba kwenye maisha yote ya ‘Âishah. Bali ilibaki kuwepo kama ilivyo kwenye zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), sehemu yake ikiwa imezibwa na sehemu nyengine ikiwa wazi. Miyale ya jua ilikuwa ikipenya ndani ya nyumba yake kama ilivyothubutu katika swahîh mbili kutoka kwa ‘Âishah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali swala ya ‘Asr wakati ambapo miyale ya jua ilipokuwa ikipenya ndani ya nyumba yake na hayakuwa yakileta kivuli. Kisha chumba kikabaki namna hiyo kikiwa kimeshikana na Msikiti wa Mtume (صلى الله عليه وسلم)... kisha chumba cha ki-Utume kikaingizwa ndani ya Msikiti. Kisha ukuta mrefu ukajengwa kuzunguka chumba kizima cha ‘Âishah, kilichokuwa na kaburi ndani yake. Kisha baada ya hivyo kukajengwa dirisha kwenye paa ili iwezekane mtu kuingia ndani yake iwapo patakuwa na haja ya kusafisha. Ama kuhusu kuwepo kwa upenyo kama huo katika uhai wa ‘Âishah, basi huo ni urongo wa wazi kabisa. Hata lau kama hayo ni ya kweli basi ingelikuwa tu ni dalili yakwamba watu hawakuwa na mazoweya ya kuomba kutoka kwa Allâh kwa njia ya haki ya kiumbe, na kwamba hawakutumia njia ya kufanya *tawassul* kwenye maombi yao kwa njia ya mtu aliyekufa, wala kumuomba Allâh kwa kupitia kwake. Bali walifungua upenyo juu ya kaburi ili yakwamba rehma zipate kuteremka juu yake. Hawakufanya maombi yoyote kwa kutumia haki yake, sasa kuna mnasaba gani baina ya hili na lile?!

“Kwahivyo kiumbe anaweza tu kumnufaisha mwengine kwa njia ya maombi yake au kitendo chake. Ndio utakona jinsi Allâh (تعالى)

[129] Ash-Sheikh al-Ghumârî aliukosa udhaifu huu katika *al-Misbâh* (Uk.43), kama ambavyo ulivyopuuzwa na mwengine ili ilete hisiya kwa watu yakwamba riwaya hii ni swahîh.

anavyotupendelea tutafute mkuruba Naye kwa njia ya Îmân, vitendo vyema, kwa kutuma maombi ili baraka zake zimshukie Mtume (صلى الله عليه وسلم), kwa mapenzi yetu juu yake, kumtwi'i yeye na kushirikiyana naye. Haya ndiyo mambo anayotupendelea Allâh tutumie katika kutafuta mkuruba Naye. Ikiwa watu wanadhani yakwamba sisi tunatakiwa kutafuta mkuruba Naye hivihivi tu kwa kuwatumia watu wanaopendwa na Allâh, na sio kwa kufanya kwetu kitu chochote ambacho Allâh anachotupendelea tufanye kwa ajili ya kujikurubisha Kwake zaidi, kama vile Îmân na vitendo vizuri, basi wazo hili ni urongo na *bâtwil*, kama ilivyo-onyeshwa na busara na Sheriya.

"Ama kuhusiana na busara: Basi ukweli yakwamba ati mtu fulani makhsusi anapendwa na Allâh, haiwezekani kwa njia yoyote iwayo, kumaanisha au kuwajibisha yakwamba mahitaji yangu yatatimizwa kwa kufanya kwangu *tawassul* kwa njia ya dhati yake, ikiwa si mimi wala si yeye atakayefanya kitu chochote ambacho ndiyo sababu ya kutimizwa kwa mahitaji yangu. Iwapo hatahivyo ataniombea mimi, au nikawa na Îmân naye (صلى الله عليه وسلم) na nikafanya vitendo vya utwi'ifu kwake, basi hapana shaka yakwamba hii ni njia ya mkuruba. Lakini kuna njia gani ya mkuruba (*wasîlah*) kwangu mimi kwenye dhati ya mtu aliye kipenzi cha Allâh, iwapo sifanyi kitu chochote kinachohitajika kutoka kwangu kuhusiana naye, jambo kama hilo litakalozalisha matokeo kama hayo."

"Ama kuhusu sheriya: Basi ni kwamba Ibada yote imeegemezwa juu ya kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم), sio kwa kuzua mambo mapya. Kwahivyo hapana mwenye haki ya kuwajibisha kitu chochote katika dini ikiwa Allâh hajaliruhusu jambo hilo. Kwahivyo hairuhusiwi kwa mtu yoyote kuswali kwenye kaburi lake (صلى الله عليه وسلم), na kisha akasema, 'yeye ana haki zaidi yakwamba tuswali kumuelekea yeye kuliko al-Ka'bah'. Imethubutu kwenye swahîh yakwamba yeye (صلى الله عليه وسلم) alisema:

« لَا تَجْلِسُوا عَلَى الْقُبُورِ، وَلَا تُصَلُّوا إِلَيْهَا »

"Musikae juu ya makaburi wala musiswali mukiwa mumeyaelekea."

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Licha ya hayo baadhi ya watu wenye kupindukia mipaka kwenye hali zote huswali kwenye makaburi ya mashekhe zao, mpaka pia hukipa Qiblah mgongo na badala yake huswali kuelekea makaburi, kisha husema: 'Hiki ni Qiblah cha wateule wenye kufanya Ibada na *Ka'bah* ni Qiblah cha watu tu wa kawaida'! Watu wengine wanadhani yakwamba swala zenye kuswaliwa karibu na makaburi ya mashekhe zao ni bora kuliko swala za kwenye misikiti, bora hata kuliko swala katika *al-Masjidul-Harâm* (mjini Makkah), *al-Masjidun-Nabawî* (Mjini Madînah) na *al-Aqswâ* (Mjini Jerusalem). Kisha watu wengi hudhani yakwamba kufanya maombi kwenye makaburi ya Mitume na watu wema ni bora kuliko kufanya maombi misikitini. Mambo yote haya yanayojulikana na kila mmoja ambaye ni mwanachuoni wa dini ya ki-Islamu kuwa ni yenye kukhalifu moja kwa moja sheriya ya Uislamu. Kwahivyo yoyote ambaye asokuwa na msimamo kuhusiana na mas'ala haya na mas'ala yote, kwenye Kitâb na Sunnah, basi atapotoka kwenye upotofu na kwenye kuwapotoa wengine, na ametumbukia ndani ya dimbwi la maangamivu. Kwahivyo mja ni lazima ajisalimishe kikamilifu kwenye sheriya iliyokamilika, yenye utakaso na iliyo wazi, aliyokuja nayo Muhammad (صلى الله عليه وسلم), na ni lazima akubali yakwamba inaleta kila kilicho kizuri na hufanya hivyo kiukamilifu pasi na kasoro yoyote, na kwamba inaondosha madhara yote. Sasa kwahivyo anapo-ona jinsi za aina yoyote yenye kujikurubisha kwa Allâh au Ibada na kadhaalika, mambo ambayo watu wanayodhania kuwa ni mazuri na yenye kunufaisha, lakini haya siyo mambo yaliyopendekezwa kwenye sheriya, kisha ndipo atakapojua kwa yakini yakwamba madhara yake yatabeba uzito zaidi kuliko manufaa yoyote ndani yake, na uovu wake utakuwa na uzito kuliko zuri lolote, kwani sheriya haiwachi nje kabisa, jambo lolote lenye kufaidisha." Kisha akasema: "Na *du'â'* ni mojawapo miongoni mwa sampuli za Ibada, kwahivyo mtu anatakiwa ajifungamanishe na *du'â'* zenye kukubalika katika sheriya kwani zimehifadhiwa kutokamana na madhambi ya aina yoyote, kama ilivyo katika sampuli nyenginezo za Ibada zinatakiwa kutekelezwa kwa jinsi zilivyoshurutishwa katika sheriya, kwani hii ndiyo njia iliyonyooka, na twamuomba Allâh (تعالى) atuafikiye sisi katika kufaulu, ndugu zetu waliobaki na waumini wote."

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Tanbihi: Kitabu hiki cha ad-Dârimi kimeandikiwa na utaratibu wa *Sunan* Nne, kwenye mpangilio wa vitabu vyake na Milango, kwahivyo yaliyo ya sawa ni kwamba kimesifiwa kama: '*as-Sunan*', kama kilivyoitwa na muheshimiwa Sheikh Dahmân kwenye chapa yake ya kitabu hicho. Kilikuwa ni maarufu hapo awali kikijulikana kama *Musnadud-Dârimî*, na haya ni makosa yasiyokuwa na msingi wowote kutoka kwa wanavyuoni. Na tena kosa kubwa zaidi ni kukisifu kwa *ibara* ya *as-Swahîh* na jambo hilo si sawa kabisa kwani ndani mwake kumejaa *ahâdîth* zilizo *marfû'* ambazo silsila za riwaya zake ni *dha'îf*, na pia nyengine zina kiungo kilichokosekana, kimoja/nyingi, nyengine ni *athar* zilizo *mawqûf,* nyingi zao zikiwa ni *dha'îf* kama ilivyo hali ya hiyo *athar* tuizungumzayo hapa. Sasa kitasifiwaje kitabu kuwa ni '*as-Swahîh*'!! Kosa jengine kama hilo ni matumizi ya *ibara* 'vitabu vilivyo swahîh' kuvihusu vitabu Vinne vya *Sunan*, kama wanavyoviita baadhi ya watu! Huku si kukhalifu anwani zake za kweli tu '*as-Sunan*', bali vilevile inakhalifiana na ukweli jinsi ulivyo, kwani vilevile vinavyo ndani mwake ahâdîth nyingi zilizo *dha'îf*. Vilevile vimekhalifu mambo waliyoyafanya waandishi wake, *yaani;* yakwamba wao wenyewe mara nyengine wameziashiriya ahâdîth zilizo *dha'îf* ndani ya vitabu vyao wenyewe, khususan Imâm at-Tirmidhî aliyechambua udhaifu wa ahâdîth nyingi kwenye kitabu chake. Katika Sunan Ibn Mâjah kuna idadi kubwa ya hadîth za kuzuliwa, licha ya kuzitaja ahâdîth *dha'îf*, kwahivyo hapana mwengine isipokuwa mtu mjinga tu au mtu mwenye maslahi yake ya kibinafsi atakayerejelea kwenye vitabu vya Sunan kama 'vitabu vilivyo swahîh.'

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

❖ **SHAKA YA NNE**

KUWEKA VIPIMO VYA MAKISIO YA ULINGANISHAJI BAINA YA MUUMBA NA VIUMBE

Wenye kutukhalifu sisi wanadai: Hakika *tawassul* kwa njia ya dhati za watu wema na kwa njia za utukufu wao ni jambo linalopendekezwa na kuruhusiwa kwani imeegemezwa juu ya fikra za kimantiki. Hii ni kwa sababu iwapo mmoja wetu anahitaji kitu kutoka kwa mfalme, au waziri, au mtu aliye kwenye nafasi ya mamlaka, basi hatomuendea yeye mwenyewe moja kwa moja, kwani atakuwa anafahamu yakwamba pana uwezekano wa kutohudumiwa kwenye maombi yake, akidhani yakwamba asije akafukuzwa kwa haraka. Kwahivyo ni jambo la kawaida kwake pindi anapohitaji kitu kutoka kwa mtu kama huyo, yakwamba amtafute mtu mwenye kumjua, mtu aliyekaribu naye mwenye uzito fulani naye, na amfanye mtu huyo kuwa ni wa kati na kati na yeye. Litakapofanywa hilo basi huyo mtu atapata jawabu na afanye alipendalo. Kisha wanadai: Hali ni kama hiyo kuhusiana na mafungamano yetu na Allâh (سبحانه), kwani Allâh (عزّ وجلّ) ni mtukufu wa watukufu na mkubwa zaidi mwenye kiburi, haliyakuwa sisi ni wa'asi wenye kutenda madhambi na kwahivyo tuko mbali sana na Allâh, kwahivyo hatufai sisi yakwamba tumlinganie Yeye moja kwa moja. Lau kama tungelitaka kufanya hivyo basi tutakuwa na khofu yakwamba atatukatalia mbali, au angalau asitujali ili tujirudie zetu patupu. Lakini kuna watu wema kama vile Mitume, na Manabii, na Mashahidi (waliouwawa kwa ajili ya Allâh) walio karibu zaidi na Allâh (سبحانه), Naye atawajibu kama wao watamlingania Yeye, na Yeye atawakubalia maombi (*shifâ*) yao iwapo wao watamuombea mtu yoyote. Kwahivyo, wanasema, basi hatufai sisi kutumia heshima zao kama njia ya mkuruba (*tawassul*) Kwake, na tukaanza maombi yetu kwa kuwataja majina yao. Tukitumai yakwamba Allâh atatusikiliza sisi kwa ajili ya daraja zao Kwake, za heshima, na kwahivyo atujibu maombi yetu. Sasa ni kwa nini, wao wanasema, watu wanaipinga sampuli hii ya *tawassul* ambapo ni jambo ambalo watu hutumia baina yao wenyewe, ni kwanini wasiweze kufanya kama hivyo kuhusiana na Mola wanayemuabudu?

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Sisi tunasema kwa kuijibu *shubha* hii: Kwahivyo munalolifanya ni kufanya Makisio ya kulinganisha baina ya Muumba na viumbe. Munawaza hapo kuwepo na mambo yenye kulingana baina ya Mwenye kuzihimili Mbingu na Ardhi, Hakimu wa mahakimu, Muadilifu wa hali ya juu, Mpole sana na Mwenye rehema na wale viongozi madhalimu, wale wafalme madikteta wasiojali kabisa kuhusu hali njema za raiya wake, wale wenye kuweka vikwazo na vizuizi baina yao na raiya wao, wasioruhusu mtu yoyote kuwakurubia isipokuwa kwa njia za mtu mwenye wâsita ambaye itakupasa umuhonge na umpe tunu, inakupasa ujisalimishe na kujidhalilisha kwao, itakubidi upate idhini yao na uwasababishe wawe na furaha na wewe. Basi Enyi masikini!, ishawahi kupita kwenye fahamu zenu yakwamba munapofanya hivyo huwa munamkashifu Mola wenu, mukimtuhumu Yeye, yakwamba anawafanyia nyinyi dhulma, na kumsifu Yeye kwa jambo analolichukia na lenye kumuudhi?

Haijapita kwenye fahamu zenu yakwamba munamsifu Allâh (تعالى) kwa sifa mbovu kabisa munapofanya makisio ya kulinganisha baina yake Yeye na viongozi madhalimu, na wafalme waovu? Dini yako inakuruhusu vipi wewe ufanye hivi? Inaendana vipi hali hii kwa uhakika yakwamba ni wajibu juu yako kumuheshimu Mola wako na kutangaza sifa za Muumbaji wako? Sasa kwani wewe huoni yakwamba lau kama ingelikuwa inawezekana kwa watu kumsemesha kiongozi uso kwa uso, na kwamba walikuwa na uwezo wa kuzungumza naye moja kwa moja pasi na mtu wa kati na kati, basi hilo lingelikuwa ni jambo la usawa kabisa na lenye kumstahiki sifa, kuliko kuwa anaweza tu kuzungumziwa kwa kupitia njia ya mwenye wâsita ambaye anyeweza kuyafanya mambo mazito zaidi au rahisi kama wapendavyo wao?

Enyi watu! Hakika nyinyi munajifakhiri pindi munapozungumza kumuhusu ‘Umar ibn al-Khattwâb na munamsifu na kumpongeza, na munawafahamisha watu yakwamba yeye alikuwa ni mtu mkarimu sana, na wala hakuwa kabisa na majivuno au kiburi, na kwamba mara nyingi yeye alikuwa pamoja na watu. Aliye mnyonge kabisa miongoni mwao alikuwa na uwezo wa kumkabili na kuzungumza naye pasi na mtu yoyote mwenye wâsita au yoyote mwenye kupata ruhusa ya kumuingiza mtu yoyote. Kisha alikuwa akichunguza mahitaji yao na kuwasaidia iwapo watakapokuwa na haki. Wewe hudhani yakwamba mpango huu wa mamlaka ni bora na mzuri zaidi, au ule mfano unaoufanya kuwa ndio wa Mola wako? Lakini wewe una nini haswa?

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Unahukumu vipi? Fahamu zako ziko wapi? Zimekwenda wapi? Fahamu zako njema zimepotelea wapi, na mutajiruhusu vipi mpaka mufanye ulinganishaji baina ya Allâh (تعالى) na mfalme aliye katili? Au ilikuwaje mpaka Sheitwani akawaongoza nyinyi kufanya makisio ya kulinganisha baina ya Allâh (تعالى) na mfalme aliye dhalimu? Enyi watu! lau kama mungelifanya makisio ya kulinganisha baina ya Allâh (تعالى) na watu ambao ni wema, na walio bora miongoni mwao, basi mungelikuwa na hatia ya Ukafiri, sasa jee iwapo mulifanya makisio ya kulinganisha baina yake Yeye Allâh (تعالى) na aliye dhalimu zaidi, muovu na mpotofu miongoni mwa watu?

Enyi watu! Lau kama mungelifanya makisio ya kulinganisha baina ya Mola wenu Mkuu na ‘Umar ibn al-Khattwâb, aliye mtu mwema na muadilifu, basi mungelitumbukia ndani ya *shirk*, sasa ilikuwaje mpaka Sheitwani akawaongoza nyinyi mukaingia kwenye hali hiyo ambayo muliyotosheka nayo tu alipowaongoza kufanya makisio ya kulinganisha baina ya Mola wenu na wafalme makatili na mafisadi, viongozi na mawaziri? Kwa hakika kumfanya Allâh (تعالى) kuwa ni kama viumbe Vyake ni Ukafiri kwa hali yoyote iwayo, na Yeye (سبحانه) alionya kuhusu jambo hilo pindi aliposema:

وَيَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَمۡلِكُ لَهُمۡ رِزۡقٗا مِّنَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ شَيۡـٔٗا وَلَا يَسۡتَطِيعُونَ ٧٣ فَلَا تَضۡرِبُواْ لِلَّهِ ٱلۡأَمۡثَالَۚ إِنَّ ٱللَّهَ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ ٧٤

“Na wanamwacha Allâh wakawaabudu wasiowamilikia riziki hata kidogo si kutoka mbinguni wala katika ardhi, wala hawana uweza wa lolote. Basi msimpigie Allâh mifano. Hakika Allâh anajua, na nyinyi hamjui (lolote).”[130]

Kama ambavyo Yeye alivyokataa kufanana kwa aina yoyote baina yake Yeye na kitu chochote kutokamana na viumbe vyake, kama alivyosema:

[130] Sûrah an-Nahl (16):73-74

لَيۡسَ كَمِثۡلِهِۦ شَيۡءٞۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡبَصِيرُ ١١

“Hakuna chochote mfano wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona.”[131]

Ulinganisho muovu zaidi awezao kuufanya mtu ni kwamba anamdhania Yeye kuwa ni kama viongozi waovu, wenye mambo machafu na mafisadi, akidhania yakwamba anafanya jambo lililo zuri! Kwa hakika ni jambo hili ndilo ambalo lenye kuwasababisha baadhi ya wanavyuoni na wenye kuhakiki kuwa ni wagumu na wakali sana katika kukabiliana na *tawassul* kwa njia ya dhati ya Mitume. Hii ndiyo sababu wakaitangaza kuchangia kwenye *shirk* hata kama kitendo chenyewe kwa mtizamo wetu sio *shirk*. Lakini inatakiwa ihofiwe pakubwa yakwamba itapelekea kwenye *shirk*, na kwa hakika hilo haswa ndilo lililofanya katika hali ya wale wenye kutafuta kuhalalisha *tawassul* zao kwa kutumia makisio haya ya kulinganisha, ambayo yenyewe ni ukafiri, lau kama wanajua hayo. Kufikia hapa itadhihirika waziwazi yakwamba leo, kauli ya mlinganizi mmoja wa ki-Islamu, kwenye msingi wa Kumi na Tano katika misingi yake ishirini amesema: “Iwapo *du’â’* itaunganishwa pamoja na *tawassul* kwa Allâh kwa kutumia njia ya mmojawapo wa viumbe Vyake, basi hii ni tafauti ndogo tu kuhusiana na adabu za *du’â’*, na wala sio miongoni mwa mas’ala ya ‘Aqîdah,” Sio sawa bila ya kuwepo masharti, kama ambavyo ulivyoona jambo hilo uhakika wake ni kutokubaliana kuhusu mas’ala ya kimsingi, kwani linapelekea kwenye *shirk* ya wazi kabisa kama ilivyotangulia. Labda mfano wa kauli hii unaosababisha watu kutojishughulisha kuhusiana na upotofu huu ni mojawapo ya sababu zenye kuwazuiya watu na kufanya utafiti kwenye mas’ala haya na kutafuta ukweli unaofungamana na hayo, inayoleta matokeo hatimae katika kuwaruhusu wazushi kuendelea juu ya uzushi wao, na kuuruhusu ukuwe katika uzito wake na hatari. Kwahivyo amesema Imâm al-‘Izz ibn ‘Abdis-Salâm kwenye risala yake: *al-Wâsitah* (Uk.5): “Yoyote mwenye kuwafanya Mitume, na wanavyuoni wa dini, kuwa ni wenye *wâsita* baina ya Allâh na viumbe vyake, kama washika zamu walioajiriwa na wafalme wa kilimwengu wenye kuwajia baina yao na raiya zao, na wakadhani yakwamba wao ndiwo wenye kunyanyua juu mahitaji ya viumbe vya Allâh (تعالى), na kwamba Allâh (تعالى), huongoza,

[131] Sûrah ash-Shûrâ (42):11

hutoa riziki na misaada kwa viumbe vyake kwa kupitia kwao, kwa maana yakwamba viumbe huleta maombi yao kwao na wao nao hupeleka maombi hayo kwa Allâh, kama ambavyo wale wenye *wâsita* kwa wafalme wa hapa ulimwenguni hupeleka maombi ya raiya kwao, na watu huwaomba kwani halionekani hilo kuwa ni sawa kwao kuwaomba wafalme moja kwa moja, na ni jambo la faida zaidi kwao kupeleka maombi yao kwa wale wenye *wâsita* kuliko kumuomba mfalme moja kwa moja, kwani wao wako karibu zaidi na mfalme. Kwahivyo yoyote mwenye kuwachukulia wao kuwa ni wenye *wâsita* **kwa njia hii,** basi huyo ni Kâfir na ni Mushrik. Anahitajika afanye toba, na ema na atubie au na auwawe. Watu kama hao hufanya makisio ya ulinganishi na Allâh; wao humfanya kuwa ni kama viumbe vyake, na kumfanya Allâh kuwa na washirika...” ’

❖ SHAKA YA TANO

KUNA JAMBO LOLOTE LIWEZALO KUZUIYA *TAWASSUL* YA UZUSHI KUWA NI KITU TU KILICHORUHUSIWA LAKINI SI JAMBO LILILOPENDEKEZWA?

Huwenda mtu akasema: Ni sawa yakwamba hakuna kilichothibitishwa katika Sunnah ambacho ni dalili ya kuonyesha kupendekezwa kwa *tawassul* kwa njia ya dhati za Mitume na watu wema, lakini ni kipi kilichoko hapo chenye kutuzuiya sisi iwapo tutakifanya tu kuwa ni kitu kinachoruhusiwa kwetu, kwani hakuna kilichopokewa chenye kukataza?

Hii ni shaka iliyo *bâtwil* ambayo tuliyowahi kuisikiya kutoka kwa baadhi ya watu ambao wanaopendelea kuchukuwa msimamo wa kati na kati baina ya pande mbili, kwa ajili ya kuwaridhisha wao wote wawili na kujiepusha na kulaumiwa na wote hao wawili! Kisha jawabu ni kwamba: "Sisi hapa ni lazima tusisahau ni nini maana ya *wasîlah*, ni jambo ambalo kwa kupitia njia yake baadhi ya malengo hupatikana, kama ilivyotangulia. Kisha lengo tunalotarajia kulifikia litakuwa ema ni la ki-dini au ni la kilimwengu. Sasa iwapo la kwanza ndilo lengo lenyewe, basi haiwezekani kujua njia itakayoleta lengo la ki-dini isipokuwa kwa njia ya sheriya. Sasa ikiwa mtu anadai kwa mfano yakwamba atatumia mojawapo ya alama kubwa za Allâh (تعالى) katika uumbaji Wake, kama vile usiku na mchana, na kwamba ndiyo iliyokuwa sababu ya *du'â'* yake kutakabaliwa. Basi hilo litakataliwa isipokuwa iwapo atakuja na dalili yake, na hatoweza kujisemea tu hivihivi yakuwa ilikuwa ni sampuli ya *tawassul* inayoruhusiwa. Hiyo itakuwa ni kauli ya kujichanganya yenyewe kwani ameiita kwa jina la '*tawassul'* na hili halijathibitishwa katika sheriya, na hana njia nyengine ya kuithibitisha. Hii ni tafauti na ile ya pili katika zile hali mbili, *yaani;* hali ya kilimwengu, kwani njia za kilimwengu zinaweza kujulikana kwa kutumia akili, au kwa kupitia kwenye ilimu au tajriba na kadhaalika. Kama mtu anayefanya biashara ya kuuza mvinyo. Hii ni njia maarufu ya kujipatia utajiri, kwahivyo ni njia ya kujipatia malengo ya ukusanyaji wa utajiri. Lakini hatahivyo hii ni njia ambayo Allâh aliyoiharamisha, kwahivyo imekatazwa kuiuza, kama ilivyo kinyume na hali iwapo angeliuza kitu ambacho Allâh (عزّ وجلّ) alichokiharamisha, hapo itakuwa inafaa. Lakini kuhusu kitu ambacho

imedaiwa kuwa ni njia ya kujikurubisha kwa Allâh, na kwamba inasababisha *du'â'* ya mtu kutakabaliwa zaidi – basi hili haliwezi kujulikana isipokuwa kwa njia ya sheriya. Kwahivyo pindi inaposemwa: Hili halipatikani katika sheriya, hairuhusiwi hata kuiita hiyo kuwa ni '*wasîlah*' wala kisha kufuata hilo kwa kusema yakwamba inaruhusiwa kuitumia kama njia ya *tawassul*. Haya yamezungumziwa kwa kina katika mlango wa pili wa kitabu hiki.

Suala La Pili ni kwamba sampuli hii ya *tawassul* tuliyoikubali haipatikani katika sheriya – haliyakuwa iko kwenye sheriya ile ambayo itakayokututosheleza kikamilifu ili tusiwe na haja nayo tena. Sasa ni jambo gani litakalowasababisha Waislamu kuifadhilisha *tawassul* hii ambayo isiyopatikana katika sheriya, na wakaiwacha *tawassul* ipatikanayo kwenye sheriya? Wanavyuoni wote wamekubaliana yakwamba *bid'ah* itakapokhalifiana na Sunnah, basi hiyo itakuwa ni *bid'ah* ya upotofu, na *tawassul* hii ni mfano wake – kwahivyo hairuhusiwi kuitumia, wala hata kama kitu ambacho hakikupendekezwa, lakini ni kama kitu kilichoruhusiwa!

Suala La Tatu ni kwamba *tawassul* kwa njia ya dhati za watu inafanana na *tawassul* ambayo watu hufanya kwa njia ya watu wenye *wâsita* kwa wafalme na viongozi wa kilimwengu. Haliyakuwa hakuna kitu kama Allâh (تبارك وتعالى) – kama inavyokubalika hata na wale wenye kuifanya *tawassul* hiyo. Kwahivyo ikiwa Muislamu atafanya *atatawassal* Kwake (تعالى) kwa dhati za watu, basi kwenye kitendo chake hicho atakuwa amefananisha baina Yake na hao wafalme na viongozi – kama ilivyoelezwa, na hilo haliruhusiwi.

❖ SHAKA YA SITA

KUFANYA MAKISIO BAINA YA *TAWASSUL* KWA NJIA YA DHATI AU JAHA YA MTU NA *TAWASSUL* KWA 'AMALI NJEMA

Hii ni shaka nyengine iliyoletwa na hao wazushi[132] Sheitwani ameifanya iwashawishi, na akawapelekea kusema: "Umesema yakwamba miongoni mwa *tawassul* za kisheriya zilizokubaliwa, ni kufanya *tawassul* kwa Allâh (تعالى) kwa njia ya amali njema. Sasa ikiwa *tawassul* hii imeruhusiwa, basi *tawassul* kwa njia ya mtu mwema aliyeifanya hiyo amali njema ina haki zaidi kuthibitishwa kuruhusiwa kwake. Vilevile ina haki zaidi yakwamba inafaa ipendekezwe, na wala isikashifiwe." Kwahivyo majibu yake yanatokamana na pande mbili:

1. Hii ni hali ya makisio na makisio kuhusiana na sampuli za Ibada ni *bâtwil* kama ilivyotangulia, na mfano wa mtu mwenye kusema kauli hii ni kama ya mtu mwenye kusema: "Ikiwa inaruhusiwa kwa mtu kufanya *tawassul* kwa njia ya amali zake njema, ambazo bila ya shaka yoyote ni za daraja ya chini kuliko amali za watu wema wanaopendwa na Allâh, na Mtume Wake, basi kwahivyo inaruhusiwa kwake kufanya *tawassul* kwa njia ya amali za Mtume na watu wema. Kwahivyo jambo hili pamoja na litakalofuata kutokamana na hayo ni ya urongo na *bâtwil*.

2. Hili ni kosa la wazi kabisa, kwani sisi hatusemi, na wala hajawahi kusema Mtu Mwema yoyote kabla yetu, yakwamba inaruhusiwa kwa Muislamu kufanya *tawassul* kwa njia ya amali njema za mtu mwengine. Bali *tawassul* iliyoashiriwa ni *tawassul* kwa njia ya amali zake yeye mwenyewe. Kwahivyo hili litakapobainika twawageuzia juu yao kauli yao iliyotangulia na kusema: inapokuwa hairuhusiwi kufanya *tawassul* kwa njia ya amali njema iliyofanywa na mtu asiyekuwa yule mwenye kuomba, basi inakuwa ni haki zaidi na kufaa yakwamba hairuhusiwi kufanya *tawassul* kwa dhati yake. Hili si zito kuliangalia, na kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh.

[132] Miongoni mwao ni muandishi wa *at-Tâj*

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

❖ SHAKA YA SABA

KUFANYA MAKISIO BAINA YA *TAWASSUL* KWA NJIA YA DHATI YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NA KUTABARUKU KWA ATHARI ZAKE

Hii ni shaka nyengine ambayo haikujulikana kwenye karne zilizopita, lakini ilibuniwa na kupewa msukumo na yeye mwenyewe, Dr. Al-Bûtwî, kwani amethibitisha katika kitabu chake: *Fiqhus-Sîrah* (Uk.344-355) alipokuwa akijadili mafunzo yanayopatikana kutokamana na matukio ya Hudaibiyyah, yakwamba yanaonyesha ruhusa ya kutafuta manufaa kutoka kwenye mambo yaliyoachwa nyuma na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kisha analeta makisio baina ya hayo na *tawassul* kwa njia ya dhati yake baada ya kufa kwake. Na matokeo yake anakuja kwenye hatima mpya na ya kushangaza mno, nayo ni mambo ambayo hayajawahi kutamkwa na mtu yoyote mwenye kujishughulisha na 'ilmu, hata pia si wale waliozama katika ufuasi kwa njia za upofu, wakishikilia kwa ushupavu kwenye maoni yao wenyewe, na kuzua katika dini. Kumzuiya mtu yoyote mwenye kudhani yakwamba sisi tunamkandamiza yeye kwa kumbandikiza mambo ambayo hakuwahi kuyasema, sisi tutanukuu kauli zake kikamilifu, na twaomba radhi kwa wasomaji kutokana na urefu wake. Alisema: "Unapojua yakwamba *tabarruk* ni kutafuta manufaa kwa kutumia kitu na kupitia kwenye kitu hicho, ndipo utakapojua yakwamba *tawassul* kwa njia ya athari za Mtume (صلى الله عليه وسلم) zilizoachwa nyuma ni jambo lililopendekezwa na kufaradhishwa. Licha ya kutaja *tawassul* kwa njia ya dhati yake iliyo tukufu. Hakuna tafauti kwenye hilo baina ya kuwepo kwake hai au baada ya kufa kwake, kwani athari zake na yale mambo aliyoyaacha nyuma, si viumbe vyenye uhai; Kwahivyo, kutafuta manufaa kutokamana navyo au kufanya *tawassul* kwa njia ya kuvitumia ni sawa katika uhai wake na baada ya kufa kwake. Maswahaba walitafuta kufanya *tawassul* kwa njia ya nywele zake baada ya kufa kwake, kama ilivyothubutu katika swahîh al-Bukhârî katika mlango wa mvi (nywele za kijivu) za Mtume (صلى الله عليه وسلم), na wanapinga *twassul* kwa njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake, kwani wanasema yakwamba athari za Mtume (صلى الله عليه وسلم) zilikatika kwa kufa kwake, kwahivyo *tawassul* kwa njia ya kumtumia yeye ni *tawassul* kwa njia ya kitu kisichokuwa na athari yoyote kabisa. Hii ni dalili tu inayo-onyesha kiwango cha

kushangaza cha ujinga, kwani imethubutu kuhusiana na Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba alikuwa na athari ya utendakazi kwenye dhati yake pindi alipokuwa hai, kama vile lenye kuwajibisha yakwamba tufanye utafiti ili tuone ilikuwaje hiyo hali ya utendakazi na athari baada ya kifo chake? Hakuna yoyote miongoni mwa Waislamu awezae kunasibisha kwa mtu yoyote yakwamba wao, kwa nafsi zao, wana uwezo wa kutenda na kuleta athari juu ya hali ya aina yoyote, isipokuwa Mola Mmoja tu, aliye peke Yake. Yoyote mwenye kuamini kitu chochote kilicho kinyume cha haya atakuwa ni kafiri **KWA MUAFAKA WA WAISLAMU WOTE**. Kwahivyo sababu iliyoko nyuma ya kutafuta manufaa kutoka kwake, na kumtumia yeye kama athari zake kama njia ya *tawassul*, sio yakwamba yeye ndiye sababu ya athari yoyote, lakini sababu yake ni kwamba yeye alikuwa ndiye mbora zaidi wa viumbe vyote kwa Allâh, pasi na pingamizi yoyote, na kwa sababu yeye alikuwa ni rehma kutoka kwa Allâh kwa watu. Kwahivyo ni *tawassul* kwa njia ya mkuruba wake (صلى الله عليه وسلم) kwa Mola wake, na kwa sababu ya rehma yake kubwa kwa viumbe. Kwa njia hii, yule mtu-kipofu alifanya *tawassul* kwa kumtumia yeye (صلى الله عليه وسلم) ili yakwamba arudishiwe uwezo wake wa kuona, kwahivyo Allâh alimrudishia maono yake.[133] Kwa ajili hii na katika hali kama hiyo Maswahaba walikuwa na mazoweya ya kufanya *tawassul* kwa kutumia athari zake na mambo yanayotokamana na yeye bila ya kupokea lawama kutoka kwake. Imekwisha kutangulia huko nyuma yakwamba imependekezwa kutafuta maombezi (*shafâ'ah*) kutoka kwa watu wazuri na wema na jamii ya nyumba ya ki-Utume kwa lengo la kutafuta mvua na kundi kubwa la ma-Imâm na wanavyuoni, miongoni mwao akiwemo ash-Shawkânî, Ibn Qudâmah, as-San'ânî na wengineo. Kisha kutafautisha kuhusu jambo hilo baina ya uhai wake na wakati wa baada ya kufa kwake (صلى الله عليه وسلم) ni makosa ya ajabu yenye kushangaza na kuleta mtafaruku usiokuwa na chochote cha kuliruhusu."

[133] Dr. Bûtwî alitaja katika nukta za chini katika hadîth ya mtu-kipofu yakwamba kwenye baadhi ya riwaya pametokea nyongeza: "Kwahivyo kila unapokuwa na haja basi nawe fanya kama hivyo."! Mjinga katika udhaifu wake. (Tizama Uk.38)

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Tuna pingamizi nyingi za kusimamisha dhidi ya maneno haya, miongoni mwa zilizo muhimu zaidi ni haya yafuatayo:

1. Hapo nyuma tumetangulia kutaja mashambulizi ya al-Bûtwî juu ya ma-Salafi na tuhuma zake yakwamba nyoyo zao hazina athari za mapenzi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na misingi yake ya madai hayo ni kwamba wanakataa kufanya *tawassul* kwa kutumia njia yake (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake. Hii ni tuhuma ya urongo iliyo *bâtwil*, na kashfa ya maonevu na dhulma. Hapana shaka yakwamba Allâh (تعالى) atamsimamishia hisabu kali iwapo hatotubia kwa ikhlasi kutokamana na madai hayo. Hii ni kwa sababu ina maana amewasingizia dhidi yao maelfu ya Waislamu yakwamba wao ni makafiri, bila ya dalili yoyote au ushahidi isipokuwa dhana na udanganyifu tu, ambazo hakuna miongoni mwazo zilizo na manufaa yoyote katika kuufikia ukweli.

2. Ameukoroga ukweli na urongo na kufikia kwenye kiwango cha kushangaza. Kisha akautumia ukweli aliokuwa nao kuwa ni kama dalili ya urongo wake. Kwa ajili hii aliifikia rai ambayo hakuna mtu yoyote aliyewahi kumtangulia katika hilo. Kwahivyo iwapo tukipendelea kutafautisha baina ya sampuli mbili za maneno, basi tunasema: Ukweli uliomo ndani ya maneno yake ni:

a) Yakwamba kwa hakika Mtume (صلى الله عليه وسلم) yuko karibu kabisa na Allâh (تبارك وتعالى), na alikuwa ni rehma kutoka kwa Allâh (تعالى) kwa viumbe wote.

b) Yakwamba hakuna yoyote, hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) pia, aliye na ushawishi wa kibinafsi na athari juu ya kuupeleka ulimwengu, bali ushawishi wote juu ya upelekaji wa ulimwengu unapelekwa na Allâh, Mola mmoja wa Pekee.

c) Yakwamba imependekezwa kutafuta manufaa kutoka kwenye athari zilizotokamana na Mtume (صلى الله عليه وسلم)[134], na kwamba Maswahaba walikuwa wakifanya hivyo katika wakati

[134] Nukta ya Mfasiri: Kwa mfano nywele zake zinapokatwa na maji aliyokwisha kutumia baada ya kutawadhia...

wa uhai wake (صلى الله عليه وسلم) naye akaidhinisha hilo kwa kuwanyamazia.

Nukta hizi tatu ziko sawa na hakuna utesi kuhusiana nazo, na iwapo mtunzi alikoma baada ya hapo, basi hapatokuwa na haja ya kutoa maoni. Ama kuhusu urongo uliomo kwenye maneno yake, kuhusiana na ambayo kwa hakika yaliyo na utesi mkubwa, ni haya yafuatayo:

a) Yakwamba inaruhusiwa kufanya *tawassul* kwa kutumia athari zilizokuwa zikitokamana na Mtume (صلى الله عليه وسلم), na kwamba Maswahaba walikuwa na mazoweya ya kufanya *tawassul* kwa njia ya kuzitumia athari zake na kila kinachotokamana na yeye.

b) Alikuwa akifanya *tawassul* na *tabarruk* (kutafuta manufaa) yote yakiwa ni mamoja.

c) Yakwamba inaruhusiwa kufanya *tawassul* kwa kutumia dhati yake kama ambavyo inavyoruhusiwa kutafuta manufaa kutokamana na athari zake na mambo yenye kutokamana na yeye.

d) Sababu inayoruhusu *tawassul* kwa kutumia njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba yeye ni mbora wa viumbe vyote.

e) Ujinga wake wa maana ya neno 'al-*istishfâ*' (maombezi makubwa) kiyasi cha kwamba analitumia kama dalili ya sampuli ya uzushi ya *tawassul*.

f) Amewashutumu ma-Salafi kwa urongo kwa kudai kuwa wana msimamo yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na mazoweya ya kuwa na athari za kibinafsi na ushawishi juu ya upelekaji wa ulimwengu katika uhai wake, na kwamba hilo lilimalizika pindi alipokufa, na kwamba hii ndiyo sababu wao wanakataa *tawassul* kwa kupitia kwake (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake.

g) Alidai yakwamba yule mtu-kipofu alifanya *tawassul* kwa kutumia njia ya ukuruba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Mola wake.

h) Alidai yakwamba Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ndiye mbora wa viumbe vyote bila ya kuwa na mipaka yoyote.

Kwahivyo sasa tutazichambua nukta zote hizi kwa kina, na ndio tunasema:

1. MAKOSA YA AL-BÛTWÎ KATIKA KUIFANYA *TABARRUK* (KUTAFUTA MANUFAA) NA *TAWASSUL* KUWA NI HICHOHICHO KITU KIMOJA

Amesema Dr. Al-Bûtwî: "Kufanya *tawassul* kwa kutumia athari alizoziacha Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni jambo lililopendekezwa na ni la kisheriya, licha ya kuitaja *tawassul* kwa njia ya dhati yake mwenyewe." Kwahivyo imedhihirika kutokamana na maneno yake yakwamba anafanya makisio baina ya *tawassul* kwa njia ya dhati yake (صلى الله عليه وسلم) na kutabaruku kutoka kwenye athari zake alizoziacha, na kuithibitisha hapo uhalali wake. Kisha akiita hiyo tabarruk '*tawassul*', na tuliyoyasema yamezidi kutiliwa mkazo kwa aliyoyasema kwenye Uk.196 katika kitabu hicho-hicho ambapo, baada ya kuzitaja baadhi ya riwaya kuhusu Maswahaba wakitafuta baraka kutokamana na athari zilizowachwa naye (صلى الله عليه وسلم), akasema: "Kwahivyo ikiwa hali ni kama hiyo kuhusiana na *tawassul* kwa kutumia njia ya athari zake za kuonekana alizoziacha, sasa itakuwaje kuhusu *tawassul* kwa kutumia njia ya utukufu wake mbele ya Allâh (جلّ جلاله)? Na itakuwaje kuhusu *tawassul* kwa njia ya kuwepo kwake kama rehma juu ya walimwengu wote?" Lakini kwa haraka sana alirudi nyuma kutokana na haya na kisha akadai yakwamba kutafuta baraka na *tawassul* ni hicho-hicho kitu kimoja, na akakataa yakwamba alifanya makisio baina ya hayo mambo mawili. Basi akasema: "Kwahivyo usijiachilie kufanya makosa ya kudhania yakwamba sisi tuna makisio baina ya *tawassul* na *tabarruk*. Hili ni suali ambalo lisiloweza kutatuka kwa njia ya makisio, kwani *tawassul* na *tabarruk* (kutafuta manufaa) ni maneno mawili tu yenye maana moja, ambayo ni kutafuta yaliyo mazuri na baraka kwa kutumia njia (*wasîlah*). Kwahivyo zote mbili, *tawassul* kwa Jaha yake (صلى الله عليه وسلم) mbele ya Allâh, na *tawassul* kwa njia ya athari zake alizoziacha, na kila kilichotokamana na yeye, na nguo zake, yote haya yakiwa ni

mifano na sehemu moja zinazoingia kwenye ufahamu wa ujumla, ambao ni *tawassul* isiyokuwa na mipaka, ambayo hukmu zake zimethibitishwa katika ahâdîth zilizo swahîh. Kisha sampuli zote zenye kutafautiana zinaingia chini ya ujumla wa maandiko (*nass*), kwa njia ya kinachojulikana kwa wanavyuoni kama 'kutotilia maanani kilichopita kiyasi'." Lakini ukweli wa mambo ni kwamba kilichodhihirika kutokamana na matamshi yake ya mwanzo ambayo uovu wake ni sahali kuliko aliyoyasema mwishoni mwake, kwani *tawassul* kwa uwazi kabisa ni kitu ambacho kilicho tafauti na *tabarruk*. Yoyote aliyejaribu kusema yakwamba hivyo viwili ni kitu kimoja atakuwa amefanya makosa makubwa, na ametumbukia ndani ya ujinga mkubwa wa uhakika wa sheriya, mambo kama hayo hayaruhusiwi kwa mwanafunzi yoyote wa ki-ilimu mwenye kujistahi. *Tabarruk* ni kutafuta manufaa kwa mtu aliyejipatia wadhifa wa kitu fulani chenye kutokamana na mabaki na athari zilizowachwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kutarajia mazuri kutokana nazo, kama kitu chake (صلى الله عليه وسلم) makhsusi. Ama kuhusu *tawassul*, basi ni mtu kujiambatanisha na maombi yake kwa Allâh (تعالى) na mojawapo ya njia za kujikurubisha ambazo Allâh (تعالى) alizowawajibishia waja Wake. Kwa mfano amesema yakwamba: "Yâ Allâh nakuomba Wewe kwa kupitia kwenye mapenzi yangu kwa Mtume Wako (صلى الله عليه وسلم) yakwamba unisamehe mimi" na kadhaalika. Kwahivyo tafauti inaweza kuonekana kwenye mambo mawili:

i. Yakwamba kwa kupitia kwenye *tabarruk*, mtu huwa anatarajia kupata mambo mazuri ya kilimwengu tu, kinyume cha *tawassul* kwa njia ambayo mtu anaweza kutarajia kupata mazuri ema ya kilimwengu ama ya Akhera, ama yote mawili.

ii. *Tabarruk* ni njia ya kutafuta manufaa ya haraka na mazuri, kama ilivyotangulia, kinyume cha *tawassul* ambayo ni mtu kujiambatanisha na maombi yake tu, haiwezi kutumika isipokuwa ifuatane na maombi.

Kwahivyo katika uchambuzi wa haya yote, tunasema: Imewajibishwa ki-sheriya kwa Muislamu kufanya *tawassul* anapo-omba *du'â'* kwa kutumia mojawapo ya Majina yaliyokamilika ya Allâh (تبارك وتعالى), kwa mfano, na jambo hilo kwa kupitia kwenye *tawassul* hii anatafuta kujitosheleza kwa mahitaji yoyote ya kilimwengu, kama vile

kuongezewa riziki, au mahitaji yoyote yanayohusiana na Akhera, kwa mfao; kuokolewa na Moto. Kwahivyo anasema: “Yâ Allâh! Nakuomba, na kujikurubisha Kwako kwa uhakika yakwamba Wewe ni Allâh, uliye Mpweke, Mwenye kustahiki kukusudiwa, yakwamba uniponye maradhi yangu,” au, “Uniingize nami Peponi...”

Hakuna yoyote awezae kumkashifu mtu huyu kwa lolote katika haya. Lakini hata hivyo, hairuhusiwi kwa Waislamu kufanya hivi haliyakuwa wakitafuta manufaa kutokamana na kitu kilichowachwa nyuma na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwahivyo hawezi na hairuhusiwi kwake kusema, kwa mfano: “Yâ Allâh! Nakuomba Wewe na kutumia kama njia ya kujikurubisha Kwako, kilemba cha Mtume Wako, au muundi wake, au mkojo wake, yakwamba unisamehe mimi na unirehemu...” Yoyote aliyefanya mfano wa haya bila ya shaka yoyote atawapa watu fursa ya kuwa na shaka kubwa juu ya akili yake na uwezo wa fahamu yake, licha ya kutaja ‘aqîdah yake na hali ya dini yake.

Yaliyodhihirika kutoka kwenye maneno ya Dr. Al-Bûtwî ni, hatahivyo, yakwamba ataikubali *tawassul* hii ya kiajabu, na kwamba ataizingatia hiyo na *kutabaruku* kwa athari alizoziacha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni kitu hicho-hicho kimoja. Kwahivyo kwa kufanya hivi haogopi kuwatuhumu ma-Salafi kwa kutumbukia ndani ya makosa ya kushangaza na kuchanganyikiwa kwa kudhani yakwamba hakuna lenye kuliruhusu. Lakini hatahivyo, wasomaji sasa hivi wataweza kubainikiwa ni nani kihakika aliyetumbukia ndani ya kosa la upofu na kuchanganyikiwa. Hili linatukumbusha sisi kuhusu kipande cha hikma ya ki-Arabu kisemacho: “(Mwanamke) alinilaumu mimi kuhusu kosa lake mwenyewe na kisha akaponyoka.” Kwa hakika ni ukweli ulioje aliposema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

« إِنَّ مِمَّا أَدْرَكَ النَّاسُ مِنْ كَلَامِ النُّبُوَّةِ الْأُولَى: إِذَا لَمْ تَسْتَحِ فَاصْنَعْ مَا شِئْتَ »

“Kwa hakika kutokamana na kile walichopokea watu kutoka kwa Mitume waliotangulia ni: ‘Ikiwa huoni haya basi fanya upendavyo.’”[135]

[135] Imepokewa na Ahmad, al-Bukhârî (tafsiri 8/89/141) na wengineo.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Kuna nukta ya hatari kubwa sana ambayo hapana budi tahadhari itanabahishwe, nayo ni kwamba anadai yakuwa *tawassul* yoyote, pasi na mipaka, ithibitishwe na ahâdîth zilizo swahîh. Huu ni urongo na *bâtwil* kwani si chochote zaidi ya dhana na madai tu yasiyokuwa na uhakika wowote, isipokuwa kwenye fikra zake. Bali *tawassul* ya kipekee yenye kumuhusu Mtume (صلى الله عليه وسلم) iliyothibitishwa ni *tawassul* ya kupitia njia ya *du'â'* za Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama ilivyotangulia.

Ama kuhusu *tawassul* kwa kupitia Jaha ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au athari zake alizoziacha nyuma, basi hakuna chochote kutokamana na haya kilichothibitishwa katika Kitâb wala Sunnah. Kwa hakika tunamtaka Dr. Atuonyeshe hadîth moja iliyo swahîh inayo-onyesha madai yake, na sisi tuna hakika yakwamba hatokuwa na uwezo wa kupata kitu chochote kama hicho. Kwa hakika sisi tumemzoweya akithibitisha hukmu za hatari sana bila ya hata chembe ya ushahidi! Vilevile analeta madai makubwa sana yasiyokuwa na misingi yoyote, isipokuwa yakwamba hivyo ndivyo inavyojitokeza kwa mtazamo wake. Inatosheleza kwake yakwamba msomaji anaamini na kukubali kikamilifu lolote asemalo, lakini msomaji na ajitahadhari na kuuliza dalili kwa lolote asemalo, kwa sababu jambo hilo kwa mtazamo wake linaonyesha tabia mbaya na ukosefu wa dini, na hii ndiyo njia ya ma-Salafi. Kwahivyo twaomba Allâh atuhifadhi. *Jitahadharini*!

2. KUTOFAA KWA *TAWASSUL* KWA NJIA YA ATHARI ALIZOZIACHA MTUME (صلى الله عليه وسلم) BAADA YA KUFA KWAKE

Baada ya kuthibitisha tafauti ya *tawassul* na *tabarruk*, kisha tutajua yakwamba hatutafuti kutumia athari zilizoachwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni kama njia ya kufanya *tawassul* kwa Allâh, lakini badala yake tunatafuta kujipatia manufaa kwa kuzipitia njia hizo tu, kwa maana yakwamba kule kujipatia hizo tutatarajia kupata baadhi ya manufaa ya kilimwengu, kama ilivyotangulia. Msimamo wetu kuhusu kufanya *tawassul* kwa kutumia athari zilizoachwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) halijakuwa ni jambo lililoruhusiwa kisheriya, na kwamba ni urongo dhidi ya Maswahaba (رضوان الله عليهم), kudai yakwamba walikuwa na mazoweya ya kufanya *tawassul* kwa athari hizi. Yoyote apendae

kudai kitu chochote kilicho kinyume cha haya basi na alete dalili na athibitishe yakwamba Maswahaba walikuwa na mazoweya ya kusema katika *du'â'* zao, kwa mfano: "Yâ Allâh! Kwa kutumia mate ya Mtume Wako, au kinyezi chake, tuokoe na Moto"!! Hakuna mtu mwenye akili zake timamu atakaeruhusu jambo kama hilo lisimuliwe, basi itakuwaje kuhusu kutumia njia kama hiyo. Kisha lau kama Dr. Al-Bûtwî bado angali kwenye shaka kuhusu hilo, na anadhania yakwamba linaruhusiwa, basi na alithibitishe hili kwa kulifanya kwa kuomba *du'â'* kama hizi akiwa juu ya minbar. Ikiwa hatolifanya, na hawezi kulifanya, *insha'Allâh*, maadamu ataendelea kudumu na akili zake timamu, na maadamu chembe ya Imani imebaki moyoni mwake, basi hiyo ni dalili yakwamba anatamka kwa ulimi wake mambo asiyoitakidi moyoni mwake. Jambo hili hapana budi kuliashiriya yakwamba sisi tunaamini kujuzu kufanya *tabarruk* kwa athari zake (صلى الله عليه وسلم) na wala hatulipingi hilo, kinyume na hisiya inayotolewa na wapinzani wetu. Lakini hata hivyo, hilo la kufanya *tabarruk* lina shuruti zake, miongoni mwazo ni kuwa na Imani swahîh kama inavyowajibishwa na sheriya na inavyokubalika kwa Allâh. Kwahivyo mtu asiyekuwa Muislamu wa kweli, mwenye *ikhlasi*, basi Allâh hatompa uzuri wowote kwa kutafuta kwake kupenda manufaa kwa njia hii. Sharuti la zaidi kwa mwenye kupenda *tabarruk* kama hizo ni kwamba kwa hakika anajipatia athari za mabaki yaliyoachwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo kisha anayatumia kwa malengo haya. Lakini sisi tunajua yakwamba athari alizoziacha Mtume (صلى الله عليه وسلم), ema ziwapo ni kilemba, au nywele, au vitu vinavyotokamana na yeye, ambavyo sasa hivi vimetupotea, na haiwezekani kwa mtu yoyote kuthibitisha kwa yakini yakwamba kumebaki kitu chochote miongoni mwavyo. Kwa vile hali ni kama hii basi kutabaruku kwa athari hizo sio mas'ala ya kujitokeza kwenye zama zetu[136], bali limekuwa ni suala la kutakasika

[136] Dr. anayezungumzwa hapa amejaribu katika nukta ya chini (Uk.197) ya kitabu chake kilichotangulia kutajwa, kujibu jambo ambalo nililoandika kwenye *risala* yangu *Naqd Nusûs Hadîthiyyah* nilipokuwa nikimjibu al-Khattânî. Alinukuu yakwamba nilisema ndani yake: "Kusitarajiwe manufaa yoyote kutoka kwenye ahâdîth zinazohusu *tabarruk* kutokamana na athari zilizoachwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye zama zetu hizi..." Ni masikitiko yakwamba Dr. ameweza, kwenye nukuu hii kwa mukhtasari, kudhihirisha mfano ulio wazi wa udanganyifu katika kunukuu wanayoyasema watu, kwani aliyageuza maneno yangu vibaya sana, bali uhakika wa niliyoyasema ni:

la kitaalamu, kwahivyo halifai kujadiliwa kwa urefu. Lakini hatahivyo, kuna mas'ala ambayo ni lazima yafafanuliwe nayo ni kwamba hata kama Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaruhusu Maswahaba zake katika vita vya Hudaibiyyah na katika nyakati nyenginezo, kutabaruku kutokamana na kuzitafuta athari alizoziacha, basi hayo yalikuwa ni kwa sababu muhimu ambayo iliyokuwa na umuhimu wake makhsusi katika wakati huo. Sababu hii ilikuwa ni kutia khofu kwa makafiri wa ki-Qureysh, na kuonyesha kiwango cha unyenyekevu walichokuwa nacho Waislamu kwa Mtume wao, na mapenzi yao kwake, na jinsi walivyojitolea nafsi zao katika kumuhudumikia, na heshima walizokuwa nazo. Lakini hairuhusiwi kuyafumbia macho, wala kuuficha ukweli yakwamba baada ya vita hivi Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahimiza Waislamu, kwa uslubu wa hikima na kwa njia nzuri ya upole na adabu, kuwaepusha na njia hii ya *tabarruk*, na badala yake akawaongoza kwenye vitendo vizuri vilivyokuwa ni bora kwao mbele ya Allâh (عزّ وجلّ), na vyenye faida kubwa zaidi. Haya yameonyeshwa na hadîth ifuatayo: Kutoka kwa 'Abdur-Rahmân ibn Abî Qurâd (رضي الله عنه) yakwamba siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitawadha na Maswahaba wakajipangusa kwa maji yaliyobaki kwenye wudhû' wake, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *Ni mambo gani yaliyowapelekea nyinyi kufanya hivyo?* Wakasema: "Mapenzi ya Allâh na Mtume Wake." Basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia:

« مَنْ سَرَّهُ أَنْ يُحِبَّ اللهَ وَرَسُولَهُ، أَوْ يُحِبَّهُ اللهُ وَرَسُولُهُ فَلْيَصْدُقْ حَدِيثَهُ إِذَا حَدَّثَ، وَلْيُؤَدِّ أَمَانَتَهُ إِذَا ائْتُمِنَ، وَلْيُحْسِنْ جِوَارَ مَنْ جَاوَرَهُ »

"Hakuna faida kubwa katika kuthibitisha maagizo ya kutafuta *tabarruk* kutokamana na athari alizoziacha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye zama zetu." Sasa tizama, Allâh Akurehemu, jinsi Dr. alivyobadilisha na kuyageuza maneno yangu. Sioni iwapo alikuwa na malengo mengine yoyote katika kufanya hivyo isipokuwa kuitumia kama kisibabu cha kunishambulia na kuwachochea watu wa kawaida dhidi yangu. Sasa Jee, ewe ndugu yangu msomaji, unadhani yakwamba tabia kama hiyo inakubaliana na wema na ucha Mungu, na kwa mapenzi ya ikhlasi kuufikia ukweli? Nimeujibu kikamilifu urongo huu..., na hivi karibuni yametokeza kwa mfumo wa risala ndogo: *Difâ' 'anil-hadîth in-Nabawî was-Sîrah*...

"Yoyote aliyeridhika yakwamba ampende Allâh na Mtume Wake, au apendwe na Allâh na Mtume Wake, basi na ayaswadikishe maneno yake anapozungumza, na atekeleze amana yake pindi anapoaminiwa, na awe na tabia nzuri kama jirani mwema."[137]

[137] Ni hadith iliyothubutu yenye idadi ya silsila na ushahidi katika *Mu'jam* ya at-Twabarânî na asili nyenginezo. Ameashiriya al-Mundhirî katika *at-Targhîb* (3/26) yakwamba ni *hasan* na nimeinukuu na kuifanyia utafiti katika *as-Swahîhah* (no.2998)

3. KASHFA KUBWA

Inaonekana kana kwamba huyu Dr. hawezi kupumbazika kimaisha au akawa na utulivu wa akili mpaka azue kashfa dhidi ya ma-Salafi, na urongo dhidi yao. Mara nyengine ule urongo huwa uko wazi na mara nyengine huwa umezibwa. Sasa hapa ametuzulia sisi kashfa, akidai yakwamba sisi tunatumia kama dalili kupinga *tawassul* kwa njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), baada ya kufa kwake, matamshi yakwamba ushawishi wake wa kibinafsi (athari zake) juu ya matukio ya kilimwengu yalimalizika baada ya kufa kwake, na kwamba kwahivyo haifai kufanya *tawassul* kwa kumtumia yeye (صلى الله عليه وسلم) baada ya kufa kwake. Akajumlisha uhakika wa ziyada yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwa na athari zozote juu ya matukio ya kilimwengu, si katika uhai wake wala baada ya kufa kwake, si mahali kokote wala wakati wowote, na kwamba wa Pekee anayeupeleka ulimwengu ni Allâh, Peke Yake, (سبحانه وتعالى). Kwahivyo ni jambo la wazi kutokana na haya yakwamba anawakashifu ma-Salafi kwa kuamini yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na uwezo wa kibinafsi juu ya matukio ya kilimwengu katika uhai wake. Lakini hata hivyo huu ni urongo wa wazi na kashfa ya wazi, hakuna Salafi yoyote asemae hayo. Kwa hakika hakuna kitu kama hicho kiwezacho hata kupita kwenye fahamu za ma-Salafi. Kwa hakika watawezaje kuyasema haya inapokuwa wao ndiwo walinganizi wa *tawhîd* iliyotakasika na kwenye dini ya sawa. Wao ndiwo wale wenye kujitolea kuhusika kwao kukubwa katika kufanya Ibada zao wakimtakasia Allâh (تعالى), aliye Pekee, na kutakasa ‘Aqidah zao kutokamana na kila doa la *Shirk*, na kutokamana na kila madhara ya *tawhîd*, hata kama ni kosa tu la tamko. Kisha juu ya njia hii wamekabiliwa na madhara kutoka kwa watu, kukashifiwa, kuzuliwa urongo na tuhuma za urongo. Lakini watu, na akiwemo miongoni mwao Dr. al-Bûtwî, hawana walichonacho juu yao isipokuwa ni kuonewa kijicho kutokana na ulinganizi wao wa haki. Licha ya haya haogopi kuwakashifu kwa hatia yao ya *bâtwil* na urongo ambayo hata yeye mwenyewe, kama tunavyoamini sisi, kabla ya kuyajua yoyote mwengine kuwa hiyo ni kashfa. Vinginevyo na atufafanulie, iwapo ataweza, asili ya madai ya kauli hii, na ni nani miongoni mwa ma-Salafi aliyeyasema hayo, na yamenukuliwa kutoka kwenye vitabu vyao vipi au vikao gani vyao vya ki-ilimu. Ikiwa hatofanya hivyo, na

atawezaje kufanya hivyo, basi urongo wake na kashfa zake za urongo utadhihirika kwa kila mmoja ajionee mwenyewe.

Jambo jengine ambalo halina budi kutajwa hapa ni maneno ya al-Bûtwî: “Na yoyote mwenye kudai kitu chochote kutokamana na hayo ni kafiri kwa muafaka wa Waislamu.” Kwahivyo yanapochangia matamshi haya (pamoja na madai yake kwenye nukta iliyotangulia), lau yatazingatiwa kwa hadhari, ni tangazo la ujumla la Ukafiri dhidi ya ma-Salafi wote. Huu ni urongo wa zaidi na tuhuma za dhulma. Hapana shaka yakwamba Allâh atamuhukumu kwa hayo, kwani ma-Salafi ni Waislamu. Kwa hakika wao ndio watu wenye haki zaidi katika kusifiwa na Uislamu. Vilevile wao wanajua kwa yakini yakwamba kutangaza kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) mwenyewe, au mtu mwengine yoyote, huwa na kiyasi fulani cha ushawishi juu ya matukio ya kilimwengu ni *Shirk* kuhusiana na Uola wa Allâh na unamtoa mtu nje ya dini. Wao ni miongoni mwa wenye umakinifu zaidi kwenye nukta hii na wanaotahadharisha dhidi yake. Haliyakuwa huyo al-Bûtwî mwenyewe na jinsi yake hutafuta sababu tafauti mbalimbali na uhalali kwa wale wenye kutumbukia ndani yake. Haifai hali kuwa ni yenye kutukosesha fursa ya kumkumbusha yeye na walio mfano wake ya yale ambayo tuliotangulia kuyataja kwenye risala hii, kuhusiana na sababu ya uhakika, yenye kutupelekea sisi kuizuiya *tawassul* kwa kupitia kwenye njia za dhati, daraja na Jaha za watu wema, na ilivyo yakwamba ni jambo ambalo halikupokewa wala kupatikana kwenye sheriya iliyotwahirika. Wala halikufanywa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), wala Maswahaba zake. Kwahivyo hizo ni hekaya za Uzushi. *Nusûs* (maandiko ya kisheriya) zilizotumiwa na wapinzaani wetu ni ema swahîh ambazo, zisizo-onyesha madai yao, au nyengine si swahîh, na haya yametangulia kwa kina.

Hii ndiyo sababu inayotupelekea sisi kuikataa sampuli hii ya *tawassul* na tunasema waziwazi: Ikiwa ilipokewa kwenye sheriya basi tungeliikubali na kuishikilia kuwa ni kauli yetu, na hakuna kiwezacho kutuzuiya nacho kwani sisi twajivunia na sheriya. Kila inachotupa ruhusu, na sisi twakiruhusu, na kila inachotukataza nacho, na sisi twakikataza. Ni jambo la kushangaza jinsi Dr. huyu anavyoipuuza sababu hii ya kimsingi na badala yake anazua sababu ambayo mapendelewa ya nafsi yake yeye mwenyewe yanamdanganya. Kisha anaitumia hiyo kama njia ya kutushambulia na kutuzulia masingizio

maovu, na kuwashawishi watu wa kawaida dhidi yetu. Sasa hebu tizama, *Allâh Akurehemu*, uslubu huu wa kushangaza wenye kwenda kinyume na dini na 'ilmu, na tumshtakie Allâh (عزّ وجلّ) kwa pamoja, kwa uhakika yakwamba kwa hakika, haki na watu wake bila ya shaka ni wageni kwenye zama hizi.

4. KOSA LAKE KATIKA KUDAI YAKWAMBA SABABU YA *TAWASSUL* KWA KUPITIA NJIA YA MTUME (صلى الله عليه وسلم) NI KWAMBA YEYE NDIYE MBORA WA KILA KITU KATIKA VIUMBE

Hili ni kosa jengine la zaidi ambalo Dr. huyu ametumbukia ndani yake kama matokeo ya pupa alilokuwa nalo na ukosefu wa kufikiriya kwa makini kuhusu anayoandika. Anatangaza wakwamba sababu ya *tawassul* kupitia kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba yeye , bila ya sharuti zozote, ndiye mbora wa viumbe vyote kwa Allâh, na pia yakwamba yeye ndiye rehma kutoka kwa Allâh kwa waja wote, kama tulivyotangulia kuayataja hayo. Basi twamwambia yeye: Yakwamba kwa maoni yako hii ina maana, kwahivyo, yakwamba ama kwa ambaye asiyekuwa hivyo, (*yaani*; si mbora wa viumbe wa Allâh...), yakwamba hairuhusiwi kumtumia yeye kwa *tawassul,* kwani sababu yenye kuliruhusu hilo halipo kwa mtu kama huyo. Hii ni kwa sababu, iwapo hii ndiyo sababu na sharuti lake, basi pindi likiwa halipo, kila lenye kulitegemea ni lazima likosekane kuwepo. Kwahivyo maana ya maneno yake, hata kama yeye mwenyewe hayazingatii anayoyasema, ni kwamba hairuhusiwi kufanya *tawassul* kwa kupitia njia ya mtu yoyote isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Lakini sisi twajua kwa yakini yakwamba yeye anaamini jambo lililo kinyume cha haya, na yeye anaruhusu *tawassul* kwa kupitia njia ya kila Mtume, mja mwema mwenye kupendwa na Allâh, na mtu mwema. Kwahivyo yeye mwenyewe anasema kitu ambacho asichokiamini, na anajichanganya mwenyewe. Sababu ya haya ni mojawapo ya mambo mawili: Ema hafahamu maana ya neno *manât* (sababu inayofuata jambo, ambalo lililojengewa na sharuti) ni nini kulingana na wanavyuoni, au hajazingatia ni yapi matokeo yanayojiri kutokana na matamshi yake, na hili ndilo lenye uwezekano zaidi, na Allâh ndiye Mjuzi zaidi.

AT-TAWASSUL – SAMPULI NA HUKMU ZAKE

Jambo jengine ambalo inatupasa kulieleza katika nukta hii ni kama ilivyoafikiwa na wanavyuoni wa msingi wa *Fiqhi* – yakwamba kwa jambo kukubalika kuwa ni sababu iliyopelekea baadhi ya hukmu, zilizoekewa sharuti, ni lazima liwe ni jambo lililo makhsusi katika *nass* ya Kitâb au Sunnah, na haliwezi kuegemezwa juu ya dhana au kupatikana kwa njia ya ubunifu wa kibinafsi. Lakini tukiyachunguza maneno ya Dr. basi twaona yakwamba anadai kitu kuwa ni sababu fulani, ambayo isiyokuwa na kitu chochote chenye kufanana na dalili kutoka kwenye Kitâb au Sunnah. Bali mategemezi yake ya hilo jambo ni dhana tupu na makisio ya kibinafsi. Sasa jee, hivi ndivyo ambavyo anavyodhania Dr. yakwamba 'ilmu za uhakika wa kisheriya zinavyothibitishwa, yeye ambaye aliyetunga anwani kwenye baadhi ya vitabu vyake kwa ibara: *"Abhâth fil-Qimmah"* [Makala katika Kilele cha Utafiti]?

Suala la tatu na la mwisho ni kwamba madai ya Dr. yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiye mbora zaidi kuliko viumbe vyote vya Allâh, na hili ni suala la Imani na 'aqîdah, na kulingana na rai yake ni kwamba kitu kama hicho hakiwezi kuthibitishwa[138] isipokuwa kwa kupitia kwenye *nass* (mandiko) ambayo kuthubutu kwake kumedhihirika kutokana na kukosekana kwake uwezekano wa makosa, na ambako maana yake vilevile iko wazi na ni *ndumila kuwili* (maana yake ni hiyo hiyo moja)[139] *yaani;* kwa âyah ambayo maana yake iko wazi na ambayo ni *ndumila kuwili*, au kwa hadîth ambayo ni *mutawâtir* katika kutangazwa kwake na vilevile iko wazi na *ndumila kuwili* kulingana na maana yake. Sasa iko wapi *nass* kama hiyo yenye kuthibitisha yakwamba yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiye mbora wa viumbe vyote mbele ya Allâh bila ya sharuti zozote? Kama ijulikanavyo, hili ni suala ambalo ndani yake kuna ikhtilafu baina ya wanavyuoni, Imâm Abû Hanifah (رحمه الله) alijizuiya kuhusu suala hili, bila ya kujieleza rai yake, na yoyote apendaye kulifanyia utafiti wa zaidi na arejee kwenye sherhe ya 'aqîdatul-Imâm Abî Ja'far at-Twahâwiyyah al-Hanafiyyah *Sharhut-Twahâwiyyah* (Uk.337-348 – Al-Maktabatul-Islâmî, kwa tahqîq

---

[138] Kama alivyothibitisha kwenye zaidi ya kimoja katika vitabu vyake, kwa mfano *kubral-Yaqînât al-Kawniyyah* (Uk.26, chapa ya pili) na *al-Lâmadhhabiyyah*.

[139] Katika kuliona kosa la rai hii rejea kwenye kitabu changu: *"Hadîth ni dalili ya kivyake katika Hukmu na Imani."*

yangu). Kisha labda msingi wa Dr. wa kuthibitisha nukta hii ya ‘aqîdah ni kilichotokea kwenye kisa cha kuhusiana na *Mi’râj* ambacho kilichonasibishwa kwa njia ya urongo na uadui na Swahaba Mtukufu ‘Abdullâh ibn ‘Abbâs (رضي الله عنهما), licha ya uhakika yakwamba yeye mwenyewe, al-Bûtwî amesema[140] kuhusu kisa hiki: “Ni kitabu ambacho kilichobuniwa kwa kuzichanganya pamoja ahâdîth ambazo ni *bâtwil* zisizokuwa na asli wala sanad.”! Kwa kweli maneno yake hapa kama yalivyosimama ni ya *bâtwil*, kwani kitabu tunachokijadili hapa kwa hakika vilevile kimeleta ahâdîth nyingi zilizo swahîh, baadhi yake kutoka katika riwaya zilizopokewa na ma-Imâm wawili, al-Bukhârî na Muslim. Lakini hata hivyo, mtunzi amezichanganya pamoja na ahâdîth nyengine, baadhi yake ni *mawdhû’* na nyengine hazina asli, na nyengine ni *dha’îf*. Mimi nikayabainisha hayo katika majibu yangu kwa Dr. al-Bûtwî, yaliyochapishwa kwanza kwenye jarida la *at-Tamaddun al-Islâmî* na kisha baadae katika kitabu cha kujitegemea chenyewe kama ilivyotangulia.

5. UJINGA WAKE KATIKA MAANA YA KI-LUGHA YA ‘KUMTAFUTA MTU KUMSHUFAIYA KWA NIYABA YAKE.’ (AL-ISTISHFÂ’)

Hili ni kosa jengine la ukatili ambalo Dr. ametumbukia ndani yake, twamuomba Allâh amrekebishe na amuongoze, ambamo alitumia tamko *istishfâ’* (kumtafuta mtu amshufaiye kwa niyaba yake), iliyotokea kwenye ahâdîth kuhusu swala ya kuomba mvua, kama dalili ya sampuli ya *tawassul* ya uzushi. Basi hapo alisema: “Mapendekezo ya kutafuta maombezi kutoka kwa watu wema na wacha Mungu na wale walio kwenye jamii ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambayo iliyopokewa kuhusiana na Swala ya mvua na kwengineko, imeshatangulia kuelezwa hapo awali. Hili ni jambo linalohusu kuwepo kwa muafaka wa idadi kubwa ya ma-Imâm na wanavyuoni, wakiwemo miongoni mwao ash-Shawkânî, Ibn Qudâmah, as-San’ânî na wengineo.” Kwahivyo Dr. hawezi kutumbukia kwenye kosa kama hilo kama angelikuwa ameifahamu maana ya lugha ya *istishfâ’*. Ili kuwaelimisha wasomaji na kuwafaidisha, mimi nitanukuu ambayo baadhi ya vitabu vya lugha vinavyosema katika kuyafafanua hayo. Mtunzi wa *al-Qâmûsul-Muhît* amesema: “*ash-Shaf’*: (idadi

[140] Kwenye kitabu chake *Fiqhus-Sîra* (Uk.155)

inayogawanyika kwa mbili) ndicho kitu kilicho kinyume cha 'idadi isiyogawanyika kwa mbili', na ndicho chenye kukamilisha jozi moja. Kwahivyo *ash-Shafa'ah* ni kuongeza mtu mwengine na uje pamoja naye pindi unapotafuta kitu. Kondoo hupewa sifa ya *Shâfi'* akiwa ni kondoo jike na kondoo mchanga tumboni mwake kwa jozi moja. Kwahivyo maana ya *istishfâ'* ni: "kumtaka mtu ili mupate kukamilisha jozi pamoja." Katika *al-Mu'jamul-Wasît* kilichobuniwa na *ta'sisi* ya lugha ya kiarabu ya Misri kunapatikana ndani yake: "Kitu kinapofanywa kuwa *Shaf'* ina maana yakwamba kumeongezwa kitu pamoja nacho kukamilisha jozi... na maana ya *istashfa'a* ni: alikuwa akimtafuta mtu mwengine amsaidie, na *ash-Shafî'* na *ash-Shafâi'* ni jozi, na *ash-Shafâ'ah* ni maneno ya rafiki wa mtu, na *ash-Shafî'* ni mwenye kumuunga mwengine wakakamilisha jozi."

Katika *an-Nihâyah* cha Ibnul-Athîr munapatikana ndani yake: "*ash-Shuf'ah* imetokamana na nyongeza kwani *ash-Shafî'* ni mwenye kuongezea kitu kwenye bei juu ya kitu anachokimiliki na kwahivyo akaifanya kuwa ni jozi (mwenzake ile). Kwahivyo kutokamana na maana ya lugha ya asili ndipo ilipopatikana lugha ya kisheriya. Hii ni kwamba unachotafuta kutoka kwa wanavyuoni na watu wema ni yakwamba wao waombe *du'â'* kwa Allâh pamoja na Waislamu, kwenye misimu ya misiba, na kwahivyo kuongezea juu ya idadi ya wale wanaofanya maombi, na kwahivyo hilo linatarajiwa yakwamba maombi yatakuwa yanastahiki zaidi kujibiwa. Kwahivyo kwa kupitia haya tunaweza kufahamu vyema ni nini Shafâ'ah Kubwa (*ash-Shafâ'atul 'Adhmâ*) itakayokuwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika siku ya Qiyâmah. Kwa hakika hiyo ndiyo, kwa muafaka wa ma-'Ulamâ, *du'â'* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa watu baada ya kumjia yeye na kumtaka awaombee kwa Allâh (تعالى) awaharakishie hisabu zao.

Hakuna miongoni mwa wanavyuoni aliyefahamu kutokamana na haya yakwamba watu watasema, kwa mfano: "Yâ Allâh! Kutokana na daraja aliyonayo Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kwako Wewe tuharakishie hisabu zetu." Kilicho cha kushangaza kihakika ni kwamba Dr.al-Bûtwî anatakiwa awe na ujasiri wa kudai yakwamba kuna muafaka wa ma-Imâm na wanavyuoni, wakiwemo miongoni mwao ash-Shawkânî, Ibn Qudâmah na as-San'ânî juu ya ufahamu wake wa kushangaza na usio wa kawaida (*shâdh*), uliojegwa juu ya ujinga mkubwa wa maana za istilahi za lugha na sheriya zilizotumiwa. Tutatosheka katika kumjibu

yeye kwa kuyanukuu maneno ya mmoja wao tu hao ma-Imâm ambaye jina lake alilitumia na ambaye aliyedai kumuhusu yeye yakwamba alimshirikisha katika ufahamu wake wa *istishfâ'*, kwa maana yakwamba Imâm Ibn Qudâmah al-Maqdisî aliyeandika kitabu kukibwa zaidi cha *fiqhi* ya Hanbalî, '*al-Mughnî*'. Amesema ndani yake (2/295): "Imependekezwa kuomba mvua kwa kutumia njia ya mtu anyeonekana kuwa ni mwema, kwani hilo litamaanisha yakwamba maombi yana uwezekano mkubwa wa kukubalika. Kwa hakika 'Umar aliomba mvua kwa kutumia njia ya al-'Abbâs, mjombake Mtume (صلى الله عليه وسلم) . Amesema Ibn 'Umar: "Katika mwaka wa ukame na maangamivu, 'Umar aliomba mvua kwa kupitia njia ya al-'Abbâs, alisema: 'Yâ Allâh! Huyu ni mjombake Mtume Wako na sisi twakuelekea Wewe kwa kumtumia yeye, basi tupe nasi mvua.' Na bila ya kuchelewa, Allâh akawapa mvua." Vilevile imepokewa yakwamba Mu'âwiyah alitoka kwenda kuomba mvua, basi alipokaa kwenye minbar alisema: "Yuko wapi Yazîd Ibn al-Aswad al-Jurashî?" Basi akasimama Yazîd, na Mu'âwiyah akaomba na akamkalisha Yazîd kwenye miguu yake, kisha akasema: "Yâ Allâh! Sisi twamtumia aliye mbora miongoni mwetu na aliye na fadhla, Yazîd Ibn al-Aswad atushufaiye kwa niyaba yetu," kisha akasema: "Ewe Yazîd, inua mikono yako," basi akainua mikono yake na kuanza kuomba kwa Allâh (تعالى). Basi mara mawingu mazito yakatokeza kutoka upande wa magharibi, na upepo ukaanza kuvuma na wakabarikiwa kwa kiwango cha kiyasi cha mvua ambacho ikawa ni uzito kwao kufika majumbani mwao. Wakati mwengine adh-Dhahhâk vilevile aliomba mvua kwa kumtumia yeye. Kwahivyo ni jambo la wazi kutokana na maneno ya Ibn Qudâmah yakwamba alichomaanisha kwa neno *istishfâ'* iliyopokewa kwenye hadîth kuhusiana na swala ya mvua ni kwamba kiongozi wa Waislamu anatakiwa amchague mtu yoyote miongoni mwa wanavyuoni na ucha-Mungu aombe pamoja na Waislamu, waelekee kwa Mola wao (سبحانه), yakwamba aondoe dhiki kwa waja wake Waumini. Ibn Qudâmah hakumaanisha, na sisi tunaweza kuwa na yakini yakwamba hata haikupita kwenye fahamu yake, mfano kama huu wa ufahamu wa kimakosa ambao al-Bûtwî na wazushi kama yeye wanatafuta kutumia kwenye matamshi ya ki-sheriya. Kwani wewe huoni jinsi al-Bûtwî anavyodai mfano wa muafaka-ghushi na kisha wanatafuta kumtangaza Ibn Qudâmah na wengineo kuwa ni mashahidi wa hayo. Lakini haya hapa ndiyo matamshi ya Ibn

Qudâmah, ambayo hung'oa kabisa ufahamu wake ulio *bâtwil*. Labda ni kwamba yeye hawezi kuyafahamu yaliyoandikwa kwenye vitabu, au labda hali ni kama hivyo yakwamba analeta madai yoyote apendayo bila ya hata kurejea kwenye vitabu kabisa. Labda pengine hali ni kama hivyo yakuwa anajiona amesalimika yakwamba wasomaji wake watakubali tu ki-upofu chochote anachowaambia wao, na kwamba hakuna yoyote miongoni mwao atakayefanya utafiti, au kujisomea nafsi zao kuthibitisha lisemwalo? Kwa hakika hili ni la kujijutia, *Wallâhi,* na mojawapo ya misiba mikubwa ambayo tunayoyaona katika maisha ya Waislamu. Vilevile, hapana shaka yoyote, mojawapo ya sababu kubwa ya kuwarudisha Waislamu nyuma, kudhoofika kwao, na kuharibikiwa. Vilevile haiwezekani kubadilisha hali hii mpaka wao wenyewe wabadilishe tafauti zao na ugumu walio nao, kufuata kwao Usufi, upindanifu wao wa kufuata *madh-hab* moja, na kukubali kwao 'ilmu za filosofia na kufuata akili zao kwenye mas'ala ya Imân. Haitowezekana mpaka wawache mambo haya yote yanayopatikana kwao na kurudi kwenye uongofu wa haki kama unavyopatikana katika Kitâb na Sunnah, na ambayo iliyodhihirishwa na *Salafi da'wah* iliyo safi na angavu.

6. KOSA LAKE KATIKA KUDAI YAKWAMBA TAWASSUL YA MTU-KIPOFU ILIKUWA NI KWA KUPITIA NJIA YA DARAJA ALIYONAYO MTUME (صلى الله عليه وسلم) MBELE YA ALLÂH

Twakamilisha majibu yetu kwa Dr. al-Bûtwî kwa kuashiriya kwenye makosa yake katika kudai yakwamba *tawassul* ya mtu-kipofu ilikuwa ni kwa njia ya daraja ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), na kwa kutumia Jaha yake kama mbora wa viumbe vyote kwa Allâh. Kwa hakika haya ni madai tu matupu na hayana chochote cha kuyaunga mkono, na Dr. hawezi hata kuleta kitu chenye kufanana na dalili ya kuithibitisha. Bali imekwisha kutangulia katika risala hii yakwamba *tawassul* ya mtu-kipofu ilikuwa ni kwa njia ya *du'â'* ya Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Vilevile tumezikosoa shaka zote tunazozijua zilizoletwa na wenye kutukhalifu na ambazo wanazozitumia kama ushahidi wao wa rai za kimakosa. Vilevile pia tumeueleza udhaifu wa nyongeza ya kwenye hadîth iliyonukuliwa na Dr. ambayo aliyoinyamazia, ema kutokana na ujinga au kujifanya kuwa ni mjinga, na huo ndio msemo: "Kwahivyo

kila unapokuwa na haja basi fanya kama hivyo.” Basi hatutorudia tena hayo kwa kukhofiya kuyarefusha zaidi mas’ala.

Kutokamana na yote hayo yaliyotangulia itamdhihirikia kila mtu muadilifu apendae haki yakwamba shaka hizi zilizoletwa hazina msingi wowote na ni *bâtwil*. Kwa hakika Allâh (تبارك وتعالى) amesema:

بَلۡ نَقۡذِفُ بِٱلۡحَقِّ عَلَى ٱلۡبَٰطِلِ فَيَدۡمَغُهُۥ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٞۚ وَلَكُمُ ٱلۡوَيۡلُ مِمَّا تَصِفُونَ ١٨

“Bali (tulifanyalo ni hili:) Tunaitupa haki juu ya batili ikalivunja bufuru (fuvu) la kichwa chake; na mara (batili) ikatoweka, (ikaondoka). Na adhabu inawangojeeni kwa ajili ya haya mnayonena (kumsingizia Allâh).”[141]

Na akasema:

وَلَا يَأۡتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئۡنَٰكَ بِٱلۡحَقِّ وَأَحۡسَنَ تَفۡسِيرًا ٣٣

“Wala hawatakuletea mfano (wowote), ila tutakuletea (aya iliyo ya) haki (kujibu mfano huo) na (kukuletea) tafsiri iliyo bora.”[142]

Kila sifa njema na shukrani zinamstahiki Allâh mwanzoni mwake na mwishoni mwake juu ya taufiki Yake na uongofu Wake. Yeye peke Yake ndiye ambaye msaada Wake tunaoutaka. Hapana mola anayepasa kuabudiwa kwa haki asiyekuwa Yeye, na hapana mola isipokuwa Yeye. Na kutakasika na kila sifa za upungufu, ni kwako Wewe, Ewe Mola, na kila aina ya shukrani ni zako Wewe. Nashuhudia yakwamba hapana mola anayestahiki kuabudiwa ila Wewe. Nakuomba msamaha Wako na natubia Kwako Wewe.

[141] Sûrah al-Anbiyâ’ (21):18
[142] Sûrah al-Furqân (25):33